**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Sita — Tarehe 25 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninamwita Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake.

Na. 422

**Jimbo la Ndanda Kupata Halmashauri**

**MHE. FARAJI B. NANDALA** aliuliza: -

Je, upi mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba Jimbo la Ndanda linapata halmashauri yake baada ya kukidhi vigezo vyote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa

Faraji Buriani Nandala, Mbunge wa Jimbo la Ndanda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ndanda katika Wilaya ya Masasi lina jumla ya watu 314,778 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Uanzishaji wa Maeneo ya Utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2025, ugawaji wa mipaka ya maeneo ya utawala huanza na kusudio ambalo hupaswa kujadiliwa katika vikao vya ngazi ya halmashauri, wilaya na mkoa. Kusudio hilo huwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kupitia Katibu Tawala wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Mwongozo wa Uanzishaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2025, uanzishaji wa halmashauri tarajiwa unahitaji kukidhi vigezo mbalimbali ikiwemo uwezo wa kujitegemea kwa 50% kwa kipindi cha miaka 10 mfululizo pamoja na kuwa na idadi ya watu isiyopungua 500,000 ambapo 300,000 ni kwa halmashauri mama na 200,000 kwa halmashauri tarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi inashauriwa kukamilisha taratibu za suala hili na kuliwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kupitia Katibu Tawala wa Mkoa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, swali la nyongeza.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tutakuwa wa kweli, ni miaka saba sasa imepita tangu Serikali ilipotoa tamko la kuzitaka halmashauri 31 zihamishe maeneo ya utawala kutoka mijini na

kupeleka vijijini. Wazo hili lilikuwa ni zuri kwani lilikuwa linalenga kwenda kupeleka huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wananchi wa Jimbo la Ndanda imekuwa ni tofauti, wananchi wa Jimbo la Ndanda sasa hivi wanakuwa wanasafiri umbali mrefu zaidi ya kilometa 192 kufuata huduma za kiutawala. Swali langu: -

(a) Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kufanya marejeo upya ya tamko hili ili kubaini yale maeneo ambayo yalipelekwa kwenye sehemu siyo sahihi yarudishwe kwenye sehemu sahihi na yale maeneo ambayo yamekidhi kupata halmashauri litoke tamko la dharura ili waweze kupata halmashauri ikiwemo Jimbo la Ndanda?

(b) Je, kulingangana na majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kufuatana na mimi ama kuambatana na mimi kwenda Jimbo la Ndanda kwenda kuona namna ambavyo wananchi wa Jimbo la Ndanda wanavyopata tabu na shida ya kusafiri kufuata huduma za kiutawala, ili pia aone vigezo tulivyokidhi na ikiwezekana itoke hati ya dharura kutupatia halmashauri na kuwasaidia wale wananchi wa Jimbo la Ndanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Faraji Nandala, Mbunge wa Ndanda, amelifuatilia suala la kuomba kupata halmashauri mpya ya Ndanda mara kadhaa. Sisi kama Serikali tumhakikishie kwamba kwanza Serikali inatambua kwamba Jimbo la Ndanda liko mbali kutoka makao makuu ya halmashauri kule Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uhitaji huo viko vigezo ambavyo ni muhimu vikazingatiwa wakati wa kuanzisha makao mapya au hasa maeneo mpya ya utawala katika halmashauri zetu; mojawapo ni uwezo wa halmashauri kujiendesha; kwa

sababu kila ukianzisha halmashauri mpya maana yake unaongeza gharama za uendeshaji katika halmashauri husika. Kwa hiyo, kigezo cha kwanza ni angalau halmashauri iwe na uwezo wa kujiendesha yenyewe kwa angalau 50%; kigezo cha pili, ni idadi ya watu angalau 300,000 kwa halmashauri mama inayobaki na angalau 200,000 kwa halmashauri ile mpya ambayo inazaliwa; na suala la tatu, ni suala la umbali kutoka makao makuu ya halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na kigezo cha idadi vipo vigezo vingine. Tumshauri yeye na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi waanze utaratibu wa vikao vya ngazi ya halmashauri, ngazi ya mkoa, wawasilishe maombi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Serikali itafanya tathmini kulingana na mazingira na kuona uwezekano wa kupandisha hadhi na kupata eneo jipya la utawala kwa kadri itakayowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda Ndanda kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo, lakini pia na mambo mengine ili kuhakikisha kuwa wananchi wa Ndanda wanapata huduma bora za Serikali yao.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru, kwa kuwa Wilaya ya Same imeketi kwenye 46.9% ya Mkoa wote wa Kilimanjaro; na Wilaya ya Same ina takribani kilometa za mraba 6,221 kuonesha kuwa imechukua takribani nusu ya Mkoa wa Kilimanjaro. Jimbo la Same Mashariki ieleweke kwamba lina uwezo mkubwa, linalima 72% ya tangawizi ya nchi nzima.

Je, Serikali hawaoni kwamba kwa ukubwa wa wilaya hii, ni vyema sasa Same Mashariki wakawa na halmashauri yao na Same Magharibi wakawa na halmashauri yao ili kuwezesha majimbo haya kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Same ni moja ya halmashauri kubwa sana hapa nchini, kama alivyosema Mbunge, Mheshimiwa Mama Malecela.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba kumekuwa na uhitaji wa kupata mamlaka mpya au halmashauri mpya ya Same na tunafahamu viko vigezo ambavyo Halmashauri ya Same inakidhi, lakini viko vigezo ambavyo bado haijakidhi, na tunafahamu kwamba kwa kufuata utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwanza kumwomba Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Same kuanza taratibu za vikao na mapendekezo ili yale maombi yaweze kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Wakati huo huo, Serikali yetu ilifanya maamuzi kwamba kwa sababu tunayo maeneo mengi ya utawala ambayo hayana miundombinu wezeshi zikiwemo ofisi za Wakurugenzi, Watendaji wa Kata, Maafisa Tarafa, Vijiji na kadhalika, tuliona ni busara kwanza kuboresha miundombinu katika mamlaka zilizopo na baadaye tukiona inafaa basi tutaona namna ya kuendelea kuanzisha maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuendelee na hatua hizo kimsingi na wakati huo ukifika basi mamlaka husika tutaona namna nzuri ya kufikia hatua ambayo itakuwa njema kwa upande wa Halmashauri ya Same. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaona mko wengi, ninaomba maswali ya nyongeza yawe mafupi. Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali la nyongeza.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dodoma ndilo jiji lenye eneo kubwa zaidi kuliko jiji lolote katika nchi hii likiwa na *square kilometre 2,607,* lakini mpaka sasa jiji hili lina majimbo mawili na halmashauri moja tu ya Jiji la Dodoma.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza halmashauri katika Jiji la Dodoma ili kupambana na changamoto za makao makuu ikiwemo ongezeko kubwa la watu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na mpango wa Serikali wa kuboresha kwanza maeneo ya utawala yaliyopo, ni kweli kwamba Jiji la Dodoma ni jiji kubwa. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Menejimenti ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuona uwezekano wa kukaa kupitia vigezo na kuanza taratibu za awali wakati Serikali ikiona uwezekano wa kufanya hatua hizo huko baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Je, Serikali haioni kwamba kwa kuendelea kuwaacha wananchi wa Jimbo la Ndanda mbali na halmashauri yao inawanyima kuwaunganisha katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii? Haioni haja ya kutumia majengo ya zamani ya Halmashauri ya Masasi ili waendelee kupata huduma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ziko halmashauri nyingi ambazo zina vigezo vya

kupata mamlaka mpya ikiwemo Halmashauri ya Masasi kwa maana ya upande wa Ndanda, isipokuwa baadhi ya vigezo bado havijatimia ikiwemo idadi ya watu na uwezo wa halmashauri kujitegemea.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kusogeza huduma za kijamii karibu na wananchi wakiwemo wananchi wa Ndanda. Hivyo tutaendelea kupitia vigezo, kufanya tathmini na kuona uwezekano wa kupandisha hadhi halmashauri hizo huko baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene, sasa aulize swali lake.

Na. 423

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mambali**

**MHE. JOHN S. LUHENDE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mambali – Bukene?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Jimbo la Bukene, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mambali ina wakazi 30,398, ni kata yenye idadi kubwa ya watu kuliko kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na ipo kilometa 44 kutoka

kwenye kituo cha afya cha karibu na kilometa 84 kutoka hospitali ya karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kata hii inakidhi vigezo vya kujengewa kituo cha afya kutokana na idadi ya watu pamoja na umbali kufikia huduma za dharura na upasuaji. Tayari Serikali imeweka Kituo cha Kata ya Mambali katika mpango wa ujenzi ambao unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia Mpango wa Uwekezaji wa Afya ya Mama na Mtoto *(TMCHIP)* kwa kiasi cha shilingi milioni 600.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Stephano Luhende, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; tunacho kituo kingine cha afya cha pale Bukene na kimeelemewa sana; je, Serikali ina mpango gani wa kukipanua Kituo hicho cha Afya cha Bukene?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, kuna mpango gani kwa kata nyingine ikiwemo Kata ya Semembela na Kata ya Sigili, maana zina idadi kubwa ya watu, lakini hazina vituo vya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimpongeze Mheshimiwa John Luhende, Mbunge wa Bukene kwa kuwasilisha maombi Serikalini. Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imesikia kilio cha wananchi wa Kata hii ya Mambali na tayari imetenga shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba bado kuna kata za kimkakati zinazokidhi vigezo katika Jimbo la Bukene ambazo zinahitaji vituo vya afya. Ninaomba nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kuwa maswali yake yote mawili Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu katika kata zote zenye sifa ya kuwa na vituo vya afya na tutaendelea kufanya ujenzi katika maeneo hayo kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumsisitiza pia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega kwamba waanze kutenga fedha za mapato ya ndani angalau kwa awamu ili kuanza ujenzi wa vituo katika kata hizo na Serikali itakuja kuunga mkono juhudi za wananchi na Serikali ya halmashauri katika ujenzi wa vituo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Exaud Kigahe, swali la nyongeza.

**MHE. EXAUD S. KIGAHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru; ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Ihanu kama ambavyo waliahidi ambayo ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha sekta ya afya katika Jimbo la Mufindi Kaskazini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ihanu katika Jimbo la Mufindi Kaskazini ni moja ya kata ambazo ziliwasilishwa na Mheshimiwa Kigahe, Mbunge wa Jimbo hilo kama kata ya kimkakati na tayari ilishaingizwa kwenye orodha ya vituo vya kata za kimkakati katika kata za Jimbo la Mufindi Kaskazini.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea na taratibu za kibajeti kwa ajili ya kuona namna ambavyo tutapeleka fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kata ya Ihanda ina watu wengi sana na ina uhitaji mkubwa wa kituo cha afya kutokana na sehemu ilipo.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kujenga vituo vya afya kote nchini ikiwemo katika Jimbo la Vwawa kwa Mheshimiwa Hasunga. Tunafahamu kwamba bado kuna kata ikiwemo aliyoitaja na kata nyingine zenye vigezo vya kujengwa vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, safari ni hatua, tunakwenda kwa awamu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Serikali inatambua umuhimu wa kusogeza huduma ya afya kwenye kata hiyo, tutaendelea kutenga fedha kwa awamu ili tuanze ujenzi wa kituo cha afya katika eneo hilo kwa fedha ya Serikali Kuu na pia kwa fedha ya mapato ya ndani ya halmashauri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Balang'dalalu ina wakazi zaidi ya 19,000 na hakuna zahanati wala kituo cha afya. Umbali wa kutoka Kata ya Balang'dalalu mpaka huduma iliyopo karibu ni kilometa zaidi ya 21. Wananchi wamekwishatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Balang'dalalu hasa ukizingatia umbali pamoja na idadi ya wakazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze wananchi wa Kata ya Balang'dalalu

katika Jimbo la Hanang na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri kuwasilisha kata hiyo kama ni kata ya kimkakati katika jimbo hilo ili tuanze kuifanyia mpango wa kupata fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa awamu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kulikuwa na mpango wa kujenga kituo cha afya kitakachohudumia kata tatu za Ndilimalitembo, Matogoro pamoja na *Seed Farm* katika Manispaa ya Songea. Je, ni lini kituo hicho cha afya muhimu sana kitajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Songea Mjini kwa kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ni eneo ambalo tuliainisha kata kadhaa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya ikiwemo kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatambua umuhimu wa kituo cha afya katika kata hiyo. Tunaendelea na taratibu za kibajeti ili tuweze kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kata za Nanjota, Mchauru na Mnavira zote zinastahili kuwa na vituo vya afya. Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya katika kata hizi ambazo zina uhitaji mkubwa sana wa huduma hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kata ambazo amezitaja Mheshimiwa Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, ni kata ambazo halmashauri ilishawasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, lakini pia Mheshimiwa Mbunge amewasilisha na kufuatilia mara kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Lulindi kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na vituo vya afya katika kata hizo na tunaendelea na taratibu.

Mheshimiwa naibu Spika, kama ambavyo tulishajenga hospitali ya halmashauri na vituo vya afya kadhaa na zahanati, tuko kwenye mpango na mpango huu ni endelevu. Tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya afya katika kata hizo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata. Swali la Mheshimiwa Salum Khamis Salum, Mbunge wa Meatu, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Thomas Kampala.

Na. 424

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya – Meatu**

**MHE. THOMAS K. MAGANGA K.n.y. MHE. SALUM K. SALUM** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Meatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa

Salum Khamis Salum, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya Meatu ilipandishwa hadhi kutoka kituo cha afya mwaka 1977. Baada ya kituo hiki kupandishwa hadhi, Serikali imeendelea kupeleka fedha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Meatu kwa lengo la kuongeza miundombinu ya hospitali hiyo ili iendane na mahitaji ya sasa. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilipeleka shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi, jengo la upasuaji, jengo la maabara na nyumba ya mtumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024, Serikali ilipeleka shilingi bilioni 1.15 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kutolea huduma mbalimbali za afya ambayo ujenzi wake umekamilika na yanatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuendelea kuongeza miundombinu mipya katika hospitali hiyo ambapo itajenga jengo la wazazi, kumalizia jengo la maabara, kujenga *walkway* na kujenga visima vya kukusanya maji ya mvua. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Meatu mpaka miundombinu yote muhimu kwenye hospitali hiyo itakapokamilika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Thomas Kampala, swali la nyongeza.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, hospitali inayotumika sasa ina upungufu mkubwa sana wa watumishi na vifaa tiba. Je, ni lini Serikali itatuletea watumishi na vifaa tiba ili kupunguza tatizo kubwa la wananchi wa Jimbo la Meatu wanalopata kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Naibu Spika, Serikali imeendelea kupeleka watumishi katika halmashauri kote nchini ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Meatu na katika siku 100 za kwanza za Serikali ya Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Halmashauri ya Meatu pia ilipokea watumishi wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi la ajira za watumishi wa sekta ya afya ni endelevu na kila kibali cha ajira kitakapopatikana tutahakikisha tunawapa kipaumbele kupeleka watumishi ili kupunguza pengo la watumishi katika halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, Serikali ilikwishapeleka vifaa tiba katika Halmashauri ya Meatu na tutaendelea kuhakikisha kila bajeti tunatenga fedha na kupeleka vifaa tiba, dawa na vitendanishi ili wananchi wa Halmashauri ya Meatu wapate huduma bora katika hospitali ya wilaya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mafupi. Mheshimiwa Profesa Pius Yanda, swali la nyongeza.

**MHE. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Jimbo la Buhigwe lina kata 20 na kati ya hizo kata 20 ni kata tisa tu ndizo ambazo zina vituo vya afya. Ni lini Serikali itaweza ku-*support* ujenzi wa vituo vya afya vya ziada kwenye hizi kata 11 ambazo hazijapata vituo vya afya ili wananchi waweze kupata huduma kwenye umbali wa jirani kama inawezekana?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tukumbushane tu, swali la nyongeza litokane na swali la msingi. Swali hili linaongelea ujenzi wa hospitali za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Profesa Yanda, Mbunge wa Buhigwe alikwishawasilisha baadhi ya kata za kimkakati kati ya kata zile 11 ambazo hazina vituo vya afya. Mimi nikuhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iliweka mpango wa kujenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati na sera yetu au mwongozo wetu siyo kila kata itakuwa na kituo cha afya kwa sababu ya vigezo vya idadi, umbali na vigezo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunatambua kwamba Jimbo la Buhigwe lina kata za kimkakati ambazo zina idadi kubwa ya wananchi na umbali mkubwa. Nikuhakikishie kwamba tutaziweka kipaumbele kwenye mipango yetu kuhakikisha kwamba kata hizo zinapata vituo vya afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Simiyu ina upungufu wa wodi za kulaza wagonjwa na kwa kuwa hospitali hii inahudumia wilaya zote tano za Mkoa wa Simiyu; je ni lini Serikali itaongeza wodi katika hospitali hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, Nyaumata ni moja ya hospitali mpya ambazo zimejengwa na Serikali ya Awamu ya Sita. Nikuhakikishe tu Mheshimiwa Mbunge Mama Chenge kwamba ujenzi wa miundombinu katika hospitali ile ya mkoa unaendelea chini ya Wizara ya Afya. Nikuhakikishie tu kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba miundombinu yote muhimu ikiwemo wodi zinajengwa ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Simiyu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali yetu ya Wilaya ya Karatu bado ina mapungufu mengi ikiwemo upungufu wa wodi za wagonjwa, ukosefu wa *fence,* lakini pia na ukosefu wa jiko kwa ajili ya huduma kwa wagonjwa. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuliahidiwa kwamba fedha zitaletwa kwa ajili ya kipaumbele cha kwanza ambacho ni ujenzi wa jiko kwa ajili ya huduma kwa wagonjwa. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za viongozi wetu wa kitaifa ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa mipango yetu. Tayari tumeshaanza uratibu wa kupata fedha kwa ajili ya kupeleka Halmashauri ya Karatu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jiko, lakini pia tutakwenda kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa wodi na *fence*. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Cecilia Paresso kwamba Serikali tayari inaendelea na uratibu wa suala hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Waziri, mlipokuja tarehe 17 Mei na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuliwaomba jengo la dharura kwa hospitali yetu ya Wilaya ya Chemba kutokana na adha kubwa tunayoipata kuhudumia watu wanaopata ajali kutokana na barabara yetu. Ni lini Serikali mtatuletea fedha ile ili tuweze kupata jengo hilo muhimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Chemba iko kwenye *main road* ya Arusha - Dodoma na ni sehemu ambayo inahitaji kuwa na jengo la matibabu ya dharura, kwa maana ya

*Emergency Medical Department*. Mheshimiwa Mbunge aliwasilisha mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na tumelichukua Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tunafanya uratibu ili tupate fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la *EMD* katika Halmashauri ya Chemba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 425

**Utekelezaji wa Mradi wa *FYDP IV***

**MHE. MGORE M. KIGERA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa *FYDP IV* kwa kujenga *Great Lake Industrial Hub* Musoma kama mradi wa kielelezo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Chaya, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uendelezaji wa viwanda na uongezaji thamani katika kuchochea maendeleo kupitia mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Hivyo, kupitia Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, yaani 2026/2027 hadi 2030/2031 yaani *FYDP IV,* Serikali imejipanga

kutekeleza programu saba za kielelezo ikiwemo Programu ya Kitovu cha Viwanda na Uchumi wa Buluu Kanda ya Ziwa *(Great Lakes Smart Industrial and Blue Economy Hub)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu hii itatekelezwa katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara na Kagera na inalenga kuunganisha uzalishaji viwandani, biashara, usafirishaji, shughuli za uchumi wa buluu katika ushoroba wa Kanda ya Ziwa ikiunganisha Tanzania na nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na DRC.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu hii inahusisha miradi shikizi *(anchor projects)* takribani tisa ikiwemo mradi wa reli ya *SGR,* ujenzi wa barabara mbalimbali, ujenzi na uboreshaji wa bandari na viwanja vya ndege, uendelezaji wa viwanda vya bidhaa za afya zinazotumia malighafi ya pamba na viwanda vya uzalishaji dawa, uendelezaji wa migodi mbalimbali ikiwemo Mgodi wa Dhahabu wa Kata ya Kiabakari – Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile programu hii inajumuisha uendelezaji wa minyororo ya thamani ya kimkakati *(strategic value chains)* katika maeneo ya uvuvi, uchimbaji na uchakataji madini, kilimo hususan pamba na kahawa, ufugaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo programu ya Kitovu cha Viwanda na Uchumi wa Buluu Kanda ya Ziwa inatarajiwa kutekelezwa sambamba na kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 hadi 2030/2031) ambao utaanza Julai, 2026 na hivyo Jimbo la Musoma Mjini litakuwa miongoni mwa wanufaika wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, swali la nyongeza.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza ninapenda niishukuru Serikali kwa majibu mazuri na kuonesha dhamira ya dhati ya kuamua kuja kuwakwamua

wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini hasa katika sekta nzima ya uchumi pamoja na ajira. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mpango wa *FYDP IV,* tumeona reli ya *SGR* ya kutoka Tanga – Arusha – Musoma ipo kwenye mpango huu. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha inaingia ubia na kufanya *PPP* kuhakikisha ujenzi wa reli hii unafanyika haraka iwezekanavyo kama ilivyo kwa reli ya Mtwara – *Mbamba Bay?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tunayo hoteli yetu ya *New Musoma Hotel,* hiyo imekuwa ndio *icon* ya Mkoa wa Mara na Jimbo la Musoma Mjini. Serikali haioni sasa ni muda muafaka *TRC* kurudi kuiinua hoteli hiyo ili kuweza kufungua fursa za ajira na kuvutia watalii ili uchumi wa Musoma Mjini uweze kuimarika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, kwa kuendelea kuwatetea watu wa Musoma Mjini na niwahakikishie watu wa Musoma Mjini sisi kama Serikali tutampa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika mpango wetu wa miaka mitano, tuna mpango wa kujenga reli ya kisasa *(SGR)* kutoka Tanga – Kilimanjaro – Arusha – Manyara – Singida – Simiyu – Musoma. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na ushauri wake kwamba kwa nini Serikali isione haja ya kutumia *PPP;* sisi tunapokea ushauri wake na sisi kama Serikali tutaufanyia kazi. Lengo la Serikali lakini vilevile Ilani ya Chama Cha Mapinduzi yam waka 2025/2030 imeelekeza kujenga reli ya *SGR*

kutoka Tanga – Musoma, lengo ni tuweze kufungua fursa za Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusu Hoteli ya Musoma. Ni kweli pale Musoma kuna eneo ambalo lilikuwa hoteli ya Serikali na ilikuwa inaitwa *Musoma Hotel* na hiyo hoteli ipo chini ya wenzetu wa *TRC* ikiwa sehemu mojawapo ya ujenzi wa hii *SGR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufungua fursa za uwekezaji Kanda ya Ziwa, hususan suala la utalii, sisi kama Serikali vilevile tuna kipaumbele cha kuhakikisha kwamba tunatafuta wawekezaji kwa ajili ya kujenga hii hoteli ya Musoma ili iweze kutumika. Tunapokuwa tunajenga ile *SGR* kutoka Tanga – Musoma, hii hoteli ya Musoma itatumika sana kwa ajili ya wale wanaosafiri, lakini vilevile kwa ajili ya watalii wanaoenda kule Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kafiti William Kafiti, swali la nyongeza.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela na mimi naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Ilemela ni moja ya wilaya za kimkakati katika Mkoa wa Mwanza, na moja ya wilaya inayochangia mapato makubwa katika Mkoa wa Mwanza, sasa ni lini Serikali itaandaa eneo maalum la uwekezaji katika Wilaya ya Ilemela? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Kafiti, Mbunge wa Ilemela, kwa kuuliza maswali, lakini vilevile kwa kuwatetea watu wa Ilemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali katika ile miradi saba ya kielelezo tuna mpango wa kuandaa eneo maalum la uwekezaji Mwanza na mojawapo ya eneo ambalo tumeliandaa ni eneo la Ilemela na tayari Ilemela wameshawasilisha andiko la kuruhusu lile eneo litumike kama *Special Economic Zone (SEZ)* na tayari tuko kwenye mpango wa kwenda kulipima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lile eneo vilevile linahitaji fidia na katika mpango wetu huu wa mwaka mmoja tumeweka fedha kwa ajili ya kuanza kulipa fidia wananchi ili waliache lile eneo kwa ajili ya kuwekeza viwanda. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inalifanyia kazi na tutahakikisha lile eneo tunaliendeleza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 426

**Huduma ya Mawasiliano ya Simu – Kata ya Kalalani**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua changamoto ya kukosekana kwa huduma ya mawasiliano ya simu kwenye Kata ya Kalalani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imefanya tathmini ya hali ya mawasiliano katika Kata ya Kalalani yenye Vijiji vya Mtoni Bombo na Kalalani. Kijiji cha Mtoni Bombo kimethibitika kuwa na changamoto za mawasiliano. Kwa upande wa Kijiji cha Kalalani, licha ya kuwa na minara miwili yenye watoa huduma watatu *(Yas, Vodacom* na *Airtel)* inayotumika kutoa huduma za mawasiliano ya simu, bado kuna changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya uhakika kutokana na ukubwa wa kijiji hicho chenye shughuli nyingi za kiuchumi ikiwemo uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utaijumuisha Kata ya Kalalani kwenye miradi ya mawasiliano ya simu ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo katika Kijiji cha Mtoni Bombo na Kijiji cha Kalalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano kwa kipindi cha mwaka 2025-2030 wenye lengo la kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yote nchini ifikapo mwaka 2030.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri yenye uhalisia, pamoja na majibu hayo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; eneo la Kijiji cha Kalalani ambalo lina changamoto ya mawasiliano ni eneo muhimu sana kwa uchumi kwa sababu ndiko kuna uchimbaji wa madini kwenye eneo la Kigwasi. Serikali haioni kwamba iko haja sasa ya kuwaelekeza kwa dharura watoa huduma hawa bila kuathiri mpango ilionao ili waimarishe minara ile iliyopo ili eneo lile lipate mawasiliano na biashara ya madini iendelee kufanyika vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; pamoja na Kata ya Kalalani, yapo baadhi ya maeneo kwenye Kata za Magila Gereza, maeneo kama ya Kiloza na maeneo ya Kwasunga, lakini pia maeneo machache ya Kata ya Mkomazi pamoja na Kata ya Mkalamo yana changamoto ya mawasiliano. Ni lini Serikali itatatua changamoto hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mnzava, amekuwa mstari wa mbele kufuatilia changamoto ya mawasiliano katika jimbo lake la Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza, ni kweli tumefanya tathmini pale, kuna changamoto ya mawasiliano kubwa na katika eneo hili la kata aliyoieleza kuna changamoto ya mawasiliano ukizingatia kwamba eneo hili lina uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, kumuelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kutuma wataalam katika kata hiyo kwenda kufanya tathmini ya kina ya changamoto hii ya mawasiliano na kuwaelekeza watoa huduma wenye minara katika kata hiyo kuiboresha, kuiongezea nguvu minara hiyo *(optimization)* ili kutatua changamoto ya mawasiliano kwa sasa wakati Serikali ikiendelea kuangalia uwezekano wa kujenga minara mingine kuiongezea nguvu hiyo minara iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la kata nyingine ambazo zina mawasiliano, pia wataalam wetu wamekwenda. Tumefanya tathmini na kubaini kwamba katika Kata ya Magila Gereza, pamoja na kwamba kuna mnara wa *Halotel* na *Yas,* bado kuna changamoto ya mawasiliano. Kata ya Mkalamo kuna mnara wa *Yas* na *TTCL,* lakini nayo ina changamoto ya mawasiliano, na Kata ya Mkomazi pamoja na kwamba kuna minara ya *Vodacom, Airtel, Yas, Halotel* na *TTCL,* bado pia kuna changamoto ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaendelea kumuelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kutuma wataalam kufanya tathmini. Pia Mheshimiwa Mnzava katika mradi wa Awamu ya 11 tunaoutekeleza kwa mwaka ujao wa fedha, kata hii pia itajengewa minara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe pia Waheshimiwa Wabunge, najua tatizo hili la minara kupungukiwa nguvu kutokana na watumiaji kuongezeka lipo katika maeneo mengi ya Wabunge. Kwa hiyo, tunaomba Wabunge wote wenye changamoto katika maeneo yao tupate hizo taarifa Wizarani ili wataalam wetu waweze kuzifanyia kazi na kutatua changamoto hizi zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Kata ya Kalalani iliyotajwa ipo jirani kabisa na Kata ya Mng'aro ambayo iko Wilaya ya Lushoto. Vijiji vya Kikumbi, Kishumai pamoja na Ngwalu vina matatizo hayo ya mawasiliano, lakini vipo karibu sana na mpakani mwa nchi jirani ya Kenya. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuhakikisha kwamba maeneo yale mawasiliano yanakuwa thabiti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri eneo hili pia ninamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kupita eneo hili pia kufanya tathmini kwa sababu liko karibu sana na Halmashauri ya Korogwe. Wakati wanafanya eneo la Korogwe Vijijini, wafanye pia eneo hili waangalie changamoto iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninamhakikishia kwamba kwenye awamu hii, kwenye mkakati wetu wa Wizara wa Serikali wa miaka mitano ijayo kufikia mwaka 2030, tuna uhakika

kwamba nchi hii yote tutakuwa tumeifikia na changamoto ya mawasiliano tutakuwa tumeitatua kwa kiasi kikubwa kama siyo kuimaliza kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na ninamshukuru sa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Ninamshukuru kipekee Mheshimiwa Timotheo Mnzava kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia sana mawasiliano katika Kata ya Kalalani na nyinginezo ikiwemo Mkomazi, lakini pia Mheshimiwa Shangazi na Waheshimiwa Wabunge wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba maeneo ya hifadhi ni maeneo ya kipaumbele katika Awamu yetu ya 11, lakini maeneo yote yanayopitiwa na *SGR*, *TAZARA* na vilevile maeneo mengine ambayo yapo katika barabara kuu na yenyewe pia ni maeneo ambayo tunayafanyia kazi kwa haraka kuhakikisha mawasiliano yanakuwa thabiti na hakuna mawasiliano yanayokatikakatika. Tayari tuna zaidi ya miradi minne ambayo tunaelekea kuitekeleza, tumeshamaliza mmoja wa minara 758. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika mradi huo, Mkoa wa Tanga uliweza kupata minara zaidi ya 43 na tutaendelea kuwaongezea minara hiyo, lakini tunao mradi wa minara 632 na wenyewe tunakusudia kuumaliza ifikapo Machi, 2027. Tunao mradi wa minara 201 ambao na wenyewe pia utakamilika mwaka 2027 ambapo Tanga watapata takribani minara nane, na tumekusudia kuweka shilingi bilioni 19.7 kwa ajili ya kunufaisha Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawahakikishia Wana-Tanga wote kwamba kwa kuwa tunatambua Tanga iko maeneo ya mpakani, lakini pia wana shughuli nyingi sana za madini ikiwemo madini ya *graphite* pamoja na mengineyo. Ni eneo ambalo

tunalipa kipaumbele na msukumo mkubwa na tutahakikisha kwamba mnapata mawasiliano ya dhati. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Utamadani, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Moses Lodovico Kaegele, Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 427

**Ujenzi wa Shule za Michezo – Nkasi Kusini**

**MHE. MOSES L. KAEGELE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule za michezo kwa kila jimbo hasa katika Jimbo la Nkasi Kusini ili kuibua vipaji vya wanasoka nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kujenga shule 56 za michezo katika mikoa yote nchini ambapo baada ya kukamilika kwa shule hizo, kila mkoa unatarajiwa kuwa na shule za michezo angalau mbili. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali imeanza na shule saba za michezo katika Mikoa ya Singida, Tanga, Ruvuma, Pwani, Dodoma, Kagera na Mtwara ambapo zabuni ya utekelezaji wa mradi huo tayari imetangazwa ili kupata mkandarasi wa mradi husika. Kukamilika kwa shule hizo kutasaidia kuibua na kukuza vipaji vya wanafunzi katika michezo mbalimbali huku wakipata fursa ya kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa katika awamu zinazofuata za

utekelezaji wa mradi huu, Mkoa wa Rukwa utafikiwa na unatarajiwa kunufaika kwa kuwa na shule mbili za michezo ambazo zitasaidia kuibua vipaji vya michezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mchezo wa soka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moses Ludovico Kaegele, swali la nyongeza.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri na yenye matumaini kwa wanasoka, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Jimbo la Nkasi Kusini ni miongoni mwa majimbo yanayopatikana pembezoni mwa nchi hii na jimbo hili lina maeneo ya kutosha sana katika baadhi ya shule za sekondari kujenga miundombinu ya michezo; na kwa kuwa Serikali imejiandaa kwamba baadaye itapeleka shule mbili kujengwa katika Mkoa wa Rukwa.

Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka katika kipindi hicho kwenda kujenga shule moja ndani ya Jimbo la Nkasi Kusini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza; kwa kuwa shule hizi zitahitaji kuwa na wataalam na hasa walimu wa kufundisha mchezo wa mpira, lakini pia riadha pamoja na *netball*. Ni upi mpango mkakati wa Serikali wa kuzalisha walimu hawa ili basi shule hizi zitakapojengwa wawe tayari kwenda kuibua vipaji vya vijana wetu ndani ya nchi yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, kwanza ninachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kaegele kwa kuwapambania Wana-Nkasi kwa nguvu nyingi. Mimi na yeye tumeshakuwa na mijadala kadhaa na huu wa kituo cha michezo na elimu kwenda Nkasi, tumelijadili mara kadhaa. Sasa kama ambavyo nilijibu wakati ninajibu swali la msingi, kwanza kwa bahati nzuri, Mkoa wa Rukwa haujafikiwa, zamu yake haijafika kwenye hii awamu ya

kwanza ya utekelezaji wa mradi huu. Tunayo mikoa saba, lakini Mkoa wa Rukwa zamu yake haijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na jambo la pili ni kwamba mapendekezo ya vituo hivi vya michezo na elimu tukavijenge wapi, huwa yanatoka mkoani. Kwa hiyo, ipo nafasi ya Mheshimiwa Kaegele kujadiliana na wenzetu wa mkoani ili kuweka msingi wa hoja yake ambayo ni nzito kusema ukweli, kuhakikisha kwamba kituo hiki kinapelekwa Nkasi ili watoto wa Nkasi waweze kupata nafasi ya kuonesha vipaji vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili kuhusiana na walimu wa michezo ambao watakwenda kufundisha kwenye vituo hivi, Serikali kupitia Kituo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya, inaendelea kutoa elimu ya michezo kwa walimu kwa ngazi ya astashahada na stashahada kwenye michezo yote, lakini halikadhalika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinaendelea kufundisha walimu wa michezo yaani fani hiyo hiyo kwenye ngazi ya shahada na shahada ya umahiri, na wataalam hao tutakapomaliza ujenzi wa shule hizi 56, watasambazwa ili kwenda kutoa elimu kwenye vituo hivi ambavyo Serikali imevijenga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa michezo ni ajira, michezo ni afya na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi sana katika Bunge lako wamekuwa wakianzisha mashindano ya michezo mbalimbali katika majimbo, wilaya na mikoa.

Je, Serikali iko tayari sasa kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge hao ili tuweze kuibua vipaji na kuhakikisha kwamba kila halmashauri inakuwa na viwanja bora vya michezo yote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, kwa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kweli Serikali inawaunga mkono taasisi zote binafsi ambazo zimekuwa zikionesha nia ya kuendeleza michezo katika maeneo mbalimbali wakiwamo Waheshimiwa Wabunge. Hatujawa na bajeti ya kuhakikisha tunawapa Waheshimiwa Wabunge ili kusaidia kutengeneza michezo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia huko tunakoelekea tutaendelea kuangalia utaratibu wa namna ya kuwaunga mkono na kuhakikisha kwamba vipaji katika majimbo ya Waheshimiwa Wabunge wote, vinaendelea kupatikana, lakini halikadhalika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaisema hapa ya kwamba tumetoa rai kwa halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya utengenezaji wa miundombinu ya michezo kwenye halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapomaliza ujenzi wa miundombinu ya *AFCON* ambapo Serikali imeweka nguvu zote sasa hivi, tutaona namna ya kuziunga mkono halmashauri hizi hasa ambazo zitakuwa zimeanza kujenga miundombinu ya michezo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi. Kwa kuwa mchezo wa riadha ni moja ya mchezo muhimu sana na imeletea Taifa letu medali mbalimbali, na chimbuko kubwa la wachezaji hawa ni hasa kutoka Mkoa wa Manyara na hasa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.

Je, Serikali haioni haja ya kujenga miundombinu ya michezo hiyo katika maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, Serikali inaona haja ya kujenga miundombinu ya mchezo wa riadha katika Mkoa wa Manyara na tunao mpango huo huko katika hatua za usoni za utekelezaji. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tunafahamu kwamba wanariadha wengi wanatokea ukanda huo na Serikali iko na Mkoa wa Manyara pamoja kuhakikisha ya kwamba tunavigundua, tunavitunza na kuviendeleza vipaji vya riadha kutoka Mkoa wa Manyara.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan, Mbunge wa Bumbwini, sasa aulize swali lake.

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sasa niko tayari kupokea majibu swali langu namba 48.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ni swali namba 428

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kupokea majibu ya swali namba 428.

Na. 428

**Kufungwa kwa Ofisi Ndogo za Ubalozi Zanzibar**

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN** aliuliza: -

Je, kwa nini Ofisi Ndogo za Ubalozi wa Marekani, Uingereza na Italia zilizokuwa Zanzibar zilifungwa?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaomba kwa ruhusa yako nimjibu Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan, Mbunge wa Jimbo la Bubwini, Zanzibar, swali lake namba 428 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa nchi za Marekani na Uingereza ziliwahi kuwa na Ofisi Ndogo za Ubalozi upande wa Zanzibar. Hata hivyo, ofisi hizo zilifungwa kwa sababu za mabadiliko ya kisera katika uendeshaji wa Ofisi Ndogo za Balozi za nchi zao wenyewe huko ulimwenguni. Siyo Tanzania tu pekee iliyoathirika, bali nchi nyingi ziliathirika. Kwa sasa majukumu ya ofisi hizo yanaendelea kutekelezwa kupitia Balozi zao zilizopo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa nchi ya Italia bado ina Ofisi Ndogo ya Ubalozi Zanzibar iliyopo eneo la Kiembesamaki, barabara ya kwenda uwanja wa ndege. Mwakilishi wake *Consul* hiyo anaitwa Bwana Stefano Totisco. Aidha, hivi karibuni nchi ya Italia imeiomba Wizara ya Mambo ya Nje rasmi nia ya kupandisha hadhi ya Ofisi hiyo kutoka *Vice-Consulate* (Konsuli Mdogo) kuwa *Consulate General* yaani Konseli Mkuu yenye mwakilishi wa hadhi ya juu zaidi wa Serikali ya Italia nchini Tanzania kupitia uwakilishi wake uliopo Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwana Stefano Totisco, tayari ameshathibitishwa na Wizara yangu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuwa Konseli Mkuu ambapo sasa ataweza kushughulikia masuala ya wananchi wa Italia wenye makazi yao huko Zanzibar ama biashara zao, lakini pia kwa sekta ya utalii zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ataweza kushughulikia masuala ya kikonseli ya Watanzania wenye muingiliano wa usafiri na biashara na Italia. Huduma nyingi zaidi za uwakilishi wa Italia zitaweza kutolewa na Ofisi hiyo iliyopo Zanzibar kuliko hapo awali

kabla ya kupandishwa hadhi yake na hii ni taarifa njema na ya faraja kwa Zanzibar hasa kwa sekta ya utalii ambayo bado nchi ya Italia inaongoza kwa idadi ya wageni kwenda Zanzibar. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan, swali la nyongeza.

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutambua umuhimu wa kuwa na Balozi Ndogo Zanzibar, lakini pamoja na hiyo, kakiri kwamba kwa Balozi za Marekani na Uingereza kwa sasa hazipo na mazungumzo yanaendelea. Ninataka kujua, je, mazungumzo haya yataisha lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ofisi ya Italia mmekiri kwamba ipo, Wizara yake ina mkakati gani kutangaza ili wananchi wa Zanzibar kujua na kwenda kupata huduma bora zinazoweza kutolewa hapo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba alirudie swali la pili sijaweza kulisikia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge rudia swali la pili hajasikia vizuri, swali la nyongeza la pili.

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kakiri kwamba Ofisi Ndogo ya Ubalozi wa Italia ipo Zanzibar, lakini je, Wizara yake ina mkakati gani kuweza kutoa matangazo ili wananchi wajue huduma hiyo ipo na ipo ofisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye diplomasia,

mazungumzo huwa yanaendelea hadi pale Taifa moja linapoamua kukubali ama ombi, ama maombi ya Taifa lingine. Kwa hiyo, mazungumzo yetu na Serikali za Uingereza pamoja na Marekani yanaendelea. Bahati nzuri sana, juzi yule Mwakilishi wa Heshima wa Serikali ya Uingereza amestaafu, anaitwa Bwana *Captain* Carl Salisbury na katika hafla yake ya kuagwa nilibahatika kushirika akiwa amekwenda kuagwa na Balozi wa Uingereza baada ya kutumikia miaka 30 nafasi hiyo Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameshathibitishwa mwakilishi wa heshima mwingine ambaye anaitwa Bi. Julia Bishop, umaarufu wake hodihodi wa pale Zanzibar. Kwa hiyo, Uingereza ina uwakilishi wake kupitia Bi. Julia Bishop na ofisi ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Marekani, bado hawana, lakini mazungumzo yetu yanaendelea, siwezi kusema kwamba yataisha lini isipokuwa yanaendelea vizuri mazungumzo kati yetu sisi na wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upande wa Italy kutoa matangazo, nami ninaomba kukiri kwamba tunatakiwa tuongeze nguvu zaidi ya kutoa matangazo. Ile ofisi inajulikana, ipo Barabara ya Kiembesamaki, kuna bendera pale ya Italy, lakini siyo kila Mzanzibari au kila Mtanzania atajua hii ni bendera ya Italy. Tutawaambia kwa kuanzia wao wenyewe Ubalozi waweke bango kubwa pale la tangazo la kusema hapa ndiyo Konseli Mkuu wa nchi ya Italia Mjini Zanzibar, lakini na sisi kupitia Idara yetu ya kutoa Mawasiliano ya Serikali katika Wizara ya Mambo ya Nje, tutahakikisha tunaongezea hilo. Ninamshukuru sana kwa wazo hilo zuri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Lucy Simirya Kombani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na 429

**Mazingira Bora kwa Watoto Kwenye Vituo vya Kulelea Watoto**

**MHE. LUCY D. S. KOMBANI** aliuliza: -

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha watoto wanaoishi kwenye vituo vya kulelea watoto wanaishi kwenye mazingira bora na kwa usalama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, makao ya watoto yote nchini yanaanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Sura ya 13, Kanuni za Makao ya Watoto za mwaka 2012 na Mwongozo wa Taifa wa Uanzishaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Makao ya Watoto wa mwaka 2024 ambapo utaratibu wa maombi ya usajili unaanzia ngazi ya kata, halmashauri na kuletwa Wizarani kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kupata leseni ya usajili pindi makao yanapokuwa yamekidhi vigezo vilivyowekwa vya usajili. Aidha, Maafisa Ustawi wa Jamii kuanzia ngazi ya Wizara, Mikoa na Halmashauri, wanafanya ufuatiliaji na usimamizi wa mara kwa mara katika makao ya watoto ili kuhakikisha huduma bora za malezi zinazotolewa kwa watoto na kuhakikisha ulinzi na usalama kwa watoto unazingatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY D. S. KOMBANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Wizara, ninauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vituo hivi kuna muda vimekuwa vikipata changamoto katika kuwapatia mahitaji watoto hawa na hivyo kulazimika kuomba msaada kwa wananchi. Je, Serikali haioni haja sasa ya kutenga hata asilimia mbili kutoka kwenye mapato ya halmashauri zetu ili kuwasaidia hawa watoto katika kuboresha mazingira yao hasa kwenye afya, elimu na hata wakati mwingine kwenye huduma za chakula bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa hawa watoto wamekuwa wakipelekwa kwenye vituo hivi wakiwa na umri mdogo sana, umri ambao mtoto anahitaji kujengwa hasa kisaikolojia. Je, Serikali ina utaratibu upi wa kuhakikisha kwamba watumishi wa kwenye vituo hivi wana ujuzi na mafunzo sahihi kwa ajili ya makuzi na malezi ya watoto hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, awali ya yote ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Lucy Kombani, amekuwa mdau mzuri sana wa maendeleo ya jamii na yeye ni *professional* bibi maendeleo ndiyo maana anafanya vizuri katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutenga asilimia mbili angalau kuona kwamba zinaboresha vituo hivi, kwanza ninapenda kutoa taarifa, vituo hivi vya watu binafsi pekee viko 424 na vituo vya Serikali viko viwili, kituo kilichopo hapa Dodoma, Kikombo pamoja na Dar es Salaam pale Kurasini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika vituo hivi 424, tukisema tuendelee kuwezesha, huenda tukasababisha utitiri wa vituo kwa sababu watu wanaweza wakaona pia ni moja ya sehemu ya kujipatia kipato, lakini vilevile tayari Serikali iliweka alama ilishatoa maelekezo asilimia tatu itengwe kwa ajili ya afua za ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na ufinyu wa bajeti katika halmashauri zetu halikutekelezwa kikamilifu na pia hatukuweka mkazo sana kuona kwamba hizi fedha zinatengwa ili kusaidia hivi vituo kwa sababu sisi kama Serikali mlengo wetu mkubwa ni kusisitiza malezi sahihi ngazi ya familia. Kama hawa watoto imetokea kwa sababu ya mvurugano wa baba na mama, basi familia kwa maana ya mjomba na shangazi ama baba mdogo wa-*take charge* ili waweze kuona kwamba hawa watoto badala ya kwenda kulelewa kwenye vituo hivi vya watoto basi walelewe kwenye ngazi ya kifamilia ili waweze ku-*adapts traditions*, mila, desturi za koo kwa sababu kila wanapokwenda kulelewa wanalelewa kimchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tunaendelea kutoa wito, wazazi wasiwe na moyo mgumu hasa akina baba hawa ndio mara nyingi unakuta wanamwachia huyu mama analea mtoto peke yake, anasubiria mtoto ameshakuwa mkubwa anasema sasa ana uwezo wa kuchukuliwa na baba. Wakati malezi yanatakiwa kuanza tokea huyu mtoto yupo tumboni baba awajibike, mtoto anazaliwa baba awajibike hata kama huwezi kurudiana na huyo mama basi akina baba wawajibike ili kutupunguzia hili wimbi la watoto wa mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anasema Serikali ina utaratibu upi katika kuona kwamba wale Maafisa Ustawi wetu wanawapatia mafunzo ya mara kwa mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kusema tu kwamba kwanza katika halmashauri zetu zote 184 kuna Maafisa Ustawi wa Jamii, maafisa ambao wamepewa elimu ya *Case Management System* kwa maana ya Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri ya Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wanafanya *supervision* ya karibu pamoja na hivi vituo vya watu binafsi na mimi mwenyewe nimeshiriki kufanya ziara kuona kwa namna gani Maafisa Ustawi wetu wanashiriki kutoa mafunzo sahihi kwa wale watoto wote ambao wapo kwenye vituo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile usimamizi wa kuhakikisha haki ya mtoto kupata elimu, haki ya mtoto kupata afya wameweza kupewa hata bima za afya zile za watoto, lakini vilevile wanaendelea kupewa mafunzo ya mara kwa mara na kusimamia mara kwa mara, kwa sababu ushirikiano kati ya sekta binafsi kwa maana hivi vituo binafsi 424 ni ya karibu sana na Wizara yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Santiel Kirumba, swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 430

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji Pachasita – Kihungu**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji Pachasita katika Kata ya Kihungu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka lengo la kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa miradi yote ya maji inayoendelea kote nchini; mijini na vijijini. Mradi wa Maji wa Pachasita uliopo Wilaya Mbinga Mkoani Ruvuma unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita

150,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 21 sanjari na ujenzi wa vituo 12 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 90% ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026 na kunufaisha wananchi wapatao 2,874 waishio katika Vijiji viwili vya Pachasita na Lipembe Wilayani Mbinga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa kuendelea kutekeleza huu Mradi wa Pachasita na kuahidi kwamba mradi huu utakuwa umekamilika ifikapo Juni 30, 2026. Nina maswali ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Mji wa Mbinga unapata maji kutoka katika Kijiji cha Tukuzi na kuna kipindi Mheshimiwa Aweso, Waziri na Maji alitembelea katika kijiji hicho na aliahidi kuwajengea mradi wa maji kwa sababu kijiji hicho hakina maji. Sasa swali langu; je, ni lini Serikali itaanza kujenga mradi huo katika Kijiji cha Tukuzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kijiji cha Kagugu, Kata ya Kagugu kina changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama; lini Serikali itaanza kujenga mradi wa maji katika Kijiji cha Kagugu ili wananchi hao waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Mbunda kwa kazi kubwa anayoifanya na sasa upatikanaji wa maji katika Jimbo lake ni 78%. Sambamba na hivyo katika kata zote za Mheshimiwa Mbunda kila kata ina maji angalau kwa kijiji kimojawapo, tunatambua na Serikali inatambua

bado kuna vijiji ambavyo bado vinahitaji kupata huduma ya maji safi na salama kikiwepo Kijiji cha Tukuzi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika programu ya vijiji 1,575 Mheshimiwa Mbunge tumemwekea vijiji vitatu, kijiji cha kwanza ni hiki ambacho Mheshimiwa Mbunge amekiongelea cha Tukuzi, lakini pia kuna Kijiji cha Kikolo, lakini sambamba hiyo kuna Kijiji cha Mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu katika kijiji hiki cha pili alichokitaja nikiri kabisa kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2026/2027 kijiji hicho hakipo katika mpango wa utekelezaji, lakini tunaamini kwamba katika awamu ya pili ya fedha mwaka 2027/2028 kijiji hicho tutakizingatia kuhakikisha kwamba kinapata huduma ya maji safi na salama. Tunatambua vipo vijiji vingi, lakini tutaenda awamu kwa awamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtakaopata nafasi nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kwamba kuna miradi imesimama ya zaidi ya shilingi bilioni nane kwenye Jimbo la Bunda Mjini, kazi haziendelei, wakandarasi hawajalipwa. Kuna changamoto imejitokeza na ni kero *very serious* ya kukatika kwa maji kwenye Jimbo la Bunda Mjini tatizo ni nini? Ni hujuma wananchi wangu wanakaa zaidi ya wiki tatu, wiki mbili maji hakuna, shida ni nini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana dada yangu tulishafanya ziara katika jimbo lake na tukajionea miradi inayoendelea. Ni kweli kabisa kwamba kuna uwekezaji mkubwa sana wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na alituelekeza kupeleka shilingi bilioni nane ambapo miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala hili la maji kukatikakatika katika Mji wa Bunda, nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, hakuna hujuma yoyote kutoka kwa wananchi na hakuna hujuma yoyote kutoka kwa wataalam wetu, isipokuwa tulikuwa na changamoto ya bomba ambalo liliwekwa mwaka 2019 ambalo ni bomba la *GRP* kasi na *pressure* ya maji ambayo yamepatikana yanayafanya haya mabomba yaweze kukosa ustahimilivu na matokeo yake yanapasuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi iliyofanyika ni kuhakikisha kwamba tunaenda kubadilisha mabomba. Tumeshaanza kuweka *steel pipe* maana yake mabomba ya chuma ili yaweze kwenda kuendana na *pressure* ambayo imetengenezwa. Tayari kwa sasa tumeanza sasa kuhamisha mtandao uliokuwepo kwenye *GRP* tunapeleka kwenye *steel pipe* ili kuhakikisha sasa kwamba kusiwepo na changamoto yoyote ya maji kupotea ama mabomba kupasuka kwa sababu ya kukosa nguvu ya kustahimili ile *pressure,* ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika mkoa wangu wa Singida upatikanaji wa maji safi na salama bado ni changamoto. Ningependa kupata *commitment* ya Serikali, ni lini Serikali

itakamilisha Miradi ya Miji 28 ya Singida, Manyoni na Kiomboi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana dada yangu kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kuendelea kuwasemea Wana-Singida na nikiri kwamba leo siyo mara ya kwanza kusimama amesema kama sikosei ni mara ya tatu kuongelea suala hili na upande wa Miji 28 ambapo tuna mradi huu wa Miji 28 upande wa Singida, Manyoni pamoja na Kiomboi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi unaendelea vizuri isipokuwa kwa upande wa Singida tulipata changamoto ya namna ambavyo visima vilivyokuwa vinachimbwa baadaye vinapata matatizo na baadaye ule udongo unarudi ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tumeshapata wataalam na wakandarasi ambao wanaweza kuutekeleza mradi huu bila kuwa na changamoto yoyote. Namtoa hofu kuwa Manyoni, Singida pamoja na Kiomboi miradi hii tutahakikisha kwamba tunaipa kipaumbele na tunaisimamia kwa ukaribu, lakini kwa ubora unaotakiwa ili wananchi wa Singida wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ado Shaibu, swali la nyongeza.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Tunduru hasa Mji wa Tunduru pale Mjini tunao mradi mkubwa sana wa maji ambao gharama zake ni shilingi bilioni 3.4. Mradi ule mkataba wake umekwishasainiwa, lakini unashindwa kuendelea kwa sababu kuna malipo ya awali kwa ajili ya mkataba shilingi milioni 500 ambayo yamekwama kwa muda mrefu.

Swali langu ni kutaka kufahamu ni lini mkandarasi yule atalipwa fedha zake ili kuleta neema kwa Wana-Tunduru ya kupata maji ya uhakika? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ado, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Ado kwa kufuatilia falsafa ya kumtua mama ndoo kichwani ambayo iliasisiwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na hii inadhihirisha kabisa kwamba maendeleo hayana chama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba tunao mradi mkubwa ambao ni uwekezaji mkubwa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Jimbo la Mheshimiwa Shaibu na wananchi ambao wamemchagua Mheshimiwa Ado wanatarajia mradi huu ukamilike ili uweze kutoa ile adha ya ukosefu wa maji. Nakuhakikisha Mheshimiwa Mbunge tunaenda kulisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kipaumbele chetu cha Wizara ya Maji ni kuhakikisha miradi ambayo inaendelea na ile ambayo tayari wakandarasi wameshapatikana kwa kufuata utaratibu rasmi tunawalipa ili waweze; lakini kwa hiyo, shilingi milioni 500 nimtoe hofu, tutamwita mkandarasi na nitamshirikisha Mheshimiwa Mbunge awepo katika kikao hicho tuone namna bora ya kwenda kuanza mradi huu ili wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Ado waweze kuona sauti ya Mbunge wao ikiwa na matokeo halisi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni muda mrefu sasa Serikali iliahidi kupeleka maji katika Shule ya Sekondari Tingirima, Shule ya Sekondari Machimolo, Shule ya Sekondari Mikomarilo, Shule ya Sekondari

Nyamang'uta mpaka leo shule hizo hazijapata maji; lini maji yataenda kwenye shule hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuelekeza tushirikiane na wenzetu Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunabainisha mahitaji katika maeneo ya shule, maeneo ya zahanati pamoja na vituo vya afya. Ili twende tukatumie sasa mitambo ambayo Mheshimiwa Rais amenunua mitambo 25 ili kuhakikisha kwamba shule, zahanati na vituo vya afya visiweze kukosa maji ambayo ndiyo msingi wa usafi na ambao ndiyo unaweza ukasababisha sasa magonjwa yasiwe yanaibuka mara kwa mara. Mpango huu utakapokamilika tutamshirikisha Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya utekelezaji, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, Mbunge wa Chato Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 431

**Kurejesha Safari za Ndege Chato**

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itarejesha safari za ndege katika kiwanja cha ndege Chato?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, Mbunge wa Chato Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ndege ya *ATCL* inaendelea kupanua mtandao wa safari kwa kuzingatia upatikanaji wa ndege na mahitaji ya soko. Kwa sasa *ATCL* inahudumia vituo 32 vikiwemo vituo 15 vya ndani ya nchi huku ikikabiliwa na upungufu wa ndege za masafa mafupi na hivyo kushindwa kupanua mtandao zaidi kwa vituo vya ndani kikiwemo kituo cha Geita. Serikali inaendelea na mchakato wa ununuzi wa ndege mbili za masafa mafupi zinazotarajia kuwasili mwaka wa fedha 2026/2027. Pindi ndege hizo za masafa mafupi zitakapopatikana, *ATCL* itaanzisha safari katika kiwanja cha ndege Chato.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cornel Magembe, swali la nyongeza.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwanza kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Naibu Waziri yanazungumzia kiujumla jumla, lakini hayajasema *specific time* kwamba ni lini ndege sasa Chato zinaanza kutua?

Kwa hiyo, ningependa kujua je, ni lini muda maalumu watu wa Chato wajiandae kuanza kukata tiketi kwa ajili ya kuanza kusafiri ili tupate kujua ni siku gani ndege hizi zinaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Uwanja wa Ndege wa Chato kama ni sawa na viwanja vingine, lakini mpaka sasa hivi hakujawekwa taa. Kwa hiyo, ndege haziwezi kutua pale usiku na wala haziwezi kuruka usiku, je, Serikali ina mpango gani pia

pamoja na kuleta ndege kuanza kutua pale, kuweka taa katika huu Uwanja wa Ndege wa Chato? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Magembe kama ambavyo ameeleza umuhimu wa huu uwanja wetu wa Chato, uwanja mkubwa ambao Serikali imetumia mabilioni ya fedha kuutengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunajiandaa kununua ndege zingine tayari kilio cha Wana-Chato kimefika mezani kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ameidhinisha sasa ndege zianze kuruka. Ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Magembe kwamba Serikali imepanga kuanza rasmi safari za ndege *ATCL* Mkoani Geita kwenye Uwanja wa Chato tarehe 2 Juni, 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tumeingiza kwenye mtandao tayari abiria wamejitokeza kwa wingi kuanza kupata tiketi na karibu tiketi 77 zimekwishakatwa mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa swali hili litaulizwa na Wabunge wengine, naomba uridhie nitumie nafasi hii kueleza na maeneo mengine machache ambayo Serikali inaanza ratiba mpya za ndege hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha pili ni cha Wana-Sumbawanga ambapo ndege zitakuwa siku ya Jumatano na Jumapili na wategemee ndege kuanzia tarehe 10 Juni, 2026. Kituo cha tatu ni safari za Mwanza na Dodoma. Nimesema kituo cha tatu itakuwa ni safari za Mwanza na Dodoma ambapo Serikali itapeleka ndege siku ya Ijumaa na Jumapili kuanzia tarehe 5 Juni, 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha nne ni safari za Kilimanjaro kwenda Mwanza ambazo zitapangwa Jumatano na Jumamosi kuanzia tarehe 3 Juni, 2026. Pia Mheshimiwa Profesa

Mbarawa amenituma niwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inakwenda kuongeza ndege kwenye kituo kati ya Mbeya na Dar es Salaam ambapo awali ilikuwepo jioni na sasa zitakuwepo kila siku asubuhi kuanzia tarehe 1 Juni, 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi kwa kuhitimisha, safari za Arusha na Zanzibar nazo Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa kutambua umuhimu wa utalii imeongeza ndege kila siku asubuhi kwa Jumatatu, Alhamisi na Jumamosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kabla sijahitimisha kuleta maelezo haya ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ambaye mimi nimetumwa tu na Mheshimiwa Profesa Mbarawa tutaendelea katika mwaka wa fedha huo kufanya majaribio kwa ajili ya Musoma na Shinyanga ambako viwanja vimekamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chiku Issa, swali la nyongeza.

**MHE. CHIKU A. ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mkoa wa Arusha ni lango kuu la utalii nchini, je, Serikali haioni kuna umuhimu sasa wa kuanzisha pia safari za kutoka Makao Makuu Dodoma kwenda Arusha na *KIA* tukielekea *AFCON?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Chiku kwa ushauri wake mzuri wa kuwapigania Wana-Arusha. Kwa sasa ninaomba Mheshimiwa Chiku akubali tuanze kwanza na ile ambayo tumesema ya Zanzibar na ile ambayo tumeanza ya kwenda Kilimanjaro – Mwanza, halafu Serikali iendelee kufanyia kazi ushauri wake mzuri ili kuweza kutazama kutoka Arusha kuja mpaka hapa Dodoma.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 432

**Ujenzi wa Meli ya Mizigo na Abiria Tanzania – Comoro**

**MHE. ASHA S. MOTTO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza mpango wa kujenga meli kubwa ya mizigo na abiria kati ya Mtwara na Moroni (Comoro)?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania inaendelea na upembuzi yakinifu kutambua kiwango cha soko na aina ya meli itakayojengewa, kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri katika mwambao wa Bahari ya Hindi kwa masafa mafupi, ikiwemo kuhudumia soko la Tanga, Dar es Salaam, Zanzibar, Mtwara na Visiwa vya Mayote, Moroni na Comoro. Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa ya uwekezaji kwa njia ya ubia au binafsi, kujenga meli ya mizigo na abiria na kuhudumia soko la nchi za mwambao wa Bahari ya Hindi kwa kuwa soko hilo ni la uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Salum Motto, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa majibu mazuri ya kutia moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, soko la bidhaa kati ya Tanzania na Moroni au Mayote ni la uhakika hususan kwa bidhaa za chakula na nyama. Sisi ndiyo wanaotutegemea sana ku-*supply* nyama na mazao tofauti tofauti ya chakula ambayo yanapatikana hapa

Tanzania. Mpango wa Serikali ni kujenga meli kubwa ya mizigo, pamoja na mwalo katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Mkoa wa Mtwara kuelekea Comoro, Moroni, una takribani *miles* 7,000 maana yake ni karibu sana. Sasa ni lini Serikali itatenga bajeti ya kujenga meli hii kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Tanzania kuelekea Comoro kwa ajili ya hizo bidhaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, ni kwa kiasi gani sasa sekta binafsi imeshirikishwa katika kupata fursa za uwekezaji kwenye sekta hii ya usafirishaji, hasa ya majini kati ya Tanzania na Comoro? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Asha Motto kwa jinsi anavyofuatilia usafiri katika mwambao wa Bahari ya Hindi, fursa ambayo Mwenyezi Mungu amewawekezea Watanzania. Swali lake la kwanza, anataka kufahamu kuhusu bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu mkubwa wa biashara iliyopo kwenye ukanda huu wa bahari, Serikali ilianza usanifu, ili kufahamu mahitaji halisi na kiwango cha mzigo uliopo, sambamba na biashara nzima ambapo mwaka wa fedha uliopita tumekamilisha. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali imeidhinishiwa kwa kuanzia shilingi bilioni 10, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa meli katika mwambao wa Bahari ya Hindi ambayo tunategemea itafanya biashara kati ya Mtwara – Tanga na visiwa vingine vilivyo jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ameuliza ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuhakikisha kwamba eneo hili wengi wanalichangamkia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakubaliana naye kwa sababu kwenye uhalisia Serikali pamoja na kutenga shilingi bilioni 10 kwenye mwaka wa fedha 2026/2027 kuanza ujenzi wa meli

hiyo moja au hata kama zitakuwa mbili, bado mahitaji kwenye mwambao ni makubwa zaidi. Hivyo, ni lazima sekta binafsi ishirikishwe, kama ambavyo Dira ya 2050 inavyoelekeza kwamba 70% ya rasilimali tunategemea tuitoe kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini Serikali imefanya? Cha kwanza, Serikali inaimarisha ulinzi na usalama, kama bidhaa namba moja, kama *tool* namba moja ili kuvutia wawekezaji. Bila usalama, bila amani kama iliyopo, wengi hawataweza kukubali kuleta meli zao, kwa hiyo, hili ni jambo la kwanza ambalo Serikali inalifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni uboreshaji wa miundombinu; katika hatua za kuanzia, Serikali imepeleka shilingi bilioni 429 kwenye Bandari ya Tanga ili kufanya maboresho makubwa na inaendelea.

Pili, imepeleka shilingi bilioni 157 kwenye Bandari ya Mtwara ili kuiboresha bandari hiyo na kazi inaendelea. Tatu, Serikali imepeleka shilingi bilioni 435 kwenye Bandari ya Kisiwa Mgao ambayo ni maalum kwa ajili ya kusafirisha bidhaa chafu, ikiwemo simenti pamoja na vitu vingine. Sehemu ya bidhaa hizo itakwenda kwenye Visiwa vya Comoro, lakini pia maboresho kwenye Bandari ya Dar es Salaam nayo ni sehemu mojawapo ya maandalizi ya jambo hili ambalo Mheshimiwa amezungumza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, Serikali yetu hii inaimarisha diplomasia ya uchumi ili ujirani wetu uweze kunufaisha Watanzania. Mojawapo ni pamoja na kufanya kliniki ya pamoja ambayo ilihusisha taasisi 17 za Tanzania kule Moroni na Comoro kujadili fursa zilizopo na kuvutia wawekezaji waweze kuleta meli katika ukanda wetu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kabla sijahitimisha, ni pamoja na kuimarisha mifumo na kuboresha mazingira ya kibiashara nchini, ambapo taasisi zetu za umma, ikiwemo za uratibu kama *TASAC,* zimepewa maelekezo maalum na

zinaendelea kutoa elimu vizuri kwa watu wote. Taasisi mbalimbali zinazohitaji kuleta meli hapa nchini kwetu zichangamkie biashara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa rai kuwaomba Watanzania na wasio Watanzania kuchangamkia fursa za kuleta meli kwenye Bahari ya Hindi kwa sababu mzigo upo, biashara ipo, vitendea kazi ni vichache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa biashara kati ya Comoro na Mtwara imekuwa kubwa na siyo tu Comoro na Mtwara, lakini kwa Tanzania nzima na hususan shughuli za kilimo pamoja na mifugo.

Je, nini sasa mpango wa Serikali kuhamasisha sekta binafsi, ili ziweze kuleta meli kubwa wakati tukisubiria bajeti ya Serikali itengemae na kuleta meli kubwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Nawanda ambaye anataka kufahamu ni upi mkakati wa Serikali kuhamasisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi nchi yetu imenufaika na sekta ya bandari kupitia upakuaji, kwa maana mzigo ukifika tunaupakua na kwenda kuhudumia. Sasa Serikali inataka kunufaika, kwanza kupitia mzigo wenyewe unaotoka nje au mahali pengine, lakini mbili ni kuhakikisha tunapata meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli hizi zinaweza kuletwa kupitia sisi wenyewe Serikali kujenga au kushirikiana, kuhamasisha wawekezaji wengi zaidi na hapa ndipo mzizi ulipo. Tunawaomba

sana, sisi Wabunge ndiyo chombo kikubwa, tujaribu kutazama fursa mbalimbali zilizopo, watu waje, mazingira yameboreshwa. Fursa zipo nyingi, mzingo umeongezeka zaidi na utaongezeka maradufu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu…

**NAIBU SPIKA:** Hitimisha, Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuhitimisha.

**NIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, Mbunge wa Ulyankulu, sasa aulize swali lake.

Na. 433

**Ujenzi wa Barabara ya Kahama – Ulyankulu – Kaliua – Mpanda kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kahama – Ulyankulu – Kaliua hadi Mpanda kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kahama – Ulyankulu – Kaliua – Mpanda yenye urefu wa kilometa 456 ni barabara ya mkoa na inahudumiwa na *TANROADS* Mikoa ya Katavi, Tabora na

Shinyanga. Kwa sasa *TANROADS* ipo kwenye hatua za mwisho za kusaini mkataba kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kujua gharama halisi za ujenzi. Baada ya kukamilika kwa hatua hiyo Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Barabara ya Kahama – Ulyankulu – Kaliua – Mpanda ni barabara ambayo imekuwa ikiahidiwa mara kwa mara. Toka mwaka 2015 na sasa mwaka 2025, wakati Mheshimiwa Rais wetu amefanya mkutano pale Kaliua aliwaahidi Watanzania kwamba barabara hii itajengwa, lakini pia Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi alifanya mkutano pale Kona Nne akawaahidi wananchi kwamba barabara hii itajengwa. Je, ninataka kujua, nini kauli ya Serikali kupata uhakika kwamba baraara hii itajengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Waziri au Naibu Waziri, mko tayari kuongozana na mimi baada ya Bunge hili kwenda kufanya mikutano katika Jimbo la Ulyankulu angalau kuleta matumaini kwa wananchi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu sana na ni vyema pia Bunge hili likafahamu kwamba hii barabara yapo maeneo ambayo hayajafunguliwa kabisa na yanatakiwa yafunguliwe. Ni barabara ambayo tunaifungua upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii ambayo hatujamaliza mwaka wake, tumetenga fedha kuanza kuisanifu. Kama nilivyosema, tunaanza kuisanifu hata kabla ya kumaliza

mwaka huu wa fedha na ndiyo tuko kwenye hatua za mwisho kumpata Mhandisi Mshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii ambayo mmetupitishia wiki iliyopita, tumetenga fedha pia kuendelea na usanifu wa barabara hiyo. Ili hii barabara ianze kwanza kupitika kutokea Mpanda kwenda Tabora, kuna Mto Ugalla ambao tayari tumeanza kujenga makalvati ya kutufikisha Mto Ugalla. Katika bajeti hii pia, tumetenga bajeti ya kuanza kujenga hilo daraja ili tuweze kwanza kuvuka na kuifungua hiyo barabara. Kwa hiyo, ninadhani Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Tabora, hasa Jimbo la Ulyankulu, wataona kwamba tayari Serikali iliamua kuijenga na ndiyo maana imetenga fedha na tumeanza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutakubaliana naye lini baada ya mkutano huu wa Bunge tuweze kutembelea Jimbo la Ulyankulu na kuwaeleza wananchi nini tunategemea kufanya kuhusu hiyo barabara. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ninaona mpo wengi, muda umekwisha sana. Mheshimiwa Martha Mariki swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana katika Mikoa ya Katavi, kwa maana ya Shinyanga ambapo ni Kahama pamoja na Tabora kupitia Ulyankulu. Je, nini *commitment* ya Serikali kuhusiana na ujenzi wa Daraja la Ugalla ambapo litawawezesha wananchi wa Mkoa wa Katavi kuweza kupita katika eneo hili tukiwa tunasubiri barabara ya kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, moja ya *commitment* si tu maneno, kwanza tumelisanifu lile

Daraja la Ugalla, tumekamilisha usanifu. Ninavyoongea sasa hivi, kwenye kitabu chetu cha bajeti tumetenga fedha kwa ajili ya kulijenga daraja hilo ambalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uvuke upande kwenda upande wa pili basi ni lazima uvuke hilo daraja, lakini pia lina makalvati ambayo kama nilivyosema kwenye jibu la msingi wakati ninamjibu Mheshimiwa Mbunge wa swali la msingi, tayari tumeanza kujenga makalvati, ili kulifikia hilo daraja. Hilo daraja limetengewa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haidary Sumry, swali la nyongeza.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ameuliza Mheshimiwa Martha, kwa hiyo, sina tena swali la nyongeza. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea.

Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni sasa aulize swali lake.

Na. 434

**Deni la Mradi wa Daraja la Nyerere, Kigamboni**

**MHE. HARAN N. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itagharamia deni la Mradi wa Daraja la Nyerere ili wananchi wa Wilaya ya Kigamboni wapite bila kulipia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa Daraja la Nyerere (Kigamboni) ulitekelezwa kwa makubaliano maalum kati ya Serikali na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*. Aidha, ilikubalika kuwa daraja hilo litakuwa ni la kulipia ili kuweza kurejesha fedha za mwekezaji zilizotumika katika ujenzi wa daraja hilo. Mara baada ya kukamilisha urejeshaji wa gharama hizi, Serikali itatoa mwongozo kuhusu matumizi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Ninataka kujua kwamba nini *commitment* ya Serikali katika kutoa hiyo 40% ili kuweka sehemu ya punguzo kwa wananchi wa Kigamboni na kuwapunguzia adha ya kodi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ninaomba kama Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda na mimi Kigamboni kuweza kuwaeleza au kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na Mradi wa Daraja la *NSSF* pale Kigamboni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni kweli kwamba urejeshaji wa gharama kwa maana ya deni la *NSSF* bado halijakamilika, kwa hiyo, tumesema katika jibu la msingi kwa kuwa yalikuwa ni makubaliano kwamba hawa wachangie hiki na sisi tuchangie hiki, huo utaratibu bado upo unaendelea. Pengine tu nitoe taarifa kwamba kwa kweli, kwa sasa mwelekeo wa sasa wa Serikali ni uwekezaji kwa ubia yaani kwa maana ya *PPP*, kwa hiyo, ninadhani huo ndiyo muelekeo wa Serikali kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwenda Kigamboni, sisi kama Wizara tuko tayari, lakini pia si tu Wizara ya Ujenzi kwa sababu Wizara ya Ujenzi ni wajenzi na wasimamizi, kwa maana ya kulitengeneza, lakini ni daraja ambalo ni *asset* ya Serikali. Kwa hiyo, sisi kama Ujenzi tutafanya nafasi yetu na pia Wizara nyingine

ambazo zinahusika na hilo daraja, ninadhani kama Serikali, tutakuwa tayari kuwapa elimu wananchi wa Kigamboni na wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali dira yetu ni kwenda 70% kwa maana ya *private sector* na 30 kwa Serikali kwenye miradi mingi ya kimaendeleo ambayo tunaanza kuitekeleza kuanzia bajeti hii na kuendelea, ili kufikia *Vision* yetu ya 2050. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ninatambua Serikali imetenga fedha kwenye bajeti hiyo iliyopita kwamba waweze kujenga barabara ya kutoka Kifulu kwenda *Pugu Station*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu barabara hii ni mbovu sana, wananchi wanashindwa kupita, lakini pia mifugo inayopelekwa kule *Pugu Station,* mnadani inapata adha kubwa kupita kwenye hii barabara. Swali langu kwa Serikali, je, mko tayari kuikarabati kwa muda ili watu waweze kupita wakati tunasubiri sasa ule ujenzi ambao bajeti yake imetengwa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali liliuliza deni la Mradi wa Daraja la Nyerere, siyo ujenzi wa barabara kwa hiyo, tunaendelea.

Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda, Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 435

**Fidia kwa Wananchi wa *Mnanila Centre* Waliopisha Ujenzi wa Barabara**

**MHE. PIUS Z. YANDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa *Mnanila Centre,* Wilayani Buhigwe, waliopisha maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Pius Zebhe Yanda, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara *(The Highway 167 Ordinance Cap 167)* ya mwaka 1932, hifadhi ya Barabara ya Mwandiga – Manyovu ilikuwa mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kila upande. Wakati wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi Barabara ya Mwandiga – Manyovu, *TANROADS* Mkoa wa Kigoma ilitoa notisi kwa wananchi kubomoa vibanda vilivyojengwa ndani ya hifadhi ya barabara ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo ambapo wananchi hao walitii agizo na kubomoa vibanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wa Mnanila walijenga vibanda hivyo ndani ya hifadhi ya barabara kinyume na Sheria ya Barabara ambayo nimeisoma, hivyo hawakuwa na sifa kisheria ya kulipwa fidia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda, swali la nyongeza.

**MHE. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri hasa ya swali langu, lakini nilikuwa na swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kujenga uwezo kwa wananchi ambao wapo karibu na hifadhi ya barabara, hasa yale maeneo ambayo hayana *beacon* ili kupunguza uwezekano wa wananchi kujenga ndani ya hifadhi ya barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamwelewa, ile sentensi yake ya mwanzo sikumpata vizuri Profesa, kama ungeweza kuridhia aweze kurudia.

**NAIBU SPIKA:** Profesa, hebu rudia swali lako kwa ufasaha na kwa ufupi.

**MHE. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanatokea kwa sababu ya kutokuwa na uelewa kuhusu mipaka ya *road reserves* (hifadhi ya barabara). Je, Serikali ina mpango gani au mkakati gani wa kujenga uwezo kwa wananchi ili waweze kujua mipaka ya hifadhi ya barabara, hasa yale maeneo ambapo zile *beacons* hazijajengwa, kwa sababu itakuwa vigumu wao kuweza kujua mpaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, na kwamba barabara nyingi kwa mfano zile ambazo zilikuwa zipo chini ya wenzetu wa TAMISEMI zinakuwa hazina *beacon* na zinakuwa na upana ambao ni tofauti na hizi barabara ambazo zinahudumiwa na *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni kweli kwamba barabara awali zilikuwa kilometa 22.5 kutoka katikati kwenda mpaka mwisho. Kwa hiyo, zilikuwa na mita 45 ambapo baada ya kubadilika kwa sheria tumekwenda mita 60, kwa maana ya 30 kwenda upande mwingine na ndiyo maana tunakuwa na kazi kubwa sasa hivi ya kufanya usanifu. Maana tukishafanya usanifu tunakuwa tunajua barabara itapita wapi na *beacon* zile ikishasanifiwa, kwa hiyo, tunaweka *beacon* ili wananchi wasije wakajenga kuingia kwenye hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana utaona kwamba tunafanya usanifu barabara nyingi sana, ikiwa ni kulinda zile *road reserve* na kuwaelekeza wananchi kwamba wasipite

kwenye zile *beacon* ambazo tumeshazipanda baada ya kufanya usanifu. Bila usanifu huwezi ukaweka *beacon* kwa sababu hujui barabara itapita wapi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kutoka kwetu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Ninaomba niwaletee matangazo; tunao wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni kama ifuatavyo: -

Tunaye Ndugu Ally Gugu - Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, na tunaye Dkt. Maduhu Kazi - Naibu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Pia, tunaye *IGP* Camilius Wambura; tunaye *CGP* Jeremiah Katungu ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza; na tunaye *CGF* John Masunga - Kamishina Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia *CGI* Dkt. Anna Makakala, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Uhamiaji. *(Makofi/Vigelegele)*

Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge.

Tunaye Balozi Ernest Mangu, *IGP* mstaafu; na tunaye Balozi Abdulrahman Kaniki - Naibu *IGP* mstaafu. *(Makofi)*

Pia, tunaye Ndugu James Kaji - Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA);* tunaye Ndugu, Abdallah Mmanga, Mkurugenzi wa *NIDA* kwa upande wa Zanzibar; tunaye Jaji Steven Magoiga ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa Huduma kwa Jamii; na tunaye *DCI* Gharib Yusuph ambaye ni Naibu Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Amani Mashaka ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Sera na Mipango - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Pia, tunaye Ndugu Mabala Mlolwa - Mwenyekiti CCM Mkoa wa Shinyanga; tunaye Mheshimiwa Mboni Mhita ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga; na tunaye Sheikh Dkt. Alhad Mussa Salum, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania. Ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile, tunaye Ndugu Gabriel Mwita ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Tunaye Mchungaji Dkt. Baraka Kihoza ambaye ni Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa ya Pentekosti Tanzania; tunaye Ndugu, Thabit Jongo, ambaye ni Mshauri wa Mufti wa Zanzibar na Mjumbe wa Baraza la Ulamaa Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Katambi, ambao ni familia yake kutoka Shinyanga na Dodoma kama ifuatavyo: -

Tunaye Dkt. Katambi Kwiligwa, baba wa Mheshimiwa Waziri; tunaye Ndugu Specioza Katambi, mama wa Mheshimiwa Waziri; tunaye Ndugu Violeth Katambi, mke wa Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, hawajamuona mke wa Mheshimiwa Waziri, mke wa Mheshimiwa Waziri, simama, karibuni sana. *(Makofi)*

Ahsante sana Waheshimiwa, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Tunaye Ndugu Ernestina Patrobass ambaye ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri; tunaye Ndugu Prais'eve Patrobass ambaye ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri; tunaye Ndugu Michelle Patrobass - mtoto wa Mheshimiwa Waziri; tunaye Ndugu JohnDenzel Patrobass - mtoto wa Mheshimiwa Waziri; tunaye Ndugu Emmanuel Katambi, mdogo wake na Mheshimiwa Waziri; ahsante sana na karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, kama ifuatavyo: -

Tunaye Ndugu Iddi Ali Ame, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja; tunaye Mheshimiwa Juma Usonge, Mwakilishi Jimbo la Chaani ambaye pia ni Mbunge Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; tunaye Ndugu Ali Khamis Dilunga, Mwenyekiti wa CCM Kaskazini A; tunaye Ndugu Rashid Mohamed Mahmoud, kaka wa Mheshimiwa Naibu Waziri; na tunaye Ndugu Mussa Mohamed Mahmoud, mdogo wa Mheshimiwa Naibu Waziri. Ahsante sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge: tuna wageni 40 wa Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani; Masheikh na Viongozi wa CCM kutoka Jimbo la Chaani, Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge na Naibu Waziri wa Madini, Ndugu Ole Suyanda Sadala kutoka Longido, Mkoani Arusha, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na mgeni wa Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu ambaye ni Ndugu Marco Bundala kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa ambaye ni Mheshimiwa Diwani Kata ya Nyakufulu, Ndugu Vicent Yutuba kutoka Mkoani Geita, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe ambaye ni Ndugu Prosper Salema *a.k.a* Shujaa Salema, mpiga kura na mhamasishaji wa kuzungumza Kimachame kutoka Hai, Mkoani Kilimanjaro, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Haiderali Hussein Gulamali ambao ni Madiwani, Katibu wa Mbunge, Mshauri wa Mbunge,

Mwenezi wa Chama, Katibu wa Chama wa Kata kutoka Ilongero, Mkoani Singida, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunaye Ndugu Irene Thadeo kutoka Taasisi ya Jakaya Kikwete Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna madaktari na wataalam wa lishe wawili kutoka Taasisi ya *Afya Yangu Initiative* ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 47 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Kawawa JKT kutoka Mkoani Iringa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 101 na walimu saba kutoka Shule ya Awali na Msingi Montfort ya Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wote karibuni sana katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Ninalo tangazo lingine kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake wa Majimbo, Ndugu Anne Kilango Malecela, anawatangazia Wabunge Wanawake wa Majimbo kuwa siku ya Ijumaa, tarehe 29 Mei, 2026 mara baada ya Bunge kusitishwa saa 7.00 mchana, kutakuwa na kikao. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi namba 20 uliopo Jengo Dogo la Utawala *(Utawa Annex)*. Ahsante.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Patrobass Katambi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa ajili ya kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Waziri, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka 2025/2026 na kupitisha makadirio na mapato ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, pamoja na muhtasari huu ninaomba hotuba yangu ipokelewe na kutambuliwa kama Kumbukumbu Rasmi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, ninamshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tarehe 8 Januari, 2026. Ninamuahidi utii usiogawanyika kwake, kwa Mwenyezi Mungu na Katiba; na muda wote nitaviishi viapo vyangu kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa letu kwa umahiri mkubwa na kuhakikisha kuwa maendeleo yaliyokusudiwa yanapatikana. Ninamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumjaalia afya njema, hekima, busara katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninatoa pongezi kwa viongozi wote wa kitaifa akiwemo Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge na Naibu Spika na Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha niwashukuru pia Wenyeviti wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi hawa kwa pamoja wameonesha uwezo mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais, kuliongoza Taifa letu na kupata mafanikio makubwa ya kitaifa tunayojivunia. Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaahidi kuendelea kupokea na kutekeleza maelekezo ya viongozi hawa katika kuimarisha amani na usalama nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninatumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ikiwa ni pamoja na Wabunge mahiri na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) chini ya uongozi wa Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele. Kamati hiyo imechambua kwa kina makadirio na mapato ya matumizi ya Wizara na kutoa ushauri uliosaidia kuboresha bajeti ya mwaka 2026/2027 na utendaji wa Wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa ninaomba kutoa pole kwa wananchi wa majimbo yaliyopoteza Wabunge wao; Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Jenista Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Peramiho na Mheshimiwa Halima Iddi Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Tunaomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2025/2026; katika utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2025/2026 Wizara ya Mambo ya Ndani ya

Nchi imepata mafanikio mbalimbali kama ilivyoainishwa katika kitabu cha hotuba yangu. Mafanikio hayo ni pamoja na kuendelea kudumisha amani, utulivu na usalama nchini. Mbili, kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya Mahakama Mtandao katika magereza 18 na hivyo kufikia magereza 84; huduma hiyo kati ya magereza 125 iliyopo nchini imekuwa ikitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio hayo ni sehemu ya matokeo ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 13 Januari, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kukamilisha mradi wa ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuzima moto na uokoaji yenye thamani ya dola za Marekani milioni 100. Mradi huo umewezesha upatikanaji wa mitambo 150, boti 23, helkopta moja kwa ajili ya uzimaji moto na uokoaji, magari matatu ya kuzima moto na wa kemikali. Pia magari matano ya kubeba maji na mitambo miwili ya kuvuta magari mabovu yaliyopata ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupata vitendea kazi ambavyo vitaongeza ufanisi na tija kubwa katika utendaji wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, mafanikio mengine ni kufunga mifumo ya *Advance Passengers Information System (APIS)* na *Passenger Name Record (PNR)* katika viwanja vya ndege vya kimataifa; Kiwanja cha Ndege cha Julius Kambarage Nyerere, Kiwanja cha Ndege Mkoa wa Kilimanjaro, Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Mwanza, Jijini Mwanza. Mifumo hiyo itawezesha upatikanaji wa taarifa za abiria mapema, kuzichambua na

kufanya maamuzi stahiki kabla ya abiria hao kuruhusiwa kuanza safari ya kuja nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano; kusajili na kutambua watu 1,145,334 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea na hivyo kufanya jumla ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa mpaka sasa kuwa 27,186,421 sawa na 86% ya lengo la kusajili watu 31,447,938 kwa mujibu wa makadirio ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kukamilisha ujenzi na kuanza kutumika kwa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa usimamizi wa jumuiya ambapo kwa sasa huduma zote za usajili zinapatikana kupitia mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, kuanzishwa kwa Kituo cha Kupokea Taarifa za Uhalifu na Usafirishaji Haramu wa Binadamu kinachowezesha wananchi kutoa taarifa na kupata elimu kwa kupiga simu bure kupitia namba 193.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2024 - 2034 katika magereza 129. Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati *(REA)* limewapatia majiko na mitungi ya gesi watumishi wote na kununua mashine 61 za kutengeneza mkaa mbadala kwa kutumia mabaki ya mimea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, vyuo vya majeshi vyote nchini ambavyo viko chini ya Wizara vimeachana na matumizi ya kuni katika kupikia na kuanza kutumia nishati safi. Hivyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027; katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itatekeleza maeneo nane ya kipaumbele kama ifuatavyo: -

(i) Kuendelea kuboresha miundombinu ya vyombo vya usalama chini ya Wizara ikiwa ni pamoja na makazi ya maafisa, wakaguzi, askari na watumishi wasio askari;

(ii) Kuendeleza na kuboresha upatikanaji wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri na usafirishaji wa vyombo vya usalama vilivyoko chini ya Wizara;

(iii) Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kubaini sababu za makosa mapya na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo;

(iv) Kuendelea kuboresha matumizi ya TEHAMA katika huduma zinazotolewa na Wizara pamoja na vyombo vyake;

(v) Kuendelea kujengea uwezo watumishi na askari kwa kuwapatia mafunzo ili kuwaongezea weledi katika utekelezaji wa majukumu yao;

(vi) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya *NIDA* Jijini Dodoma na ofisi 31 za usajili wa wilaya pamoja na kituo cha mafunzo na matengenezo ya vifaa vya TEHAMA hapo Kibaha;

(vii) Kuanza ujenzi wa nyumba salama kwa ajili ya waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu Jijini Dar es Salaam; na

(viii) Kuimarisha shughuli za uzalishaji mali kupitia kilimo na mifugo, viwanda pamoja na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya usalama nchini. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 makosa makubwa ya jinai yalikuwa 39,027 yaliyotolewa taarifa katika vituo vya polisi ikilinganishwa na makosa ya jinai 40,022 yaliyotolewa taarifa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Kupungua kwa makosa hayo umetokana na kuongezeka kwa uelewa na ushirikiano wa jamii katika kubaini na kuzuia uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kudhibiti uhalifu nchini ikiwemo matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, udukuzi wa taarifa kimtandao na kukamilisha uanzishaji wa Ofisi za Kanda za Upelelezi wa Makosa ya Jinai na Uhalifu wa Kimtandao katika Jiji la Dodoma, Zanzibar na kuimarisha Kikosi Maalum cha Kudhibiti Taarifa Potofu na Uchochezi Mtandaoni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za kusambaza taarifa za uongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama barabarani; Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kudhibiti makosa ya usalama barabarani yanayosababisha vifo na majeruhi na kufanya doria katika barabara mbalimbali hapa nchini. Kupitia doria hizo, jumla ya madereva 3,051,541,000 walikiuka sheria za usalama barabarani, walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kuwapa onyo, kuwatoza faini na kuwafikisha mahakamani kwa kuwafungulia kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaendelea na mikakati ya kusimamia ipasavyo sheria ya usalama barabarani kwa kufanya doria, kuchukua hatua kwa wanaokiuka sheria hiyo na kutoa elimu ya umma kuhusu matumizi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulinzi wa amani nje ya nchi; Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kutoa mchango katika kuboresha ulinzi wa amani nje ya nchi. *Operation* hizo zimehusisha ulinzi wa amani nchini Sudan, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ushiriki huo unawaongezea askari hao ujuzi, uzoefu na weledi na nidhamu inayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa, hali inayoliletea Taifa letu sifa na heshima kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa majengo ya polisi; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi 2026 jumla ya shilingi bilioni 18.58 zimetolewa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miradi sita ya Jeshi la Polisi iliyopo maeneo mbalimbali nchini pamoja na kukarabati majengo ya Makao Makuu ya Jeshi Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara kupitia jeshi hilo imepokea shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuendeleza miradi ya ujenzi wa majengo nane ya ghorofa ya kuishi familia 96 ya Kambi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia hapa Jijini Dodoma. Ujenzi wa jengo moja umekamilika na majengo saba yako katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine iliyotekelezwa na Jeshi la Polisi ni kama inayoonekana katika ukurasa wa 21 hadi ukurasa wa 23 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa vitendea kazi; Wizara kupitia Jeshi la Polisi imepokea kiasi ya shilingi bilioni 247.48 kwa ajili ya ununuzi wa magari 412 na pikipiki 29 za kuongozea misafara. Hadi kufikia Aprili, 2026 magari 26 na pikipiki 24 zimepokelewa na magari 336 yanatarajiwa kupokelewa ifikapo mwezi Juni, 2026. Pia Wizara imenunua vifaa vya kisasa vya uchunguzi na mawasiliano pamoja na doria, mitambo yenye thamani ya shilingi bilioni 182 kwa ajili ya kudhibiti uhalifu unaotokana na kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi inayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027; katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara kupitia Jeshi la Polisi imetenga shilingi bilioni 171.54 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama ilivyoainishwa katika ukurasa wa 25 na 26 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Shirika la Uzalishaji Mali ya Jeshi la Polisi; Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi linatekeleza majukumu ya kibiashara na uwekezaji katika miundombinu ya kisasa inayosaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi. Miongoni mwa miradi na shughuli zinazotekelezwa na shirika hilo ni mradi wa ujenzi wa vituo vya ukaguzi wa vyombo vya moto, utoaji wa huduma saidizi katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na bandari ndogo zilizopo nchini chini yake, utoaji wa huduma za ushonaji na usambazaji wa sare na vifaa vya ushonaji, utoaji wa mafunzo ya usalama kwa taasisi mbalimbali na utoaji wa huduma za ulinzi na miundombinu

ya kimkakati katika Serikali ikiwemo Mradi wa Mwendokasi wa Awamu ya Pili *(DART Phase II)* Posta - Mbagala na Soko Kuu la Kimataifa la Kariakoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ulinzi na usalama magerezani; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya wafungwa na mahabusu 23,516 walihifadhiwa na kupatiwa huduma za msingi ikilinganishwa na wafungwa na mahabusu 27,088 walioko magereza katika kipindi hicho cha mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu huo umechangiwa na uimarishaji wa ushirikiano miongoni mwa taasisi za haki jinai katika kuhakikisha hali ya uhifadhi wa wafungwa na mahabusu magerezani inaimarika. Ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ridhaa yake ya kutoa msamaha kwa wafungwa pamoja na utekelezaji wa adhabu mbalimbali unaohusisha mpango wa *parole* na kifungo cha nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za urekebishaji; hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya wafungwa 148 walipatiwa mafunzo ya ujuzi kupitia vyuo vya magereza. Aidha, katika kipindi husika wafungwa 239 wamehitimu mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara. Vilevile, Jeshi la Magereza limezindua mwongozo wa urekebishaji wa wafungwa unaotokana na kusimamia utekelezaji wa programu za urekebishaji magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shughuli za kilimo, utunzaji wa mazingira na viwanda kutumika katika kuwapatia wafungwa stadi za kazi za maisha na sehemu ya huduma ya urekebishaji; katika msimu wa kilimo wa mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya ekari 10,455.12 za mazao ya kilimo zimelimwa katika mashamba mbalimbali ya magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza maelekezo ya kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na

Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 9 Mei, 2026 wakati akifunga rasmi Mafunzo ya Uongozi ya Kozi ya Juu ya 28 na Uongozi Daraja la Pili la Kozi Namba 48 Wizara kupitia Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza imetenga shilingi bilioni 10 ya bajeti ya mwaka 2026/2027 kwa ajili ya kuanzisha mradi wa kimkakati wa shamba la kilimo kielelezo katika Gereza la Molo lililopo Wilaya ya Sumbawanga Mkoani Rukwa. Mradi huo utatekelezwa kupitia kilimo cha umwagiliaji na uwezeshaji wa Jeshi la Magereza kujitosheleza kwa chakula cha mahindi pamoja na maharage.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya magereza; hadi kufikia Aprili, 2026 shilingi bilioni 2.22 zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mbili za Wakuu wa Magereza wa Mkoa wa Songwe na Geita pamoja na ukarabati wa Gereza la Isanga - Dodoma, Uyui - Tabora, Ukonga - Dar es Salaam na Liungu - Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi na ukarabati wa ofisi ya magereza hayo unaendelea na upo katika hatua mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 shilingi bilioni saba zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya magereza kama ilivyobainishwa katika ukurasa wa 41 na ukurasa wa 42 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji na ulipaji wa fidia; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Jeshi la Magereza limepokea shilingi milioni 329 kwa ajili ya upimaji wa maeneo 17 nchini pamoja na ulipaji wa fidia kwa wananchi wa Wilaya ya Kaliua, Tabora ambapo maeneo yao yote yametwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa gereza jipya la Wilaya ya Kaliua. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 shilingi milioni 900 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia katika maeneo ya Msanga, Dodoma, Liwale - Lindi na Ilemela, Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya uangalizi wa wafungwa na vifungo vya nje; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Wizara imewezesha wafungwa 4,815 kutumikia adhabu zao za nje ya magereza. Aidha, wafungwa 4,200 wa

vifungo vya nje walimaliza kutumikia vifungo vyao. Katika utekelezaji wa adhabu za nje ya magereza umesaidia kupunguza msongamano wa wafungwa gerezani na kuwezesha Serikali kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 14.33 ambazo zingetumika kuhudumia wafungwa hao endapo wangetumikia kifungo magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kazi zinazofanywa na wafungwa hao zimeokoa jumla ya shilingi bilioni 9.6 ambazo zingetumiwa na Serikali kuwalipa vibarua. Hivyo jumla ya fedha zote zilizookolewa kupitia huduma hizo ni shilingi bilioni 29.93. Hili ni jambo la kupongeza sana uongozi wa magereza na mpango mzuri ambao umewekwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imepanga kutumia shilingi bilioni 4.97 kwa ajili ya kuwaweka kwenye programu ya vifungo vya nje na kuwasimamia wafungwa zaidi ya 6,500. Pia itatoa elimu ya utekelezaji wa programu hiyo kwa wadau na haki jinai na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa za wafungwa wa vifungo vya nje gerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Shirika la Magereza, (SHIMA); hadi kufikia Aprili, 2026 Shirika la Magereza limekamilisha miradi ya ujenzi wa majengo na Ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro na Ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao *(e-GA)* Mkoa wa Iringa. Shirika pia limeendelea na miradi ya ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokoaji katika Mkoa wa Mara, Singida na ujenzi wa vituo hivyo unatarajiwa kukamilika ifikapo Oktoba, 2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli nyingine zinazotekelezwa ni ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo, Handeni - Tanga na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Manispaa ya Iringa. Vilevile, kupitia Kampuni Tanzu ya Ulinzi *(SHIMA Guard Company Limited),* Shirika limefanikiwa kutoa huduma ya ulinzi kwa taasisi za umma 42 na binafsi 19. Huduma hiyo imetoa ajira kwa vijana wa Kitanzania 927. Miradi mingine

inayotekelezwa na shirika hilo ni kama ilivyobainishwa katika ukurasa wa 46 hadi ukurasa wa 49 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za zimamoto na uokoaji; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi 2026, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limezima moto na kufanya uokoaji katika matukio 4,436 ambapo majeruhi 1,713 waliokolewa. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, jeshi hili litaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ili kupunguza madhara yanayotokana na moto na majanga mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto; hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imefanya ukaguzi wa kinga na tahadhari za moto na majanga mengine katika maeneo 62,100 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 12.29 kilikusanywa sawa na 98.38% ya lengo la kipindi husika. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 jumla ya maeneo 110,000 yalikaguliwa na shilingi bilioni 17 zilitarajiwa kukusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi na ukarabati wa *fire hydrants;* kutokana na uhitaji mkubwa wa mabomba maalum ya kuchukulia maji ya magari ya kuzima moto *(fire hydrants)* hasa katika ngazi ya wilaya na halmashauri, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na Mamlaka za Miji zinatekeleza mpango wa miaka mitano (2025/2030) kwa ajili ya kufunga *fire hydrants* 4,256 katika ngazi za wilaya na halmashauri zinazowezesha upatikanaji wa maji ya kuzima moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2026 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeweza kupokea *fire hydrants* 56 kutoka mamlaka za maji zilizofungwa katika mikoa 13 nchini. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 shilingi milioni 600 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa *fire hydrants* 272.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa vituo na makazi ya askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imeendelea na ukamilishaji wa vituo saba vya zimamoto na uokoaji nchini. Hadi kufikia Aprili, 2026 ujenzi wa vituo viwili umekamilika katika Mikoa ya Njombe na Simiyu. Aidha

umaliziaji wa vituo vitano katika Mikoa ya Manyara, Katavi, Geita, Kagera na Songwe unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Jeshi limepokea shilingi bilioni 2.46 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokoaji katika Wilaya za Bunda, Gairo, Nzega, Sengerema pamoja na Halmashauri za Chalinze na Mafinga na kufanya ukarabati wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Mkoani Ruvuma. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 shilingi bilioni 10.6 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo saba vya zimamoto na uokoaji katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa umma; hadi kufikia mwezi Aprili, 2026 elimu ya kinga na tahadhari ya zimamoto na majanga mengine imetolewa katika maeneo 23,327 yenye mikusanyiko mikubwa ya watu pamoja na kupitia vyombo vya habari na kurasa mbalimbali za mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 669.21 kwa ajili ya kukamilisha utoaji wa elimu kwa umma na kuhamasisha wananchi kujiunga na vikundi vya wazimamoto kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa huduma ya uhamiaji nchini; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya wageni 2,529,000 waliingia nchini ikilinganishwa na wageni 1,839,342 walioingia katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ongezeko hili la wageni limetokana na jitihada zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, ikiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira bora ya kuwavutia wageni katika sekta ya utalii na utekelezaji wa huduma za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya Watanzania 476,190 walitoka nchini na 443,561 walirejea nchini ikilinganishwa na Watanzania 400,434 waliotoka nchini na 376,011waliorejea katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, pasipoti na hati nyingine za safari; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya pasipoti 78,583 zilitolewa kwa Watanzania ikilinganishwa na pasipoti 114,448 zilizotolewa katika kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, hati za safari za dharura 226,400 zilitolewa ikilinganishwa na hati za safari za dharura 204,387 zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa mwaka 2026/2027 Idara ya Uhamiaji itaendelea na kutoa pasipoti na hati za safari kwa raia wa Tanzania ili kuwawezesha kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, operesheni, misako, doria na ukaguzi; Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeendelea kufanya operesheni, misako, doria na ukaguzi katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kubaini na kuwakamata na kudhibiti wahamiaji haramu wanaoingia nchini. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya watuhumiwa 49,469 wa makosa ya kiuhamiaji walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ambapo kati ya hao, wahamiaji haramu 34,099 waliondoshwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na wahamiaji haramu hususan katika mikoa ya mipakani, Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeanzisha Kanda Maalum ya Uhamiaji katika Mikoa ya Kagera na Kigoma. Aidha, Idara itaendelea kufanya misako na doria na kuanzisha kanda nyingine katika maeneo ya kimkakati yenye muingiliano mkubwa wa wageni, ili kuhakikisha wahamiaji haramu wanadhibitiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa rai kwa Watanzania kuendelea kushirikiana na Idara ya Uhamiaji katika kuwafichua wageni wanaoishi katika maeneo kinyume na sheria, kanuni na taratibu za nchi na kufanya hivyo kutaifanya Tanzania kuendelea kuwa nchi salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli nyingine zinazotekelezwa na Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji ni kama ilivyobainishwa katika ukurasa wa 61 na 62 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili na utambulisho wa watu nchini; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 Wizara kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* imesajili na kutambua watu 1,145,334 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Aidha, katika kipindi husika, jumla ya watu 857,244 wamepatiwa Namba za Utambulisho wa Taifa na hivyo kufanya jumla ya watu waliopata namba hizo mpaka sasa kuwa 22,654,206. Namba hizo zinawawezesha wananchi kutambulika wakati wa kupata huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika taasisi za umma na taasisi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwahimiza waajiri wote nchini kuhakikisha kuwa waajiriwa wao wanahakikiwa kwa kutumia *NIDA* ili kujiridhisha kuhusu uraia wao pamoja na taarifa nyingine za utambuzi, hivyo kuendelea kuimarisha usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi husika vitambulisho 232,535 vimechapishwa na kusambazwa katika Ofisi za Usajili wa Wilaya na zile Ofisi za *NIDA*, kufanya jumla ya vitambulisho vilivyochapishwa na kusambazwa kuwa 21,553,057. Aidha, jumla ya vitambulisho 275,682 vimegawiwa kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyogawiwa kuwa 20,894,235.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuongeza huduma ya ugawaji wa vitambulisho karibu na wananchi na kuanzisha huduma ya kutuma ujumbe mfupi kwa wananchi ambapo vitambulisho vimechapishwa na kuwataka kufika katika ofisi za wilaya walizojisajili ili kuvichukua. Bado kuna vitambulisho 668,822 katika ofisi za wilaya za *NIDA* ambavyo havijachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *NIDA* imeanzisha namba maalum ya kutuma ujumbe mfupi bila malipo *(sms)* ambayo ni 15274. Namba hiyo inamwezesha mwananchi kufuatilia hatua ya maombi yake ya Kitambulisho cha Taifa ilipofikia, pamoja na kupata namba yake ya utambulisho bila kulazimika kufika katika Ofisi za *NIDA*. Aidha, katika kuhakikisha *NIDA* inakuwa na kanzidata yenye taarifa sahihi za watu, Serikali imetoa kibali maalum cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Oktoba, 2025 hadi

Septemba, 2026 cha kuruhusu wananchi waliotoa taarifa sahihi wakati wa usajili kufanya mabadiliko ya taarifa na kutoa taarifa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge waliopewa taarifa ya kuchukua vitambulisho vyao, kujitokeza kwenda kuvichukua, pia wanaoomba kutumia namba 15274 kupitia simu zao za mkononi kufuatilia maombi ya vitambulisho vya Taifa. Aidha, natoa rai kwa wananchi wenye changamoto za taarifa zao katika mfumo wa *NIDA*, kutumia fursa iliyotolewa ya kufanya maboresho ya taarifa hizo kwa kutoa taarifa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uunganishaji wa mfumo wa *NIDA* na mifumo ya taasisi nyingine; *NIDA* inaendelea kutekeleza maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hasa katika kuhakikisha mifumo ya taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi zinasomana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi 2026 *NIDA* imeunganisha taasisi 17 na mfumo wa usajili na utambuzi na kufanya jumla ya taasisi 147 zilizounganishwa na mfumo huo. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara kupitia *NIDA* imetenga shilingi bilioni 132.26 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali kama ilivyobainishwa katika ukurasa wa 68 hadi 70 katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma kwa wakimbizi; hadi kufikia Aprili, 2026 nchi yetu ilikuwa na hifadhi jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi 158,954 ambapo kati ya hao 70,952 ni wenye asili ya nchi ya wenzetu Burundi na 87,303 wana asili ya ndugu zetu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na 699 kutoka katika mataifa mengine mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Wakimbizi Duniani *(UNHCR)* pamoja na wadau wengine muhimu, imekamilisha zoezi la mahojiano ya kina na wakimbizi wenye asili ya nchi ya Burundi

waliopo katika kambi zote na makazi, ili kuweza kuwatafutia suluhisho la kudumu. Matokeo ya zoezi hilo yamebainisha kuwa zaidi ya 95% ya wakimbizi hao hawakuwa na sababu za msingi za kuendelea kuwepo katika hifadhi za kimataifa kwa kuwa nchi hiyo sasa ina amani, ina utulivu wa kisiasa unaowezesha urejeaji salama kwa kuzingatia utu na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hilo lilifuatiwa na mkutano wa pande tatu baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya nchi ya Burundi na *UNHCR* uliofanyika tarehe 26 hadi 28 Novemba, 2025 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulithibitisha kuwa wakimbizi hao hawana sababu ya kuendelea kuwepo nchini kwa kuwa nchi yao ni salama na hivyo kuweka makubaliano kuwa wao wanaweza kurejea nchini kwao ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni, 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya wakimbizi 76,403 walirejeshwa nchini Burundi kwa hiyari yao na hivyo kusababisha kufungwa kwa kambi ya wakimbizi ya Nduta iliyopo Wilayani Kibondo, Mkoani Kigoma. Vilevile, wakimbizi 561 walihamishwa nchini kwenda nchi za Australia, Canada, Sweden, Ufaransa na Uingereza. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imetenga fedha shilingi bilioni 3.62 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za usimamizi wa masuala ya wakimbizi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili na ukaguzi wa jumuiya za kiraia; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya jumuiya za kiraia 126 zimesajiliwa ambapo 12 ni jumuiya za kidini na 114 zisizo za kidini. Pia ukaguzi wa jumuiya za kiraia 350 umefanyika katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Ruvuma na Songwe. Lengo la ukaguzi huo ni kufuatilia utekelezaji wa masharti ya usajili pamoja na kubaini mchango wa jumuiya hizo katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara imeanzisha programu ya ushirikishwaji ili kuimarisha uelewa na uwajibikaji wa viongozi wa jumuiya za kiraia katika uendeshaji wa jumuiya zao. Kupitia programu hiyo, jumla ya viongozi wa jumuiya za kidini na zisizo za kidini 2,500 walipatiwa mafunzo kuhusu uendeshaji wa jumuiya

unaozingatia sheria na kuimarisha amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imetenga shilingi bilioni 1.57 kwa ajili ya shughuli za usimamizi na uratibu wa shughuli za jumuiya za kiraia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu; katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya waathirika 160 wa usafirishaji haramu wa binadamu waliokolewa na kusaidiwa. Kati ya waathirika hao, 126 waliokolewa nchini na waathirika 34 waliokolewa kutoka katika mataifa mengine. Vilevile katika kipindi husika, watuhumiwa 57 walikamatwa kutokana na kujihusisha na uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu. Kati ya hao, watuhumiwa 45 walifikishwa katika mahakama na 12 uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara imetoa mafunzo maalum ya kupambana na uhalifu unaosababisha na usafirishaji haramu wa binadamu kwa wadau 314 wa haki jinai katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Kagera, Mwanza na Singida. Mafunzo hayo yalilenga kujengea uwezo wa kuwatambua waathirika na kutoa huduma stahiki na kufanya upelelezi na kuendesha mashtaka kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Wizara imetoa elimu ya kukabiliana na usafirishaji haramu wa binadamu kwa jamii kupitia mitandao ya kijamii, vipindi vya redio, televisheni na makongamano, semina na mikutano, maonyesho mbalimbali ambapo jumla ya wananchi 19,076 walifikiwa. Wizara ilianzisha Kituo cha Kupokea Taarifa za Uhalifu wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu *(Counter-Trafficking in Persons Call Center)* ambapo wananchi wanaweza kutoa taarifa za dharura, kupata elimu na kupiga simu bure kupitia namba 195. Napenda kutoa rai kwa wananchi waendelee kutoa taarifa na kupata elimu kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu kupitia namba 195.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imetenga shilingi bilioni 2.76 kwa ajili ya kuendelea kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na kutoa huduma kwa waathirika wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani; ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge wa Chaani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, kwa kazi yake nzuri anayoifanya katika kunisaidia majukumu kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, nimshukuru sana Dkt. Ally Senga Gugu - Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, yeye pamoja na Dkt. Maduhu Kazi Isack - Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wao wanaonipatia katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli kazi yao imetukuka, uzalendo wao na uchapakazi wao umekuwa msaada sana kwa Taifa letu, lakini pia kwa nchi yetu. Vilevile, nawapongeza wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama vilivyopo nchini, chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kuendelea kuhakikisha nchi inakuwa na amani na utulivu, hivyo kuweka mazingira rafiki kwa wananchi na wageni na kuwashirikisha kikamilifu katika maendeleo ya uchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi hao ni *IGP* Camillus Mongoso Wambura, *CGP* Jeremiah Yoram Katungu; *CGF* John William Masunga na *CGI* Dkt. Anna Peter Makakala. Pamoja na hao nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Ndugu James Wilbert Kaji kwa uongozi wao makini na kunipa ushirikiano wa kutosha na hakika watu hawa wana uzalendo uliotukuka, wanafanya kazi yao kwa kuangalia maslahi mapana ya Taifa letu na wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama na hivyo ni hakika kwamba tunamsaidia vizuri Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana pia Mheshimiwa Jaji Stephen Magoiga, Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa kwa Huduma kwa Jamii, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *Parole*, *IGP* Mstaafu Ernest Mangu, Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Ndugu Omar Issa - Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi,

*Major General* Mstaafu Hamis R. Semfuko - Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Magereza kwa uongozi wao mahiri katika kusimamia kamati na bodi hizo. Uongozi wao umeongeza ufanisi katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutambua mchango wa Wajumbe wote wa Kamati na bodi hizo ambao umeongoza ufanisi katika kuimarisha utendaji wake. *(Makofi)*

Pia nitumie fursa hii pia kuwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wakiwemo Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Makamishna, Naibu Makamishna, Wakuu wa Vitengo, Maafisa, Wakaguzi na Askari kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na jitihada zao zimechangia kuleta tija kubwa katika utekelezaji wa mipango ya bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2025/2026 lakini kuendelea kulilinda Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inazishukuru jumuiya za kikanda na nchi mbalimbali zikiwemo Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*; pamoja na wanachama wa nchi hizo. Pia inashukuru nchi za Brazil, China, India, Indonesia, Jamhuri ya Korea Kusini, Misri, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Urusi na Uturuki kwa ushirikiano wao katika masuala mbalimbali kwenye nyanja za ulinzi na usalama wa Taifa letu na hata zile ambazo sijazitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawashukuru Mashirika na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa zikiwemo *FSDT*, *GIZ*, *IOM*, *UNDP*, *UNHCR*, *UNICEF*, *World Bank*, *WFP*, *CAMARTEC*, Chuo cha Uhasibu – Arusha, Chuo cha Ustawi wa Jamii – Dar es Salaam, *NACTVET*, *PUMA Energy*, *REA*, *RUSUMO Power Company Ltd.*, *STAMICO*, *Taifa Gas*, *TPA*, *VETA*, Benki za CRDB na NMB kwa kuunga mkono Serikali katika shughuli za kuimarisha amani na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazishukuru jumuiya za kidini na zisizo za kidini na mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na vyombo vya habari kwa kushirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu, jitihada na juhudi za kuhimiza amani na umoja wa Taifa letu hapa nchini. Pia napenda kutoa shukrani za dhati kwa

wananchi wote kwa moyo wa uzalendo na ushiriki wao katika kulinda na kuendeleza amani na utulivu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee na kwa moyo wa dhati naishukuru familia yangu wakiwemo wazazi wangu Dkt. Katambi na *Mrs. Katambi;* mke wangu Violeth Shoo Katambi na watoto wangu Ernestina, Prais'eve, Michelle na John Denzel kwa kunipa ushirikiano unaoniwezesha kutekeleza vema majukumu ya Wizara. Pia ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Shinyanga Mjini kwa upendo wao, kunichagua na kwa kushirikiana nami kwa maendeleo ya Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi, viongozi wangu wa mkoa na wilaya, lakini pia viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi Taifa kwa ushirikiano wao mzuri. Tunaye Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa hapa na viongozi wote wa Mkoa wetu wa Shinyanga, Mkuu wetu wa Wilaya, lakini maalum Mwenyekiti wetu Mzee Mabala, lakini pia Wabunge wote wa Mkoa wa Shinyanga kwa kazi nzuri na ushirikiano wao na wale wengine wote ambao sijawataja, ninawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kuhusu makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027; katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepanga kukusanya jumla ya shilingi 499,090,000,000 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itaendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki na ununuzi wa vitendea kazi vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2026/2027; kwa heshima na taadhima, naomba sasa Bunge lako liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 2,443,215,927,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2026/2027. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Shilingi 1,953,366,486,000 sawa na 80% ya bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,183,766,640,000 ni mishahara na shilingi 769,599,846,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; na

(ii) Shilingi 489,849,441,000 sawa na 20% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 453,955,843,000 ni fedha za ndani na shilingi 35,893,598,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara *www.moha.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo heshima kubwa, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE. PASCHAL KATAMBI PATROBASS (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 yanayojumuisha Fungu 51 – Makao Makuu ya Wizara na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Fungu 28 – Jeshi la Polisi; Fungu 29 – Jeshi la Magereza; Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; na Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2026/27 kwa mara ya kwanza

nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, namshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 08 Januari 2026. Namuahidi utii usiogawanyika kwake, kwa Mungu na Katiba, na muda wote nitaviishi viapo vyangu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuliongoza vema Taifa kwa umahiri mkubwa na kuhakikisha kuwa maendeleo yaliyokusudiwa yanapatikana. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu yake.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia natoa pongezi kwa Viongozi wote wa Kitaifa akiwemo Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb.), Naibu Spika na Mhe. George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. Aidha, nawashukuru pia Wenyeviti wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** viongozi hawa kwa pamoja wameonesha uwezo mkubwa katika kumsaidia Mhe. Rais kuliongoza Taifa letu na kupata mafanikio makubwa ya kitaifa tunayojivunia. Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaahidi kuendelea kupokea na kutekeleza maelekezo ya viongozi hawa katika kuimarisha amani na usalama nchini.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, natumia nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ikiwa ni pamoja na Wajumbe mahiri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) chini ya uongozi wa Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Paschal Inyasi Chinyele (Mb.). Kamati hiyo imechambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na kutoa ushauri uliosaidia

kuboresha bajeti ya mwaka 2026/27 na utendaji wa Wizara kwa ujumla.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa naomba kutoa pole kwako na wananchi wa majimbo yaliyopoteza wabunge wao ambao ni Mhe. William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mhe. Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Peramiho na Mhe. Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi). ***Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina***.

**Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2025/26**

8. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi tilioni 2.06. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 950.31 ni za Mishahara; Shilingi bilioni 701.70 za Matumizi Mengineyo; na Shilingi bilioni 415.14 za Miradi ya Maendeleo. Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, Shilingi bilioni 388.61 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 26.53 ni fedha za nje.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara imepokea jumla ya Shilingi tilioni 2.19. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 887.36 ni Mishahara; Shilingi bilioni 632.09 ni Matumizi Mengineyo; na Shilingi bilioni 670.34 za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Fedha zilizopokelewa ni sawa na asilimia 106 ya bajeti yote ya Wizara na zinajumuisha Shilingi bilioni 414.34 zilizopokelewa kutoka Bajeti Kuu ya Serikali kwa ajili ya operesheni maalum pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali**

10. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/26 Wizara iliwekewa lengo la kukusanya maduhuli ya jumla ya Shilingi bilioni 428 kutokana na vyanzo vya ndani. Hadi kufikia Aprili 2026 jumla ya Shilingi bilioni 332.33 zimekusanywa sawa na asilimia 77.65 ya lengo.

## B. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/26 NA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2026/27

### Mafaniko Yaliyopatikana katika Mwaka wa Fedha 2025/26

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo: kuendelea kudumisha amani, utulivu na usalama nchini kwa kuwalinda raia na mali zao. Hali hiyo imechangia nchi yetu kuendelea kuwa kivutio kwa wageni wanaokuja nchini kwa shughuli mbalimbali ikiwemo uwekezaji na utalii.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia Wizara imefanikiwa kutoa hifadhi salama kwa wafungwa na mahabusu katika magereza yote nchini pamoja na kupunguza hali ya msongamano magerezani kutoka wafungwa na mahabusu 27,088 katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 na kufikia 23,516 katika kipindi kama hicho mwaka 2025/26. Vilevile, imefanikiwa kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya Mahakama Mtandao kutoka magereza 66 hadi kufikia magereza 84 yenye huduma hiyo. Mafaniko hayo ni sehemu ya matokeo ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 13 Januari 2023.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imefanikiwa kukamilisha mradi wa ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuzima moto na uokoaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100. Kupitia mradi huo, Jeshi limepokea mitambo 150, boti 23 na helikopta moja (1) kwa ajili ya kuzima moto na uokoaji; magari matatu (3) ya kuzima moto wa kemikali; magari matano (5) ya kubeba maji; na mitambo miwili (2) ya kuvuta magari mabovu na yaliyopata ajali.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeboresha mifumo ya usalama katika viwanja vya ndege kwa kusanifu na kufunga mifumo ya *Advance Passengers Information System (APIS)* na *Passenger Name Record (PNR)* katika Viwanja vya Ndege vya

Kimataifa vya Mwalimu Julius Nyerere, Kilimanjaro na Abeid Amani Karume pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Mifumo hiyo itawezesha kupatikana kwa taarifa za abiria mapema, kuzichambua na kufanya maamuzi stahiki kabla ya abiria hao kuruhusiwa kuanza safari ya kuja nchini.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imefanikiwa kuanzisha Kanda Maalum za Kiuhamiaji katika Mikoa ya Kagera na Kigoma kwa lengo la kuongeza udhibiti wa wahamiaji haramu. Kupitia hatua hiyo, idadi ya ukamataji wa wahalifu wa makosa ya kiuhamiaji imeongezeka kutoka 19,071 kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 na kufikia 49,469 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2025/26.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NIDA kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 imefanikiwa kusajili na kutambua watu 1,145,334 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea ikilinganishwa na watu 844,994 waliosajiliwa na kutambuliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/25, hivyo kufanya jumla ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa kuwa 27,186,421; kutoa Namba za Utambulisho wa Taifa kwa watu 857,244 hivyo kufikisha jumla ya watu 22,654,206 waliopata Namba za Utambulisho; na kuunganisha taasisi 17 katika Mfumo wa Usajili na Utambuzi hivyo kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa kuwa 147.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Mfumo wa kielektroniki wa Usajili na Usimamizi wa Jumuiya (RSMIS) na umeanza kutumika ambapo kwa sasa idadi ya jumuiya zilizosajiliwa ni 12,966. Aidha, huduma zote za usajili zinapatikana kupitia mfumo huo bila wateja kulazimika kufika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya Makao Makuu ya Wizara Jijini Dodoma. Pia, imeanzisha Kituo cha Kupokea Taarifa za Uhalifu wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu kinachowawezesha wananchi kutoa taarifa za dharura na kupata elimu kwa kupiga simu bure kupitia namba 195.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika suala la utunzaji wa mazingira, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) katika magereza yote 129. Aidha, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati

Vijijini (REA) limewapatia majiko na mitungi ya gesi watumishi wote na kununua mashine 61 za kutengenezea mkaa mbadala kwa kutumia mabaki ya mimea. Vilevile, vyuo vya majeshi yote chini ya Wizara vimeachana na matumizi ya kuni katika kupikia na kuanza kutumia nishati safi.

**Maeneo ya Kipaumbele katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/27**

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itatekeleza maeneo nane (8) ya kipaumbele kama ifuatavyo:

(i.) Kuendelea kuboresha miundombinu ya vyombo vya usalama chini ya Wizara ikiwa ni pamoja na makazi ya maafisa, wakaguzi, askari na watumishi wasio askari;

(ii.) Kuendelea kuboresha upatikanaji wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa vyombo vya usalama vilivyopo chini ya Wizara;

(iii.) Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kubaini sababu za makosa mapya na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo;

(iv.) Kuendelea kuboresha matumizi ya TEHAMA katika huduma zinazotolewa na Wizara pamoja na vyombo vyake;

(v.) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi na askari kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ili kuwaongezea weledi katika utekelezaji wa majukumu yao;

(vi.) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya NIDA Jijini Dodoma na Ofisi 31 za Usajili za Wilaya pamoja na Kituo cha mafunzo na matengenezo ya vifaa vya TEHAMA Kibaha;

(vii.) Kuanza ujenzi wa nyumba salama kwa ajili ya waathirika wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu Jijini Dar es Salaam; na

(viii.) Kuimarisha shughuli za uzalishaji mali kupitia kilimo, mifugo na viwanda pamoja na utunzaji wa mazingira.

## C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27

### Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu

#### (i) Ajira kwa Watumishi

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 Wizara imeajiri jumla ya watumishi 10,238. Kati ya watumishi hao, Makao Makuu ya Wizara 84; Jeshi la Polisi 5,650; Jeshi la Magereza 1,564; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 1,444; Idara ya Uhamiaji 1,487 na NIDA tisa (9).

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 10,919. Kati ya hao, watumishi wa Makao Makuu ya Wizara 249; Jeshi la Polisi 8,040; Jeshi la Magereza 1,046; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 500; Idara ya Uhamiaji 1,000 na NIDA 84.

#### (ii) Mafunzo kwa Watumishi

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utendaji kazi, Wizara imewezesha upatikanaji wa mafunzo kwa jumla ya watumishi 13,475 ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, Makao Makuu ya Wizara watumishi 172, Jeshi la Polisi 8,457; Jeshi la Magereza 2,030; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 1,358; Idara ya Uhamiaji 1,324 na NIDA 134.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Wizara imetenga jumla ya Shilingi bilioni 38.81 za kuwezesha mafunzo kwa watumishi 23,547. Kati ya hao, watumishi wa Makao Makuu ya

Wizara 85; Jeshi la Polisi 15,508; Jeshi la Magereza 3,500; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 1,508; Idara ya Uhamiaji 2,789 na NIDA 157.

### (iii) Upandishaji Vyeo

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kupandisha vyeo watumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambapo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya watumishi 9,689 wamepandishwa vyeo kwa mchanganuo ufuatao: Makao Makuu ya Wizara watumishi 106; Jeshi la Polisi 5,539; Jeshi la Magereza 3,220; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 75; Idara ya Uhamiaji 693; na NIDA 56.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 23,089. Kati ya hao, watumishi wa Makao Makuu ya Wizara 73; Jeshi la Polisi 13,487; Jeshi la Magereza 6,579; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 833; Idara ya Uhamiaji 2,028 na NIDA 89.

### (iv) Upimaji wa Utendaji Kazi

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji kazi. Wizara inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa maafisa, wakaguzi na askari wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara. Jumla ya Shilingi bilioni 1.43 zimetumika, ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 93 na unatarajia kukamilika ifikapo Juni 2026. Mfumo huo utasaidia kuboresha utekelezaji wa hatua mbalimbali za kiutumishi ikiwa ni pamoja na upandishaji cheo, likizo na mafunzo.

### (v) Maeneo ya Ujenzi wa Ofisi, Vituo na Makazi

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika Wizara imepokea Shilingi bilioni 1.37 ili kuwezesha upatikanaji wa maeneo 133 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, vituo na makazi kwa watumishi. Kati ya maeneo hayo, Makao Makuu ya Wizara eneo moja (1); Jeshi la Polisi 20; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 32; Idara ya Uhamiaji 71 na NIDA tisa (9).

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa mwaka 2026/27 jumla ya Shilingi bilioni 3.2 zimetengwa ili kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, vituo na makazi kwa watumishi. Kati ya fedha hizo, Jeshi la Polisi Shilingi milioni 300; Jeshi la Magereza Shilingi milioni 900; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Shilingi milioni 605; Idara ya Uhamiaji Shilingi bilioni 1.1 na NIDA Shilingi milioni 300.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa ajira, mafunzo, kuwezesha upandishaji vyeo na upatikanaji wa maeneo hayo. Hali hii imeongeza morali na tija kwa watumishi katika utendaji kazi wa Wizara.

**HALI YA USALAMA NCHINI**

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha usalama wa raia na mali zao, Wizara kupitia Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama imeendelea kufanya doria, misako na operesheni ili kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu. Ushirikiano huo umewezesha nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu, hivyo kuwezesha raia kufanya kazi zao za kiuchumi na kijamii. Aidha, elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa falsafa ya Polisi jamii inaendelea kutolewa.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa katika vituo vya Polisi yalikuwa 39,027 ikilinganishwa na makosa 40,022 yaliyotolewa tarifa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/25. Kupungua kwa makosa hayo kumetokana na kuongezeka kwa uelewa na ushirikiano wa jamii katika kubaini na kuzuia uhalifu. Kati ya makosa hayo 9,603 ni makosa dhidi ya binadamu, 13,986 makosa dhidi ya maadili ya jamii, 14,794 makosa ya kuwania mali na 644 makosa ya uhalifu wa kifedha.

**Uhalifu wa Kimtandao (Cyber Crimes)**

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 makosa ya uhalifu wa kimtandao yaliyotolewa taarifa katika vituo vya polisi, yameongezeka kutoka makosa 748 mwaka 2024/25 hadi 1,323. Idadi ya makosa hayo imeongezeka kutokana na askari kutumia vifaa vya kisasa vya uchunguzi, kufanya operesheni, doria mtandaoni na mwitikio chanya wa wananchi kutoa taarifa kuhusu uhalifu wa mtandao.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/27 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kudhibiti uhalifu wa kimtandao ikiwemo matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii na udukuzi wa taarifa za kimtandao kwa kuanzisha ofisi za kanda za upelelezi wa makosa ya uhalifu wa kimtandao katika Jiji la Dodoma na Zanzibar; kuweka mifumo ya ufuatiliaji wa shambulio la kimtandao; kuimarisha kikosi maalum cha kudhibiti taarifa potofu na uchochezi mtandaoni; kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za kusambaza taarifa za uongo; na kufuatilia na kudhibiti akaunti hatarishi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania – TCRA.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kutekeleza programu maalum za mafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa, wakaguzi na askari ili kukabiliana na uhalifu mpya ikiwemo uhalifu wa mtandaoni. Hadi kufikia Aprili 2026 maafisa, wakaguzi na askari 157 wamepata mafunzo ya uchunguzi wa makosa ya kimtandao, sayansi ya uchunguzi wa alama za vidole na uchunguzi wa hati zenye mashaka.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** watumishi hao wamepatiwa mafunzo ya uchambuzi wa tabia za wahalifu, uchunguzi wa kisayansi wa vifaa vya kielektroniki, usimamizi wa masuala ya kiusalama wakati wa majanga, kupambana na ugaidi wa kimataifa na kuwajengea uwezo katika uchunguzi wa kisayansi. Mafunzo hayo yametolewa katika nchi za Brazil, India, Uturuki, Korea Kusini, Misri na Urusi.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama imeendelea

kuimarisha ulinzi na usalama katika miradi ya kimkakati ikiwemo: Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR), Daraja la John Pombe Magufuli - Kigongo Busisi, Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Mradi wa Gesi ya Asili, Bandari Kavu ya Kwala na Viwanja vya Ndege kwa kupanga askari na kufanya doria katika miradi hiyo.

**Operesheni Zilizofanyika**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Jeshi la Polisi limefanya operesheni mbalimbali nchini za kudhibiti matukio ya uhalifu. Kupitia operesheni hizo, Jeshi limefanikiwa kukamata silaha 187 na risasi 196. Silaha zilizokamatwa ni aina ya *Shortgun* 45, Bastola sita (6), *Rifle* 10, *Mark IV* nne (4) na Magobole 122. Aidha, jumla ya watuhumiwa 169 walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kesi zao zinaendelea.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kupitia operesheni hizo jumla ya nyara za Serikali 3,618 zenye uzito wa kilogramu 99,642 na gramu 94 zimekamatwa. Makosa hayo yalihusisha watuhumiwa 1,175 ambao walifikishwa mahakamani na kesi zao ziko katika hatua mbalimbali.

**Usalama Barabarani**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kudhibiti makosa ya usalama barabarani yanayosababisha vifo na majeruhi kwa kufanya doria katika barabara mbalimbali nchini. Kupitia doria hizo, jumla ya madereva 3,051,541 waliokiuka sheria za usalama barabarani walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kuwapa onyo, kuwatoza faini, kuwafikisha mahakamani na kuwafungia leseni. Aidha, Jeshi limeendelea kushirikiana na wadau wa usalama barabarani kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya barabara kupitia vyombo vya habari, shule za msingi na sekondari, vituo vya maegesho ya pikipiki na bajaji na vituo vya mabasi.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** takwimu zinaonesha kuwa, matukio ya usalama barabarani yaliyotolewa taarifa katika vituo vya Polisi nchini yamepungua kutoka 1,322 katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 na kufikia 1,233 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2025/26.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika matukio hayo, jumla ya watu 1,066 walipoteza maisha ikilinganishwa na watu 1,275 waliopoteza maisha katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/25 ikiwa ni upungufu wa asilimia 16.4. Vilevile, watu 1,869 walijeruhiwa ikilinganishwa na watu 2,278 waliojeruhiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/25 ikiwa ni upungufu wa asilimia 18.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaendelea na mikakati ya kusimamia ipasavyo sheria ya usalama barabarani kwa kufanya doria na kuchukua hatua stahiki kwa wanaokiuka sheria hiyo. Pia, Wizara kupitia Jeshi itaendelea kushirikiana na wadau wengine kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu matumizi sahihi ya barabara kwa mujibu wa sheria. Hatua hizo zinalenga kuimarisha hali ya usalama barabarani.

**Ushirikishwaji wa Wananchi katika Kubaini, Kuzuia na Kutanzua Uhalifu**

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ulinzi na usalama kwenye jamii, Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kuwapangia vituo vya kazi wakaguzi wa polisi katika kata na shehia zote nchini. Hadi kufikia Aprili 2026 kata 2,645 na shehia 307 tayari zimepangiwa wakaguzi wa polisi. Aidha, kata 1,315 na shehia 81 zilizobaki wamepangwa askari wa vyeo vya chini wakati taratibu za kuwapata wakaguzi zinaendelea. Vilevile, kata 195 na shehia 10 tayari zimepatiwa pikipiki kwa ajili ya kuwawezesha wakaguzi/askari hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia falsafa ya Polisi Jamii, Wizara kupitia Jeshi la Polisi imetoa elimu ya ulinzi shirikishi kwa wananchi katika kata 3,960 na shehia 388. Elimu hiyo imetolewa katika makanisa, misikiti, vyuo, shule, madrasa, vituo vya maegesho ya

pikipiki na bajaji, mikutano na vikao. Pia, elimu hiyo imetolewa kupitia mitandao ya kijamii ya polisi (TPF website, Instagram, X - Twitter, Youtube channel – Usalama TV) na kufuatiliwa na wananchi 1,943,515 na vipindi 17,952 vya redio na runinga vimefanyika.

**Dawati la Jinsia na Watoto**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na makosa ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto, Wizara kupitia Jeshi imetoa elimu ya kubaini na kuzuia makosa hayo kwa wananchi 503,750. Vilevile, wakufunzi 20 walipata mafunzo ya polisi jamii na 30 mafunzo ya jinsia na ulinzi wa mtoto kutoka vyuo vya polisi na kufanya mapitio ya vitini vya kufundishia na kiongozi cha mwalimu. Aidha, wataalamu 25 wa sayansi ya uchunguzi wa makosa ya jinai kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini Magharibi, Pwani, Tanga na Mkoa wa Kipolisi Rufiji walipewa mafunzo ya namna ya kukusanya vielelezo vya kesi za ukatili wa kijinsia na unyanyasaji. Mafunzo hayo yaliwezeshwa na wataalamu kutoka nchini Uingereza na kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani – GIZ.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na uhalifu wa ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto katika mwaka 2026/27, Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kuwajengea uwezo watendaji waliopo kwenye Dawati la Jinsia na Watoto. Pia, kuimarisha ushirikiano na wadau, matumizi ya vifaa vya kisasa na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia na watoto. Aidha, Shilingi bilioni 1 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa ofisi ya Jinsia Makao Makuu ya Polisi Dodoma.

**Ulinzi wa Amani Nje ya Nchi**

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kutoa mchango katika operesheni za Ulinzi wa Amani (Peace Keeping Missions) nje ya nchi. Operesheni hizo zinahusisha ulinzi wa amani Sudani Kusini (UNMISS), Sudani (UNISFA) na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (MONUSCO). Ushiriki huo unawaongezea

ujuzi, uzoefu, weledi na nidhamu inayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa hali inayoileteа sifa Taifa letu.

**Ujenzi wa Majengo ya Polisi**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya Shilingi bilioni 18.58 zimetolewa kwa ajili ya kuendeleza mradi wa maboresho ya Shule ya Polisi Tanzania - Moshi ikiwemo mabweni matano (5) ya ghorofa yenye uwezo wa kuishi wanafunzi 2,870 na nyumba mbili (2) za ghorofa zenye uwezo wa kuishi familia 24; kuendeleza ujenzi wa jengo moja (1) lenye ghorofa mbili (2) la makazi ya familia 12 za askari katika kambi ya Polisi Buyekera Mkoa wa Kagera; kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe; kumalizia ujenzi wa ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara na *Rest House* ya Polisi Mkoa wa Arusha; na ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Jijini Dodoma (RUWASA).

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia Jeshi imepokea Shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kuendeleza mradi wa ujenzi wa majengo nane (8) ya ghorofa ya kuishi familia 96 katika kambi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia Dodoma. Ujenzi wa jengo moja (1) umekamilika na majengo saba (7) yapo katika hatua mbalimbali.

**Miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Tuzo na Tozo ulianzishwa mwaka 2010 kwa mujibu wa Kifungu cha 66 (1) na (2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322. Mfuko huo unalenga kutoa huduma ya ustawi wa askari ikiwemo kulipa fidia kwa askari wanaoumia au kufariki wakiwa kazini, kugharamia matibabu nje ya nchi na kuboresha miundombinu ya kazi na makazi ya askari.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mfuko huo, Wizara imeendelea kujenga na kuendeleza miradi mbalimbali kama ifuatavyo: kuendeleza ujenzi wa vituo vinne (4) vya Polisi Daraja “A” kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.5 katika Mikoa ya Dodoma, Ruvuma, Rukwa na Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya. Pia, Shilingi bilioni 2.55

zimetumika kuanza na kuendeleza ujenzi wa vituo nane (8) vya Polisi vya Daraja "B" katika Wilaya za Kiomboi – Singida, Kilindi na Korogwe – Tanga, Buhigwe - Kigoma, Mpimbwe - Katavi, Magharibi "A" - Mjini Magharibi, Karagwe – Kagera na Micheweni - Kaskazini Pemba.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi bilioni 1.9 zimetumika kumalizia ujenzi wa vituo vitano (5) vya Polisi vya Daraja "B" katika Wilaya za Bagamoyo, Kisarawe, Kibiti na Mkuranga – Pwani na Wilaya ya Kishapu – Shinyanga. Vilevile, Shilingi bilioni 1.14 zimetumika kuanza ujenzi wa vituo nane (8) vya Polisi Daraja "C" katika Kata za Bukanga na Mugeta – Mara; Gwanumpu na Kitanga – Kigoma; Mutukula, Mrongo na Nyakaiga – Kagera; na Lukumbule – Ruvuma. Pia, Shilingi bilioni 2.3 zimetumika kuendeleza ujenzi wa ofisi saba (7) za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Geita, Manyara, Mtwara, Simiyu, Songwe, Temeke na Rufiji.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Polisi imetumia Shilingi milioni 350 kujenga ukuta wa nyumba saba (7) za makamishna katika maeneo ya Mwangaza Jijini Dodoma, Shilingi milioni 100 kuendeleza ujenzi wa nyumba tatu (3) za kuishi askari kambi ya Mfikiwa Mkoa wa Kusini Pemba. Pia, Shilingi milioni 500 kuendeleza ujenzi wa bweni la ghorofa tano (5) lenye vyumba 40 vya kulala wanafunzi 80 katika chuo cha Maafisa wa Polisi Kidatu. Vilevile, Shilingi milioni 600 zimetumika kujenga Hospitali ya Rufaa ya Jeshi la Polisi Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam na Shilingi milioni 270 kujenga Zahanati ya Polisi Mkoa wa Songwe.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi milioni 174.54 zimetumika kufanya ukarabati wa maghorofa 13 ya kuishi askari katika Kambi ya Polisi Barabara ya Kilwa Mkoa wa Kipolisi Temeke Dar es Salaam. Ukarabati wa majengo hayo umeanza na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2026. Aidha, Shilingi milioni 359 zimetumika kumalizia ujenzi wa jengo moja (1) lenye kituo cha Polisi Daraja "C" na nyumba ya kuishi familia mbili (2) za askari eneo la Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja.

## Upatikanaji wa Vitendea Kazi

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi imepokea kiasi cha Shilingi bilioni 247.48 kwa ajili ya ununuzi wa magari 412 na pikipiki 24 za kuongozea misafara. Hadi kufikia Aprili 2026 magari 76 na pikipiki 24 zimepokelewa na magari 336 yanatarajiwa kupokelewa ifikapo Juni 2026. Aidha, Jeshi limepokea Shilingi bilioni 64.79 ambazo zimetumika katika ununuzi wa vifaa vya kijeshi.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara kupitia Jeshi imenunua vifaa vya kisasa vya uchunguzi na mawasiliano pamoja na vifaa vya doria mtandaoni vyenye thamani ya Shilingi bilioni 182 kwa ajili ya kudhibiti uhalifu unaotokana na kukua kwa teknolojia. Upatikanaji wa vitendea kazi hivyo umeongeza ufanisi wa kazi kwa kufanya doria mtandaoni ili kuzuia matukio ya uhalifu na kuwezesha shughuli za upelelezi kufanyika kwa wakati**.**

## Miradi ya TEHAMA

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika uimarishaji wa matumizi ya TEHAMA Jeshi limetumia Shilingi milioni 500 kujenga Mfumo wa udhibiti wa taarifa za Afya katika Hospitali za Jeshi la Polisi (Police Health Management Information System - PHMIS) kwa kuzingatia mahitaji ya Jeshi na miongozo ya Wizara ya Afya. Pia, mfumo huo umeboresha ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na matibabu, udhibiti wa utendaji kazi na ufanisi wa vifaa na watumishi.

## Upimaji na Ulipaji wa Fidia kwa Maeneo ya Polisi

***58. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara kupitia Jeshi la Polisi imepokea Shilingi milioni 249 kwa ajili ya fidia na upimaji wa maeneo 166 katika Mikoa ya Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Njombe, Manyara, Mara, Morogoro, Pwani, Rukwa, Singida, Shinyanga na Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya. Upimaji wa maeneo hayo utasaidia kuepuka migogoro ya ardhi na kuboresha mazingira ya kazi na makazi kwa maafisa, wakaguzi na askari. Aidha, Shilingi milioni 300 zimetengwa katika mwaka 2026/27 kwa ajili ya kupima maeneo na kulipa fidia.

**Miradi Itakayotekelezwa katika Mwaka 2026/27**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itatekeleza miradi ya kipaumbele ifuatayo kwa gharama ya Shilingi bilioni 171.59: ununuzi wa magari 190 ya operesheni kwa gharama ya Shilingi bilioni 30, pikipiki 1,500 za Polisi kata/shehia kwa gharama ya Shilingi bilioni 6, usimikaji wa mifumo ya TEHAMA na ununuzi wa redio 6,010 za masafa marefu kwa gharama ya Shilingi bilioni 14.36 pamoja na ununuzi na usimikaji wa mfumo wa alama za vidole (AFIS) kwa gharama ya Shilingi bilioni 15.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia Jeshi linatarajia kufanya ununuzi wa vifaa vya kijeshi kwa gharama ya Shilingi bilioni 91.73; ununuzi wa sare za Polisi na vifaa vya ushonaji kwa gharama ya Shilingi bilioni 15.24; na ufungaji wa minara 15 ya mawasiliano ya redio ya masafa mafupi katika mikoa ya Iringa, Kagera, Kaskazini Unguja, Katavi, Morogoro, Mbeya, Mwanza, Mara, Njombe, Pwani na Songwe kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.84. Pia, kulipa fidia za viwanja vya Polisi na upimaji wa maeneo kwa gharama ya Shilingi milioni 300 na kulipa madeni ya wazabuni kwa gharama ya Shilingi milioni 100.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27 Wizara kupitia Jeshi la Polisi itatekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya polisi wa miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2026/27 hadi 2030/31 kwa kuendeleza miradi ifuatayo: ujenzi wa ofisi na nyumba za makazi ya askari kwa gharama ya Shilingi bilioni 8.99; ukarabati wa nyumba za askari kwa gharama ya Shilingi milioni 880; ujenzi wa vituo vya Polisi 42 vikiwemo vituo 12 kati ya 23 vilivyochomwa moto wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa gharama ya Shilingi bilioni 16.68; kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Jeshi la Polisi Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam kwa gharama ya Shilingi milioni 912; ujenzi wa *rest house* Mkoa wa Dodoma kwa gharama ya Shilingi milioni 689; kukarabati na kukamilisha mabweni saba (7) ya wanafunzi katika vyuo na Shule ya Polisi Tanzania Moshi kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.41.

**SHUGHULI ZA SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA JESHI LA POLISI**

**62. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi linatekeleza majukumu ya kibiashara na uwekezaji katika miundombinu ya kisasa itakayosaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi kama ilivyo azma ya uanzishwaji wake.

**Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati**

**Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Vyombo vya Moto Nchini**

**63. *Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa vituo vya ukaguzi wa vyombo vya moto unaendelea kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya uendeshaji wa miradi ya Ubia. Napenda kulijulisha Bunge kuwa Kamati ya Uendeshaji wa Miradi ya Ubia (PPP Steering Committee) imeridhia Shirika kuendelea na uwekezaji katika mradi huo. Aidha, Kampuni ya *Mandatory Vehicle Inspection Tanzania* imeanzishwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambao utahusisha ujenzi wa vituo 26 Tanzania Bara. Mkataba wa ubia umesainiwa tarehe 30 Aprili 2026 na kazi inayoendelea sasa ni maandalizi ya kuanza ujenzi wa vituo hivyo. Matarajio ni kuwa na vituo kumi (10) vilivyokamilika katika miezi nane ya kwanza baada ya kusainiwa kwa mkataba wakati ujenzi wa vituo vingine ukiendelea.

**Mradi wa Udhibiti wa Makosa Barabarani katika Barabara Kuu (Highway Patrol)**

**64. *Mheshimiwa Spika,*** pia, Shirika linaendelea na maandalizi ya utekelezaji mradi wa ubia wa udhibiti makosa barabarani katika barabara kuu kwa awamu. Rasimu ya mkataba wa utekelezaji wa mradi imeandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka na utaanza baada ya kusainiwa kwa mkataba huo.

**Utekelezaji wa Miradi ya Kibiashara**

**65. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kutekeleza miradi ya kibiashara ili kukuza mtaji. Katika mwaka 2025/26, Shirika

limeendelea kutoa huduma saidizi katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na bandari ndogo zilizo chini yake katika kusimamia watendaji wa kutwa 858 pamoja na kazi ya upakuaji wa magari na kuyapeleka katika bandari kavu zilizopo Dar es Salaam. Vilevile, Shirika linatoa huduma za ushonaji na usambazaji wa sare na vifaa vya ushonaji, mafunzo ya usalama kwa taasisi pamoja na usafirishaji wa mizigo.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine wa kibiashara unaotekelezwa na Shirika ni Usafirishaji na Usindikizaji wa Fedha na Vito vya thamani ambapo hadi kufikia Aprili 2026 Shirika limetoa huduma ya usindikizaji fedha katika *Automated Teller Machine* (ATM) za Benki ya NMB nchini. Ili kuongeza ufanisi katika mradi huo, Shirika limenunua magari matatu (3) maalum ya kusafirishia fedha yatakayoanza kutoa huduma hiyo kwa wateja. Kupatikana kwa magari hayo, kunatoa fursa kwa Shirika kuendendelea kuimarisha huduma zake kwa wateja. Pia, mwezi Aprili 2026 Shirika limesaini mkataba mwingine na Benki ya NMB kwa ajili ya kuongeza mawanda ya huduma.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Shirika linatoa huduma za ulinzi kwa watu binafsi pamoja na taasisi za umma. Katika kutekeleza huduma hii, Shirika linatoa huduma ya ulinzi wa miundombinu ya kimkakati ya Serikali ikiwemo mradi wa Mwendokasi Awamu ya Pili (DART Phase II – Posta – Mbagala) na Soko Kuu la Kimataifa la Kariakoo.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Shirika limekusanya mapato ghafi ya Shillingi bilioni 7.66 kutokana miradi ya kibiashara inayotekelezwa ikilinganishwa na Shilingi bilioni 3.4 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/25.

**HALI YA ULINZI NA USALAMA MAGEREZANI**

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Magereza imeendelea kudumisha hali ya ulinzi na usalama magerezani kwa kuimarisha operesheni za kiusalama pamoja na usimamizi wa magereza nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya wafungwa na mahabusu 23,514 walihifadhiwa na

kupatiwa huduma za msingi ikiwemo chakula, malazi, mavazi na huduma za afya. Kati ya hao, wafungwa walikuwa 19,704 na mahabusu 3,810.

**70. *Mheshimiwa Spika,*** takwimu hizo zinaonesha idadi ya wafungwa magerezani imepungua kwa asilimia 13.2 ikilinganishwa na idadi ya wafungwa na mahabusu 27,088 (wafungwa 19,400 na mahabusu 7,688) waliokuwepo magerezani katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Hali hiyo imetokana na kuimarishwa kwa ushirikiano na taasisi za haki jinai katika kuhakikisha hali ya uhifadhi inaimarika magerezani.

**71. *Mheshimiwa Spika,*** kupungua kwa idadi hiyo ya wafungwa pia kumetokana na msamaha wa Mhe. Rais kwa wafungwa na matumizi ya adhabu mbadala yanayohusisha Mpango wa Parole na kifungo cha nje. Hatua hizo zimeleta matokeo chanya katika kupunguza msongamano magerezani, kuchochea mabadiliko ya tabia kwa wafungwa na zimesaidia kuboresha utoaji huduma za uhifadhi kwa viwango stahiki vinavyozingatia haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika magereza yote nchini.

**72. *Mheshimiwa Spika,*** wafungwa 2,405 walinufaika na msamaha wa Mhe. Rais uliotolewa wakati wa Maadhimisho ya Miaka 64 ya Uhuru wa Tanganyika yaliyofanyika tarehe 09 Desemba 2025 na Miaka 62 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yaliyofanyika tarehe 26 Aprili 2026. Kufuatia msamaha huo, wafungwa 458 waliachiwa huru na wafungwa 1,947 walipunguziwa sehemu ya vifungo vyao na kuendelea kutumikia adhabu zilizobaki magerezani. ***Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ridhaa yake ya kutoa msamaha kwa wafungwa hao***.

**73. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia matumizi ya adhabu mbadala magerezani kupitia huduma ya Parole na kifungo cha nje. Katika kipindi husika wafungwa 412 wamenufaika na huduma ya Parole na wafungwa 897 wametolewa magerezani kwa utaratibu wa Kifungo cha Nje (Extra Mural Labour - EML). Hatua hizo zimesaidia kupunguza hali

ya msongamano na kuhamasisha mabadiliko chanya ya tabia za wafungwa waliopo magerezani.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha huduma ya Parole, Jeshi limetoa mafunzo kwa wajumbe 66 wa Bodi za Parole, Wakuu wa Magereza wa Mikoa sita (6) na Maafisa Parole 78 waliopo katika Mikoa ya Geita, Kagera, Mara, Shinyanga, Simiyu na Singida. Aidha, elimu kuhusu Sheria ya Bodi za Parole imetolewa kupitia vyombo vya habari, maonesho mbalimbali ya kitaifa, mitandao ya kijamii pamoja na maadhimisho ya sherehe ya miaka 64 ya Jeshi la Magereza. Katika mwaka 2026/27 Shilingi milioni 402.70 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Parole.

**Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA Magerezani**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha ulinzi, usalama na usimamizi wa magereza nchini kupitia uboreshaji wa miundombinu ya kiusalama, matumizi ya mifumo ya kisasa ya upekuzi, pamoja na kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa wafungwa na mahabusu. Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi wa utendaji, kuzuia vihatarishi vya kiusalama na kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa taarifa muhimu za wafungwa na mahabusu.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026 Shilingi milioni 900 zimepokelewa kwa ajili ya kujenga Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Wafungwa na Mahabusu waliopo magerezani (PIMIS). Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 50, hatua inayowezesha mfumo kuanza kupokea taarifa za wafungwa na mahabusu. Kwa sasa, kazi ya kuingiza taarifa hizo inaendelea katika gereza la Isanga – Dodoma na Karanga – Kilimanjaro. Katika Mwaka wa Fedha 2026/27 Shilingi bilioni 1.50 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa mfumo huo na kugharamia kazi ya uingizaji wa taarifa za wafungwa na mahabusu katika magereza makuu matano (5) ya Arusha, Karanga, Keko, Segerea na Ukonga.

**77. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Jeshi kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania limeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri ya mahabusu kupitia huduma ya Mahakama Mtandao. Katika kipindi husika, Jeshi limeongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hiyo kutoka magereza 66 hadi 84. Hatua hii imeendelea kuchangia upatikanaji wa haki kwa wakati.

**Huduma ya Usafirishaji wa Mahabusu na Wafungwa**

**78. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Magereza imeendelea kuboresha huduma ya usafirishaji wa mahabusu na wafungwa kwenda na kurudi mahakamani. Lengo la huduma hii ni kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wakati, kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashauri ya jinai na kupunguza ucheleweshaji wa kesi unaotokana na changamoto za usafirishaji wa wafungwa na mahabusu.

**79. *Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026, Jeshi limenunua mabasi mawili (2) ya kusafirisha mahabusu kwenda na kurudi mahakamani yenye thamani ya Shilingi milioni 878. Upatikanaji wa magari hayo, umewezesha utolewaji wa huduma hiyo katika mkoa wa Mbeya. Hatua hii imewezesha kuongeza wigo wa utoaji wa huduma hiyo na kufikia mikoa mitano (5) ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Pwani.

**80. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/27, Shilingi bilioni 10.70 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 9 ni kwa ajili ya magari ya shughuli za utawala na Shilingi bilioni 1.70 magari ya utoaji wa huduma ya kusafirisha mahabusu kwenda Mahakamani katika Wilaya za Kyela, Tukuyu na Mbarali - Mbeya pamoja na Mkoa wa Mwanza. Aidha, Jeshi litaendelea na utoaji wa huduma ya usafirishaji wa mahabusu katika mikoa mingine kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

## Huduma za Urekebishaji

**81.** ***Mheshimiwa Spika***, urekebishaji ni hatua ya kubadilisha tabia, fikra, mwenendo, hisia za mkosaji ili kumjenga na kumfanya kuwa raia mwema katika jamii. Jukumu la urekebishaji wa wafungwa magerezani linatekelezwa kupitia utoaji wa mafunzo rasmi, ushauri nasihi na huduma za kiroho. Pia, urekebishaji huo hufanyika kupitia michezo na burudani pamoja na kuwapatia wafungwa stadi za maisha zinazotolewa katika shughuli za kilimo, ufugaji, ujenzi, viwanda na utunzaji wa mazingira ambazo zinatekelezwa magerezani. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 wafungwa 12,172 wameshiriki katika shughuli hizo.

### (i.) Utekelezaji wa Shughuli za Urekebishaji Kupitia Programu za Elimu na Mafunzo ya Stadi za Kazi

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026 jumla ya wafungwa 148 walipatiwa mafunzo ya ujuzi kupitia Vyuo vya Magereza kwa mchanganuo ufuatao: wafungwa 73 wamepatiwa mafunzo ya Ufundi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi kilichopo Ruanda Mbeya, wafungwa 9 wamehitimu mafunzo ya elimu na ujuzi kupitia Gereza la Wami Vijana - Morogoro na 66 wanaendelea na mafunzo katika chuo hicho. Pia, Jeshi kwa kushirikiana na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) linaendelea na utoaji wa programu maalumu ya mafunzo na elimu kwa njia ya kidijitali katika Gereza Arusha. Aidha, katika kipindi husika wafungwa 239 wamehitimu mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Jeshi limezindua Mwongozo wa Urekebishaji wa Wafungwa utakaotumika kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa programu za urekebishaji magerezani. Mwongozo huo unalenga kuweka mwelekeo wa pamoja katika utekelezaji wa programu za urekebishaji kwa kuimarisha misingi ya uwajibikaji na ufuatiliaji, kusimamia na kulinda haki na utu wa wafungwa, kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya urekebishaji, kuweka utaratibu na uratibu madhubuti wa utekelezaji wa programu hizo, kukuza ushirikishaji wa wadau katika shughuli za

urekebishaji wa wafungwa, pamoja na kuimarisha utoaji wa taarifa na utunzaji sahihi wa kumbukumbu.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwongozo huo umeainisha hatua kuu nne katika mzingo wa urekebishaji (Rehabilitation Circle), ambazo ni hatua ya mapokezi, kipindi cha kutumikia kifungo (incarceration), maandalizi kabla ya kutoka gerezani (prerelease) na utangamanisho wa mfungwa katika jamii (reintegration). Hadi kufika Aprili 2026 maafisa mapokezi 762 kutoka magereza yote wamejengewa uwezo kuhusu matumizi ya mwongozo huo ambao unatarajiwa kuanza kutumika Julai 2026.

**(ii.) Urekebishaji kupitia Shughuli za Kilimo, Viwanda na Utunzaji wa Mazingira**

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za kilimo, utunzaji wa mazingira na viwanda hutumika katika kuwapatia wafungwa stadi za kazi na maisha kama sehemu ya huduma za urekebishaji. Programu hizo hutekelezwa sambamba na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na viwanda, mazao ya misitu, kilimo na mifugo.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa kilimo wa mwaka 2025/26 jumla ya ekari 10,455.12 za mazao ya kilimo zimelimwa katika mashamba mbalimbali ya Magereza. Kati ya ekari hizo, 4,687.6 zimelimwa zao la mahindi, 955.52 maharage, 1,192 mpunga, 1,513 alizeti na 2,107 mazao mengine. Mazao hayo bado yapo shambani na matarajio ya mavuno ni tani 5,643.8 za mahindi, 824.8 za mpunga, 334.71 za maharage na tani 713.88 za alizeti. Mavuno hayo yanatarajia kutosheleza mahitaji ya chakula cha wafungwa na mahabusu kwa asilimia 102.3 za mahindi; 82.5 mpunga; 33.3 maharage na mafuta ya kula asilimia 78.2.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maelekezo ya kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 09 Mei 2026 wakati akifunga rasmi Mafunzo ya Uongozi Ngazi za Juu Kozi Na. 28 na Uongozi Daraja la Pili Kozi Na. 48. Wizara kupitia Jeshi la Magereza imetenga Shilingi bilioni 10 katika mwaka 2026/27 kwa

ajili ya kuanzisha mradi wa kimkakati wa shamba la kilimo la kielelezo katika Gereza Mollo lililopo Wilaya ya Sumbawanga, mkoani Rukwa.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** shamba hilo lenye ekari 4,500 litalimwa mazao ya mahindi (ekari 3,000) na maharage (ekari 1,500) kwa matarajio ya kuzalisha tani 5,400 za mahindi na tani 1,500 za maharage. Mradi huo utatekelezwa kupitia kilimo cha umwagiliaji na utawezesha Jeshi la Magereza kujitosheleza kwa chakula cha mahindi na maharage na kutoa mafunzo endelevu kwa wafungwa ili kuwapatia ujuzi katika shughuli za kilimo.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kutekeleza programu za utunzaji wa mazingira, Jeshi kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) na wadau wengine limefanikiwa kuhifadhi ekari 84,712.68 za misitu asilia na kupanda miti 2,001,258 ya aina mbalimbali katika mashamba ya magereza. Aidha, jumla ya miti 31,500 ilivunwa, kuuzwa na kuchangia maduhuli ya Serikali ya Shilingi milioni 331.85. Katika mwaka 2026/27, Jeshi linatarajia kupanda miti 2,200,000 pamoja na kuendelea kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwenye maeneo ya magereza.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, urekebishaji wa wafungwa kupitia shughuli za viwanda umeendelea kuimarishwa katika magereza mbalimbali nchini. Katika kipindi husika Shilingi milioni 197.19 zimepokelewa kwa ajili ya kugharamia ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la karakana katika Gereza la Vijana Wami – Morogoro. Jengo hilo litatumika kwa ajili ya kutolea mafunzo ya stadi kwa wafungwa vijana.

### (iii.) Ushirikiano na Taasisi Nyingine za Urekebishaji Nje ya Nchi

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Magereza imeendelea kuimarisha mahusiano, kujifunza na kubadilishana uzoefu kutoka taasisi za magereza katika nchi mbalimbali duniani. Katika kipindi husika, askari wa Jeshi la Magereza wameenda nchini Shelisheli kupitia utaratibu wa kubadilishana uzoefu wa

watumishi. Aidha, wataalamu wameshiriki ziara za kikazi katika nchi za Afrika Kusini, Burundi, China, Ghana, Indonesia, Kenya, Marekani, Misri, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Uganda, Ujerumani na Zimbabwe. Ziara hizo zimewapatia nafasi ya kujifunza na kubadilishana uzoefu. Vilevile, maafisa wengine wanatekeleza jukumu la ulinzi wa amani katika nchi za Somalia – UNMIT na Sudani Kusini – UNMISS.

**(iv.) Uimarishaji wa Utoaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii na Ushauri wa Kisaikolojia Magerezani**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za ushauri nasihi zimeendelea kuimarishwa magerezani kwa kuyawezesha madawati ya utoaji wa huduma hizo kufanya kazi kwa kuzingatia weledi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 Maafisa Ustawi wa Jamii 349 wametoa huduma hizo kwa wafungwa katika magereza yote nchini. Aidha, askari 40 wenye taaluma ya ustawi wa jamii wameajiriwa na wanaendelea na mafunzo ya awali katika Chuo cha Mafunzo Kiwira - Mbeya. Kutokana na umuhimu wa wataalam hao katika kuimarisha jukumu la urekebishaji, katika mwaka 2026/27 Jeshi linatarajia kuajiri askari 60 wenye taaluma hiyo.

**Matumizi ya Nishati Safi Magerezani**

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, kupitia Jeshi la Magereza, imeendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu magerezani ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia. Hadi kufikia Aprili 2026, Shilingi bilioni 3.1 zimetumika kugharamia matumizi hayo ikiwemo kuviwezesha vituo 57 kutumia nishati zaidi ya moja inayohusisha gesi asilia, gesi vunde, LPG na mkaa mbadala kulingana na upatikanaji wa nishati katika kituo husika. Aidha, mashine 61 zimenunuliwa na kusambazwa magerezani kwa ajili ya kuchakata mkaa mbadala kwa kutumia mabaki ya mimea.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Magereza imeshirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuwapatia

watumishi wote majiko na mitungi ya gesi. Utekelezaji huo ni jitihada zinazolenga kuimarisha matumizi ya nishati safi kwa watumishi wa Jeshi hilo ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi kwa jamii zinazozunguka vituo vya magereza. Katika mwaka 2026/27, Shilingi bilioni 7 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia magerezani.

**Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Magereza**

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya magereza kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi na makazi kwa watumishi pamoja na huduma za uhifadhi na urekebishaji wa wafungwa na mahabusu. Hadi kufikia Aprili 2026, Shilingi bilioni 2.22 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Magereza. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 1.06 ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mbili (2) za Wakuu wa Magereza wa Mikoa ya Songwe na Geita na Shilingi bilioni 1.15 kwa ajili ya kugharamia ukarabati wa Gereza Isanga – Dodoma, Uyui – Tabora, Ukonga – Dar es Salaam na Lilungu – Mtwara. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya magereza hayo unaendelea na upo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Shilingi bilioni 7 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya magereza. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 2.90 zitagharamia ujenzi wa nyumba moja (1) ya makazi ya Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza na nyumba mbili (2) za makazi ya Makamishna wa Jeshi la Magereza Jijini Dodoma; Shilingi milioni 500 kujenga Ofisi ya Mkuu wa Magereza Mkoa wa Njombe; Shilingi bilioni 2 kuendeleza ujenzi wa Magereza mapya ya Msalato – Dodoma na Kaliua – Tabora; na Shilingi bilioni 1.60 ni kwa ajili ya kufanya ukarabati katika Gereza Kuu Uyui – Tabora.

**Upimaji na Ulipaji wa Fidia**

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Jeshi la Magereza limepokea Shilingi milioni 329 kwa ajili ya upimaji na ulipaji wa fidia. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni 132 ni

za kugharamia kazi ya upimaji wa maeneo 17 ya Magereza yaliyopo Wami Kuu, Mwamngomboli na Kiberege – Morogoro; Mlele – Katavi; Kalambo – Rukwa; Mayamaya na Sanzawa kwa Mtoro – Dodoma; Farm Kigongoni na Kifaru – Kilimanjaro; Kiwira (KK), Chunya na Lugombo – Mbeya; Farm Mavuji na Chikwale – Lindi; Farm Mbulu – Manyara; Kimara – Pwani na Mgwisha – Tanga ambapo upatikanaji wa hati miliki za maeneo hayo zipo katika hatua ya ukamilishaji. Pia, Shilingi milioni 197 zilizobaki ni kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wa Wilaya ya Kaliua, Tabora ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa gereza jipya la Wilaya ya Kaliua.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi limeendelea kutekeleza mikakati ya kuzuia na kutatua migogoro ya ardhi iliyopo maeneo ya magereza. Katika kipindi husika migogoro miwili (2) ya ardhi iliyokuwepo katika maeneo ya Gereza Mgagao - Iringa na Kambi Kiberege – Morogoro imefanikiwa kutatuliwa. Aidha, Jeshi litaendelea kutekeleza mikakati ya kuwa na hati miliki za maeneo ya Jeshi ambapo katika mwaka 2026/27 Shilingi milioni 900 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia katika maeneo ya Msanga - Dodoma, Liwale - Lindi na Ilemela – Mwanza.

**HUDUMA ZA UANGALIZI WA WAFUNGWA WA VIFUNGO VYA NJE**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa huduma za uangalizi wa wafungwa wa vifungo vya nje katika mikoa yote Tanzania Bara. Kupitia huduma hizo, jumla ya Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii 6,051 ziliwasilishwa mahakamani. Taarifa hizo zimewezesha Mahakama kutoa hukumu kwa wafungwa 4,815 kutumikia adhabu zao kwenye jamii, ambapo wanaume ni 3,848 na wanawake ni 967.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, wafungwa 4,100 wa vifungo vya nje walimaliza kutumikia vifungo vyao ambapo wanaume ni 3,315 na wanawake ni 785. Utekelezaji wa adhabu nje ya Magereza, umeendelea kusaidia kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani na kuiwezesha Serikali kuokoa Shilingi bilioni 14.33

ambazo zingetumika kuwahudumia wafungwa hao endapo wangetumikia kifungo gerezani.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanywa na wafungwa wanaotumikia vifungo nje ya magereza ni usafi wa mazingira, utunzaji wa bustani, kuzibua na kusafisha mitaro ya barabara. Vilevile, wafungwa hao walipanda miti 13,581 ya vivuli na matunda katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kutekeleza kazi hizo, Serikali imeokoa jumla ya Shilingi bilioni 9.6 ambazo zingetumika kuwalipa vibarua.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa adhabu nje ya magereza huenda sambamba na utolewaji wa programu za urekebishaji wa tabia za wafungwa ili kuwawezesha kuachana na vitendo vya uhalifu. Katika kipindi husika wafungwa 4,815 walipewa ushauri nasihi kulingana na mahitaji na changamoto zao binafsi; wafungwa 206 walipewa ujuzi wa ujasiriamali wa biashara ndogondogo ikiwemo mafunzo ya kilimo cha uyoga, upandaji wa majani ya mifugo, uandaaji wa vitalu vya miche ya miti ya vivuli na matunda na wafungwa 1,153 walifundishwa stadi za kazi na maisha.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maelekezo ya Tume ya Rais ya kuangalia jinsi ya kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini, Wizara kwa kushirikiana na taasisi za Haki Jinai imeanza ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Wafungwa wa Vifungo vya Nje (*Non-Custodial Offenders Management Information System - NCO-MIS*). Ujenzi wa mfumo huo umefikia asilimia 85 na unatarajia kukamilika ifikapo Juni 2026. Mfumo huo utakapokamilika utasomana na mifumo ya taasisi nyingine za Haki Jinai ili kurahisisha usimamizi na ufuatiliaji wa wafungwa wa vifungo vya nje.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa elimu kuhusu adhabu ya vifungo vya nje kwa wananchi na wadau wa haki jinai 387,617. Elimu hiyo imetolewa katika mahakama, maonesho mbalimbali ya kitaifa, kupitia vyombo vya habari na vituo vya maegesho ya pikipiki na bajaji katika mikoa 26 ya Tanzania Bara. Kutolewa kwa elimu hiyo kumeleta matokeo chanya katika utekelezaji wa sheria

za vifungo vya nje ikiwa ni pamoja na kueleweka kwa dhana ya adhabu mbadala.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27 Wizara imepanga kutumia Shilingi bilioni 4.97 kwa ajili ya kuwaweka kwenye programu ya vifungo vya nje, kuwasimamia na kuwafuatilia wafungwa 6,500. Pia, itatoa elimu ya utekelezaji wa sheria kwa wadau wa haki jinai, kufanya uchunguzi wa kijamii kwa wahalifu na kuanza kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Wafungwa wa Vifungo vya Nje ya Gereza.

**SHUGHULI ZA SHIRIKA LA MAGEREZA (SHIMA)**

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Magereza linatekeleza majukumu yake ya msingi ya uzalishaji katika shughuli za ujenzi, uchimbaji madini ya ujenzi, viwanda na kilimo kwa lengo la kujiendesha kibiashara na kuchangia katika urekebishaji wa wafungwa waliopo magerezani. Utekelezaji wa shughuli za miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

**Shughuli za Ujenzi**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026, Shirika limekamilisha miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro wenye thamani ya Shilingi bilioni 1.46 na ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) Mkoa wa Iringa wenye thamani ya Shilingi milioni 490.33.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika pia linaendelea na miradi ya ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji katika Mkoa wa Mara kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.76 na Mkoa wa Singida kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.46. Ujenzi wa vituo hivyo unatarajiwa kukamilika Oktoba 2027.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine zinazotekelezwa ni: ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo, Handeni - Tanga wenye thamani ya Shilingi bilioni 2.66 ambao unatarajiwa kukamilika Aprili 2028; na

ujenzi wa jengo la Ofisi ya Manispaa ya Iringa wenye thamani ya Shilingi bilioni 4.30 ambao unatarajiwa kukamilika Aprili 2029.

**Uzalishaji Chokaa Eneo la *Wazo Hill***

**110. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea na uchimbaji wa madini ya mawe ya chokaa na kifusi cha ujenzi katika eneo la Wazo Hill. Hadi kufikia Aprili 2026 jumla ya Shilingi bilioni 2.05 zimekusanywa kutokana na mauzo ya mawe ya chokaa tani 47,725.20 na kifusi cha ujenzi tani 268,017.39. Matarajio ni kufikia Shilingi bilioni 2.50 ifikapo Juni 2026.

**Kampuni Tanzu ya Ulinzi – SHIMA *Guard Company Limited***

**111. *Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026 Shirika la Magereza kupitia kampuni tanzu ya ulinzi (SHIMA Guard Company Limited) limefanikiwa kutoa huduma ya ulinzi kwa taasisi za umma 42 na binafsi 19. Kupitia huduma hiyo, Shirika limetoa ajira kwa vijana wa kitanzania 927 na kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 2.26.

**Viwanda**

**112. *Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea kutekeleza shughuli za uzalishaji katika viwanda vifuatavyo: Kiwanda cha Seremala, Kiwanda cha Ushonaji na Karakana Ukonga – Dar es Salaam; Kiwanda cha Chumvi Lilungu – Mtwara; Kiwanda cha Samani – Arusha; Kiwanda cha Samani Uyui – Tabora; Kiwanda cha Sabuni Ruanda – Mbeya; na Kiwanda cha Maziwa Kingolwira – Morogoro. Hadi kufikia Aprili 2026 Shirika limekusanya mapato ghafi ya Shillingi milioni 808.66 kutokana na mauzo ya bidhaa zinazotengezwa viwandani.

**113. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27 Shirika limetenga Shilingi milioni 650 kwa ajili ya kununua mashine na vitendea kazi kwa matumizi ya viwanda vya Samani vya Arusha, Ukonga – Dar es Salaam na Uyui – Tabora. Aidha, ili kuboresha huduma ya usafiri na usafirishaji Shirika limetenga Shilingi milioni 350 kwa ajili ya kununua magari ya kusafirisha mazao na mizigo.

**Miradi ya Kilimo**

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026, Shirika limevuna jumla ya tani 5,976.04 za mazao yaliyolimwa na kuhudumiwa katika ekari 8,262 zilizopandwa msimu wa mwaka 2024/25 kama ifuatavyo: mahindi tani 3,221.01; mpunga tani 297.83; maharage tani 54.7; ngano tani 9.1; alizeti tani 8.48; miwa tani 2,345.8; na mafuta ya mawese tani 39.12.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya ekari 7,631 zimelimwa mazao yafuatayo: mahindi ekari 4,125; mpunga ekari 899; maharage ekari 153; alizeti ekari 100; miwa ekari 326 na michikichi ekari 2,028. Matarajio ya mavuno ni tani 6,746.52 kwa mchanganuo ufuatao: mahindi tani 3,712.3; mpunga tani 337.12; maharage tani 30.6; alizeti tani 12; miwa tani 2,608 na mafuta ya mawese tani 46.5.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea kuboresha mazingira ya uzalishaji katika miradi ya kilimo kwa kununua zana za kilimo. Hadi kufikia Aprili 2026, Shirika limenunua trekta saba (7) aina ya *New Holland* zenye thamani ya Shilingi milioni 575. Aidha, katika mwaka 2026/27 Shirika linatarajia kulima na kuhudumia jumla ya ekari 8,993. Mazao yatakayolimwa ni kama ifuatavyo: mahindi ekari 5,000; mpunga ekari 1,230; maharage ekari 200; alizeti ekari 155; miwa ekari 350 na kuhudumia michikichi ekari 2,058. Makadirio ya mavuno yanayotarajiwa ni mahindi tani 4,500; mpunga tani 461.25; maharage tani 40; alizeti tani 18.6; miwa tani 3,150 na mafuta ya mawese tani 46.5. Mavuno yanayopatikana kwa ujumla yanasaidia kuimarisha usalama wa chakula magerezani na kuongeza mapato ya Shirika.

**HUDUMA ZA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inatekeleza jukumu la kuokoa maisha na mali katika majanga mbalimbali yanayotishia uhai na mali. Hadi kufikia Aprili 2026 Jeshi limezima moto na kufanya uokoaji katika matukio 4,436 ambapo majeruhi 1,713 waliokolewa. Baadhi ya matukio yaliyoleta madhara makubwa kwa jamii ni: ajali ya mabasi

kugongana kisha kuwaka moto mkoani Kilimanjaro; watu kufukiwa na kifusi cha mgodi wa nyandorwa mkoani Shinyanga; maporomoko ya udongo Mbeya; na moto wa lori la kubeba mafuta Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro. Katika mwaka 2026/27 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi ili kupunguza madhara yatokanayo na moto na majanga mengine.

**Ukaguzi wa Kinga na Tahadhari ya Moto**

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa huduma ya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto na majanga mengine katika maeneo mbalimbali nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Jeshi limefanya ukaguzi katika maeneo 62,100 kati ya maeneo 109,895 ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 12.29 kilikusanywa sawa na asilimia 98.38 ya lengo la kipindi husika. Katika mwaka 2026/27 jumla ya maeneo 110,000 yatakaguliwa na Shilingi bilioni 17 zinatarajiwa kukusanywa.

**Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokoaji**

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo wa usimamizi wa kinga na tahadhari za moto umeendelea kuboreshwa zaidi ili kukidhi mahitaji ya sasa ikiwemo kuwawezesha watoa huduma binafsi za zimamoto na uokoaji kufanya maombi ya usajili na uhuishaji wa hati za umahiri. Hatua hii inalenga kuwaondolea usumbufu wananchi pamoja na kuimarisha kanzidata ya watoa huduma hao. Aidha, mfumo huo umeendelea kuwarahisishia wananchi kuomba huduma ya ukaguzi na tahadhari dhidi ya moto na kuimarisha usalama katika maeneo yao nchi nzima. ***Natumia fursa hii kuwahamasisha wananchi kuendelea kutumia mfumo huo unaopatikana kupitia https://portal.zimamoto.go.tz.***

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi linaendelea na maandalizi ya awali ya utengenezaji wa mfumo wa operesheni utakaogharimu Shilingi milioni 349. Mfumo huo unatarajiwa kukamilika Aprili 2027 na utarahisisha upatikanaji wa taarifa za

miito ya matukio ya moto na majanga mengine kwa haraka pamoja na kusimamia namna ya uendeshaji wa mitambo ya kuzima moto na uokoaji.

**Mitambo, Magari na Vifaa vya Kuzima moto na Uokoaji**

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utoaji wa huduma za zimamoto na uokoaji kwa wananchi, Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imekamilisha mradi wa ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuzima moto na uokoaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imepokea mitambo 150, boti 23 na helikopta moja (1) kwa ajili ya kuzima moto na uokoaji, magari matatu (3) ya kukabiliana na moto wa kemikali, magari matano (5) ya kubeba maji na mitambo miwili (2) ya kuvuta magari mabovu yaliyopata ajali.

***122. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupata vitendea kazi ambavyo vitaongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi.***

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imepokea magari 17 ya shughuli za utawala na ukaguzi na mitambo mitatu (3) ya kuzima moto. Magari 17 yamenunuliwa kupitia fedha za Serikali; mitambo miwili (2) imetolewa na Serikali ya Ujerumani; na mtambo mmoja (1) umetolewa kupitia mradi wa *Rusumo Power Plant*. Pia, Jeshi linaendelea na taratibu za ununuzi wa magari sita (6) ambayo yanatarajiwa kupokelewa Juni 2026. Katika mwaka 2026/27 Shilingi bilioni 1.03 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari matano (5) ya utawala na ukaguzi.

**Ununuzi na Ukarabati wa *Fire Hydrants***

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na uhitaji mkubwa wa *Fire Hydrants* hasa katika ngazi ya Wilaya na Halmashauri, Jeshi kwa kushirikiana na mamlaka za maji linatekeleza mpango wa miaka

mitano ambao ulianza 2025 na unaratajiwa kukamilika 2030 kwa ajili ya kufunga *Fire Hydrants* 4,256 katika ngazi za Wilaya na Halmashauri zitakazowezesha upatikanaji wa maji ya kuzima moto. Hadi kufikia Aprili 2026, Jeshi limepokea *Fire Hydrants* 56 kutoka mamlaka za maji zilizofungwa katika Mikoa 13 nchini. Aidha, katika mwaka 2026/27 Shilingi milioni 600 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa *Fire Hydrants* 272.

**Ujenzi wa Vituo na Makazi ya Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kusogeza huduma za zimamoto na uokoaji karibu na wananchi, Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na uokoaji imeendelea na ukamilishaji wa vituo saba (7). Hadi kufikia Aprili 2026 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekamilisha ujenzi wa vituo viwili (2) vya Zimamoto na Uokoaji katika Mikoa ya Njombe na Simiyu. Pia, umaliziaji wa ujenzi wa vituo vitano (5) vya Zimamoto na Uokoaji unaendelea na umefikia katika hatua zifuatazo; Manyara asilimia 97, Katavi 93, Geita 92, Kagera 95.5 na Songwe 98.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mwishoni mwa mwezi Februari, 2026 Jeshi limepokea Shilingi bilioni 2.46 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji katika Wilaya za Bunda, Gairo, Nzega na Sengerema pamoja na Halmashauri za Chalinze na Mafinga na kufanya ukarabati wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ruvuma. Ujenzi na ukarabati wa vituo hivyo upo katika hatua za awali. Aidha, katika mwaka 2026/27 Shilingi bilioni 10.6 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo saba (7) vya Zimamoto na Uokoaji katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Pwani na Shinyanga.

**127.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha makazi ya maafisa na askari, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea na ujenzi wa nyumba za Makazi ya askari katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia Aprili 2026, ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa yenye uwezo wa kuishi familia 20 za askari katika eneo la Kikombo, Jijini Dodoma umefikia asilimia 70.

**Elimu kwa Umma**

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuweka kipaumbele katika kulinda maisha na mali za wananchi kupitia utoaji wa elimu ya kinga na tahadhari dhidi ya moto na majanga mengine. Hadi kufikia Aprili 2026, elimu hiyo imetolewa katika maeneo 23,327, ikiwemo nyumba za ibada, taasisi za elimu na maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kufikisha elimu kwa wananchi wengi kwa wakati mmoja, vipindi 52 vya runinga na 997 vya redio pamoja na kurasa za mitandao ya kijamii vimetumika kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu kinga na tahadhari za majanga.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** ushirikishwaji wa vijana hususan wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ni nguzo muhimu katika kujenga jamii salama dhidi ya majanga ya moto na majanga mengine. Ushirikishwaji huo unahusisha utoaji wa elimu ya vitendo vya namna ya kutambua hatari za mapema na kuchukua hatua stahiki. Katika kipindi husika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeanzisha klabu za zimamoto 158 na vikundi vya skauti 23 vyenye jumla ya wanachama 17,992 katika shule za msingi na sekondari na kuwapatia mafunzo ya kinga na tahadhari dhidi ya moto na majanga mengine.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2026/27, Serikali imetenga jumla ya Shilingi milioni 669.21 kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma na kuhamasisha wananchi kujiunga na vikundi vya wazimamoto jamii. Hii inaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kujenga jamii yenye uelewa, utayari na uwezo wa kukabiliana na majanga.

**UWEZESHAJI NA UDHIBITI WA UINGIAJI, UKAAJI NA UTOKAJI WA WAGENI NCHINI**

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji inatekeleza jukumu lake la msingi la kuwezesha na kudhibiti uingiaji, ukaazi na utokaji wa wageni nchini kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uhamiaji. Wageni hao huingia nchini kwa

shughuli mbalimbali zikiwemo za uwekezaji, utalii, biashara na kijamii.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya wageni 2,005,209 waliingia nchini ikilinganishwa na wageni 1,839,342 walioingia katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/25. Aidha, wageni 1,762,314 walitoka nchini ikilinganishwa na wageni 1,698,420 waliotoka nchini mwaka 2024/25. Pia, wageni 171 walizuiliwa kuingia nchini kutokana na sababu za kiusalama pamoja na kutokidhi vigezo na sifa zinazowawezesha raia wa kigeni kuingia na kuendelea kuishi nchini.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeendelea kuwezesha na kudhibiti huduma za kiuhamiaji kwa raia wa Tanzania wanaotoka na kuingia nchini kwa shughuli mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya Watanzania 476,190 walitoka nchini na 443,561 walirejea nchini ikilinganishwa na Watanzania 400,434 waliotoka na 376,011 waliorejea katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/25. Aidha, jumla ya Watanzania 229 walizuiwa kutoka nchini kwa kukosa vigezo vya kusafiri nje ya nchi na Watanzania 203 walirejeshwa kutoka mataifa mbalimbali kwa kukiuka sheria za nchi husika ikiwemo uingiaji na ukaazi usiozingatia taratibu zilizowekwa.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeendelea kuratibu maombi ya wageni wanaoomba kuwa raia wa Tanzania na Watanzania wanaokana uraia wao baada ya kupatiwa uraia wa nchi nyingine kwa mujibu wa Sheria ya Uraia, Sura 357 rejeo la mwaka 2023. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026 jumla ya wageni 64 walipewa uraia wa Tanzania na Watanzania 17 waliukana uraia wao na kupata uraia wa Mataifa mengine.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla idadi ya wageni walioingia nchini imeongezeka kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia

Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira bora ya kuwavutia wageni katika sekta za utalii, uwekezaji na huduma za kijamii.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usalama wa mipaka na kuhakikisha wageni wanaoingia nchini wanakidhi vigezo vya kiusalama, Serikali imeboresha mifumo ya usalama katika viwanja vya ndege kwa kusanifu na kufunga mifumo ya *Advance Passengers Information System* (APIS) na *Personal Name Records* (PNR) katika Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere, Kilimanjaro na Abeid Amani Karume pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Mifumo hiyo itawezesha kupatikana kwa taarifa za abiria mapema, kuzichambua na kufanya maamuzi stahiki kwa mujibu wa sheria kabla ya abiria hao kuruhusiwa kuanza safari ya kuja nchini.

**Utoaji wa Vibali vya Ukaazi na Visa kwa Wageni**

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeendelea kutoa vibali vya ukaazi kwa wageni wanaoingia, kuishi na kufanya kazi nchini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya vibali vya ukaazi 20,339 vimetolewa kwa mchanganuo ufuatao: Daraja "A" 2,597; Daraja "B" 14,748; na Daraja "C" 2,994. Vibali 2,040 vimeongezeka ikilinganishwa na vibali 18,299 (Daraja "A" 2,566; Daraja "B" 12,090; na Daraja "C" 3,643) vilivyotolewa kipindi kama hiki mwaka 2024/25.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, jumla ya Hati za Mfuasi 4,739 zilitolewa ikilinganishwa na hati 4,225 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/25. Vilevile, hati za msamaha 580 zilitolewa ikilinganishwa na hati 680 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/25. Aidha, visa 1,002,031 zilitolewa ukilinganisha na visa 908,960 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024/25. Kwa mwaka 2026/27, Idara itaendelea kutoa vibali vya ukaazi na hati nyingine za kuingia nchini kwa wageni wanaokidhi vigezo vya kuwepo nchini.

## Pasipoti na Hati Nyingine za Safari

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya pasipoti 78,583 zilitolewa kwa Watanzania. Kati ya pasipoti hizo 555 zilikuwa za kibalozi, 258 za kiutumishi na 77,770 za kawaida ikilinganishwa na pasipoti 114,448 zilizotolewa kipindi kama hiki mwaka 2024/25. Aidha, hati za safari za dharura 226,400 zilizotolewa ikilinganishwa na hati za safari za dharura 204,387 zilizotolewa 2024/25. Kwa mwaka 2026/27, Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa pasipoti na hati nyingine za safari kwa Raia wa Tanzania ili kuwawezesha kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali.

## Operesheni, Misako, Doria na Ukaguzi

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeendelea kufanya operesheni, misako, doria na ukaguzi katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuwabaini, kuwakamata na kuwadhibiti wahamiaji haramu wanaoingia nchini. Hadi kufikia Aprili 2026 jumla ya watuhumiwa 49,469 wa makosa ya kiuhamiaji walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria, ambapo kati ya hao wahamiaji haramu 34,099 waliondoshwa nchini.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na wahamiaji haramu hususan katika mikoa ya mipakani, Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeanzisha Kanda Maalum za Uhamiaji Mikoa ya Kagera na Kigoma. Lengo la kuanzisha kanda hizi ni kudhibiti wahamiaji haramu kwa kuongeza askari na vitendea kazi katika maeneo hayo. Aidha, Idara itaendelea kufanya misako, doria na kuanzisha kanda nyingine katika maeneo ya kimkakati na yenye mwingiliano mkubwa wa wageni ili kuhakikisha wahamiaji haramu wanadhibitiwa ipasavyo.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Idara ya Uhamiaji imeendelea kutoa elimu ya uhamiaji na uraia kwa wananchi kupitia kampeni ya **"Mjue Jirani yako"** ili kubaini na kuzuia uhamiaji haramu. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya vipindi 1,033 vilifanyika kupitia redio, televisheni, shule na mitandao ya kijamii. Kupitia kampeni hiyo uelewa wa wananchi kuhusu madhara na

athari za kiusalama za wahamiaji haramu umeongezeka na hivyo kuwezesha upatikanaji wa taarifa za wahamiaji hao waliopo katika makazi ya wananchi.

**143.** ***Mheshimiwa Spika*, *napenda kutoa rai kwa Watanzania kuendelea kushirikiana na Idara ya Uhamiaji katika kuwafichua wageni wanaoishi katika maeneo yao kinyume na sheria, kanuni na taratibu za nchi. Kufanya hivyo kutaifanya Tanzania kuendelea kuwa salama.*** **Uboreshaji wa Mfumo wa Uhamiaji Mtandao**

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026 Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imepokea Shilingi bilioni 68.14 kwa ajili ya kuboresha huduma za uhamiaji mtandao. Fedha hizo zimetumika kununua vifaa vya TEHAMA, magari matano (5), malighafi za uchapaji wa pasipoti, ujenzi wa ofisi za wilaya tatu (3) ambazo ni Kahama, Karagwe na Nyasa, vibali vya ukaazi na vituo 23 vya kuingia na kutoka nchini. Katika mwaka 2026/27 Shilingi bilioni 69.94 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi katika wilaya tisa (9); ununuzi wa magari 50; na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya ofisi za uhamiaji 46 zilizopo katika Balozi za Tanzania nje ya nchi ikiwa ni sehemu ya kuboresha mfumo huo.

**Vitendea Kazi, Majengo ya Ofisi na Makazi ya Askari wa Uhamiaji**

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026 Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imepokea jumla ya Shilingi bilioni 5.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miradi hiyo ni ununuzi wa magari 11 na pikipiki 90, ujenzi wa ofisi ya uhamiaji Mkoa wa Songwe ambao umefikia asilimia 28; ujenzi wa ofisi ya uhamiaji Mkoa wa Simiyu upo katika hatua za awali, ujenzi wa nyumba za makazi ya maafisa na askari katika eneo la Msalato Jijini Dodoma umefikia asilimia 5; ujenzi wa Chuo cha Uhamiaji Raphael Kubaga umefikia asilimia 70; na ukarabati wa Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda Tanzania – TRITA umefikia asilimia 75. Aidha, mradi wa ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Dodoma kupitia programu ya Serikali kuhamia Dodoma umefikia asilimia 85 ya utekelezaji wake.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27 Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imetenga jumla ya Shilingi bilioni 29.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo: ununuzi wa magari 47; kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji mikoa ya Songwe na Simiyu na kuanza ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Njombe; ujenzi wa nyumba za makazi ya maafisa na askari Msalato, Dodoma na Raphael Kubaga; na ununuzi wa majengo ya (National Social Security Fund – NSSF) Moshi - Kilimanjaro na nyumba za makazi ya (National Housing Cooperation – NHC) Mkinga Tanga.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Singida; Ofisi ya Uhamiaji Kurasini; nyumba za makazi Mkoa wa Tanga; nyumba za makazi katika vituo vya uhamiaji vya Manyovu, Namanga na Holili; kiwanda cha uchapaji nyaraka Kijichi; na Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda Tanzania.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** ipo pia miradi inayotekelezwa na Ofisi ya Uhamiaji Zanzibar ikiwemo ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi ambao umefikia asilimia 98; ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Uhamiaji Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja kwa awamu ya kwanza ukijumuisha jengo moja la madarasa na mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 620 ambao umefikia asilimia 96; na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Kusini Unguja – Paje ambao umefikia asilimia 45. Aidha, mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Kati – Dunga umekamilika na kuanza kutumika.

**USAJILI NA UTAMBUZI WA WATU NCHINI**

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - NIDA imeendelea kufanya usajili na utambuzi wa watu nchini ikiwemo raia wa Tanzania, wageni wakaazi, walowezi na wakimbizi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 NIDA imesajili na kutambua watu 1,145,334 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea ikilinganishwa na watu 844,994 waliosajiliwa na kutambuliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/25. Hivyo, kufanya jumla ya watu waliosajiliwa na

kutambuliwa kuwa 27,186,421 sawa na asilimia 86.4 ya lengo la kusajili watu 31,477,938 kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza wigo wa huduma ya usajili na utambuzi NIDA imesajili Watanzania 156 waishio nje ya nchi katika Balozi za Tanzania nchini Canada, Marekani, Uingereza na Umoja wa Falme za Kiarabu hivyo kufanya jumla ya Watanzania 1,465 wanaoishi nje ya nchi kupatiwa huduma ya usajili na utambuzi kuanzia mwaka 2023.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 watu 857,244 wamepatiwa Namba za Utambulisho wa Taifa – NIN ikilinganishwa na watu 757,189 waliopatiwa Namba za Utambulisho katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/25. Hivyo, kufanya jumla ya watu 22,654,206 waliopata Namba za Utambulisho wa Taifa. Namba hizo zinawawezesha wananchi kutambulika wakati wa kupata huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika taasisi za umma na binafsi. ***Nitumie nafasi hii kuwahimiza waajiri wote nchini kuhakikisha kuwa waajiriwa wao wanahakikiwa kwa kutumia NIDA ili kujiridhisha kuhusu uraia wao pamoja na taarifa nyingine za utambuzi na hivyo kuendelea kuimarisha usalama wa Taifa letu.***

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika vitambulisho 232,535 vimechapishwa na kusambazwa katika ofisi za usajili za wilaya za NIDA na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyochapishwa na kusambazwa kuwa 21,563,057. Aidha, jumla ya vitambulisho 275,682 vimegawiwa kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyogawiwa kuwa 20,894,235.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Serikali kusogeza huduma za ugawaji wa vitambulisho karibu na wananchi, na kuanzisha huduma ya kutuma ujumbe mfupi kwa wananchi ambao vitambulisho vyao vimechapishwa kuwataka kufika katika ofisi za wilaya walizojisajili na kuvichukua, bado kuna vitambulisho 668,822 katika ofisi za wilaya za NIDA ambavyo havijachukuliwa. ***Hivyo natoa wito kwa wananchi wote waliopewa taarifa ya kuchukua vitambulisho vyao kujitokeza kwenda kuvichukua kwa kuwa***

***vitambulisho hivyo vitawawezesha kupata utambulisho rasmi katika kupata huduma mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kiusalama ikiwemo Bima ya Afya, Ruzuku za Pembejeo za Kilimo, Ruzuku ya Wanufaika wa Mfuko wa TASAF na mikopo inayotolewa na Serikali na Sekta Binafsi pamoja na kutumia kitambulisho kama nyaraka ya kusafiria.***

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA imeanzisha namba maalum ya kutuma ujumbe mfupi bila malipo (sms) ambayo ni 15274. Namba hiyo itamuwezesha mwananchi kufuatilia hatua ya maombi ya kitambulisho cha Taifa ilipofikia pamoja na kupata namba yake ya utambulisho bila kulazimika kufika katika ofisi za NIDA. ***Nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao kutumia namba 15274 kupitia simu zao za mkononi kufuatilia maombi ya Vitambulisho vya Taifa.***

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha NIDA inakuwa na kanzidata yenye taarifa sahihi za watu, Serikali imetoa kibali maalumu cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Oktoba 2025 hadi Septemba 2026 cha kuruhusu wananchi waliotoa taarifa zisizo sahihi wakati wa usajili, kufanya mabadiliko ya taarifa hizo na kutoa taarifa sahihi. Hadi kufikia Aprili 2026 NIDA imepokea na kufanyia kazi maombi ya mabadiliko ya taarifa kutoka kwa wananchi 873. ***Hivyo, nitoe rai kwa wananchi wenye changamoto ya taarifa zao katika mfumo wa NIDA kutumia fursa iliyotolewa ya kufanya maboresho ya taarifa zao na kuhakikisha taarifa wanazotoa ni sahihi.***

**Upatikanaji wa Vitendea Kazi**

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha utendaji kazi wa NIDA kwa kununua magari 20, kompyuta 397, *scanner* 159, *printer* 116 na *UPS* 364 ambavyo vimesambazwa katika Ofisi zote za usajili nchini. Vitendea kazi hivyo vimeongeza kasi ya usajili na utambuzi ambapo jumla ya watu 1,145,334 wamesajiliwa, kuchakata taarifa na kutoa namba za utambulisho wa Taifa kwa wananchi waliokamilisha taratibu za usajili na utambuzi.

**Uunganishaji wa Mfumo wa NIDA na Mifumo ya Taasisi nyingine**

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA inaendelea kutekeleza maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha mifumo ya taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi inasomana. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, NIDA imeunganisha taasisi 17 na Mfumo wa Usajili na Utambuzi na kufanya jumla ya taasisi 147 (Taasisi za Umma 66 na binafsi 81) zilizounganishwa na mfumo huo.

**Kazi zitakazotekelezwa katika Mwaka 2026/27**

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara kupitia NIDA itaendelea kusajili na kutambua watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea na kuwapatia Vitambulisho vya Taifa. Aidha, NIDA inatarajia kuanza kufanya usajili wa watoto kuanzia umri wa kuzaliwa ili kutoa namba ya utambulisho ya kipekee ambayo itajulikana kama JAMII NAMBA. Namba hiyo itatumika katika kupatiwa huduma mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kiusalama tangu mtu anapozaliwa hadi mwisho wa maisha yake.

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, NIDA itaanza ujenzi wa ofisi 31 za usajili za Wilaya Tanzania Bara na Zanzibar, Ofisi ya Makao Makuu Dodoma na Kituo cha mafunzo na matengenezo ya vifaa vya TEHAMA Kibaha. Kazi ya usanifu wa mradi imekamilika na taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea.

**160.** ***Mheshimiwa Spika***, NIDA itaendelea kuboresha Mfumo wa Usajili na Utambuzi kwa kuongeza njia ya alama ya kibaiolojia inayotumia umbile la uso na mboni za macho (Facial and Iris Recognition System). Mfumo huo utawezesha utambuzi wa kibaiolojia kwa wasiokuwa na alama za vidole na kuwezesha kuwatambua kwa usahihi watu wenye umri chini ya miaka 18.

**161.** ***Mheshimiwa Spika***, NIDA inatarajia kuwezesha kadi ya Kitambulisho cha Taifa kubeba taarifa za utambulisho wa mtu zilizopo katika vitambulisho vingine ikiwemo bima ya afya, hati ya kusafiria katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, leseni ya

udereva na hivyo kupunguza wingi wa vitambulisho kwa mwananchi.

**162. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, NIDA inatarajia kuboresha teknolojia ya uchapishaji vitambulisho kutoka teknolojia ya *Drop-on-Demand (DoD)* ambayo inatumika sasa na kwenda katika teknolojia ya kisasa ya *Laser Engraving* inayotumia mionzi (laser) katika kuchapisha vitambulisho. Hatua hiyo, itawezesha kuongeza ubora wa Vitambulisho vya Taifa, kuifanya kadi kuwa salama dhidi ya uharibifu au kughushi, kuiwezesha kadi hiyo kusomwa na mtu mwenye mahitaji maalum kupitia alama za mguso pamoja na kuwezesha kitambulisho kutumika kwa muda mrefu.

**163. *Mheshimiwa Spika,*** pia, NIDA itaendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa usajili na utambuzi pamoja na matumizi ya Vitambulisho vya Taifa. Elimu hiyo itaongeza uelewa na mwitikio wa watu katika kusajiliwa na kutambuliwa na hivyo kunufaika na huduma mbalimbali zinazotolewa kwa kutumia Kitambulisho cha Taifa.

**164. *Mheshimiwa Spika*,** utekelezaji wa kazi hizo unatarajia kugharimu jumla ya Shilingi bilioni 132.26. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 96.37 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 35.89 ni fedha za nje ambazo ni mkopo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini.

**HUDUMA KWA WAKIMBIZI**

**165. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwapokea, kuwasajili na kuwapatia hifadhi, ulinzi na usalama waomba hifadhi na wakimbizi na kuhakikisha wanapatiwa huduma zote za kibinadamu pamoja na kuwatafutia suluhisho la kudumu kwa njia ya urejeaji wa hiari au kuhamishiwa nchi ya tatu.

**166. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 waomba hifadhi wapya 1,214 walipokelewa na kusajiliwa. Waomba hifadhi hao walitoka mataifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Sudan, Sudan ya Kusini, Kenya, Ethiopia,

Eritrea, Uganda, Misri, Syria, Afghanistan, Pakistani, Ukraine na Yemen.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026, nchi yetu ilikuwa inahifadhi jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi 158,954 ambapo kati yao, 70,952 ni wenye asili ya Burundi, 87,303 wana asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na 699 kutoka mataifa mengine mchanganyiko.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) pamoja na wadau wengine muhimu, imetekeleza na kukamilisha zoezi la mahojiano ya kina na wakimbizi wenye asili ya Burundi waliopo katika kambi zote na makazi (Comprehensive Protection and Solution Based Assessment) ambapo mkimbizi mmoja mmoja alipata fursa ya kusikilizwa sababu zake zinazomzuia kurejea Burundi ili kuweza kuwatafutia suluhisho la kudumu. Matokeo ya zoezi hilo yalibainisha kuwa, zaidi ya asilimia 95 ya wakimbizi wa kutoka Burundi hawakuwa na sababu za msingi za kuendelea kupewa hifadhi ya kimataifa, kwa kuwa nchi hiyo sasa ina amani na utulivu wa kisiasa unaowezesha urejeaji salama na wa kuzingatia utu.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi hilo lilifuatiwa na Mkutano wa Pande Tatu baina ya Serikali ya Tanzania, Serikali ya Burundi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) uliofanyika tarehe 26 - 28 Novemba 2025 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulithibitisha kuwa wakimbizi wa Burundi hawana sababu ya kuendelea kuwepo nchini kwa kuwa nchi yao ni salama, hivyo kuweka makubaliano kuwa wakimbizi hao wawe wamerejea nchini kwao ifikapo mwishoni mwa Juni 2026.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2026 jumla ya wakimbizi 76,403 walirejeshwa nchini Burundi kwa hiari yao na hivyo kupelekea kufungwa kwa Kambi ya Wakimbizi ya Nduta iliyopo wilayani Kibondo, mkoani Kigoma. Vilevile, wakimbizi 561 walihamishiwa nchi za Australia (149), Canada (187), Sweden (205), Ufaransa (15) na Uingereza watano (5).

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa Wizara inakabiliwa na changamoto kubwa ya kifedha katika eneo la hifadhi ya ukimbizi, kutokana na kupungua kwa rasilimali zinazotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR). Kupungua huku kumeathiri kwa kiwango kikubwa utoaji wa huduma kwa wakimbizi pamoja na usimamizi na uratibu wa shughuli za hifadhi ya ukimbizi. Mathalani, tangu Juni 2025, Shirika la UNHCR lilisitisha kutoka malipo ya posho kwa Maafisa na Askari wa Jeshi la Polisi wanaohudumu katika kambi za wakimbizi, jambo lililosababisha Serikali kubeba gharama hizo kwa asilimia 100 na hivyo kuiongezea mzigo wa kifedha kwa Serikali.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara imetenga Shilingi bilioni 3.62 kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa masuala ya wakimbizi nchini zikiwemo: kupokea na kusajili wakimbizi na waomba hifadhi; kujadili maombi ya hifadhi; na kusimamia, kuratibu na kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo ambayo wakimbizi wamepangiwa kuishi.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, fedha hizo zitatumika kusimamia utoaji wa huduma zote muhimu ndani ya kambi; kuwatafutia wakimbizi suluhisho la kudumu kwa njia ya urejeaji; kufuatilia wakimbizi waliojipenyeza na kuishi nje ya kambi za wakimbizi pasipo kibali maalum; na kuhakikisha shughuli za urejeshaji mazingira zinatekelezwa katika maeneo yanayozunguka kambi.

**USAJILI WA JUMUIYA ZA KIRAIA**

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusajili na kufuatilia utendaji wa Jumuiya za Kiraia ili kudumisha amani na usalama nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya Jumuiya za Kiraia 126 zimesajiliwa, ambapo 12 ni jumuiya za kidini na 114 zisizo za kidini. Pia, ukaguzi wa Jumuiya za Kiraia 350 umefanyika katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Ruvuma na Songwe. Lengo la ukaguzi huo ni kufuatilia utekelezaji wa masharti ya usajili pamoja na kubaini mchango wa jumuiya hizo katika maendeleo ya Taifa.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia Wizara imetoa elimu kwa umma kuhusu aina za taasisi, vyama na vikundi vinavyopaswa kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337. Elimu hiyo ilitolewa kwa wajumbe 36 wa Kamati za Usalama za Wilaya ya Mbeya Mjini, Momba na Songea kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kusimamia na kubaini viashiria hatarishi vya usalama katika uendeshaji wa jumuiya. Aidha, viongozi 308 wa jumuiya za kidini katika wilaya hizo walipewa semina ya kuwajengea uwezo wa kuongoza na kusimamia uendeshaji wa jumuiya zao kwa kuzingatia miongozo ya kisheria, katiba zao na masharti ya usajili.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanzisha programu za ushirikishwaji ili kuimarisha uelewa na uwajibikaji wa viongozi wa jumuiya za kiraia katika uendeshaji wa jumuiya zao. Kupitia programu hiyo, jumla ya viongozi wa jumuiya za kidini na zisizo za kidini 2,500 walipatiwa mafunzo kuhusu uendeshaji wa jumuiya unaozingatia sheria. Aidha, viongozi hao walikumbushwa umuhimu wa kudumisha na kuimarisha amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa.

**Ushirikiano na Jumuiya za Kiraia katika Kuhamasisha Amani, Utulivu na Umoja wa Kitaifa**

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kiraia imeendelea kuhamasisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa kwa kushirikiana na Jumuiya na Taasisi za kidini na zisizo za kidini nchini. Katika mwaka 2025/26 Wizara imeendesha semina na kufanya vikao na viongozi wa Jumuiya na Taasisi za kidini na zisizo za kidini katika mikoa na wilaya mbalimbali. Aidha, jumla ya vikao na semina 26 zimefanyika kwa lengo la kujengeana uwezo na kuwakumbusha wajibu wa viongozi wa jumuiya za kiraia katika kudumisha amani, utulivu na kujenga umoja wa kitaifa.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa nyakati tofauti Wizara imeshirikiana na Jumuiya na Taasisi za Kidini katika shughuli mbalimbali kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Jumuiya za kidini, ambazo kwa muda mrefu zimekuwa ni wadau wakubwa wa maendeleo nchini. Jumuiya na Taasisi hizo ni kutoka Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza Kuu la Waislamu

Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), Kanisa la Waadventista Wasabato Tanzania na *Hindu Council of Tanzania* na Jumuiya nyingine zilizosajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: kusajili na kuhakiki jumuiya za kiraia; kufanya ukaguzi wa jumuiya zilizosajiliwa; kutoa elimu juu ya umuhimu wa usajili wa vyama na vikundi vya kiraia; kuboresha vitendea kazi; kufanya tathmini ya vihatarishi vya kiusalama na kushiriki katika maonesho ya kitaifa. Jumla ya Shilingi bilioni 1.57 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

**KUZUIA NA KUPAMBANA NA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU**

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kukabiliana na usafirishaji haramu wa binadamu nchini ikiwemo kuendesha operesheni za kuwaokoa waathirika na kuwakamata wahusika wa uhalifu huo. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, jumla ya waathirika 160 waliokolewa na kusaidiwa. Kati ya waathirika hao, 60 ni watoto, 96 ni wanawake na wanne (4) ni wanaume. Aidha, waathirika 126 waliokolewa nchini na waathirika 34 waliokolewa kutoka nchi za Bahrain (1), India (2), Malaysia (8), Misri (1), Oman (19), Syria (1) na Umoja wa Falme za Kiarabu (2).

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika kipindi husika watuhumiwa 57 walikamatwa. Kati ya hao, watuhumiwa 45 walifikishwa mahakamani na kesi zao zinaendelea kusikilizwa katika Mikoa ya Dar es Salaam (14), Dodoma mmoja (1), Iringa (3), Kagera (2), Kilimanjaro (1), Lindi (1), Manyara (4), Mara (6), Morogoro (2), Mwanza (1), Ruvuma (1), Simiyu (1), Singida (3) na Songwe (5) na uchunguzi wa watuhumiwa 12 unaendelea.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa wadau wa haki jinai kwa kutoa mafunzo maalum ya kupambana na uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu. Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wadau hao wa kuwatambua

waathirika, kutoa huduma stahiki, kufanya upelelezi na kuendesha mashtaka kwa ufanisi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya wadau 314 walipatiwa mafunzo hayo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Kagera, Mwanza na Singida.

**183. *Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Wizara imeongeza juhudi za utoaji elimu ya kukabiliana na usafirishaji haramu wa binadamu kwa jamii kupitia njia mbalimbali. Elimu hiyo ilitolewa kupitia mitandao ya kijamii, vipindi vya redio na televisheni, makongamano, semina, mikutano na maonesho ambapo jumla ya wananchi 19,076 walifikiwa.

**184. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mifumo ya upokeaji wa taarifa, Wizara imeanzisha Kituo cha Kupokea Taarifa za Uhalifu wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu (Counter Trafficking in Persons Call Centre), ambapo wananchi wanaweza kutoa taarifa za dharura na kupata elimu kwa kupiga simu bure kupitia namba 195. Kwa sasa Wizara inaendelea kuitangaza namba hiyo ili iweze kufahamika kwa wananchi wengi na kuongeza ushiriki wa jamii katika mapambano dhidi ya uhalifu huu. ***Napenda kutoa rai kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa na kupata elimu kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu kupitia namba 195.***

**185. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mapambano dhidi ya uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu, Wizara imeanzisha Ofisi ya Kanda ya Dar es Salaam itakayohudumia mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mtwara, Pwani na Tanga. Vilevile, Wizara imepokea Shilingi milioni 72.47 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kupokea, Kusimamia na Kuhifadhi Taarifa za Usafirishaji Haramu wa Binadamu (TIPMIS). Ujenzi wa mfumo huo umefikia asilimia 50 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2026.

**186. *Mheshimiwa Spika,*** pia kiasi cha Shilingi milioni 250.45 kimepokelewa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba salama moja (1) katika mkoa wa Dodoma kwa ajili ya kutoa hifadhi ya muda kwa waathirika na mashahidi wa uhalifu wa

usafirishaji haramu wa binadamu. Ujenzi huo umefikia asilimia 60 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba 2026.

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/27 Wizara imetenga Shilingi bilioni 2.76 kwa ajili ya kujenga nyumba salama moja (1) katika mkoa wa Dar es Salaam, kuandaa mpango mkakati wa kitaifa wa kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu na kuendelea kufanya uchunguzi na operesheni za kusambaratisha mitandao inayojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu. Vilevile, fedha hizo zitatumika kuwaokoa, kuwasaidia na kuwaunganisha waathirika na familia zao, kutoa mafunzo kwa wadau na elimu kwa umma na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika kupambana na uhalifu huo.

## D. SHUKRANI

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru Mhe. Ayoub Mohammed Mahmoud, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge wa Jimbo la Chaani Mkoa wa Kaskazini Unguja; Ndugu Ally Senga Gugu, Katibu Mkuu; na Dkt. Maduhu Isaac Kazi, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wao wanaonipatia katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Wizara.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nawapongeza Wakuu wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara kwa kuendelea kuhakikisha nchi inakuwa na amani na utulivu, hivyo kuweka mazingira rafiki kwa wananchi na wageni kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Viongozi hao ni: Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Camillus Mongoso Wambura; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Jeremiah Yoram Katungu; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John William Masunga; na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Peter Makakala. Pia, shukrani hizo nazitoa kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Ndugu James Wilbert Kaji.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru Mhe. Jaji Stephen M. Magoiga - Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Huduma kwa Jamii,

Mhe. Balozi Khamis Kagasheki ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Parole, IGP Mstaafu Balozi Ernest J. Mangu - Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Ndugu Omari Issa - Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi na Meja Jenerali Mstaafu Hamisi R. Semfuko Mwenyekiti Mstaafu wa Bodi ya Shirika la Magereza kwa uongozi wao mahiri katika kusimamia kamati na bodi hizo. Uongozi wao umeongeza ufanisi katika Wizara. Pia, napenda kutambua michango ya wajumbe wote wa Kamati na Bodi hizo ambayo imeongeza ufanisi katika kuimarisha utendaji wake.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kuwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakiwemo Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Makamishna, Naibu Makamishna, Wakuu wa Vitengo, Maafisa, Wakaguzi na Askari kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi. Jitihada zao zimechangia kuleta tija katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2025/26.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inazishukuru jumuiya za kikanda na nchi mbalimbali zikiwemo: Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); pamoja na nchi za Brazil, Burundi, DRC, India, Indonesia, Jamhuri ya Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Kenya, Misri, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Uganda, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Urusi, Uturuki na Zimbabwe kwa ushirikiano wao katika masuala mbalimbali kwenye nyanja za ulinzi na usalama.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninayashukuru mashirika na taasisi za Kitaifa na Kimataifa zifuatazo: FSDT, GIZ, IOM, UNDP, UNHCR, UNICEF, World Bank, WFP, CAMARTEC, Chuo cha Uhasibu – Arusha, Chuo cha Ustawi wa Jamii – Dar es Salaam, NACTVET, PUMA Energy, REA, RUSUMO Power Company LTD, STAMICO, Taifa Gas, TPA, VETA, Benki za CRDB na NMB kwa kuunga mkono Serikali katika shughuli za kuimarisha amani na utulivu nchini.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninazishukuru Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na vyombo vya habari kwa kushirikiana na Wizara katika kuendeleza juhudi za

kukuza amani na utulivu nchini. Pia, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wote kwa moyo wa uzalendo, mshikamano na ushiriki wao katika kulinda na kuendeleza amani na utulivu katika maeneo yao.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee na kwa moyo wa dhati naishukuru familia yangu wakiwemo wazazi wangu Dr. Katambi P. Kwiligwa na Mrs. Specioza Katambi, Mke wangu Violeth Shoo Katambi na watoto wangu Ernestina, Prais'eve, Michelle na JohnDenzel kwa kunipa ushirikiano unaoniwezesha kutekeleza vema majukumu ya Wizara. Pia, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Shinyanga Mjini kwa upendo wao, kunichagua na kwa kushirikiana nami kwa maendeleo ya Jimbo letu. Aidha, nashukuru Chama cha Mapinduzi (CCM) na Viongozi wake wote kwa kuniamini.

## E. HITIMISHO

### Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/27

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2026/27 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 499,090,000,000** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itaendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki na ununuzi wa vitendea kazi vya kisasa.

### Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/27

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima, naomba sasa Bunge lako liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 2,443,215,927,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2026/27. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shilingi 1,953,366,486,000** sawa na **asilimia 80** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,183,766,640,000** ni Mishahara na **Shilingi 769,599,846,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

**(ii)Shilingi 489,849,441,000** sawa na **asilimia 20** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 453,955,843,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 35,893,598,000** ni fedha za nje.

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba ya Wizara yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Nina tangazo la wageni, mgeni wa Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ni Kamishna Kombo Khamis Kombo ambaye ni Kamishna wa Polisi upande wa Zanzibar. Ahsante sana na karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo: -

Tuna Ndugu Ali Khamis ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kaskazini *B*. Ahsante sana, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Ali Maulid Khamis, Mwenyekiti Baraza la Vijana Wilaya ya Kaskazini A. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Fomu Maanzi Fomu, Mwenyekiti wa CCM Jimbo la Chaani, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna Mheshimiwa Nyange Kheri Ali ambaye ni Mstahiki Meya Manispaa ya Kaskazini *A*, ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Soud Hamza Ame, Mwenyekiti Baraza la Mji Kaskazini B, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Sasa nimwite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama awasilishe Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Paschal Chinyele.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu liweze kuipokea taarifa hii, kuikubali na kuidhinisha bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa kifungu cha 6(3) na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja, zimeweka masharti yanayohusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masharti hayo, Kamati ilitekeleza jukumu la uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na makadirio ya mapato

na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kupata maudhui ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na uchambuzi huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge yanayohusu kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kazi hiyo, ilifanyika kati ya tarehe 11 na 18 Machi, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ulitumia matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawanda ya taarifa ya uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara yanategemea muundo na majukumu ya Wizara inayohusika. Kwa kuzingatia majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi uchambuzi uliofanywa na Kamati umejumuisha mafungu matano ya kibajeti ambayo ni: -

(i) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
(ii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi;
(iii) Fungu 29 - Jeshi la Magereza;
(iv) Fungu 51 - Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*); na
(v) Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia Kanuni ya 145(a) hadi (c) ya Kanuni za Bunge, 2025 kuhusu Muundo wa Taarifa ya Kamati ya Bunge inayoingia Bungeni. Kwa msingi huo, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inayohusu maelezo ya utangulizi na kubainisha msingi, mawanda na muundo wa taarifa;

(b) Sehemu ya Pili inayobainisha uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(c) Sehemu ya Tatu ambayo inayohusu uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na

(d) Sehemu ya Nne inayoeleza Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi pamoja na kuhitimisha taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu utangulizi wa taarifa yanapatikana katika ukurasa wa 1 hadi wa 4 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mwaka wa fedha 2025/2026; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mafungu yote matano ambao umezingatia mambo muhimu yaliyobainika katika utekelezaji wa bajeti inayoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi ulihusu mambo yafuatayo: -

(i) Hali ya utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge;

(iii) Uchambuzi wa hali ya ukusanyaji wa mapato; na

(iv) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mambo hayo muhimu kwa Bunge utasaidia katika kujua namna Serikali ilivyotekeleza bajeti kama ilivyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, Bunge litakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya

kujadili na kushauri kuhusu hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 2025/2026; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, Kamati ilitembelea na kukagua miradi minne katika Mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro na Morogoro inayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Miradi iliyokaguliwa ni ile inayotekelezwa na Fungu 28 - Jeshi la Polisi, Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji, Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Fungu 29 - Jeshi la Magereza. Lengo la ukaguzi huo ni kuliwezesha Bunge kuelewa hali ya utekelezaji na upatikanaji wa fedha kama zilivyoidhinishwa na hivyo kuweza kutoa ushauri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi Na. 6339 – Ukarabati wa Majengo ya Chuo cha Uhamiaji, Mkoani Kilimanjaro; mradi huu unahusu ukarabati wa majengo ya utawala *(Administration Block)* katika Chuo cha Uhamiaji *(TRITA)* Mkoani Kilimanjaro na unatekelezwa kwa utaratibu wa *force account*. Kamati ilielezwa kuwa mradi huu ulioanza kutekelezwa tarehe 20 Oktoba, 2025 ulitengewa shilingi 240,000,000 na ulitarajiwa kukamilika Aprili, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi wakati Kamati inakagua mradi huu, kiasi cha shilingi 239,820,000 sawa na 99.9% ya fedha iliyotengwa kilikuwa kimepokelewa na utekelezaji wake ulikuwa umefikia 60%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi Na. 6582 - Ujenzi na Maboresho ya Shule ya Polisi, Kilimanjaro; mradi huu unaohusu maboresho ya Shule ya Polisi Tanzania, Mkaoni Kilimanjaro ulianza kutekelezwa mwaka 2024 kwa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Jumla ya shilingi 25,000,000,000 zilitengwa kwa ajili ya mradi huu ili kugharamia ujenzi wa mabweni ya wanafunzi, nyumba za walimu, madarasa na kumbi za kufundishia *(lecture halls)*. Hadi wakati Kamati inatembelea na kukagua mradi huu, kiasi cha shilingi 23,000,000,000 kilikuwa kimepokelewa katika awamu nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao ukikamilika utaongeza uwezo wa shule kuhudumia askari na wanafunzi. Mabweni ya wanaume yatakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,458 ikilinganishwa na wanafunzi 490 kwa majengo ya zamani, hii ni sawa na ongezeko la 197.6%. Aidha, mabweni ya wanawake yatakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,412 ikilinganishwa na wanafunzi 490 kwa majengo ya zamani, hii ni sawa na ongezeko la 188%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi Na. 6582 - Ukarabati wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji, Mkoani Morogoro; mradi huu unahusu ukarabati wa majengo ya Ofisi za Zimamoto, Mkoani Morogoro ambayo yalikuwa na zaidi ya miaka 50 bila kufanyiwa ukarabati. Utekelezaji wa mradi ulianza Juni, 2025 na ulipangwa kukamilika Aprili, 2026 kwa gharama ya shilingi 300,000,000. Hadi wakati wa ukaguzi wa Kamati, kiasi cha shilingi 299,976,000 sawa na 99% kilikuwa kimepokelewa na mradi unatekelezwa kwa utaratibu wa *force account* ukiwa umefikia 97.5%. Hivyo, Kamati ina maoni kwamba Wizara iharakishe mchakato wa upatikanaji wa samani katika kituo hicho ili maboresho yalioyofanyika yaweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi Na. 6305 - Ujenzi wa Magereza Msalato, Dodoma; utekelezaji wake ulianza Machi, 2025 kwa lengo la kuwezesha kuwa na gereza la kisasa lenye miundombinu wezeshi kwa shughuli za urekebishaji wafungwa. Mradi huu unaotekelezwa kwa awamu unakadiriwa kugharimu shilingi 20,121,846,709.43 na kukamilika kwake kutawezesha gereza kuongeza idadi ya wafungwa na mahabusu wanaohudumiwa. Aidha, gereza litawezesha mahabusu na wafungwa kufuatilia uendeshaji wa kesi kwa njia ya mtandao kutokana na mifumo ya TEHAMA itakayosimikwa katika mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 mradi ulitengewa shilingi 1,000,000,000 ambazo hadi wakati Kamati inafanya ukaguzi zilikua hazijatolewa. Hivyo, Jeshi la Magereza kutumia shilingi 83,000,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani ili kutekeleza sehemu ya mradi katika mwaka huu wa

fedha. Maelezo zaidi kuhusu ukaguzi wa miradi yanapatikana katika ukurasa wa 6 hadi 12 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya uzingatiaji wa maoni na ushauri; wakati wa kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo ambayo iliona yanatakiwa kufanyiwa kazi na kuongezewa nguvu katika utekelezaji wake. Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kutolewa ufafanuzi zilionesha kuwa Serikali imezingatia na inaendelea kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Maelezo zaidi kuhusu ufafanunuzi huo yanaonekana katika Kiambatisho Na. 1 cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa hali ya ukusanyaji wa mapato (maduhuli); uchambuzi wa hali ya ukusanyaji wa mapato umezingatia ulinganisho wa namna zifuatazo: -

(i) Ulinganisho wa hali ya ukusanyaji wa mapato kati ya kipindi cha Februari, 2025 na Februari, 2026;

(ii) Ulinganisho wa kiasi kilichokusanywa na makadirio kwa kila fungu kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 01; na

(iii) Ulinganisho wa mchango wa kinachokusanywa na mchango wa kiasi kilichokadiriwa kwa kila fungu kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 02.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo: -

(i) Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ikijumuisha mafungu yake yote matano ilikadiriwa kukusanya shilingi 517,000,000,000.00, na kiasi cha makusanyo hadi Februari, 2026 kilikuwa shilingi 345,758,373,950.00 sawa na 67% ya lengo la mwaka;

(ii) Makusanyo ya Jeshi la Polisi ikilinganishwa na makadirio yalifikia 70.6%, Jeshi la Magereza 72%, Idara ya Uhamiaji 66% na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 65%;

(iii) Makusanyo ya Wizara Makao Makuu yalifikia 42% na *NIDA* yalikuwa ni 67.2% ya lengo la makusanyo kwa mwaka; na

(iv) Makusanyo ya jumla kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hadi mwezi Februari, 2026 yalifikia 67%, kiwango ambacho ni cha kuridhisha kwani ndicho kilichotarajiwa kufikiwa katika kipindi hicho. Hata hivyo, Fungu 51 - Wizara Makao Makuu lilikuwa limekusanya kwa 42%, kiwango ambacho ni cha chini ikilinganishwa na lengo tarajiwa katika kipindi cha hadi Februari, 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli ni kama yanavyoonekana kwenye ukurasa wa 12 hadi wa 16 wa taarifa kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; Kamati ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa kuangalia kiwango cha fedha kilichopatikana ikilinganishwa na bajeti iliyopitishwa na Bunge na uwiano wa bajeti kwa mafungu yote matano ya Wizara kama ilivyopitishwa na Bunge ikilinganishwa na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa mafungu hayo kama ifuatavyo: -

(i) Kiwango cha matumizi kilichoidhinishwa na Bunge kwa kila fungu ikilinganishwa na fedha iliyopatikana kwa kila fungu kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 03;

(ii) Uwiano wa matumizi kwa kila fungu kama ilivyoidhinishwa na uwiano wa fedha zilizopatikana kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 04; na

(iii) Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge na kiasi cha fedha kilichopatikana kwa mafungu yote kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 05.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinganishaji unasaidia kuweka ulinganisho wa upatikanaji wa fedha na kubaini maeneo ambayo mwenendo wake si wa kuridhisha na upo chini ya wastani. Uchambuzi umebaini yafuatayo: -

(i) Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara hadi Februari, 2026 ni 80% ya fedha zote zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

(ii) Hadi kufikia Februari, 2026 uwiano wa bajeti kwa fedha zilizopokelewa ni mshahara 41.9%, matumizi mengineyo *(OC)* 29.5% na miradi ya maendeleo 28.5%.

(iii) Fungu 28, Jeshi la Polisi lilikuwa limepokea zaidi ya 50% ya fedha za maendeleo, wakati mafungu mengine yote yalipokea kwa kiwango cha chini ya 50% ya fedha za maendeleo.

(iv) Fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo iliyopokelewa hadi robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti ni 69.5% ya bajeti yote iliyotengwa kwa matumizi hayo.

(v) Upatikanaji wa fedha kwa mafungu yote katika mwaka wa fedha 2025/2026 ulikuwa ni kwa wastani wa zaidi ya 50%.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi huu wa Kamati umebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Makao Makuu ya Wizara na taasisi zake ni wa kuridhisha kwani ulikuwa ni zaidi ya 60%. Aidha, mtiririko wa fedha za maendeleo haukuwa wa kuridhisha kwa Fungu 14 yaani Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 29 - Jeshi la Magereza na Fungu 51 - Wizara, kwani ulikuwa chini ya 50%. Ni rai ya Kamati kwamba Wizara ijikite katika kuhakikisha kunakuwa na mtiririko bora wa fedha kutoka Hazina ili kutoathiri utekelezaji wa miradi na hivyo kuleta tija iliyotarajiwa. Maelezo zaidi kuhusu upatikanaji wa fedha ni kama yanavyoonekana kwenye ukurasa wa 16 hadi 20 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; kwa mujibu wa Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi huo wa Kamati uligusia makadirio ya makusanyo ya maduhuli, matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027; jumla ya kiasi cha fedha kilichoombwa kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa mafungu yote matano ni shilingi trilioni 2.44. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kiasi hicho kimeongezeka kwa 18% ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.1, zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya bajeti hiyo, shilingi trilioni 1.2 sawa na 48% ya bajeti yote ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 769.6 sawa na 31.4% ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* na shilingi bilioni 489.8 sawa na 20.4% ya bajeti yote ni kwa ajili ya maendeleo. Aidha, uchambuzi zaidi umebaini kuwa kuna ongezeko katika bajeti ya mishahara kwa asilimia mbili, ikilinganishwa na 46% katika mwaka wa fedha 2025/2026 na matumizi ya maendeleo kwa asilimia 0.4 ikilinganishwa na 20% katika mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa upande mwingine, kiasi kilichotengwa, kwa ajili ya matumizi mengineyo kimepungua kwa 2.5% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 ambacho kilikuwa ni 33.9%.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi zaidi wa Kamati ulibaini kuwa ongezeko la asilimia mbili katika mishahara ni kutokana na ongezeko la nafasi za ajira kwa Wizara hii, hali inayotarajiwa kuongeza nguvu kazi na hivyo kuchochea ufanisi wa kiutendaji na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027; makadirio ya mapato kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha

2026/2027 ni shilingi bilioni 577 kwa mafungu yote matano. Hii ni sawa na ongezeko la 11.6% ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 ambao makadirio yalikuwa ni shilingi bilioni 517.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa makusanyo ya mapato unaonesha kuwa Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji, itachangia kwa 60.6%, Fungu 28 - Jeshi la Polisi 22.6%, *NIDA* 13.5% na Fungu14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji 2.9%. Aidha, mafungu yaliyosalia yatachangia kwa kiwango cha chini ya asilimia moja ambayo ni Fungu 29 - Jeshi la Magereza asilimia 0.2 na Fungu 51 - Wizara Makao Makuu asilimia 0.06. Ni maoni ya Kamati kwamba Wizara ifanye tathmini ya kina kuhusu vyanzo vya mapato vilivyopo na kuibua vyanzo vipya, ili kuboresha na kuongeza wigo wa makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo; uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya maendeleo ulifanyika kwa kulinganisha na utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2025/2026. Hii inasadia kubaini mapungufu na kuakisi uhalisia wa matarajio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo: -

(i) Matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa 20.4% ya bajeti yote ya Wizara iliyotengwa, kwa ajili ya utekelezaji katika mwaka wa fedha 2026/2027, kama inavyoonekana katika Kielelezo Namba 7;

(ii) Makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa 18% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iii) Uwiano wa utekelezaji wa bajeti unaonesha kuwa hadi Februari, 2026, mapokezi ya fedha za maendeleo yalikuwa ni 28.5% kwa mafungu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 21 hadi 25 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati; uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi umejenga msingi wa jumla wa mtazamo na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja. Aidha, mtazamo huo unazingatia matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na ufuatiliaji wa kawaida wa shughuli za Wizara hii. Kwa msingi huo, Kamati ina mtazamo na maoni yafuatayo: -

(i) Ufuatiliaji wa fedha za maendeleo kutoka Hazina upewe kipaumbele ili kuwezesha upatikanaji wa fedha hizo na hivyo kutoathiri utekelezaji wa miradi kama ilivyopangwa;

(ii) Serikali iendelee kuongeza uwezo wa ndani katika fedha za maendeleo na hivyo kupunguza utegemezi wa fedha za nje ambazo mtiririko wake siyo wa uhakika;

(iii) Serikali iendelee na mikakati madhubuti na endelevu ya kuajiri watumishi wa kutosha kwa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kukidhi mahitaji yaliyopo;

(iv) Serikali iimarishe matumizi ya teknolojia na zana za kisasa kwa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara hii ili kubaini, kukabiliana na kudhibiti uhalifu na njia mpya za uhalifu zinazochagizwa na maendeleo ya kiteknolojia;

(v) Serikali iendelee kutoa kipaumbele katika kuongeza rasilimali watu, vifaa na vyombo vya usafiri kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kuimarisha utendaji wake;

(vi) Serikali iendelee kusimamia kikamilifu zoezi la urejeshwaji wa wakimbizi katika nchi walizotoka kutokana na kuimarika kwa hali ya usalama na utulivu katika nchi hizo;

(vii) Serikali iendelee kutoa kipaumbele katika kuhakikisha vyombo vya ulinzi na usalama vinatambua, kurasimisha na kulinda kikamilifu maeneo yake ili kuepusha uvamizi na migogoro kutoka kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo;

(viii) Serikali iendelee kuweka mkakati madhubuti wa kuhakikisha madai ya watumishi na madeni ya wazabuni katika vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara yanalipwa ili kutoathiri utendaji na utoaji wa huduma;

(ix) Serikali iendelee kuimarisha uwezo wa kiuzalishaji kwa vyombo vya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kuwezesha upatikanaji wa zana, mitambo na teknoplojia ya kisasa; na

(x) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa taasisi na vyombo vilivyo chini ya Wizara ni jambo la kupewa kipaumbele kwa kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya majengo ya ofisi na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa jumla; kwa msingi wa maoni na mtazamo uliotolewa hapo juu, Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iweke utaratibu mzuri wa kufuatilia na kuhakikisha fedha za maendeleo zinapatikana kama zilivyokasimiwa na Bunge kwa mafungu yote ili kutoathiri utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa;

(ii) Serikali ihakikishe inaendelea kuweka mikakati na kuajiri askari wa kutosha kuendana na mahitaji yaliyopo ili

kuendelea kuimarisha utendaji kazi wa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara; na

(iii) Serikali iimarishe matumizi ya zana na vifaa vya kidijitali katika utendaji kazi wa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara ili kubaini, kukabili na kudhibiti mbinu na aina mpya za kiuhalifu vinavyochagizwa na ukuaji wa kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mahsusi; pamoja na ushauri wa jumla, Kamati inao ushauri mahsusi kulingana na yaliyobainika. Ushauri huo ni kama ifuatavyo: -

(i) Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinatolewa kikamilifu na kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi, kama ilivyopangwa;

(ii) Serikali iendelee kuimarisha uwezo wa fedha za ndani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kupunguza utegemezi wa fedha za nje ambazo mtiririko wake si wa uhakika. Mfano, Fungu 29 yaani Jeshi la Magereza katika mwaka wa fedha 2025/2026 lilitenga 17% ya fedha za maendeleo kutokana na vyanzo vya nje na hadi kufikia robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti hiyo hakuna kiasi chochote kilichokuwa kimepokelewa. Aidha, *NIDA* katika mwaka ujao wa fedha imetenga 27% ya fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya nje;

(iii) Serikali iweke mkakati wa kuongeza rasilimali watu na vyombo vya usafiri kwa Idara ya Uhamiaji ili kuendelea kuimarisha utendaji na misako, doria na ukaguzi. Hatua hiyo itasaidia kuimarisha usalama, uzingatiaji wa sheria na kuongeza mapato ya Serikali;

(iv) Serikali iendelee kuimarisha kikamilifu urejeshwaji wa wakimbizi katika nchi walizotoka, pamoja na kuendelea kuwaelimisha wakimbizi na Watanzania

waishio katika maeneo jirani na kambi za wakimbizi kuhusu umuhimu wa zoezi hilo;

(v) Serikali iendelee kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa ikiwemo mifumo ya TEHAMA kwa taasisi na vyombo vilivyo chini ya Wizara ili kuimarisha juhudi za kukabiliana na vitendo vya kihalifu;

(vi) Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa majengo ya *NSSF*, Mjini Moshi, Kilimanjaro kwa ajili ya kuwezesha upanuzi wa Chuo cha Uhamiaji *(TRITA)*;

(vii) Serikali iendelee kuwezesha na kutenga fedha kwa ajili ya kupatikana ardhi zaidi kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji kwa malengo ya sasa na baadaye. Hatua hiyo italiwezesha jeshi hilo kuendelea kujenga miundombinu ya Vituo vya Zimamoto na Ukoaji nchini na hivyo kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii;

(viii) Serikali iendelee kuongeza rasilimali watu na vifaa vya kisasa kwa Jeshi la Polisi ili kuongeza uwiano katika utoaji huduma kwa wananchi na kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake;

(ix) Serikali iendelee kuhamasisha na kuhakikisha vyombo vya ulinzi na usalama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi vinaendelea kupima na kuweka alama za mipaka katika maeneo yake ili kuimarisha utambuzi wa maeneo husika na kupunguza migogoro na wanachi. Mfano, Jeshi la Magereza limefanikwa kupima maeneo yake 17 na linaendelea kupima maeneo mengine; na

(x) Serikali iendelee kulijengea uwezo wa kiuzalishaji Jeshi la Magereza kwa kuweka mikakati ya kuongeza mitambo na zana za kilimo, sambamba na ujenzi wa viwanda utakaosaidia katika kuongeza uzalishaji na

hivyo, kupunguza utegemezi kwa Serikali katika huduma za urekebishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa ili niweze kuwasilisha taarifa hii. Aidha, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao, kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Mbunge na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud, Mbunge na Naibu Waziri kwa ushirikiano wao mzuri kwa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Katibu Mkuu - Ndugu Ally Senga Gugu, Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Maduhu Kazi, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, naishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**25 MEI, 2026**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Naibu Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu liweze kuipokea taarifa hii, kuikubali na kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

### 1.2 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Naibu Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja, zimeweka masharti yanayohusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, Kamati ilitekeleza jukumu la uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/26 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kupata maudhui ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Naibu Spika,** sambamba na uchambuzi huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge yanayohusu kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi

iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kazi hiyo, ilifanyika kati ya tarehe 11 na 18 Machi, 2026. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ulitumia matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

### 1.3 Mawanda ya Taarifa

**Mheshimiwa Naibu Spika**, mawanda ya Taarifa ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara yanategemea muundo na majukumu ya Wizara inayohusika. Muundo na Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi umejengwa kwenye msingi wa Hati Idhini kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 383 na 385 la tarehe 7 Mei, 2021 pamoja na marekebisho yaliyofanyika kwa Tangazo la Serikali Na. 534 la tarehe 2 Julai, 2021.

**Mheshimiwa Naibu Spika,** Wizara hii ilianzishwa na kupewa majukumu ya kushughulikia uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera zinazohusu usalama wa raia na mali zao, uhamiaji, wakimbizi na uraia nchini. Aidha, Wizara hii inahusika na utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Idara ya Uhamiaji. Vilevile, Wizara imepewa wajibu wa kusimamia na kuratibu masuala ya Huduma za Wakimbizi, Vitambulisho vya Taifa, Usajili wa Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini, kupambana na Biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu na Huduma za Uangalizi (Probation).

**Mheshimiwa Naibu Spika,** kwa wigo huo wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, uchambuzi uliofanywa na Kamati umejumuisha Mafungu matano (5) ya kibajeti ambayo ni:-

i. Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
ii. Fungu 28 – Jeshi la Polisi;
iii. Fungu 29 – Jeshi la Magereza;
iv. Fungu 51 – Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*; na
v. Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Bajeti ya utekelezaji wa majukumu ya

Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilitengwa kwenye mafungu hayo, halikadhalika bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 nayo imetengwa kwenye mafungu hayo. Kwa msingi huo, uchambuzi unaozingatia mafungu hayo, umegusa wigo mpana wa dhima ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

### 1.4 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Naibu Spika**, muundo wa taarifa hii umezingatia Kanuni ya 145(a-c) ya Kanuni za Bunge, 2025 kuhusu Muundo wa Taarifa ya Kamati ya Bunge inayoingia Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya Kwanza, inayohusu maelezo ya utangulizi na kubainisha msingi, mawanda na muundo wa Taarifa;

(b) Sehemu ya Pili, inayobainisha uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(c) Sehemu ya Tatu, ambayo inayohusu uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na

(d) Sehemu ya Nne inayoeleza Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi pamoja na kuhitimisha taarifa.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mafungu yote matano, ambao umezingatia mambo muhimu yaliyobainika katika utekelezaji wa bajeti inayoisha.

## 2.2 Uchambuzi

**Mheshimiwa Naibu Spika**, sehemu hii inahusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuzingatia kifungu cha 6(3)(c) cha Nyongeza na Nane, ambacho kinaipa Kamati jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na uzingatiaji wa kifungu cha 7(1)(a-d). Uchambuzi umegusia mambo yafuatayo:-

(i) Hali ya Utekelezaji wa Miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge;

(iii) Uchambuzi wa Hali ya Ukusanyaji wa Mapato; na

(iv) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, uchambuzi wa mambo hayo muhimu kwa Bunge utasaidia katika kujua namna Serikali ilivyotekeleza Bajeti kama ilivyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, Bunge litakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kujadili na kushauri kuhusu hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

### 2.2.1 Hali ya Utekelezaji wa Miradi iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2025/2026

**Mheshimiwa Naibu Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, Kamati ilitembelea na kukagua miradi minne katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro na Morogoro inayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Miradi iliyokaguliwa ni ile inayotekelezwa na Fungu 28 -Jeshi la Polisi, Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji, Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Fungu 29 - Jeshi la Magereza.
Lengo la ukaguzi huo ni kuliwezesha Bunge kuelewa hali ya utekelezaji, na upatikanaji wa fedha kama zilivyoidhinishwa na hivy kuweza kutoa ushauri wake.

**2.2.1.1 Mradi Na. 6339 – Ukarabati wa Majengo ya Chuo cha Uhamiaji, Mkoani Kilimanjaro.**

Mradi huu unahusu ukarabati wa majengo ya utawala (administration block) katika Chuo cha Uhamiaji (TRITA), mkoani Kilimanjaro na unatekelezwa kwa utaratibu wa *force account*. Kamati ilielezwa kuwa, mradi huu ulioanza kutekelezwa tarehe 20 Oktoba, 2025 ulitengewa **shilingi 240,000,000.00/=** na ulitarajiwa kukamilika Aprili, 2026.

Hadi wakati Kamati inakagua mradi huu, kiasi cha **shilingi 239,820,000.00/=** sawa na **asilimia 99.9** ya fedha iliyotengwa kilikuwa kimepokelewa, na utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 60.** Katika ukaguzi wake, Kamati ilibaini kuwa hali ya utekelezaji wa mradi ni ya kuridhisha, licha ya kuwepo kwa changamoto ya ucheleweshaji wa fedha kutoka hazina.

2.2.1.2 Mradi Na. 6582 Ujenzi na Maboresho ya Shule ya Polisi, Kilimanjaro.

Mradi huu unaohusu maboresho ya shule ya Polisi Tanzania, mkaoni Kilimanjaro ulianza kutekelezwa mwaka 2024 kwa fedha kutoka mfuko Mkuu wa Serikali. Jumla ya **shilingi 25,000,000,000.00/=** zilitengwa kwa ajili ya mradi huu ili kugharamia ujenzi wa mabweni ya wanafunzi, nyumba za walimu, madarasa na kumbi za kufundishia (lecture halls).

Hadi wakati Kamati inatembelea na kukagua mradi huu, kiasi cha **shilingi 23,000,000,000.00/=** kilikuwa kimepokelewa katika awamu nne. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa **shilingi 475,000,000.00/=** zilizopokelewa kutoka mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi na kuelekezwa mahsusi kwenye ukarabati wa mabweni, zimeombewa kibali ili zitumike katika mradi huu ambao unatekelezwa kwa utaratibu wa *force account*. Wakati wa ukaguzi wa Kamati, ujenzi wa majengo saba (7) kwa ajili ya mabweni ya wanaume, mabweni ya wanawake na majengo ya makazi ya askari wakufunzi ulikuwa ukiendelea katika hatua mbalimbali.

**Mheshimiwa Naibu Spika,** Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao ukikamilika utaongeza uwezo wa shule

kuhudumia askari na wanafunzi. Mabweni ya wanaume yatakua na uwezo wa kuhudumia wanafunzi **1,458** ikilinganishwa na wanafunzi **490** kwa majengo ya zamani, hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 197.6.** Aidha, mabweni ya wanawake yatakua na uwezo wa kuhudumia wanafunzi **1,412** ikilinganishwa na wanafunzi **490** kwa majengo ya zamani, hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 188**. Vilevile, majengo mawili ya makazi ya askari yatakuwa na uwezo wa kuhudumia familia **24** ikilinganishwa na majengo manne ya zamani yaliyokuwa na uwezo wa kuhudumia familia **8** tu. Mradi huu unatarajiwa kuleta manufaa mengi, hivyo ni rai ya Kamati kwamba, utekelezaji wake usimamiwe vizuri na kuhakikisha unakamilika kwa wakati.

**2.2.1.3 Mradi Na.6582 Ukarabati wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji, Morogoro.**

Mradi huu unahusu ukarabati wa Majengo ya Ofisi za Zimamoto, mkoani Morogoro ambayo kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati yalikuwa na zaidi ya miaka 50 bila kufanyiwa ukarabati. Utekelezaji wa mradi ulianza Juni, 2025 na ulipangwa kukamilika Aprili, 2026 kwa gharama ya **shilingi 300,000,000.00**/=. Hadi wakati wa ukaguzi wa Kamati, kiasi cha **shilingi 299,976,000.00/=** sawa na **asilimia 99** kilikuwa kimepokelewa na mradi unatekelezwa kwa utaratibu wa *force account* ukiwa umefikia **asilimia 97.5**.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, Kamati imeridhishwa na utekelezaji uliofanyika kwenye mradi huu kwani si tu umesaidia kuboresha muonekano wa majengo na taswira ya kituo, bali pia ni jambo linachangia kuboresha mazingira ya kazi na hivyo kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa kituo hicho. Hata hivyo, Kamati ilibaini changamoto ya uchakavu na upungufu wa samani katika kituo hicho jambo linalotia doa ukarabati uliofanyika.

Hivyo, Kamati ina maoni kwamba, Wizara iharakishe mchakato wa upatikanaji wa samani katika kituo hicho ili maboresho yalioyofanyika yaweze kuwa na tija. Aidha, Wizara iliwezeshe jeshi hili kukarabati na kuboresha majengo ya vituo vya zimamoto katika maeneo mengine nchini ili kuliwezesha kutoa huduma bora zinazoendana na teknolojia ya kisasa.

**2.2.1.4 Mradi Na. 6305 Ujenzi wa Magereza Msalato, Dodoma**

Mradi huu unahusu ujenzi wa majengo mbalimbali ya Magereza Msalato, mkoani Dodoma na utekelezaji wake ulianza Machi, 2025. Lengo la mradi ni kuwezesha kuwa na gereza la kisasa lenye miundombinu wezeshi kwa shughuli za urekebishaji wafungwa. Kamati ilielezwa kwamba, mradi huu unaotekelezwa kwa awamu unakadiriwa kugharimu **shilingi 20,121,846,709.43**/= na kukamilika kwake kutawezesha gereza kuongeza idadi ya wafungwa na mahabusu wanaohudumiwa. Aidha, gereza litawezesha mahabusu na wafungwa kufuatilia uendeshaji wa kesi kwa njia ya mtandao kutokana na mifumo ya TEHAMA itakayosimikwa kupitia mradi huu.

Katika mwaka wa fedha 2025/2026 mradi ulitengewa **shilingi 1,000,000,000.00/=** ambazo hadi wakati Kamati inafanya ukaguzi zilikua hazijatolewa. Hatua hiyo ililifanya Jeshi la Magereza kutumia **shilingi 83,000,000.00/=** kutoka vyanzo vyake vya ndani ili kutekeleza sehemu ya mradi katika mwaka huu wa fedha. Kamati inaona kwamba, hatua ya kutopatikana kwa fedha za utekelezaji wa mradi kama zilivyoidhinishwa na Bunge kunaathiri na kutachelewesha kukamilika kwa mradi na hivyo kuchelewesha kufikiwa kwa mafanikio yanayotarajiwa.

**2.2.1.5 Uchambuzi wa Taarifa ya Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri**

**Mheshimiwa Naibu Spika**, wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo ambayo iliona yanatakiwa kufanyiwa kazi na kuongezewa nguvu katika utekelezaji wake. Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na kutolewa ufafanuzi zilionesha kuwa Serikali imezingatia na inaendelea kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Maelezo zaidi kuhusu ufafanunuzi huo yanaonekana katika **kiambatisho Na. 1.**

**2.2.2 Uchambuzi wa Hali ya Ukusanyaji wa Mapato (Maduhuli)**

**Mheshimiwa Naibu Spika,** uchambuzi wa hali ya ukusanyaji wa mapato umezingatia ulinganisho wa namna zifuatazo:-

(i) Ulinganisho wa hali ya ukusanyaji wa mapato kati ya kipindi cha Februari, 2025 na Februari, 2026.

(ii) Ulinganisho wa kiasi kilichokusanywa na Makadirio kwa kila fungu kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 01

(iii) Ulinganisho wa mchango wa kinachokusanywa na mchango wa kiasi kilichokadiriwa kwa kila fungu kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 02.


**Kielelezo Na. 1: Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Makusanyo kwa kila Fungu hadi Februari, 2026**

| FUNGU | | Makadirio ya Mapato mwaka 2025/2026 | Makusanyo hadi Februari, 2026 | Asilimia Ukusany | Asilimia uchangi |
|---|---|---|---|---|---|
| **14 – Zimamoto** | | 15,000,000,000 | 9,676,526,420 | 65 | 2.8 |
| **28 – Polisi** | | 120,500,000,000 | 85,089,918,157.98 | 70.6 | 24.6 |
| **29 – Magereza** | | 1,000,000,000 | 717,131,306.94 | 72 | 0.2 |
| **51- Wizara** | **Wizara** | 500,000,000 | 208,658,600 | 42 | 0.06 |
| | **NIDA** | 60,000,000,000 | 40,351,440,513.07 | 67.2 | 11.6 |
| **93- Uhamiaji** | | 320,000,000,000 | 209,714,698,952 | 66 | 60.7 |
| **JUMLA** | | **517,000,000,000** | **345,758,373,950** | **67** | **100** |


***Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027***

**Kielelezo Na. 2: Ulinganisho wa Makadirio ya Mchango wa kila Fungu katika Mapato na Mchango halisi kwenye Makusanyo**

**MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA KILA FUNGU KUTOKANA NA BAJETI.**




**MCHANGO WA MAKUSANYO KWA KILA FUNGU HADI ROBO YA TATU YA UTEKELEZAJI**




Chanzo: *Randama ya Wizara 2026/2027*

**Mheshimiwa Naibu Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo:-

(i) Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ikijumuisha Mafungu yake yote matano ilikadiriwa kukusanya **shilingi 517,000,000,000.00/=,** na kiasi cha makusanyo hadi Februari, 2026 kilikuwa **shilingi 345,758,373,950.00/=** sawa na **asilimia 67** ya lengo la mwaka;

(ii) Makusanyo ya Jeshi la Polisi ikilinganishwa na makadirio yalifikia **asilimia 70.6**, Jeshi la Magereza **asilimia 72,** Idara ya Uhamiaji **asilimia 66** na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji **asilimia 65**;

(iii) Makusanyo ya Wizara Makao Makuu yalifikia

**asilimia 42** na NIDA yalikuwa ni **asilimia 67.2** ya lengo la makusanyo kwa mwaka;

(iv) Makusanyo ya jumla kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hadi mwezi Februari, 2026 yalifikia **asilimia 67,** kiwango ambacho ni cha kuridhisha kwani ndicho kilichotarajiwa kufikiwa katika kipindi hicho. Hata hivyo, Fungu 51 - Wizara Makao Makuu lilikuwa limekusanya kwa **asilimia 42,** kiwango ambacho ni cha chini ikilinganishwa na lengo tarajiwa katika kipindi cha hadi Februari, 2026;

(v) Makusanyo ya Jeshi la Polisi yamechangia **asilimia 24.6** ya makusanyo yote hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ingawa lengo lilikuwa ni kufikia **asilimia 23.30** katika kipindi hicho;

(vi) Makusanyo ya Jeshi la Magereza, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.19** na yamechangia **asilimia 0.2** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Februari, 2026;

(vii) Makusanyo ya Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 61.8** lakini hadi mwezi Februari, 2026 taarifa ilionesha yalifikia **asilimia 60.7**;

(viii) Wizara Makao Makuu ilitarajiwa kuchangia makusanyo ya jumla ya wizara kwa **asilimia 0.09**, hata hivyo ilichangia kwa **asilimia 0.06.** Aidha, NIDA ilikusudiwa kukusanya kwa **asilimia 11.6** ya lengo na imefanikiwa kukusanya kwa **asilimia 11.7** hadi Februari, 2026; na

(ix) Makusanyo ya Jesho la Zimamoto na Uokoaji**,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 2.9**, na taarifa ya makusanyo ilionesha yalichangia kwa **asilimia 2.8**.

### 2.2.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Naibu Spika,** Kamati ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa kuangalia kiwango cha fedha kilichopatikana ikilinganishwa na bajeti iliyopitishwa na Bunge, na uwiano wa bajeti kwa mafungu yote matano ya wizara kama ilivyopitishwa na Bunge ikilinganishwa na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa mafungu hayo kama ifuatavyo:-

(i) Kiwango cha matumizi kilichoidhinishwa na Bunge kwa kila fungu ikilinganishwa na fedha iliyopatikana kwa kila fungu kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 03**.

(ii) Uwiano wa matumizi kwa kila fungu kama ilivyoidhinishwa na uwiano wa fedha zilizopatikana kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 04**.


**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na kiasi cha Fedha kilichopatikana kwa kila Fungu)**

| FUNGU | Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2025/2026 | Asilimia | Fedha iliyopatikana hadi Februari, 2026 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **28-Polisi** | 1,258,081,224,000 | 60.9 | 1,148,706,034,122.90 | 91 |
| **29-Magereza** | 330,529,808,000 | 16 | 218,392,830,497.70 | 66 |
| **93-Uhamiaji** | 227,091,159,000 | 11 | 171,779,164,327.06 | 75.6 |
| **51-Wizara** | 165,669,494,000 | 8 | 62,469,229,533.25 | 38 |
| **14-Zimamoto** | 85,791,032,000 | 4.1 | 51,997,296,011.07 | 60.6 |
| **JUMLA** | **2,067,161,717,000** | **100** | **1,653,344,554,491.98** | **80** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2026/2027 na Usanifu wa Kamati***

**Kielelezo Na. 4: Makadirio ya Uwiano wa Ainda za Matumizi ukilinganishwa na Uwiano wa Upatikanaji wa Fedha kwa aina za Matumizi**

**Uwiano wakati wa Makadirio** | **Uwiano katika upatikanaji wa fedha**





***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026 na usanifu wa Kamati***

(iii) Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge na kiasi cha fedha kilichopatikana kwa mafungu yote kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 05**;

**Kielelezo Na. 5: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na kiasi cha Fedha kilichopatikana kwa kila Fungu**

**Ulinganisho wa upatikanaji wa fedha kwa Wizara hadi Feb. 2026 kwa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge**




***Chanzo:Randama ya Wizara 2026/2027 na usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Naibu Spika**, ulinganishaji unasaidi kuweka ulinganisho wa upatikanaji wa fedha na kubaini maeneo ambayo mwenendo wake si wa kuridhisha au upo chini ya wastani. Uchambuzi umebaini yafuatayo:-

(i) Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara hadi Februari, 2026 ni **asilimia 80** ya fedha zote zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Katika fedha zilizopatikana mishahara ilikuwa ni **asilimia 33.5**, matumizi mengineyo **asilimia 23.5** na fedha za maendeleo **asilimia 22.8**;

(iii) Uwiano wa Bajeti kwa ajili ya matumizi ya Wizara hii, ulikuwa ni **asilimia 46** kwa mishahara, matumizi mengineyo **asilimia 34** na miradi ya maendeleo **asilimia 20**;

(iv) Hadi kufikia Februari, 2026 uwiano wa Bajeti kwa fedha zilizopokelewa ni mishahara **asilimia 41.9**, matumizi mengineyo (OC) **asilimia 29.5** na miradi ya maendeleo **asilimia 28.5**;

(v) Mishahara iliyopokelewa ni sawa na **asilimia 73** ya bajeti yote iliyotengwa kwa ajili hiyo katika mwaka 2025/2026, ikiwa ni wastani unaoridhisha;

(vi) **Fungu 28** - Jeshi la Polisi lilikuwa limepokea zaidi ya **asilimia 50** ya fedha za maendeleo, wakati mafungu mengine yote yalipokea kwa kiwango cha chini ya asilimia 50 ya fedha za maendeleo;

(vii) **Fungu 29** - Jeshi la Magereza lilikuwa limepokea wastani wa **asilimia 0.7** ya fedha zote zilizopokelewa kwa ajili ya maendeleo;

(viii) Kiasi cha Fedha kilichopokelewa na Wizara kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) kilikuwa asilimia 29.5 ya fedha yote iliyopokelewa;

(ix) Fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo iliyopokelewa hadi robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti ni asilimia 69.5 ya bajeti yote iliyotengwa kwa matumizi hayo; na

(x) Upatikanaji wa fedha kwa mafungu yote katika mwaka wa fedha 2025/2026 ulikuwa ni kwa wastani wa zaidi ya **asilimia 50.**

**Mheshimiwa Naibu Spika,** uchambuzi huu wa Kamati umebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa makao makuu ya Wizara na Taasisi zake ni wa kuridhisha kwani ulikuwa ni zaidi ya **asilimia 60**. Aidha, mtiririko wa fedha za maendeleo haukuwa wa kuridhisha kwa Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu – 29-Jeshi la Magereza na Fungu 51- Wizara, kwani ulikuwa chini ya **asilimia 50**.

**Mheshimiwa Naibu Spika,** ni rai ya Kamati kwamba Wizara ijikite katika kuhakikisha kunakuwa na mtiririko bora wa fedha kutoka hazina ili kutoathiri utekelezaji wa miradi na hivyo kuleta tija iliyotarajiwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi huo wa Kamati uligusia makadirio ya makusanyo ya maduhuli, matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, jumla ya kiasi cha fedha kinachoombwa kuidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa ajili ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa mafungu yote matano ni **shilingi 2,443,215,927,000.00/=**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kiasi hicho kimeongezeka kwa **asilimia 18** ikilinganishwa na **shilingi 2,067,162,717,000.00/=** zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Naibu Spika,** kati ya bajeti hiyo, **shilingi 1,183,766,640,000.00/=** sawa na **asilimia 48** ya bajeti yote ni kwa ajili ya mishahara (PE), **shilingi 769,599,845,531.00/=** sawa na **asilimia 31.4** ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), na **shilingi 489,849,441,469.00/=** sawa na **asilimia 20.4** ya bajeti yote ni kwa ajili ya maendeleo (DEV). Aidha, uchambuzi zaidi umebaini kuwa kuna ongezeko katika bajeti ya mishahara kwa **asilimia 2** ikilinganishwa na **asilimia 46** katika mwaka wa fedha 2025/2026; na matumizi ya maendeleo kwa **asilimia 0.4** ikilinganishwa na **asilimia 20** katika mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa upande mwingine, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo kimepungua kwa **asilimia 2.5** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 ambacho kilikuwa ni **asilima 33.9**.


**Mheshimiwa Naibu Spika**, uchambuzi zaidi wa Kamati ulibaini kuwa ongezeko la **asilimia 2** katika mishahara ni kutokana na

ongezeko la nafasi za ajira kwa Wizara hii, hali inayotarajiwa kuongeza nguvu kazi, na hivyo kuchochea ufanisi wa kiutendaji na kuongeza mapato.

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Naibu Spika,** makadirio ya mapato kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni **shilingi 577,090,000,000.00/=** kwa mafungu yote matano. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 11.6** ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 ambao makadirio yalikuwa ni **shilingi 517,000,000,000.00/=**

**Kielelezo Na. 6: Uwiano wa Makadirio ya Makusanyo kwa kila Fungu**




*Mgawanyo wa makadirio ya makusanyo kwa mafungu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027*

***Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Naibu Spika**, mgawanyo wa makusanyo ya mapato unaonesha kuwa Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji itachangia kwa asilimia **60.6**; Fungu 28 - Jeshi la Polisi **asilimia 22.6;** NIDA **asilimia 13.5;** na Fungu14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji **asilimia 2.9.** Aidha, mafungu yaliyosalia yatachangia kwa kiwango cha chini ya **asilimia 1** ambayo ni Fungu 29 - Jeshi la Magereza **asilimia 0.2** na Fungu 51 - Wizara Makao Makuu **asilimia 0.06.** Uchambuzi zaidi wa Kamati ulibaini kuwa, kiwango cha makadirio kwa fungu 51 kimepungua kutoka **asilimia 0.09** katika mwaka wa fedha

2025/2026. Kamati ilipohitaji ufafanuzi kutokana na hali hiyo, ilielezwa kuwa ni kutokana na kukamilika kwa zoezi la uhakiki na uhuishaji wa vyeti vya usajili na ukusanyaji madeni ya miaka ya nyuma kwa taasisi za kidini na zisizo za kidini nchini.


**Mheshimiwa Naibu Spika,** ni maoni ya Kamati kwamba wizara ifanye tathmini ya kina kuhusu vyanzo vya mapato vilivyopo na kuibua vyanzo vipya ili kuboresha na kuongeza wigo wa makusanyo.

**3.4** Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Naibu Spika**, uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya maendeleo ulifanyika kwa kulinganisha na utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2025/2026. Hii inasadia kubaini mapungufu na kuakisi uhalisia wa matarajio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo:-

(i) Matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa **asilimia 20.4** ya bajeti yote ya Wizara iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji katika mwaka wa fedha 2026/2027 kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 07:**

**Kielelezo Na. 7: Makadirio ya Fedha za Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2026/2027**




***Chanzo:Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati***

(ii) Makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **asilimia 18** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026;

(iii) Uwiano wa utekelezaji wa Bajeti unaonesha kuwa hadi Februari, 2026 mapokezi ya fedha za maendeleo yalikuwa ni **asilimia 28.5** kwa mafungu yote. Hivyo, ongezeko la **asilimia 18** linaleta mashaka iwapo litakuwa na tija ikizingatiwa kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika mwaka huu wa fedha haukuwa mzuri;

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 MAONI, USHAURI NA HITIMISHO

**4.1** Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Naibu Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi umejenga msingi wa jumla wa mtazamo na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja. Aidha, mtazamo huo unazingatia matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji na ufuatiliaji wa kawaida wa shughuli za Wizara hii. Kwa msingi huo, Kamati ina mtazamo na maoni yafuatayo:-

(i) Ufuatiliaji wa fedha za maendeleo kutoka hazina upewe kipaumbele ili kuwezesha upatikanaji wa fedha hizo na hivyo kutoathiri utekelezaji wa miradi kama ilivyopangwa;

(ii) Serikali iendelee kuongeza uwezo wa ndani katika fedha za maendeleo na hivyo kupunguza utegemezi wa fedha za nje ambazo mtiririko wake si wa uhakika;

(iii) Serikali iendelee na mikakati madhubuti na endelevu ya kuajiri watumishi wa kutosha kwa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kukidhi mahitaji yaliyopo;

(iv) Serikali iimarishe matumizi ya teknolojia na zana za kisasa kwa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara hii ili kubaini, kabiliana na kudhibiti uhalifu na njia mpya za uhalifu zinazochagizwa na maendeleo ya kiteknolojia;

(v) Serikali iendelee kutoa kipaumbele katika kuongeza raslimali watu, vifaa na vyombo vya usafiri kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kuimarisha utendaji wake;

(vi) Serikali iendelee kusimamia kikamilifu zoezi la urejeshwaji wa wakimbizi katika nchi walizotoka kutokana na kuimarika kwa hali ya usalama na utulivu katika nchi hizo;

(vii) Serikali iendelee kutoa kipaumbele katika kuhakikisha vyombo vya ulinzi na usalama vinatambua, kurasimisha na kulinda kikamilifu maeneo yake ili kuepusha uvamizi na migogoro kutoka kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo;

(viii) Serikali iendelee kuweka mkakati madhubuti wa kuhakikisha madai ya watumishi na madeni ya wazabuni katika vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara yanalipwa ili kutoathiri utendaji na utoaji wa huduma;

(ix) Serikali iendelee kuimarisha uwezo wa kiuzalishaji kwa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kuwezesha upatikanaji wa zana, mitambo na teknoplojia ya kisasa; na

(x) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa taasisi na vyombo vilivyo chini ya wizara ni jambo la kupewa kipaumbele kwa kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya majengo ya ofisi na makazi.

**4.2 Ushauri wa Jumla**

**Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa msingi wa maoni na mtazamo uliotolewa hapo juu, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iweke utaratibu mzuri wa kufuatilia na kuhakikisha fedha za maendeleo zinapatikana kama zilivyokasimiwa na Bunge kwa mafungu yote ili kutoathiri utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa;

(ii) Serikali ihakikishe inaendelea kuweka mikakati na kuajiri askari wa kutosha kuendana na mahitaji yaliyopo ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi wa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara; na

(iii) Serikali iimarishe matumizi ya zana na vifaa vya kidijiti katika utendaji kazi wa vyombo na taasisi zilizo chini ya Wizara ili kubaini, kukabili na kudhibiti mbinu na aina mpya za kiuhalifu vinavyochagizwa na ukuaji wa kiteknolojia.

### 4.3 Ushauri Mahsusi

**Mheshimiwa Naibu Spika**, pamoja na ushauri wa jumla, Kamati inao ushauri mahsusi kulingana na yaliyobainika. Ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinatolewa kikamilifu na kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi kama ilivyopangwa;

(ii) Serikali iendelee kuimarisha uwezo wa fedha za ndani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kupunguza utegemezi wa fedha za nje, ambazo mtiririko wake si wa uhakika. Mfano; Fungu 29 – Jeshi la Magereza katika mwaka wa fedha 2025/2026 lilitenga **asilimia 17** ya fedha za maendeleo kutokana na vyanzo vya nje, na hadi kufikia robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti hiyo, hakuna kiasi chochote kilichokuwa kimepokelewa. Aidha, NIDA katika mwaka ujao wa fedha imetenga **asilimia 27** ya fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya nje;

(iii) Serikali iweke mkakati wa kuongeza rasilimali watu na vyombo vya usafiri kwa Idara ya Uhamiaji ili kuendelea kuimarisha utendaji na kuimarisha misako, doria na ukaguzi. Hatua hiyo itasaidia kuimarisha usalama, uzingatiaji wa sheria na kuongeza mapato ya Serikali;

(iv) Serikali iendelee kusimamia kikamilifu urejeshwaji wa wakimbizi katika nchi walizotoka, pamoja na kuendelea kuwaelimisha wakimbizi na watanzania waishio katika

maeneo jirani na kambi za wakimbizi kuhusu umuhimu wa zoezi hilo;

(v) Serikali iendelee kuimarisha matumizi ya Teknolojia za kisasa ikiwemo mifumo ya TEHAMA kwa taasisi na vyombo vilivyo chini ya Wizara ili kuimarisha juhudi za kukabiliano na vitendo vya kiuhalifu;

(vi) Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa majengo ya NSSF, Mjini Moshi - Kilimanjaro kwa ajili ya kuwezesha upanuzi wa Chuo cha Uhamiaji – TRITA.

(vii) Serikali iendelee kuwezesha na kutenga fedha kwa ajili ya kupatikana ardhi zaidi kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika maeneo ya mijini na pembezoni mwa miji (kwa malengo ya sasa na baadae). Hatua hiyo italiwezesha jeshi hilo kuendelea kujenga miundombinu ya vituo vya zimamoto na ukoaji nchini na hivyo kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii;

(viii) Serikali iendelee kuongeza rasilimali watu na vifaa vya kisasa kwa Jeshi la Polisi ili kuongeza uwiano katika utoaji huduma kwa wanachi na kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake;

(ix) Serikali iendelee kuhamasisha na kuhakikisha vyombo vya ulinzi na usalama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi vinaendelea kupima na kuweka alama za mipaka katika maeneo yake ili kuimarisha utambuzi wa maeneo husika na kupunguza migogoro na wanachi. Mfano, Jeshi la Magereza limefanikwa kupima maeneo yake 17 na linaendelea kupima maeneo mengine; na

(x) Serikali iendelee kulijengea uwezo wa kiuzalishaji Jeshi la Magereza kwa kuweka mikakati ya kuongeza Mitambo na zana za Kilimo, sambamba na ujenzi wa viwanda utakaosaidia katika kuongeza uzalishaji, na hivyo kupunguza utegemezi kwa serikali katika huduma za urekebishaji.

**4.4 Hitimisho**

**Mheshimiwa Naibu Spika**, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

1. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Pascal Inyasi Chinyele, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dkt.Tulia Ackson, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Zainab Rashi Kawawa, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Christina Solomon Mndeme, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Fadhili Ally Liwaka, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Salum Khamis Haji, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Abdul Yussuf Maalim, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Ramadhan Muhidin Ramadhan, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Asya Ali Khamis, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Zainab Abdallah Issa, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Juma Omari Kipanga, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Angela Charles Kizigha, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Dkt. Lazaro Killian Komba, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Naibu Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Patrobasi Paschal Katambi (Mb) na Naibu Waziri, Mhe. Ayoub Mohammed Mahmoud (Mb), kwa ushirikiano wao mzuri kwa Kamati. Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu Ndg. Ally Senga Gugu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Maduhu Kazi pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Naibu Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Idelphonce Leornad, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, naishukuru Sekretariat ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Naibu Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Naibu Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kuwasilisha Taarifa ya Kamati yetu.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha ya wageni walioingia Bungeni tangu mchana huu.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; tuna wageni wa Mheshimiwa Paschal Patrobass Katabi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; tunaye Mheshimiwa Julius Mtatiro - Mkuu wa Wilaya Shinyanga Mjini. *(Makofi)*

Tunaye Sheikh Abdi Mohamed Bhatti - Naibu Amiri Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania; tunaye Sheikh Maldin Shams ambaye ni *Ahmadia Muslim Jamaat* na tunaye Sheikh Hemed Jalala, Sheikh Mkuu wa Jumuiya ya Shia, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Katambi ambao ni Makamishna na Naibu Makamishna kutoka Wizarani. Pia, wapo Wakurugenzi na Maafisa Waandamizi kutoka Wizara na Taasisi zake, na pia tunao Maaskari kutoka Chuo cha Polisi Moshi *(CCP)*. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wawakilishi kutoka taasisi za kifedha. *(Makofi)*

Tunao viongozi wa dini; viongozi wa dini kwa ujumla wenu karibuni. *(Makofi)*

Wapo viongozi wa CCM Wilaya na matawi; pia wapo wapiga kura kutoka Shinyanga Mjini. Karibuni sana wapiga kura kutoka Shinyanga Mjini, Mbunge wenu yupo makini kweli kweli. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge; tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda ambao ni wapiga kura kutoka Buhigwe, Mkoani Kigoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela ambao pia ni wapiga kura wake kutoka Kyerwa, Mkoani Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea Taarifa ya Kamati tunaendelea sasa na mjadala wetu. Tutaanza na Mheshimiwa Najma Giga, atafuata na Mheshimiwa Muhsin Ussi, na Mheshimiwa Ali Hassan King ajiandae.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ndiyo muweza wa yote katika ulimwengu wetu. Kipekee kabisa naanza kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu katika majeshi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natumia fursa hii kuwapongeza viongozi wote wanaomfuata akiwemo Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi na Waziri Mkuu wetu Dkt. Mwigulu Nchemba. Bila kuwasahau Mawaziri wa Wizara hii ya Mambo ya Ndani,

Mheshimiwa Patrobass Katambi na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kazi inayofanywa na hao wote viongozi ambao nimewataja kupitia Chama Cha Mapinduzi ni kazi ambayo inatakiwa kupongezwa kwa dhati kabisa na Watanzania wote. Tunaelewa kabisa thamani ya vyombo vyetu katika nchi yetu, tunaelewa umuhimu wa vyombo vyetu hivi ambapo tuna Jeshi la Polisi, tuna Jeshi la Magereza, tuna Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lakini pia tuna Jeshi la Uhamiaji na tuna Kitengo chetu cha *NIDA*. Hivi vyote ni muhimu katika maendeleo ya Taifa letu kwa ulinzi wa raia pamoja na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wote kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusaidia kuimarisha majeshi yetu katika Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Jeshi la Polisi; nitumie fursa hii adhimu kabisa kumshukuru *IGP* Wambura kwa kazi kubwa anayoifanya na mbinu mbalimbali anazobuni katika kuboresha mifumo ya kiusalama katika Taifa letu. Nimpongeze kwa kuanzisha Polisi Kata ambayo inatusaidia sana, lakini wakati huo huo niombe sana Polisi Kata hawa ambao wanateuliwa katika kata zao wabaki katika maeneo yao ili kuweza kuwa kiungo imara baina ya wilaya pamoja na hizo kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tuendelee kuboresha Polisi Jamii. Polisi Jamii ni muhimu sana na ni kiungo muhimu baina ya jamii na polisi wetu. Ninaomba sana hilo liendelee kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ambaye haelewi umuhimu wa Jeshi la Polisi katika Taifa letu na umuhimu zaidi ni kwamba jeshi letu ni imara na bora tokea tumapata Uhuru wa nchi hii na hilo ni jambo la kulipongeza. Hivi karibuni Kamati yetu ilikwenda kutembelea Chuo cha Polisi, Moshi, tumeona ambavyo jengo lile la chuo linavyoboreshwa. Mabweni mapya yanajengwa upande

wa kike na wa kiume. Vilevile, nyumba za walimu wa askari na askari wenyewe ni ya kisasa. Endapo itakamilika kwa wakati chuo kile basi itakuwa ni chuo cha mfano katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki na Kati. Kizuri zaidi ni kwamba wanafunzi wanaokuja pale siyo Watanzania tu, wanatoka na nje ya nchi yetu. Hili ni jambo la kujivunia na kuona ni jambo zuri kwetu sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachoomba zaidi katika suala hilo la chuo kile fedha zilizopangwa zipelekwe kwa wakati ili shule ile iweze kumalizika mapema na kuweza kuleta tija iliyokusudiwa kwa muda ambao tumeukusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya kazi hizi na Jeshi la Polisi nitoe wito kwa Watanzania; Jeshi la Polisi ni letu na kazi inayofanywa na Jeshi la Polisi inatokana na mapungufu yaliyopo katika nchi yetu katika mporomoko wa maadili. Bila kuwa na mporomoko wa maadili Jeshi la Polisi lingekuwa linajijenga kiuchumi zaidi kuliko kufanya kazi ya kukamata wahalifu. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Watanzania kuwa Jeshi la Polisi ni letu, hivyo ushirikiano unaotakiwa kutoka jamii kwenda polisi ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitanukuu kiongozi wetu wa dini ambaye ninathamini sana na kumheshimu, Mama Tereza. Mama Tereza alituambia au aliwaambia waumini wake na sisi tunaendelea kufuata kwamba; "ninachoweza kufanya mimi wewe unaweza usiweze kufanya na unachoweza kufanya wewe, mimi naweza nisifanye; lakini tukifanya kwa pamoja tutajenga kitu bora zaidi na imara."

Kwa hiyo, nasema hayo kwa sababu tukishirikiana na Jeshi la Polisi na kwa bahati mbaya Mheshimiwa Dorothy Gwajima hayupo, lakini akiwepo nitaongea. Yupo nimemuona pale, nitaongea naye kwa ndani tuweze kuhakikisha tunatengeneza mfumo bora wa kudhibiti mporomoko wa maadili katika Taifa letu ili tulipunguzie kazi Jeshi la Polisi, lionekane linafanya kazi imara zaidi ya kutengeneza uchumi wa nchi yetu kuliko kukamata wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema kuhusiana na Jeshi la Polisi ninaomba sasa nielekee magereza na nimpongeze sana Kamishna Jenerali Jeremia Katunga na yeye anasimamia vizuri katika Jeshi letu la Magereza. Pamoja na msaada mkubwa wa Mheshimiwa Rais wa kuwa na nia na dhamira njema kwa majeshi yetu yote haya ambayo nimeyataja manne bado majenerali wetu wanamsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha yale ambayo yanadhamiria yaweze kufanikiwa. Tunaona jinsi gani ambavyo miundombinu yetu ambayo inakarabatiwa katika maeneo mbalimbali ya magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Gereza Kuu ambalo linajengwa Msalato, tulikwenda kulitembelea. Gereza lile likikamilika litakuwa ni la mfano kwa Tanzania na nje ya Tanzania, na itaonesha dhana nzima ya utawala bora katika nchi yetu. Kule sasa tunaondokana na dhana ya zamani ya kikoloni ya kusema kwamba wafungwa wanaenda kuadhibiwa, sasa hivi hawaitwi wafungwa ni wanafunzi wanaoenda kurekebeshwa tabia zao baada ya kuharibu katika jamii na kuvunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni jambo la kujivunia sana kwa sababu tunaondokana na dhana mbaya zile za kizamani za kuonesha kwamba mtu akikamatwa anaenda kuadhibiwa, sasa hivi anaenda kurekebishwa. Kuna walimu wa urekebu kule wanapewa mafunzo, askari wetu wanawarekebisha wananchi na wakirudi kwenye jamii wanakuwa ni wananchi ambao wameondokana na zile tabia mbovu. Hiyo ni dhana nzuri ya kujivunia katika jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu ni kwamba zile zana ambazo tunazipata tuzitumie vizuri. TEHAMA tunajua sasa hivi inatumika kote katika magereza yetu. Tuendelee kuboresha mifumo hiyo, hata katika kuwakagua watu wetu wanaokuwa wamekamatwa na hatia mbalimbali wakaguliwe kwa vifaa na zana za kisasa kuliko kutumia mikono. Hiyo itaonesha zaidi utu wetu na ubinadamu wetu katika maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utumiaji wa nishati safi, niwapongeze sana katika magereza yetu yote. Hili

inatupa moyo kuonesha kwamba dhamira ya Mheshimiwa Rais inatekelezwa katika magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata zimamoto; tunampongeza sana Kamishna Jenerali John Masunga kwa kazi kubwa anayofanya katika hiki Kitengo chetu cha Zimamoto na Uokoaji. Tumekwenda pale Morogoro, tumeona jengo limeboreshwa na fedha ambazo zinatumika katika maeneo yote haya ninayoyataja ni *force account*. Hii *force account* kwa kweli katika magereza yetu pamoja na maeneo yote niliyoyataja imeonesha *value for money*. Kazi iliyofanyika imefanyika vizuri na fedha iliyotumika ni kidogo kulinganisha na mfumo mwingine ambao tungeweza utumia.

Kwa hiyo, hao pia niwapongeze sana, lakini niombe na Serikali wazingatie zaidi, Hazina iangalie umuhimu wa majeshi yetu haya kupeleka fedha kwa wakati na hasa fedha za maendeleo kwa mambo ambayo tunataka kuyaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikimalizia kwa mwisho ninaenda sasa kwenye Jeshi letu la Uhamiaji. Nitumie fursa hii kwa kipekee kabisa kumpongeza Kamishana Jenerali, mwanamama mwenzetu, Dkt. Anna Makalala kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuiboresha Uhamiaji. Kwa kipekee nipongeze makusanyo ambayo anaendelea kuyakusanya kila mwaka. Kwa kweli Jeshi la Uhamiaji ni imara na ninaamini chini ya uongozi wa mwanamama wetu litaendelea kuwa imara, pamoja na msaada wengine. Tuna chuo chetu pale Moshi, Chuo cha Uhamiaji ni chuo imara, chuo kizuri, chuo ambacho kinatoa wanafunzi wa Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana ndugu zetu wa *NSSF* ambao wanafanya mchakato wa kununua yaani Uhamiaji wanunue jengo la *NSSSF*. Tunaomba *NSSSF* kwa sababu ni kitengo cha Serikali wawaachie uhamiaji waanze kutumia na chuo hicho kiweze kuboreka wakati maendeleo ya kufanya utaratibu wa ununuzi yaweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikamilishe kwa kusema kwamba fedha ambazo tunazitegemea kutoka nje si salama sana kwa Wizara ya Mambo ya Ndani, nchi yetu ina dhana ya kujitegemea. Ninaomba sana tujitahidi kutafuta mapato ya ndani kwa ajili ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani kuliko kutegemea fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ninaomba sana sana ili kulinda heshima ya majeshi yetu yote tuliyonayo nchini mwetu chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, askari yeyote au afisa yeyote atayebainika anakwenda kinyume na maadili ya Taifa letu na misingi ya kazi zake basi ninaomba achukuliwe hatua ili kulinusuru jeshi letu kuonekana ni jeshi lisilo bora. Kwa sababu endapo atashughulikiwa mtu yeyote ambaye anaenda kinyume na maadili katika jeshi letu basi tutajenga heshima bora ya jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba Waheshimiwa Wabunge wote tuunge mkono hoja hii ili Wizara yetu iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Najma Giga, ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama nimekupendelea dakika moja, lakini Waheshimiwa Wabunge dakika ni tano, tano. Tumia vizuri dakika zako tano tumalize mambo.

Sasa nimwite Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi atafuatia Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ajiandae.

**MHE. MUHSIN HAJI USSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nami awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ametupa afya njema tukiwa katika Bunge hili Tukufu kujadili masuala muhimu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Rais wetu

wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea na kasi kubwa ya kuwatumikia Watanzania kwa moyo wa kizalendo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wetu, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Naibu Waziri, watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu. Hawa wote ni vijana na kwa bahati nzuri vijana hawa wanafikika sana. Waendelee kuliheshimisha Taifa na kumheshimisha Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ya Tanzania Mungu amebariki kuwa na heshima kubwa Afrika na duniani kwa ujumla, lakini heshima hii hatukuiokota jalalani wala haikuja kwa bahati mbaya, heshima hii imetokana na misingi imara, misingi madhubuti ya upendo na amani iliyoasisiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na Sheikh Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ali Mwinyi kwa kusimama imara kuendeleza misingi ya amani na misingi ya kutanguliza uzalendo wa kupenda Taifa letu kwanza kuliko jambo lingine lolote lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya leo siyo Tanzania iliyopita miaka 62 baada ya Muungano. Taifa letu limepiga maendeleo makubwa kwa sababu ya amani na utulivu ambao upo ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, niipongeze Wizara ya Mambo ya Ndani, nilipongeze Jeshi la Polisi, nipongeze Uhamiaji kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulinda amani ya nchi yetu na kulinda amani ya raia na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo haya tuliyokuwa nayo ukienda kushoto unakuta *SGR*, ukienda Kanda ya Ziwa unakuta Daraja la Kigongo – Busisi na barabara zinajengwa. Vijana wenzangu niwaambie nchi hii wakati tunapata uhuru haikuwa na lami, ni maeneo machache Dar es Salaam – Morogoro, na ni kwa sababu kulikuwa kuna kilimo cha mkonge kilichofanywa na wakoloni. Kule Tanga kulikuwa kuna barabara ya Tanga -

Korogwe kwa sababu ya kilimo cha mkonge na Arusha - Moshi. Leo barabara hizi zimejengwa nchi nzima, ni kwa sababu ya amani tuliyokuwa nayo kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, niwaombe vijana wenzangu tuitunze amani hii kwa sababu bila ya amani hatuwezi kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan licha ya changamoto zinazoikumba dunia ameuthibitishia ulimwengu ya kwamba Tanzania tuko imara na tunaendelea kuimarika kila uchao. Kutokana na maendeleo makubwa hayawezi kumpendeza kila mtu, kwa hiyo, vijana tusikubali kutumika kwa namna yoyote ile kupoteza amani ya nchi yetu ambayo ndiyo tunu inayotupa maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama Mbunge kijana, ninataka kuwahakikishia vijana wenzangu kwamba Wizara hii ya Mambo ya Ndani ipo kwa ajili ya maslahi ya kulinda Taifa letu na Wizara hii ipo kwa mujibu wa Katiba yetu. Katiba hii ya Tanzania ya Mwaka 1977 Toleo la 2005 Sura ya Tisa Ibara ya 147 imeweka wazi kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ina wajibu wa kuhakikisha ulinzi na amani wa nchi yetu na wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi vijana wa Zanzibar tumeonja athari zinazotokana na uvunjifu wa amani na ndiyo maana leo tunasimama imara kuungana na vijana wenzetu wa upande wa Tanzania Bara tunaounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kuhakikisha ya kwamba tunaungana kusimamia dhamira njema ambayo imeasisiwa na wazazi wetu ili kulinda amani kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo na vizazi vijavyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MUHSIN HAJI USSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia kwa sababu ya muda, wataalam wanasema hivi; wanadamu wengi tuna tabia na mapungufu ya kutokujua thamani ya kitu ambacho tunacho. Thamani hii tunakuja kuijua baada ya kitu hiki kututoka. Niwaambie vijana wa Kitanzania,

niwaambie umma wa Kitanzania, Tanzania yetu na Mheshimiwa Rais wetu tutakuja kumkumbuka kwa makubwa aliyoyafanya kwenye nchi hii. Tumuombe Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu, atimize ndoto na dhamira yake kwa kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu ya muda, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

Mheshimiwa Abdallah Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa muda. Mimi nianze kwa kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu, mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, lakini pia kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa salama na mahali salama zaidi katika uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi, mdogo wangu Mheshimiwa Patrobass Katambi pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud kwa kazi kubwa na nzuri sana wanayoifanya katika kazi hii. Nimpongeze Ndugu Ally Senga Gugu, Katibu Mkuu pamoja na watendakazi wote walioko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge kwamba tuunge mkono hoja hii kwa haraka sana ili wenzetu hawa waende wakatimize majukumu mazito kwa ajili ya ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo machache ya kuchangia katika hoja hii na eneo la kwanza ni eneo la Idara ya Uhamiaji; hapa Uhamiaji ningependa kufahamu tunazo nchi kadhaa ambazo hawapati *visa* wakati wa kuingia hapa nchini, tunaita *referral visa*. Sasa ni takribani miaka mingi sana karibia nchi 28

wanapotaka kuja Tanzania ni lazima waombe *visa* labda mwezi mmoja ama miezi miwili kabla. Hivi karibuni kwa mfano nchi ya Nigeria, Shirika la Ndege la Tanzania limeanza safari za kwenda Nigeria, lakini upatikanaji wa *visa* kati ya Tanzania na Nigeria una changamoto, kwamba ni lazima waombe mwezi mmoja ama miezi miwili kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niishauri Serikali kwamba sasa ni wakati wa kufanya jambo hili kuona kama vile vigezo ambavyo tuliviweka huko nyuma, je, mpaka sasa vina mashiko? Kama havina mashiko ni bora tuviondoe ili katika kutafuta kasi ya kukuza uchumi tuweze kushirikiana na wenzetu katika nchi ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kama nchi ya Nigeria wana uraia pacha, maana yake anaweza asitumie pasipoti ya Nigeria kuja Tanzania akatumia ya nchi nyingine, kwa hiyo, bado tunakuwa hatujatatua lile tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningetaka kuchangia, kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya, ninampongeza sana Ndugu James Kaji. Sasa tunawaona watu wa *NIDA* wakishuka katika ngazi za vijiji na ngazi za kata kwenda kuandikisha raia kule. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu sana na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tupitishe bajeti hii ili tuweze kuwapatia fedha, waweze kushuka zaidi kwenda kuandikisha wananchi wenzetu katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuhusu Jeshi la Polisi; tunacho kituo chetu pale Mlalo tumeshajenga kwa nguvu za wananchi. Tumetumia takriban shilingi milioni 70 na sasa tunahitaji kama shilingi milioni 35 ili tuweze kukikamilisha na ambacho kimebaki ni *tiles,* rangi na vitu vidogo vidogo. Kwa hiyo, niombe kupitia Inspekta Jenerali wa Polisi Camilius Wambura waweze kutupatia kiwango hiki kilichobaki ili tuweze kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuhusu usalama barabarani; ninalipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kuanzisha mafunzo mbalimbali ya huduma za madereva na sasa wameweza kutawanya, vyuo mbalimbali vinatoa mafunzo haya. Hata hivyo ninaomba nitoe rai kwamba wale madereva ambao tayari wameshapata mafunzo na ambao tayari wana uzoefu wanapohuisha leseni zao wasitumie muda mrefu sana siku hizi 14 za mafunzo, lakini mwezi mmoja kusubiri cheti ni muda mrefu sana. Kwa bahati mbaya sana, kwa sababu madereva wengi hawana ajira za kudumu, kipato chao kinategemea wakati wanapofanya kazi.

Kwa hiyo, ninawaomba sana pamoja na kuboresha eneo zima la usalama barabarani lazima tutambue pia kwamba madereva wengi hawana mikataba ya kazi, kiasi kwamba ajira zao zinategemea jasho la kila siku. Kwa hiyo, unapowaweka zaidi ya mwezi mmoja kupata mafunzo inawasumbua. Mafunzo haya ni muhimu, lakini ni vizuri tukaelekeza zaidi kwa wale ambao ni wapya, wako katika kutafuta hiyo kazi ya udereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, niliase sana Jeshi la Polisi hasa Idara ya Usalama Barabarani kwamba ni muhimu sana kukaa na wadau hasa hawa wamiliki wa vyombo vya moto kwa maana kupitia vyombo vyao vya *TATOA*, *TABOA* na kadhalika. Ni muhimu sana wenye magari waweke mikataba na madereva.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani ninaomba nusu dakika tu nimalizie hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana hawa wenye vyombo vya moto waweze kukaa na madereva kwa sababu una chombo cha moto chenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 200, 300, mpaka 400; unamkabidhi dereva ambaye hana mkataba na wewe na unaweza ukamfukuzisha kazi kwa njia ya simu tu popote alipo, hili sio jambo jema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sekta imeajiri watu wengi na ina watu wengi sana ambao tungewaweka katika mfumo ulio rasmi tungeweza kupata kodi. Pia hata pale watakapofikisha miaka 60 ya kustaafu wanaweza wakapata hifadhi za jamii kama wafanyakazi wengine wanavyopata katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, ahsante sana. Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija atafuatiwa na Mheshimiwa Hija Hassan Hija, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ajiandae.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kujadili hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Amiri Jeshi Mkuu wa Taifa kwa namna ambavyo anaendelea kuilinda nchi na kuhakikisha kwamba usalama wa nchi tunaendelea kuwa na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na watendaji wao wote kwa namna ambayo wanaendelea kuzitenda kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee sana ninamshukuru Mkuu wetu wa Mkoa wa Tabora, Ndugu yetu Paul Matiko Chacha na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wote wa Tabora kwa namna ambavyo Mkoa wa Tabora wameushika kuhakikisha kwamba Wana-Tabora tunaendelea kufanya kazi katika mazingira salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninamshukuru Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Ndugu Gerald Mongella

kwa kazi nzuri ya kuendelea kuimarisha usalama katika maeneo ya wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mkuu wetu wa Makazi wa Ulyankulu Ndugu yetu Jumanne Singani. Kwa nini nimeyasema hayo? Mimi ninatokea kwenye jimbo lenye kata tatu zinazokaliwa na raia wa kutoka nchi ya Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nizungumzie eneo hilo la wakimbizi; limeelezwa vizuri sana kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 165 mpaka 173. Raia hawa wapo ambao wamekwishapata uraia wa kuandikishwa, lakini ndani kuna wengine ambao bado hawajapata uraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuiomba Wizara kuharakisha jambo hili kuhakikisha kwamba sasa hao watu wanapata suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge tunaotoka kwenye maeneo hayo tunapata changamoto kubwa sana namna ya utendaji wa kazi katika maeneo hayo licha ya kwamba Wakuu wa Makazi wanatupa ushirikiano mkubwa. Kwa kuwa wananchi wanatupigia kura Wabunge na Mheshimiwa Rais, muda mwingi tunapata maswali mengi ya kuonesha kwamba wanapata wawakilishi kwa maana ya kutokea ngazi za vitongoji, vijiji, pamoja na kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuiomba Wizara ya Mambo ya Ndani waharakishe hili jambo la kupata suluhisho la kudumu katika maeneo hayo ili ikiwezekana wale wenye sifa ya kuendelea kubaki, wabaki na wawe na uhuru wa kuweza kupiga kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika Jimbo langu la Ulyankulu tunao takribani raia ambao walikuwepo walioletwa mwaka 1972 lakini walifanyiwa sensa mwaka 2007 mpaka 2008 tulikuwa na wakimbizi 54,180 lakini ambao pia walipewa uraia ni 47,918. Zoezi la uzinduaji wa kupewa vyeti vya uraia lilifanyika

tarehe 14 Oktoba, 2014 ambapo Ulyankulu zoezi hilo la ugawaji lilifanyika tarehe 25 Februari na tarehe 20 Machi, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati hili zoezi linafanyika kabla ya kusainiwa vyeti vya uraia, kulikuwepo na watoto waliozaliwa ambao kwenye utambuzi wa hivyo vyeti bado hao watoto wana changamoto kwamba wakati wa zoezi hilo walikuwa ndani ya matumbo ya mama zao. Mama alipata uraia na baba akapata uraia, lakini mtoto aliyezaliwa katikati kabla ya kusainiwa hivi vyeti vya uraia hana uraia. Kwa hiyo, hawa watoto wanashindwa waangukie kwenye eneo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka niiombe Wizara ione umuhimu wa kulifanyia kazi jambo hili na baadhi ya watu ili kuhakikisha kwamba linafikia hitimisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nilitaka kuzungumzia umuhimu wa ujenzi wa vituo vya polisi katika maeneo haya yanayozungukwa na makambi ya wakimbizi. Mimi kwenye eneo langu ninayo Kata ya Kashishi ambako tuna kituo cha polisi, lakini wamepanga kwenye Ofisi ya Serikali ya Kijiji na wanafanya kazi kubwa. Ninaomba Wizara ione haja ya kujenga au kuwapatia fedha za kujenga kituo cha polisi kwa sababu eneo wanalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo hilo kuna Kijiji cha Kigwangoko kwa maana ya Kona Nne. Askari wetu wamepanga kwenye nyumba ya mtu, raia wa kawaida, lakini pia wanalo jengo ambalo halmashauri ilitupatia fedha linahitaji ukamilishaji. Ninaiomba Wizara iweze kutupatia fedha ili tuweze kukamilisha eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumezungukwa na Msitu wa Hifadhi ya Kigosi – Muyowosi. Kwa upande wa Magharibi tunayo Kata ya Uyowa ambapo kwenye eneo hilo kuna kituo cha polisi, wafanyabiashara walijenga, lakini bado kinahitaji ukamilishaji tu. Askari wetu wamepanga ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba dakika moja nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde 30 malizia.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wamepanga kwenye nyumba ya Mwenyekiti wa Kitongoji. Ninaomba Wizara iweze kutuwezesha fedha ili kujenga vituo vya polisi pamoja na nyumba za makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jeshi ambalo linaongozwa na wananchi ambalo Baba wa Taifa alilizindua, Jeshi la Sungusungu. Ninaomba Wizara iweze kutunga sheria hili jambo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhael, muda wako ulikwisha na kengele ililia.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi, lakini hoja yangu ni Jeshi la Sungusungu liweze kutungiwa sheria ili liweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Hija Hassan Hija atafuatiwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu ajiandae.

**MHE. HIJA HASSAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na nimpongeze kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake na niwaombe Wabunge wenzangu tuiunge mkono leo hotuba hii ili tumuwezeshe Mheshimiwa Waziri afanye kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kabisa ninaomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa jinsi wanavyoendelea kufanya kazi na kujenga vituo vya polisi katika maeneo mbalimbali Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi hiyo ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uamuzi wake wa kujenga kituo cha polisi ndani ya Jimbo la Kiwani ambapo hadi ninazungumza hapa hatua ambayo imefikia, imefikia hatua nzuri ya kumalizia boma. Sasa imebakia hatua ya kuezeka na kumalizia jengo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninaomba nimpongeze Kamishna wa Polisi Zanzibar kwa kumteua *Engineer* Filbert kama *engineer* wa usimamizi wa mradi ule kwa jinsi ambavyo alivyofanya kazi ya kifanisi, ya kizalendo na utaalamu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtendaji huyu kwa kweli ana uwezo mkubwa na ana moyo na utendaji wa hali ya juu. Kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Kiwani nimpongeze kwa jinsi alivyosimamia jengo hili na leo jengo lipo vizuri, tunasubiri hatua ya umaliziaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Mheshimiwa Waziri na na Wizara nzima, Ukanda ule wa Mashariki ya Kisiwa cha Pemba askari wetu hawa wanapata kazi sana wakati wa ufanyaji wa doria. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri sasa baada ya kumalizia vituo vyetu ajipange sasa kuwatafutia usafiri wa gari ili askari wetu wafanye kazi za doria kwa ufanisi na kwa usalama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kujenga Kituo cha Polisi Kengeja. Jengo ambalo ni la muda mrefu, lakini sasa kunajengwa jengo jipya ambalo litawezesha polisi wetu kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa hoja yangu ya pili ya wizi wa mtandao. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri kwenye eneo

hili lazima nguvu iongezwe ili Watanzania wapate ufanisi na wapate usalama wa mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa minajili ya kuweka wazi, mimi ninaomba nitoe ushuhuda kama mhanga wa jambo hili ili Mheshimiwa Waziri aweze kufuatilia vizuri. Nimekuwa nikipata kazi sana ya kudukuliwa na kuibiwa tangu mwezi Januari. Nimechukua juhudi kubwa ya kutafuta ni nani anafanya uhalifu huu na kuharibu taswira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCRA* wanafanya kazi kubwa ya kuwagundua wahalifu hawa, lakini kunakuwa na tatizo la umaliziaji katika huduma ya kipolisi. Ushauri wangu Wizara ikubali sasa kuwa na dawati maalum *TCRA* ili polisi wetu wawe karibu na huduma hii ili kuzuia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba ninukuu *message* ambayo mhalifu amenitumia na uone uzito wa hili jambo. Ninaomba kunukuu ananiambia; "Nimelipia 260,000 ili nipate akaunti yako ya benki nikuibie. Leo ninaomba kutoa 600,000 kwa ajili yangu."

Mheshimiwa Naibu Spika, na kweli katoa fedha kwenye akaunti ya benki. Ninaomba benki niisitiri nisiitaje kwa usalama wa huduma, lakini jambo hili halipendezi kwamba sasa mhalifu anaingia kwenye mfumo wa benki, anachukua hela. Hofu yangu ni kwamba jambo hili likizoeleka maana yake mpaka wawekezaji watapata hasara na nchi itakula hasara katika sekta ya uwekezaji na sekta ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri nitampatia vielezo vya jambo hili, nitampatia *RB* ambayo nimelalamika ili jambo hili lifuatiliwe. *Interest* yangu ni kujua huyu jamaa akalipia wapi kupata siri zangu za benki wakati hata mke wangu hajui siri ya benki yangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hoja hizo niipongeze Wizara kwa jinsi wanavyofanya kazi na waweke sawa jambo hili ili nchi yetu iende vizuri na iwe salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hoja hiyo ninaunga mkono hoja na Waheshimiwa Wabunge wote waunge mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaongeza muda mpaka tumalize shughuli ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, atafuatiwa na Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia katika muda huu na siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza na kumpongeza zaidi Amiri Jeshi Mkuu wa Tanzania, Mkuu wa Majeshi yote Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa usimamizi mzuri wa majeshi yetu kwa kuleta amani katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niweze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutenga fungu kubwa la pesa (shilingi trilioni 2.4) katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Yote haya anayafanya kwa sababu anataka amani, utulivu, usalama na amani ya wananchi wake na wafanyabiashara wote katika nchi hii ili amani iwe imetusaidia katika nchi yetu na iweze kusaidia zaidi katika utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba katika Serikali, shilingi trilioni mbili zilizotengwa ziweze kwenda kwa wakati katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Watakapopelekewa pesa hizi watafanya kazi kwa wakati na kazi itafanyika vizuri kuliko kuwepo na ucheleweshaji au kwenda na bajeti ndogo, haitoleta tija katika kazi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya. Ninawapongeza vijana wanafanya kazi vizuri na wana ushirikiano, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza *IGP* Wambura. *IGP* huyu ni kijana, mchapakazi, msikivu, mwadilifu na ni mpenda watu na anasikiliza watu kwa ukaribu. Pia nimpongeze sana kwa kazi zake anazofanya. Anafanya kazi kwa ukaribu na kila mmoja anapokwenda katika ofisi yake ana shida naye na shida yako inashughulikiwa kwa wakati na muda huo huo. Ninampongeza sana, ni kijana ambaye anajitahidi sana na ni mtulivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika amani tunayoiona sasa hivi mabasi yetu yanatembea usiku mzima, mchana na usiku, maduka yanafunguliwa mpaka saa tano mpaka saa sita, unatembea bila mashaka yoyote mitaani kwa sababu ya amani na utulivu katika nchi yetu. Haya anayoyafanya na anayasimamia kwa sababu ametengeneza Polisi Kata katika kata zetu zote nchi nzima. Hili linaleta tija katika kupunguza uhalifu katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amelifanya kwa uadilifu mkubwa na tunampongeza kwa zaidi na zaidi na *salute* tunampigia. *IGP* unastahili sifa sana katika Tanzania yetu na umeweka heshima kubwa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka zaidi ninaomba nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Tabora. Mkuu wetu wa Mkoa wa Tabora kama tunavyoona kwenye vyombo vya habari na uhalifu mbalimbali umetokea, lakini ninampongeza yeye na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa. Peke yake asingeweza kuyafanya, lakini kwa ushirikiano Kamati yake ya Ulinzi na Usalama yapo ambayo yaliyofanyika walioiba kupitia mtandao, lakini wengine ni matapeli wameweza kufika katika mkoa wetu na wamekamatwa. Ninawapongeza sana viongozi wangu wa mkoa, na wakuu wa wilaya na ma-*OCD* wote wanaoshiriki pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yasingefanyika kama wasingeweza kuwa na bajeti nzuri. Kutafuta wahalifu kunahitaji bajeti na kama bajeti inakuwepo ni rahisi zaidi kuwapata wahalifu. Fungu linapokuwa dogo, *RPC* anakuwa na fungu lakini fungu linakuwa dogo. Je, *RC* na yeye hana fungu? Kwa hiyo, ni vigumu sana kuweza kufanya kazi yake hiyo ili kuweza kupata wahalifu katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote hayo yasingeweza kufanyika. Nimuunge mkono Mheshimiwa Mbunge ambaye amemaliza muda wake wa kuongea. Kuna uhalifu mkubwa ambao upo katika nchi yetu wa mitandaoni na uhalifu wa mitandaoni wakienda katika Airtel au Vodacom au wapi, kampuni hizi wanawapa *statement* waende polisi. Tunawapa kazi bure polisi kwa sababu mshtakiwa wa kwanza ni kampuni hizi ambazo zinaweka simu na *line*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu moja tu tulikwishasajili *line* mara mbili ili kuhakiki uhalifu katika nchi yetu, lakini muda wote tumesajili hakuna chochote kinachotokea, matatizo bado yapo, watu wanaibiwa, watu wanatapeliwa na watu wanatukanwa katika mitandao. Sasa sijui tatizo linakuwa wapi ambao tunashindwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishauri Serikali watuletee sheria hapa Bungeni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watuletee sheria hapa Bungeni ya kuweza kuzibana hizi kampuni, uhalifu wowote unapotokea kampuni hizi ziwe ni za kwanza ambazo zitawajibika bila ya kupoteza nguvu za wananchi na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niunge mkono hoja 100% na tuunge mkono Waheshimiwa Wabunge wenzangu ili tuwape nguvu, waende wakafanye kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aziza, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niungane na wenzangu kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu amejitahidi sana kusimama na kuhakikisha nchi inaendelea kuwa salama na yenye amani wakati wote. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumuunga mkono, kumpongeza lakini kumtia nguvu aendelee kufanya kazi zake na sisi tukiwa nyuma yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Wizara ya Mambo ya Ndani kwa namna ambavyo inafanya kazi vizuri. Kumekuwa na amani na usalama wa raia na mali zake wakati wote na pia wamekuwa rafiki wa raia kwa maana ya kushirikiana wakiungana na polisi jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze kwa dhati kabisa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Katambi, kijana mweledi, lakini akili kubwa. Mwenyezi Mungu akuongoze uendelee kuitumikia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Naibu Waziri kaka yangu Mheshimiwa Ayoub, mtu rahimu kabisa, anafikika, anasikiliza na hii ndio dhana nzima ya uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Makamishna Jenerali wa Polisi, Uhamiaji, Magereza, Jeshi la Uokoaji na Mkurugenzi wa *NIDA* kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongelee masuala mazima ya mazingira mazuri ya kufanyia kazi askari wetu. Mahali pengi katika nchi hii askari hawana makazi mazuri na hususan katika Mkoa wa Singida na katika Jimbo langu la Singida Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za askari zilizopo, Askari Magereza na Polisi ni nyumba ambazo ni za zamani mno. Zingine mimi nimezishuhudia tangu ninakua na mpaka leo bado wanazitumia za muundo wa kikoloni zenye chumba kimoja na sebule basi. Huu sio utu kwa watu wanaofanya kazi kubwa kama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu mkubwa pia wa nyumba za askari. Hii inasababisha askari kukaa nje ya kambi na wakati mwingine inapotokea dharura inakuwa ni vigumu kuwapata kwa wakati, lakini pia tunahatarisha usalama wao wanapokuwa wanakaa uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kunakuwa na kupoteana kwa askari wakati mwingine, maana huyu anatoka huku, huyu anatoka huku. Kwa hiyo, niombe sana tutengeneze na tuwatengenezee mazingira mazuri ya kuishi kwa maana ya kuwajengea nyumba nzuri na bora, lakini vilevile tuwatafutie vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna idara hazina magari kabisa. Uhamiaji Singida ina gari moja tu la Mkoa. Magereza ina gari moja la zamani *Land Rover* ya mwaka 2006. Utendaji kazi unakuwa mgumu kwa ajili ya kukosa vitendea kazi vizuri, lakini liko jambo zuri wanalolifanya polisi kwa maana ya kuleta Kituo Jumuishi cha Ukaguzi wa Magari pale Singida. Jambo la kusikitisha wanataka kugeuza eneo la *parade* kujenga kituo hicho. Nimwombe sana ndugu yangu *IGP*, Singida ina nafasi kubwa na yeye anajua umuhimu wa *parade*. Twende tukashirikiane tupate eneo lingine ili tuachie lile eneo la polisi kwa ajili ya kufanya *parade* na kujenga ukakamavu kama ambavyo inakusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee habari ya *NIDA*. Nipongeze sana Serikali wameweka fedha nyingi na wananchi wamefuatwa kwenye maeneo yao, na kwa siku 18 Jimbo la Singida Mjini limesajili karibu watu 10,800 na wote hawa wanategemea kupata vitambulisho vyao vya *NIDA* muda mfupi ujao. Ninaomba sana Serikali, tutoe elimu ya matumizi sahihi ya *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanasajiliana laini, mtu akisajiliwa laini na mtu mwingine anafanya uhalifu, halafu anayepata shida ni yule aliyesajili kwa jina lake, na wanafanya hayo kwa kutokujua madhara ya kumsajilia mtu laini. Tuombe elimu itolewe, watu waelewe umuhimu wa kuwa na *NIDA,* lakini matumizi sahihi ya *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nimpongeze Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Singida, Dada yangu Halima Dendegu. Yeye na Kamati yake ya Ulinzi wamesimama vizuri kuhakikisha Singida ambayo iko katikati ya nchi, lango la wahalifu kama mtu ataamua kufanya uhalifu maana yake barabara ni nzuri ya Mwanza, ya Dodoma, ya Arusha lakini wamejitahidi kudhibiti na kusimamia usalama wa wilaya yetu mkoa wetu kwa ujumla.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri na Naibu Waziri, lakini nipongeze taasisi zote zilizoko chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini Jemedari wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuhakikisha kwamba Taifa liko salama, Taifa linaendelea katika hali ya amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo kubwa sisi na Watanzania tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa sababu usalama wetu ndio kipaumbele kikubwa cha nchi yetu, ndiyo *national interest* yetu kwamba *security* ni moja kati ya maslahi makubwa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mambo machache ya kuchangia. Jambo la kwanza, la kuchangia moja kubwa ni kuhusu hali ya usalama kwenye Taifa letu. Mheshimiwa Waziri, kwanza lazima tufahamu, nchi yetu tuko na *security dilemma* katika dunia, lakini kuna *security threats* ambazo zinaendelea duniani. Kwa hiyo, *investment* yoyote ile katika nchi, *budget* yake kubwa inakuwa ni mambo ya ulinzi na usalama na kuhakikisha kwamba wananchi wako salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama nchi, tumekuwa tukikumbwa na matukio haya ya kuwa na *security dilemma*, lakini zaidi mambo ya *cyber crimes*, unafahamu mambo ya *cyber espionage* ambayo yamekuwa yakitokea. Sasa ninaushauri kwa Serikali; nchi yetu ni nchi ambayo watu wengi wanaimezea mate kutokana na hali ya utulivu tuliyonayo. Kwa hiyo, wamekuwa wakifanya matukio na mambo ambayo yanahusisha kuleta mtafaruku kwenye nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwenye ripoti yenu mnaonesha kwamba kuna wahamiaji haramu kadhaa ambao wameingia kwenye nchi yetu, takribani 49,469 wameingia kwenye nchi yetu na hii inaashiria kwamba hawa wengine wengi unakuta sio kwa ajili ya mambo mema, zaidi ni mambo mabaya. Sasa tukirejea katika msingi wa Mwalimu Nyerere ambaye alianzisha mfumo wa nyumba kumi, ulikuwa ni mfumo wa kuhakikisha kwamba nchi inakuwa salama, kuhakikisha lazima tujue nani yuko

wapi, nani anafanya nini ili nchi iwe salama. Sasa sisi kama nchi kwa sababu teknolojia imekua, lakini pia idadi ya watu imeongezeka, tunazungumzia Watanzania zaidi ya milioni 65 na kuendelea juu, lazima kuna mambo tuyafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza Mheshimiwa Waziri ni lazima turejeshe mfumo wa nyumba kumi. Kenya wameuchukua mfumo huo mwaka 2022 kuurejesha mfumo wa nyumba kumi, kutambua wananchi, nani anaingia katika kijiji, nani anaingia katika mtaa, watendaji wa mitaa na watendaji wa vijiji hili ni eneo la kulifanyia kazi kwa sababu wanalipwa na Serikali, tukiwatumia hawa wanaweza kusaidia kugundua ni nani yuko katika eneo husika ili waweze kutusaidia kuimarisha ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kama ambavyo Nelson Mandela anasema; "*safety and security don't just happen; they are the result of collective consensus and public investment.*" Jambo la pili ni lazima tudhibiti usajili wa laini za simu holela. Suala la usajili wa laini za simu holela kwenye nchi yetu umekuwa ukifanyika katika mazingira mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakutana na vijana wanatembea mitaani huko vijijini, wanasajili laini za simu au wanajitambulisha kama wao wanatoka kwenye taasisi hizi za mitandao ya simu. Ni lazima tuidhibiti ili tuweze ku-*control* suala la utapeli, wizi na kuumiza wananchi wetu na hili ili liwe *collective consensus* lazima Wizara ya Mawasiliano ishirikiane kupiga *stop* suala la kusajili laini za simu kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda Rwanda, ukienda *South Africa,* huwezi ukaenda mtaani ukasajili laini ya simu kiholela, ni lazima uende kwenye ofisi rasmi au *kiosk* rasmi, uweze kusajili laini ya simu ili watambue ni nani anayesajili laini hiyo. Hiyo ni muhimu katika nchi hii. Tulidhibiti hilo jambo, kwa sababu wananchi wanaumizwa kwa kuibiwa fedha na kwa kutapeliwa kwa sababu pia watu wanaozunguka huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wataalam kwamba tunawazuia wasifanye ajira za kujitolea, hapana, kwa sababu

tumeona takwimu ya usalama imekuwa ikiyumba kutokana na matukio kama haya, ni lazima hili eneo tulidhibiti kusajili watu laini, zisajiliwe katika utaratibu ambao ni rasmi, kwenye *viosk*. Mheshimiwa Waziri hilo ni jambo la muhimu mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Mheshimiwa Waziri, ninaipongeza Wizara mmekuwa na mfumo mzuri kwenye *traffic* kutambua kwamba hili gari ni la nani, mnafanya mfumo *verification*. Sasa lazima tutengeneze mfumo wa *verification* kwenye mahoteli, kwenye *lodges*, kwenye watu wote ambao wanafanya biashara ya kupangisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu gani Mheshimiwa Waziri? Hadi dakika hii ninavyozungumza kuna mtu anaenda kwenye hoteli anaandikisha jina ambalo sio la kwake na analala na anaondoka kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, ni lazima nchi kama tunataka kufanya mambo ambayo yanahusisha ulinzi wa nchi yetu, kwenye hoteli kote lazima tutengeneze mfumo. Mtu anayeenda kulala pale atoe *NIDA*, atoe *passport* yake, au atoe kitambulisho cha kupigia kura. Wakiingiza kwenye mfumo waone jina linalosoma ni la Mtanzania *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga hitimisha, muda wako umeisha, sekunde 30 malizia.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu.

Kwa hiyo, niwaombe, kwa sababu ninyi mmeanzisha *campaign* inaitwa mjue jirani yako; mjue jirani yako haiwezi kufanya kazi kama teknolojia hatujaisimamia. Tengenezeni mfumo wa kufanya *verification*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba zote zinazopangisha, hoteli zote na *guest* zote, lazima mtu afanye *verification* ili aweze kupata dhamana ya kupangishwa maeneo hayo. Ili vitendo vya ushoga, magenge ya watu haramu na matapeli tuweze

kuyadhibiti, ni lazima tujue nani yuko wapi na anafanya nini kwa wakati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zilikuwa chache, nina hoja nyingi za kuchangia kwa mustakabali wa Taifa letu, lakini katika haya, nitayaleta kwa maandishi Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia asubuhi hii na ninamtanguliza Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze ya pongezi nyingi kwa Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya na kuhakikisha kwamba Tanzania bado tuko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri wetu wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Katambi kwa kipindi kifupi tu amefanya kazi nzuri, lakini nimpongeze pia Naibu Waziri Mheshimiwa Ayoub Mohammed kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninawapongeza sana wakuu wa vyombo vyote vya usalama walioko hapa ndani, ningekuwa nimevaa kijeshi maana yake nami nilienda JKT, ningewapigia *salute,* lakini nimpongeze sana dada yetu afande Dkt. Anna Makakala, ametuwakilisha vizuri sana katika hicho chombo, hapo juu kwa kweli hajawahi kutuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze *RPC* wangu wa Mkoa wa Iringa kwa kazi nzuri na vyombo vyote vya Iringa kwa kazi nzuri wanayoifanya akiwepo na Mkuu wetu wa Mkoa. Ninampongeze *OCD* wetu wa Wilaya ya Kilolo na vyombo vyake, Kilolo iko salama na tunashirikiana nao vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali kwa kupatiwa gari la zimamoto na wewe ulikuwa Waziri uliniahidi, ninakushukuru sana gari la zimamoto nimelipata na tayari tulikuwa tumeunguliwa na bweni pale Ilole, dakika mbili walifika na wakazima moto, ninashukuru sana Jeshi la Zimamoto kwa kutupatia gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilolo, tumekizungumzia muda mrefu, lakini tumepata. Changamoto kubwa askari wetu hawajawahi kujengewa makazi, wanaishi kila mtu anaishi kivyake kiasi kwamba akihitajika kwa haraka ni kazi kubwa sana. Ninaomba ile kambi Kilolo ianze.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jamani msinicheleweshe dakika ni chache. Mheshimiwa kama utanipa muda nipe, la sivyo sitaki hata taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za polisi ni muhimu sana, Kilolo hawajawahi kujengewa, lakini vilevile askari Kata ya Kilolo wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, hawana vyombo vya usafiri. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na changamoto kubwa ya Kilolo barabara hazifikiki, ninaomba askari polisi wa Kilolo wapatiwe japo pikipiki na ikiwezekana hata mimi nitaanza kutoa pikipiki kwa askari polisi wa Kilolo ili wafanye kazi vizuri, tusiwalaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa Kituo cha Polisi cha Ilula, nacho kimechakaa sana maana yake kinafanya kazi kubwa, kiko barabarani, kipatiwe pesa, kijengwe upya na askari waliopo waangaliwe, hawana hata nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nielezee kuhusiana na Gereza la Kihesa Mgagao. Jamani kwa muda mrefu sana nimechangia Wabunge wote waliokuwepo Kilolo wamechangia liondolewe. Pale ilikuwa ni kambi ya wapigania uhuru, wafanye kama wenzetu wa *South Africa.*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ile kambi ilikuwa ya wapigania uhuru na pale kuna watu kutoka *South Africa,* wamelala pale akina Mandela, Angola, Zimbabwe. Tunaomba kile kiwe kivutio na ikiwezekana watu waje waangalie kutoka nchi nyingine kama zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu *South Africa* lile gereza sasa hivi si gereza, mimi mwenyewe nilitembelea lile gereza, nikalipa pesa kwenda kuangalia sehemu ambapo Mandela alifungwa. Tunaomba sasa Kihesa Mgagao jamani, sasa lile gereza lihamishwe.

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba kujua Serikali imefikia wapi mchakato wa kupata hadhi za Watanzania wenye uraia ambao sio nje kwamba lini sasa ule mchakato utafikia? Tunao Watanzania wanataka kuwekeza Tanzania, tunao Watanzania wanatakiwa watambulike, wamekuwa wakileta pesa nyingi sana hapa nchini kwa ajili ya kuwasaidia ndugu zao, lakini mpaka leo hadhi ile ambayo walisema kwamba tutaipitisha, bado haijapitishwa.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, atuambie sasa ni lini ili watoto wetu na ndugu zetu wale tulisema kwamba hautakuwa uraia pacha, lakini hadhi wapewe, kuna Watanzania ambao wamezaliwa nje ili watambulike kwenye nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho sheria za askari zimepitwa na wakati zihuishwe. Ninao mfano ningekuwa na muda ningetoa mfano jinsi ambavyo zinawatesa askari wetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabati muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI**: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, lakini ninaomba Mungu aibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Fadhili Liwaka, ajiandae Mheshimiwa Said Ali Mbarouk.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii adhimu, lakini nitumie fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa sana, kumpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Patrobass Katambi na Mheshimiwa Ayoub kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika tunapomuona Mheshimiwa Katambi na Mheshimiwa Ayoub inatupa picha namna ambavyo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu ameendelea kuwa na imani na vijana na kuwatumia katika kuendesha nchi hii iliyobarikiwa na Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niweke rekodi yangu sawa, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na moja kati ya jambo kubwa ambalo tumeliona na tumelipitia katika kipindi chote tukiwa katika Kamati ni pamoja na mapinduzi makubwa yaliyofanywa katika idara zetu za ulinzi ikiwemo Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji, Vitambulisho vya *NIDA* pamoja na vitengo vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya kazi kubwa sana. Ninafikiri alipoingia madarakani, alitazama Jeshi letu la Polisi, akalitazama Jeshi la Magereza, akaitazama Idara ya Uhamiaji na akatazama Mamlaka ya Vitambulisho *(NIDA)* na akaamua kuweka nguvu, bila kutia shaka yoyote, na kufanya mapinduzi makubwa kwenye eneo la utekelezaji wa miradi kwa ajili ya askari, mapinduzi makubwa kwenye eneo la uhuishaji Vitambulisho vya Taifa, lakini pia upatikanaji wa *passport* za kisasa ambazo zina uwezo mkubwa wa kutambua vielelezo vya mhusika bila mashaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, amefanya jitihada kubwa kuhakikisha kwamba magereza zetu nchini zinabadilika kutoka kuwa chombo kinachoonekana kama ni sehemu ya kwenda kuumiza na kubadilika kuwa chombo cha mafunzo. Mimi na Kamati, na Wabunge wenzangu watakuwa mashahidi tumetembelea, tukaona magereza zikitoa mafunzo ya ujenzi, mafunzo ya ufundi, mafunzo ya kilimo na mafunzo mengine kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya, ninaomba nizungumze na Watanzania wenzangu. Majeshi haya ni ya kwetu sisi, hatuna nchi nyingine wala hatuna majeshi mengine. Leo hii Jeshi la Polisi limepewa dhamana kubwa ya kupigania na kulinda haki za raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza kulinda mali na raia, anayeweza kudhuru mali siyo mnyama, anayeweza kumdhuru raia siyo mnyama na ndio maana wanyama tumewapa Jeshi la Uhifadhi wawafuatilie. Tumekwenda mipakani tukawapa jeshi walinde mipaka yetu. Hawa polisi, kazi yao kubwa ni kuishi na sisi kwenye jamii, na sisi ndio watu wema na sisi ndio watu wabaya ambao polisi hawa wana kazi ya kupambana nao.

Mheshimiwa Spika, kwa nia njema kabisa, na dhati ya moyo wangu, ninapenda niuhakikishie umma wa Watanzania kwamba Jeshi la Polisi ni miongoni mwa sisi Watanzania tunaoishi kila siku. Kinachotutofautisha na Jeshi la Polisi ni kwamba polisi wanaweza

kuvaa gwanda wakati wakitimiza majukumu yao kwa mujibu wa viapo, na sisi tukavaa kiraia tukafanya shughuli zetu. Kila wakati ni lazima wakae nyuma ya maisha yetu, wakae mbele ya maisha yetu, wapambane usiku na mchana. Tena ni watoto wetu, tena ni baba zetu, tena ni mama zetu. Wakifanya kazi kwa uchungu kulilinda Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pasitokee mtu mwingine yeyote mwenye maslahi ya kisiasa, maslahi ya kikabila na maslahi mengine yoyote akajaribu kuweka mpaka wowote kati ya Jeshi la Polisi na raia wa Tanzania. Jambo hili ni lazima tulikatae na lazima tuhakikishe kwamba polisi wanakuwa sehemu yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa sana amani, leo hii Wabunge hapa wamechangia vizuri sana, yapo matukio yanaweza kutokea kwenye nyakati unashangaa, yanatoka wapi, lakini baada ya muda mchache, polisi wanachukua hatua ya kwenda kudhibiti.

Mheshimiwa Spika, sote hapa ni mashahidi, hapa katikati tulikuwa tumepata shida sana namna tunavyoweza kusafiri, leo polisi hawa, Kamishna Jenerali Wambura, ndiyo wanaofanya kazi ya kulinda Watanzania wanapotembea usiku kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa hawa polisi wetu tunaowaona hapa ndio ambao wamedhibiti na kupambana na matishio mbalimbali, yale yanayotokana na uchu wa watu kutoka nchi nyingine na wale wasioitakia mema nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa dhati ya moyo na kwa sababu binadamu tumeumbiwa moyo wa shukrani, na sisi tumezaliwa, tukanyonya maziwa, tukamshukuru Mungu, lazima tushukuru pale tunapolindwa na lazima tuwaombee kheri wale wanaotulinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya ulinzi ni kazi ngumu sana, kazi ya kutetea haki ni kazi ngumu sana na kazi ya kulinda maslahi ni kazi ngumu sana. Kwa sababu unapolinda yupo unayemzuia,

unapolinda yupo unayemuumiza kwa kumzuia. Hivyo basi, kwa heshima kubwa na unyenyekevu mbele ya Bunge lako Tukufu, ninawaomba Wabunge wenzangu na Watanzania wote Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji eneo la Vitambulisho la *NIDA* ni mali yetu sisi Watanzania na mtu yeyote asiipore kuipeleka kwa mtu mwingine na kutuondolea unasaba tulionao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, ninashukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Said Ali Mbarouk.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kuzungumza machache sana katika bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, nininaomba nimuunge mkono msemaji aliyemaliza kusema kwamba tujitahidi hapa Tanzania (nchini kwetu) kusiwepo na wanasiasa au mtu mwingine yeyote ambaye atawatenganisha vijana wetu wa polisi na raia kwa ujumla. Hili ni jambo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi ninatoka Pemba Kaskazini ambako bahati mbaya taswira ya wananchi wengi na Jeshi la Polisi haiko vizuri. Sasa ninashauri sana kwamba jitihada zifanyike kulisafisha Jeshi letu la Polisi kwa raia na kwa wananchi na ninaomba sana Ripoti ya Haki Jinai ambayo Jaji Chande aliwasilisha na mapendekezo yake kuhusu Jeshi la Polisi na kulijenga upya, yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi halipaswi kuwa jeshi la kutumia nguvu kupita kiasi kwa raia, linapaswa kuwa jeshi ambalo linajenga mtengamano baina ya raia zaidi katika kutekeleza mambo yake. Miezi sita iliyopita nilikutana na askari polisi mstaafu, aliyestaafu katika cheo cha *sergeant,* ana baiskeli anachuuza samaki na tenga *(fishmonger)*. Nikamuuliza sheikh vipi? Akaniambia; "tatizo Mheshimiwa tuna kikokotoo ambacho kinatuumiza sana sisi polisi. Wenzetu askari wengine hawana, lakini

sisi tumewekewa hiki. Kiinua mgongo ambacho tunakipata kwa kweli kinatudhalilisha katika maisha.”

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye hili ninaiomba sana Serikali, ninaomba sana Waziri na Naibu Waziri, hili ni jambo la kuhakikisha kwamba vijana wetu ambao tumewatumia, wametumika na kwa namna ambavyo wametumika sasa wako mbali sana na raia. Huyu jamaa anauza Samaki, lakini anaweza kuwa na samaki wazuri wananchi hawanunui. Kwa sababu gani? Kwa sababu alipokuwa ndani ya Jeshi la Polisi matendo yake hayakuwa mazuri na raia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ni jambo la kuwasaidia kwamba watu ambao tumewatumia na wametumikia, hatimaye tunawapa jambo dogo sana kama kiinua mgongo katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninaomba nizungumze ni kwamba miaka 10 iliyopita pale Zanzibar mikoa yote mitano Makamanda wa Polisi wa Mikoa, wa Wilaya, na Makamanda wa Upelelezi wa Mikoa na Wilaya walikuwa ni vijana wa Kizanzibari ndani ya Zanzibar. Kaskazini Unguja alikuwa anaenda Kusini Pemba wa Kusini Pemba alikuwa anaenda Mjini Magharibi.

Mheshimiwa Spika, dakika hii ambayo mitano mitano hivi kuna *exchange* kubwa. Vijana wetu kutoka Bara wamekuja Zanzibar. Ni jambo zuri sana katika kujifunza na kubadilishana Mawazo, lakini ukipiga mahesabu utaona vyeo hivi 10, vitano vya polisi Makamanda *RPC* na *RCO, OCD* 11 na wapelelezi 11 utawaona kama wako 50 na wengine wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, suala langu ambalo Mheshimiwa Waziri ninaomba ajiulize; je, vijana kama wale Wazanzibari 50 wamehamishiwa huku na wamepatiwa *portfolio* zilezile, isiwezekane na hili lazima tulifanyie kazi kwamba vijana kutoka upande wa pili wa Muungano wamekuja kule halafu kusiwe na vijana wengine wanaokuja huku kwa *portfolio* zilezile ama tusione kwamba kuna angalau vijana watano au sita wamechukua

nafasi za *RPC* katika mikoa ya huku na wengine 11 ambao ni *OCD* wamechukua nafasi wamekuja huku. Ikiwa hivyo litakuwa ni jambo baya katika kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika. jambo lingine ambalo ninaomba nilizungumze, kumekuwa na hoja na mambo haya ni vizuri yafanyiwe kazi kabla hayajatufikisha katika masuala ya kero za Muungano. Tangu tupate uhuru...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante, kengele ya moja.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MOHAMMED KASSIM SALUM:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuimarisha usalama wa nchi yetu. Tanzania imeendelea kuwa moja ya nchi zenye amani na utulivu Barani Afrika jambo ambalo ni msingi mkubwa wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo pamoja na mafanikio hayo bado kuna maeneo yanahitaji nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha Polisi Jamii; Jeshi la Polisi liendelee kujenga ukaribu na wananchi. Wananchi wengi bado wana hofu ya kutoa taarifa kutokana na kutokuamini mifumo ya usiri na ulinzi wa taarifa zao. Serikali iongeze elimu ya Polisi Jamii na matumizi ya teknolojia katika utoaji taarifa za uhalifu.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya uhalifu wa kidijitali; kwa sasa vijana wengi wanatumia teknolojia, lakini pia kumekuwa na ongezeko la utapeli mtandaoni, wizi wa fedha kwa njia za simu na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii. Wizara iongeze uwekezaji katika vitengo vya *cyber crime* na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu usalama wa kidijitali.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya askari; askari wetu wanafanya kazi kubwa katika mazingira magumu. Serikali iendelee kuboresha makazi, vifaa vya kazi, huduma za afya na stahiki zao ili kuongeza morali ya kazi.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa magereza; magereza yasibaki kuwa maeneo ya adhabu pekee bali yawe sehemu ya marekebisho pia. Vijana waliopo magerezani wajengewe uwezo wa ufundi na elimu ili wakitoka wawe sehemu ya maendeleo ya Taifa badala ya kurudia makosa.

Mheshimiwa Spika, vijana na ajira; sehemu ya uhalifu inachangiwa pia na ukosefu wa ajira kwa vijana. Serikali iunganishe nguvu kati ya Wizara hii na Wizara zinazoshughulikia vijana na uwekezaji ili kupunguza mazingira yanayochochea uhali.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusisitiza kuwa usalama wa Taifa si jukumu la vyombo vya dola pekee, bali ni wajibu wa kila Mtanzania. Tuendelee kushirikiana kulinda amani, umoja na mshikamano wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kupitia Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia mambo machache katika Wizara ya Mambo ya Ndani; niombe Serikali iendelee kuboreshe mazingiza ya kufanyia kazi askari wetu sambamba na makazi yao kadri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione uwezekano wa kuwaingiza askari wetu kwenye Mfuko wa Fidia *(Workers Compensation Fund)* kwani mazingira ya kazi zao yanawaweka kwenye hatari ya kuumia na kupata ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione umuhimu wa kuandaa program maalum ya kuelimisha jamii kuwa jeshi la polisi ni jeshi la wananchi ili kujenga uelewa na kuboresha mahusiano kati ya jeshi na wananchi katika kujenga imani kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza msongamano kwenye mahabusu zetu na hasa kwa kesi ambazo sio za jinai, basi watuhumiwa wapewe dhamana mapema kwani mlundikano wa watuhumiwa kwenye mahabusu ni janga kwa afya.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali iongeze nguvu katika kuhakikisha kuwa uchunguzi wa kesi unakamilika mapema ili kutenda haki kwani kuchelewesha uchunguzi ni kuwanyima haki ya msingi watuhumiwa *(justice delayed is justice denied)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kushirikiana na taasisi nyingine kama ustawi wa jamii katika kushughulikia masuala ambayo yanaweza kupatiwa ufumbuzi bila kuhusisha mahakama ili kupunguza msongamano kwenye magereza.

Mheshimiwa Spika, kuna matukio mengi ya ajali za vyombo vya moto kama magari, malori, pikipiki na kadhalika, Serikali iendelee kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya barabara ikiwemo kuacha nafasi ya mita tatu kati ya gari na gari ili kupunguza ajali, kukagua vyombo vya moto mara kwa mara, na msisitizo juu ya madhara ya kunywa kilevi na kuendesha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ije na mpango imara wa mafunzo kwa bodaboda wetu kupunguza ajali na vifo vya nguvu kazi hii muhimu ambayo inateketea kwa ajali kwani ajali zimekuwa nyingi sana, pia Serikali iendelee kuweka kamera hasa kwenye *highways* ili kudhibiti *over speeding*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Magereza Serikali iendelee kuboresha mazingira ya magereza zetu na hasa magereza zilizopo kwenye Mkoa wa Simiyu. Gereza la Wilaya ya Bariadi majengo yanahitaji ukarabati na hasa jengo wanalolala mahabusu ambalo lilijengwa kwa udongo na miti.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya magereza ambapo kuna ardhi ya kutosha, basi wafungwa waingizwe kwenye programu za kilimo ili hatimaye magereza ziweze kujitegemea kwenye suala la chakula badala ya kusubiri fedha toka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uhamiaji, Serikali iongeze nguvu kwenye kudhibiti maeneo ya mipaka yetu kwani kumekuwa na matukio ya watu kujipenyeza nchini na tumeshuhudia pia katika matukio ya Oktoba 29 ambapo watu waliingia nchini na kushiriki katika kuleta vurugu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji iendelee kutoa elimu ya uraia kwa wananchi hasa katika kutoa taarifa ya wageni wanaoingia katika maeneo yao ili kudhibiti wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. MDOWE HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi kubwa wanayofanya. Hata hivyo, mchango wangu wa leo unalenga kuleta mageuzi makubwa ya kimfumo katika Jeshi letu la Magereza, nikijikita katika maeneo makuu mawili; ustawi na afya ya akili ya askari wetu, na mageuzi ya kiteknolojia katika ulinzi.

Mheshimiwa Spika, nikianza na afya ya akili na ustawi wa Askari Magereza, tunapotaja neno magereza, macho na fikra za wengi hukimbilia kwa wafungwa, lakini leo, nataka kusema kwa niaba ya wale wanaolinda waliofungwa ambao ni askari wetu wa magereza. Kazi ya uaskari magereza ni moja ya kazi zenye shinikizo kubwa zaidi la kisaikolojia *(high-stress job)* duniani. Askari hawa wanaishi na kufanya kazi mazingira ya msongamano, wanakutana na watu waliofanya makosa mazito na wanakabiliwa na changamoto za kijamii na kiuchumi kila siku. Sote tunajua, askari mwenye msongo wa mawazo *(depressed*

*officer)* hawezi kurekebisha tabia ya mfungwa. Badala yake, msongo huu unazaa matatizo ya kisaikolojia, migogoro ya kifamilia, na wakati mwingine matumizi mabaya ya nguvu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara ni huu; kuanzisha Vitengo Maalum vya Afya ya Akili *(Psychological Support Units)*. Ni wakati sasa kwa kila kanda au gereza kubwa kuwa na wataalamu wa saikolojia waliothibitishwa *(therapists/counselors),* ambao watakuwa na jukumu la kutoa unasihi wa mara kwa mara kwa askari na familia zao bila malipo na kwa usiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mageuzi ya makazi na maslahi; afya ya akili inaenda sambamba na mazingira anayoishi mtu. Namuomba Mheshimiwa Waziri anipe takwimu halisi, ni lini ujenzi wa nyumba za kisasa za askari utamalizika nchi nzima? Askari anapotoka kwenye lindo la saa 12 akarudi kulala kwenye nyumba iliyochakaa au kubana, tunapunguza morali yake ya kazi. Lazima tuboreshe posho zao na mazingira yao ya kuishi ili kuwapa heshima inayostahili.

Mheshimiwa Spika, kubadili teknolojia ya ulinzi magerezani; tuko katika karne ya 21, karne ya mapinduzi ya nne ya viwanda, lakini ulinzi katika magereza yetu mengi nchini bado unategemea mbinu za kale ikiwemo kuta ndefu, doria za miguu za askari usiku kucha na milango ya mbao au nondo za kawaida. Mbinu hizi hazina tija kiusalama na zinamchosha askari wetu pasipo sababu. Inasikitisha kuona tunapoteza nguvu kazi kubwa ya askari waliofunzwa vizuri, badala ya kufanya kazi za kiulinzi za kimkakati na marekebisho ya wafungwa, wanatumia saa nane hadi 12 kusimama tu kwenye mnara kuzuia wafungwa wasitoroke.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ya kiteknolojia ni kama ifuatavyo; mifumo ya *CCTV* na akili mnemba *(AI Video Analytics);* Wizara iwekeze kwenye mifumo ya kidijitali ya ulinzi. Tunahitaji kamera za kisasa zinazoweza kutambua mienendo isiyo ya kawaida *(behavioral analytics)* na kutoa ishara ya hatari *(alarm)* kabla ya tukio la kutoroka au fujo kutokea. Hii itapunguza uhitaji wa askari kusimama kwenye minara usiku kucha.

Mheshimiwa Spika, mifumo ya udhibiti wa milango na utambuzi *(access control & biometrics);* ni lazima magereza yetu makuu yaanze kutumia teknolojia ya alama za vidole au sura *(facial recognition)* kwa wafungwa, watumishi na wageni wanaoingia. Hii itazuia mianya ya rushwa na kuzuia watu wasiohusika kuingiza vitu haramu kama simu na dawa za kulevya magerezani.

Mheshimiwa Spika, ufungaji wa mifumo ya kuzuia mawasiliano *(signal jammers);* ili kudhibiti mitandao ya uhalifu inayoratibiwa na wafungwa wakiwa ndani ya magereza, Wizara ifunge teknolojia ya kukata mawasiliano ya simu za mkononi zisizo rasmi ndani ya maeneo ya magereza.

Mheshimiwa Spika, tukiwekeza kwenye afya ya akili ya askari wetu, tunajenga jeshi lenye nidhamu, utulivu na utu; na tukiwekeza kwenye teknolojia ya kisasa ya ulinzi, tunapunguza gharama za uendeshaji, tunaimarisha usalama wa nchi, na tunawapa nafasi askari wetu kufanya kazi kwa akili *(smart work)* badala ya nguvu pekee *(hard labor)*.

Mheshimiwa Spika, fedha itakayotumika kununua mifumo hii leo, itaokoa mabilioni ya fedha za walipa kodi hapo kesho.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi, naunga mkono hoja na ahsante sana.

**MHE. MWANAENZI HASSAN SULUHU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kujikita katika maeneo mawili muhimu; kwanza, mfumo wa usajili wa Vitambulisho vya Taifa kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* na pili, ustawi na utendaji wa Jeshi la Polisi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa hatua kubwa ilizochukua katika kuimarisha mifumo ya utambuzi wa wananchi kupitia *NIDA*. Mfumo huu umeendelea kusaidia katika usalama wa Taifa, utoaji wa huduma za kifedha, usajili wa laini za simu, pamoja na utambuzi wa wananchi kwenye huduma

mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, bado kuna changamoto zinazowakabili wananchi hasa vijana na wananchi wa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi bado wanakumbwa na ucheleweshaji wa kupata namba za *NIDA* au Vitambulisho vya Taifa kwa muda mrefu. Vijana wanaomaliza vyuo na wanaotafuta ajira hukosa fursa nyingi kwa sababu ya kutokuwa na vitambulisho kwa wakati. Wengine hushindwa kufungua akaunti benki, kupata mikopo ya vijana au hata kujiunga na mifumo rasmi ya kiuchumi. Naiomba Serikali kuongeza vifaa vya usajili, watumishi pamoja na mifumo ya TEHAMA ili kupunguza msongamano na kuongeza kasi ya utoaji wa vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, pia kuna haja ya Serikali kupeleka huduma za *NIDA* karibu zaidi na wananchi kupitia huduma za wilaya na kata, hasa maeneo ya vijijini. Leo hii wananchi wengi wanalazimika kusafiri umbali mrefu na kutumia gharama kubwa kufuata huduma hizi. Hali hii inawaathiri zaidi vijana na wanawake ambao uwezo wao wa kifedha ni mdogo.

Aidha, naiomba Serikali kuunganisha mifumo ya *NIDA* na taasisi nyingine muhimu kwa ufanisi zaidi ili kuondoa usumbufu wa kurudia taarifa mara kwa mara. Mfumo mmoja wa utambuzi wa Taifa utaongeza uwazi, mapato ya Serikali na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Polisi Tanzania, napenda kupongeza kazi kubwa wanayoifanya katika kulinda usalama wa wananchi na mali zao. Askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu, mara nyingi kwa kujitolea ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama na yenye amani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kuna changamoto kadhaa zinazohitaji kuangaliwa kwa karibu. Kwanza ni suala la maslahi ya askari polisi. Askari wengi bado wanakabiliwa na changamoto za makazi, vitendea kazi, usafiri pamoja na mazingira bora ya kazi. Askari akiwa na mazingira duni ya kazi huathiri morali na ufanisi wake kazini. Naiomba Serikali kuongeza

uwekezaji katika nyumba za askari, vifaa vya kisasa pamoja na huduma za afya na bima kwa askari na familia zao.

Mheshimiwa Spika, pili, kuna haja ya kuongeza matumizi ya teknolojia katika utendaji wa Jeshi la Polisi. Uhalifu wa mtandao, utapeli wa kidigitali na makosa yanayotumia teknolojia vinaongezeka kwa kasi. Hivyo, Serikali iongeze mafunzo maalum kwa askari wetu katika masuala ya usalama wa mtandao, uchunguzi wa kidigitali na matumizi ya mifumo ya kisasa ya kiintelijensia.

Tatu, ni muhimu kuendelea kujenga mahusiano mazuri kati ya polisi na wananchi. Polisi Jamii ikiimarishwa vizuri itasaidia kupunguza uhalifu na kuongeza imani ya wananchi kwa vyombo vya dola. Vijana wengi wana nguvu na uwezo mkubwa wa kusaidia katika ulinzi wa jamii kupitia elimu, teknolojia na ushirikiano wa kijamii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naiomba Serikali kuangalia namna ya kuongeza ajira kwa vijana ndani ya vyombo vya usalama ili kupunguza tatizo la ajira na wakati huo huo kuongeza nguvu kazi katika kulinda Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, pia Waziri wa Mambo ya Ndani na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuleta mageuzi makubwa na changa katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, nashauri yafuatayo; Serikali iwekeze katika kuboresha miundombinu ya baadhi ya magereza katika Wilaya, pia nashauri Serikali ifanye maboresho yafuatayo katika Kituo cha Magereza cha Wilaya ya Muleba:-

(i) Kufanya ukarabati wa Ngome ya Gereza ambayo sio imara;

(ii) Kununua na kuleta gari kwa ajili ya Kituo cha Magereza cha Wilaya ya Muleba;

(iii) Kununua na kuleta vifaa vya kulalia wafungwa na mahabusu kama vitanda na magodoro ya Kituo cha Magereza cha Wilaya ya Muleba;

(iv) Kuboresha mabweni ambayo ni chakavu ya Kituo cha Magereza cha Wilaya ya Muleba;

(v) Kukamilisha Ofisi za Utawala za Kituo cha Magereza cha Wilaya ya Muleba ambazo hazijakamilika milango, madirisha na sakafu; na

(vi) Kufanya ukarabati wa nyumba za watumishi za Kituo cha Magereza cha Wilaya ya Muleba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Kata za Wilaya za Muleba; Jimbo la Muleba Kaskazini lina Kata 18. Kati ya kata hizo, kata nne zenye wakazi takribani 59,000 zilizo karibu na pembezoni ya Wilaya ya Muleba hazina kituo cha polisi. Tunaomba Serikali ijenge kituo cha polisi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ijenge ya Ofisi ya Wilaya ya  Msajili wa Jumuiya katika Wilaya ya Muleba kutokana na uhitaji wa huduma hiyo unaongezeka.

Pia tunaomba Serikali ijenge Ofisi ya Usajili ya *NIDA* katika Wilaya ya Muleba. Wilaya ya Muleba ndio inaongoza katika Mkoa wa Kagera kwa kuwa na idadi kubwa ya watu takribani 550,000. Ofisi za *NIDA* ikiwemo ya Wilaya ya Muleba inahitaji gari na vitendea kazi vya TEHAMA zaidi ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi. Ufinyu ofisi na uhaba wa watumishi wa kutosha katika ngazi za wilaya unasababisha msongamano mkubwa kwa wananchi wanaohitaji huduma ikiwemo ya Muleba.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali itupatie gari la zimamoto na uokoaji Wilaya ya Muleba. Halmashauri ya Muleba

imeshatenga ofisi kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Tunasubiri gari hilo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ijenge Ofisi ya Uhamiaji katika Wilaya ya Muleba kutokana na uhitaji wa huduma kuongezeka na uhitaji wa miundombinu itakayowezesha huduma bora zaidi. Pia kuimarisha udhibiti uvunjaji wa sheria ukiwemo utapeli kupitia mitandao ya kijamii na simu (usajili wa laini za simu).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wa kuimarisha teknolojia kwa ajili ya kuzuia uhalifu wa kidijitali nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze na pongezi; kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa wasaa wa kuchangia katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mama yetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kwa mapenzi makubwa naipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hasa Mheshimiwa Waziri Patrobas Pascal Katambi pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ayubu Mohamedi Mahmoud. Nawapongeza pia watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu, Makamishna na Majenerali wote pamoja na watumishi wote walioko chini yao. Pongezi hizi kwa Wizara ni kwa sababu ya maandalizi makini ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yenye maono, iliyoandaliwa kwa weledi na inayoakisi mahitaji halisi ya kila Mtanzania katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa jumla; katika dunia ya sasa inayotegemea teknolojia, uhalifu wa kidijitali umeendelea

kuongezeka kwa kasi na kuwa tishio kwa usalama wa Taifa, uchumi, taasisi za Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla. Tanzania nayo imeanza kukumbwa na changamoto mbalimbali za uhalifu wa kimtandao kama vile wizi wa taarifa binafsi, utapeli wa mtandaoni, udukuzi wa mifumo ya Serikali, utakatishaji fedha kwa njia za kidijitali, pamoja na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia vyombo vyake kama Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na *RITA,* kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kuwekeza katika teknolojia za kisasa ili kuongeza tija, ufanisi na uwezo wa kudhibiti uhalifu wa kidijitali nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzisha Mfumo Jumuishi wa Kidijitali wa Usalama wa Taifa, Serikali inapaswa kuunda mfumo mmoja wa kidijitali unaounganisha taasisi zote za Wizara ya Mambo ya Ndani ili kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa kwa haraka na kwa usalama. Mfumo huo uwe na uwezo wa kutunza taarifa za wahalifu na watuhumiwa katika kanzidata moja; kufuatilia mienendo ya wahalifu wa kimtandao; kuunganisha taarifa za uraia, uhamiaji, rekodi za makosa ya jinai na taarifa za Vitambulisho vya Taifa; na kuwezesha taasisi mbalimbali kufanya kazi kwa ushirikiano bila ucheleweshaji.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia kupunguza urasimu, kuongeza uwazi na kuimarisha usalama wa taarifa muhimu za Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha Kitengo cha Uhalifu wa Mtandao *(Cyber Crime Unit);* Jeshi la Polisi linapaswa kuongezewa uwezo wa kitaalamu na kiteknolojia kupitia mafunzo ya mara kwa mara kuhusu udukuzi, uchunguzi wa kidijitali na uchambuzi wa *data*; kuajiri wataalamu wa TEHAMA, usalama wa mifumo na uchambuzi wa kijasusi wa kidijitali; kupata vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa kielektroniki; na kuanzisha maabara maalumu za uchunguzi wa kidijitali *(Digital Forensic Laboratories)*.

Mheshimiwa Spika, kupitia hatua hizi, Serikali itaweza kugundua na kudhibiti uhalifu wa kimtandao kwa haraka zaidi kabla haujasababisha madhara makubwa.

Kuhusu matumizi ya akili mnemba *(Artificial Intelligence – AI),* Serikali inaweza kutumia teknolojia ya akili mnemba katika kuchambua mienendo ya kihalifu mtandaoni; kutambua miamala yenye viashiria vya utakatishaji fedha; kufuatilia akaunti bandia na mitandao ya kitapeli; na kutabiri maeneo au mifumo inayoweza kutumiwa kufanya uhalifu.

Aidha, *AI* inaweza kusaidia katika uchambuzi wa kamera za usalama *(CCTV)* kwa kutambua sura za watuhumiwa na mienendo isiyo ya kawaida katika maeneo ya umma.

Mheshimiwa Spika, pia kuongeza matumizi ya kamera za kisasa za ulinzi *(smart CCTV);* katika miji mikubwa, mipakani, viwanja vya ndege na maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu, Serikali inapaswa kufunga kamera za kisasa zenye uwezo wa kutambua nyuso za watu *(facial recognition);* kusoma namba za magari kiotomatiki; kutuma taarifa kwa wakati halisi kwenye vituo vya usalama; na kuhifadhi kumbukumbu kwa muda mrefu kwa ajili ya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu utasaidia kudhibiti uhalifu wa barabarani, ugaidi, biashara haramu pamoja na wahamiaji haramu. Aidha, kuboresha Mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo kupitia *RITA, RITA* inapaswa kuboresha mifumo yake ya kidijitali ili kuondoa matumizi ya nyaraka za karatasi kwa kiwango kikubwa; kuweka taarifa zote katika mfumo salama wa mtandao; kuwezesha uhakiki wa taarifa kwa njia ya mtandao; na kuzuia utengenezaji wa vyeti bandia vya kuzaliwa na vifo.

Mheshimiwa Spika, mfumo madhubuti wa utambuzi wa watu utasaidia kupunguza udanganyifu wa utambulisho unaotumika katika uhalifu wa kidijitali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha usalama wa mipaka kwa teknolojia; Idara ya Uhamiaji inaweza kutumia mfumo wa

*biometric* katika mipaka yote; mashine za kisasa za kuchunguza nyaraka bandia; kamera na droni za ulinzi mipakani; na mfumo wa kidijitali wa kufuatilia wageni wanaoingia na kutoka nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zitasaidia kuzuia wahalifu wa kimataifa kutumia Tanzania kama njia ya kufanya uhalifu wa mtandao au biashara haramu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga mfumo madhubuti wa mawasiliano ya dharura; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Polisi wanapaswa kuwa na mfumo wa pamoja wa mawasiliano ya dharura; vituo vya kisasa vya kupokea taarifa za matukio; programu za simu za kuripoti uhalifu kwa haraka; na mfumo wa *GPS* kwa magari ya doria na uokoaji.

Mheshimiwa Spika, teknolojia hii itarahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza kasi ya uokoaji au udhibiti wa matukio ya kihalifu.

Kwa upande wa elimu kwa umma kuhusu usalama wa kidijitali, Serikali inapaswa kuanzisha kampeni endelevu za kutoa elimu kwa wananchi kuhusu jinsi ya kujilinda dhidi ya utapeli wa mtandaoni; umuhimu wa kulinda taarifa binafsi; hatari za matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii; na njia salama za kufanya miamala ya kidijitali.

Mheshimiwa Spika, wananchi wenye uelewa mzuri wa usalama wa mtandao huwa mstari wa mbele kwa kupambana na uhalifu wa kidijitali.

Kuhusu kuboresha Sheria na Sera za TEHAMA; ni muhimu Serikali kuendelea kufanya maboresho ya sheria ili ziendane na maendeleo ya teknolojia. Serikali inapaswa kuimarisha sheria za uhalifu wa mtandao; kuweka adhabu kali kwa wahalifu wa kidijitali; kulinda faragha na taarifa za wananchi; na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kupambana na uhalifu wa mtandao.

Mheshimiwa Spika, sheria madhubuti huongeza uwezo wa vyombo vya dola kushughulikia wahalifu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzisha Kituo cha Taifa cha Usalama wa Mtandao; Serikali inaweza kuanzisha Kituo Maalumu cha Taifa cha Kusimamia Usalama wa Mtandao kitakachokuwa na majukumu ya kufuatilia mashambulizi ya kimtandao saa ishirini na nne; kuratibu taasisi zote za usalama; kutoa tahadhari za mapema kuhusu vitisho vya kidijitali; kufanya tafiti na ubunifu wa teknolojia za usalama; na kituo hiki kitakuwa nguzo muhimu katika kulinda mifumo ya Serikali na taasisi binafsi dhidi ya mashambulizi ya kimtandao.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kwa ujumla, matumizi sahihi ya teknolojia yanaweza kuleta mapinduzi makubwa katika utendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na taasisi zake. Serikali inapowekeza katika mifumo ya kisasa ya kidijitali, mafunzo ya wataalamu, ushirikiano wa taasisi na elimu kwa wananchi, itaweza kupunguza kwa kiwango kikubwa uhalifu wa kidijitali nchini Tanzania. Aidha, mafanikio ya jitihada hizi yatategemea uwepo wa uongozi madhubuti, uwajibikaji, uwekezaji endelevu katika TEHAMA pamoja na ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi na wananchi. Teknolojia ikitumika kwa usahihi inaweza kuwa silaha muhimu ya kuhakikisha usalama, amani na maendeleo endelevu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo mahali hapa nami niweze kushiriki kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mwaka 2026/2027 iliyopo mbele yetu. Naipongeza Wizara pamoja na watendaji wote kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 nikijikita moja kwa moja kwenye hali halisi ya Jimbo la Kibaha Vijijini. Wizara hii ndiyo yenye dhamana ya ulinzi wa raia, amani,

utulivu, Uhamiaji, Magereza, Zimamoto na Vitambulisho vya Taifa. Bila amani, hakuna viwanda vya *TAMCO* vitakavyofanya kazi na hakuna mkulima atakayelima kwa uhakika. Kwa hiyo, mchango wangu utagusa changamoto, mahitaji ya msingi na mapendekezo ya nini kifanyike.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nianze na changamoto zifuatazo; uhaba wa Vituo vya Polisi na Askari linganishi na eneo na idadi ya watu. Jimbo la Kibaha Vijijini lina eneo la zaidi ya kilometa za mraba 1,200 lakini hadi sasa tuna Kituo Kikuu cha Polisi Mlandizi na vituo vidogo vitatu tu vya Ruvu, Kwala na Dutumi; baadhi ya Kata za Mtongani, na Gwata hazina kituo kabisa. Wananchi wanalazimika kutembea zaidi ya kilometa 25 kufuata huduma za polisi. Uwiano wa askari kwa wananchi ni takribani askari mmoja kwa wananchi 1,800 wakati kiwango cha kitaifa kinatakiwa kuwa askari mmoja kwa wananchi 450. Matokeo yake ni kuchelewa kwa doria, upelelezi dhaifu wa kesi za wizi wa mifugo, na kuongezeka kwa uvunjifu wa amani kwenye vijiji vya mpakani mwa mkoa.

Pili, ongezeko la uhalifu unaohusiana na miradi mikubwa; ujenzi wa barabara ya *expressway* ya Dar es Salaam – Morogoro, Kongani ya *TAMCO,* na bandari kavu ya Kwala umeleta fursa lakini pia umevuta wimbi la wahamiaji, vibaka na wafanyabiashara ya dawa za kulevya. Kwenye maeneo ya Mlandizi na Kwala kumekuwa na matukio ya uvamizi wa maduka, uporaji wa vyuma vya ujenzi, na ajali za barabarani zinazosababishwa na madereva wa malori makubwa. Jeshi la Polisi halina magari ya kutosha ya doria. Kituo cha Mlandizi kina gari moja tu la zamani ambalo mara nyingi linakwama kwa mafuta na vipuri.

Tatu, majanga ya moto na ajali – Kitengo cha Zimamoto na Uokoaji kiko mbali, Kibaha Vijijini hakina kituo cha Zimamoto. Huduma zote zinategemea Kibaha Mjini umbali wa kilometa 40. Mwaka 2025 tumepoteza nyumba tisa na stoo mbili za mazao Dutumi, Kwala na Ruvu kwa moto kwa sababu gari la zimamoto lilifika baada ya saa mbili. *TAMCO* ina viwanda 14 vya kemikali, mbolea na kuunganisha magari. Mungu apishie mbali, ikitokea

moto mkubwa *TAMCO*, hasara itakuwa ya mabilioni na hatuna uwezo wa kujibu haraka.

Nne, ni kuhusu uhamiaji haramu na usalama wa mpaka; Kibaha Vijijini ni njia panda ya wageni kutoka nchi jirani kuelekea Dar es Salaam na viwandani. Vijiji vya jirani na Mlandizi vimeripoti uwepo wa raia wa kigeni wasio na vibali wanaofanya kazi za vibarua kwenye mashamba na ujenzi. Idara ya Uhamiaji ina ofisi moja tu Mlandizi yenye maafisa wawili bila gari. Hii inafanya ukaguzi wa nyumba za kupanga na mpango kazi uwe dhaifu.

Tano, msongamano magerezani na ucheleweshaji wa haki; mahabusu kutoka Kibaha Vijijini wanapelekwa Gereza la Kibaha Mjini au Segerea. Mara nyingi kesi zinachelewa kwa sababu ya kukosekana usafiri wa mahabusu. Pia ndugu wa mahabusu wanatumia nauli kubwa kufuata kesi. Haki inachelewa na familia zinaumia kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, sita; usajili wa Vitambulisho vya Taifa *(NIDA);* wazee na walemavu wa Gwata, Dutumi na kata zingine wanatembea zaidi ya kilometa 25 kufika Ofisi ya *NIDA* Mlandizi. Mashine za kusajili ni moja tu na inapoharibika zoezi linasimama kwa wiki. Wanafunzi wengi wenye sifa ya kupata vitambulisho wamekosa.

Mheshimiwa Spika, naomba niweke bayana mahitaji ya msingi ya Jimbo la Kibaha Vijijini kama ifuatavyo; vituo vya polisi vipya na rasilimali. Tunahitaji vituo vipya vya polisi vya Daraja C kwenye Kata za Mtongani, Gwata. Kituo cha Mlandizi kipandishwe hadhi Daraja A kiwe na *OCD*. Pia tunahitaji magari matatu mapya ya doria kwa Mlandizi, Ruvu na Kwala, pamoja na pikipiki 10 kwa vijiji vya mbali. Askari wapya wasiopungua 60 waongezwe ili kufikia uwiano wa 1:500.

Pila, Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Mlandizi; kwa kuwa *TAMCO* ina viwanda vya hatari, na *expressway* ina ajali nyingi, tunahitaji Kituo cha Zimamoto cha kudumu Mlandizi. Kiwe na magari mawili ya zimamoto, gari moja la uokoaji, na kikosi cha

askari wasiopungua 25. Eneo la ujenzi lipo tayari karibu na stendi ya Mlandizi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Uhamiaji yenye meno; Ofisi ya Uhamiaji Mlandizi iongezewe maafisa hadi sita, ipatiwe gari moja la operesheni, na vifaa vya *e-passport* na *biometric verification*. Kaguzi za nyumba za kupanga na viwandani zifanyike kila robo mwaka kushirikiana na Serikali za Mitaa.

Kuhusu huduma za *NIDA* kusogezwa vijijini; Wizara ianzishe Wiki ya *NIDA* kila baada ya miezi mitatu ambapo timu itazunguka kata zote na mashine za kutosha. Pia kuwe na kituo cha kudumu cha *NIDA* kwenye majengo ya Kata ya Dutumi na Gwata ili kupunguza msongamano Mlandizi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Mwanzo na ukarabati wa Magereza; kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria tunaomba ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Mlandizi ili kesi ndogo ndogo zisimalizie Kibaha Mjini. Pia tunashauri Gereza dogo la mahabusu lijengwe Kibaha Vijijini kupunguza gharama za usafiri na msongamano Segerea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi; kwa kuwa jimbo ni kubwa, tunahitaji kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi na polisi kata. Vipewe baiskeli 100, tochi, filimbi na mafunzo ya mara kwa mara. Vijana washirikishwe kwenye mpango wa *community policing* ili wawe sehemu ya ulinzi badala ya kuwa wahalifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba nitoe ushauri wangu wa nini kifanyike kwenye maeneo mahsusi ili kujenga ufanisi mzuri: -

(a) Kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; kwa mwaka wa fedha 2026/2027 itenge shilingi bilioni 2.5 kwa ujenzi wa vituo vitatu vipya vya polisi Mtongani, Gwata, Kwala na ukarabati wa Kituo cha Mlandizi.

(b) Ununuzi wa magari; itenge magari matatu ya doria *Land Cruiser Hardtop* kwa Kibaha Vijijini na gari moja la Zimamoto kwa kituo kipya cha Mlandizi.

(c) Ajira za Askari; kati ya askari 10,000 wanaotarajiwa kuajiriwa kitaifa, Kibaha Vijijini ipatiwe askari 80; 50% wawe vijana wa jimbo hili wanaojua jiografia.

(d) Kampeni ya *NIDA* Vijijini; Wizara itume timu maalum ya *NIDA* kwa miezi miwili kusajili wazee, walemavu na wanafunzi wote kata kwa kata bila malipo ya usafiri.

(e) Ofisi ya Uhamiaji; ipandishe hadhi Kituo cha Polisi Mlandizi iwe ya Wilaya, iongeze maafisa na vifaa vya kisasa vya *digital tracking*.

Mheshimiwa Spika, kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani na *RPC*: -

(a) Operesheni Maalum; anzisha operesheni ya Ondoa Uhalifu *TAMCO* kila miezi minne kukagua nyumba za kupanga, vibarua, na dawa za kulevya.

(b) Kamati ya ulinzi ya *expressway;* unda Kamati ya Pamoja ya Polisi, *TANROADS* na madereva kupunguza ajali na ujambazi wa barabarani.

(c) Ushirikiano na viwanda; *TAMCO* na viwanda vingine vichangie *Police Post* ndani ya kongani na kusaidia mafuta ya gari za doria kama sehemu ya *CSR*.

Mheshimiwa Spika, Kibaha Vijijini ni kitovu cha uchumi wa Pwani. *TAMCO, TBPL* na *Expressway* vitafanikiwa tu kama usalama umeimarika. Tukijenga vituo, tukiongeza askari, tukileta Zimamoto, na tukisajili wananchi wote, tutakuwa tumeweka msingi imara wa Tanzania ya viwanda na usalama wa kweli.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupa uhai na uzima na kutuwezesha siku ya leo kukutana hapa kwa ajili ya Bunge lako Tukufu, lakini pia kupitia na kujadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hatimaye kuchangia na kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nitumie fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya. Vilevile na kipekee nimshukuru kwa heshima aliyonipa ya kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa na kuiongoza Zanzibar vyema, hatimaye kwa pamoja kuleta maendeleo ya kasi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Naibu Spika. Niwapongeze Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wote wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Patrobass Paschal Katambi ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kunisimamia vyema na kuniongoza katika kazi hii ya Unaibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri wenzangu wote. Nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu yetu Ally Gugu pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama

wote, Jeshi la Polisi, Zimamoto, Magereza, Uhamiaji pamoja na *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze familia yangu; mke wangu na watoto wangu kwa kunivumilia katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikipongeze Chama Cha Mapinduzi ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya, Jimbo hadi Shina ndani ya Jimbo la Chaani na niwapongeze Wana-Chaani wote kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Jimbo la Chaani na kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mchango mfupi kwa sababu ya muda, lakini kwanza nikiri kwamba hoja zilizotolewa na Wabunge ni za muhimu na kwa kweli tunazipokea na tutazifanyia kazi hatua kwa hatua. Yapo baadhi ya maswali ambayo yameshakuja wakati wa maswali na majibu na tumeshatoa majibu, lakini na leo tutajibu kwa kadri ya hali ya muda ulivyo kama ambavyo utaelekeza.

Mheshimiwa Spika, la msingi ninapenda tu kusema kwamba leo hii tumekutana mahali hapa tukiwa tumekuja kuwasilisha bajeti, lakini hatukuja tu kuwasilisha bajeti, tumekuja kuwasilisha dhamira ya kitaifa ya kujenga Tanzania salama zaidi, imara zaidi na yenye uwezo mkubwa zaidi kwa ajili ya usalama wa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira hiyo inasimamiwa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba Watanzania wote wako salama. Pia jambo hilo linasimamiwa na Katiba zetu mbili; Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara 28(1) hadi (4) inaeleza wajibu wa ulinzi na usalama wa kila mwananchi, na Katiba ya Zanzibar nayo katika Kifungu cha 23(1) hadi (5) nayo pia imeeleza kwa kina wajibu wa mwananchi katika kuhakikisha kwamba usalama wa nchi na utawala tunavilinda kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jukumu hili lisionekane kuwa ni la watu fulani, jukumu hili ni la Watanzania wote. Sisi tuliokabidhiwa dhamana ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tumekabidhiwa sehemu tu ya vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo vinasimamia nchi yetu na utawala wetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Bunge letu hili Tukufu pamoja na Baraza la Wawakilishi navyo vimepewa dhamana ya kutunga sheria ambazo zitaweza kuunda vyombo vitakavyosaidia kulinda utawala na nchi yetu. Sasa niseme tu kwamba pale ambapo vyombo hivi vinatimiza wajibu wake sawasawa tusitokee baadhi yetu au miongoni mwetu Watanzania tukaanza kuona kana kwamba labda kazi hiyo haikufanywa sawasawa.

Mheshimiwa Spika, anayejua ni utaratibu gani hutumika kufanya kazi hiyo ni yule aliyefunzwa namna ya kuifanya, mwingine yeyote atakuwa anadhani. Wale wanaodhani basi niwaombe sana wasilolifahamu basi wachukue nafasi ya kuja kujifunza ili wafahamu nini kinakusudiwa kufanyika.

Mheshimiwa Spika, dunia ya leo katika zama hizi mpya ina ushindani mkubwa kwenye mambo ya ulinzi na usalama, lakini kwa upande wetu wa Tanzania (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) tuna weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba dakika japo mbili tu nimalizie hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, dunia ya leo ina zana mpya za ushindani na sisi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutambua hilo tuna vyombo imara sana ambavyo vinabeba maono ya Taifa hili kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vyombo ambavyo vimejengwa kwa nidhamu kubwa vinasimamia utulivu jambo ambalo linapelekea ukuaji wa uchumi, jamii yetu kuwa na utulivu na Taifa kuendelea siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, msingi wa hili unatokana na nini? Msingi wa hili kwa sasa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kutokana na maono yake kupitia Dira ya 2050 imezingatia suala la kujenga utawala kwamba Dira hii ya 2050 nguzo zile tatu za dira zinabebwa na msingi mzima wa kuhakikisha kwamba utawala, amani, usalama na utulivu lazima vipatikane kwanza.

Mheshimiwa Spika, sasa wenzetu wanaotanguliza maendeleo na kusahau ule msingi wa dira ambao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, malizia.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, msingi wa dira unatimizwa. Niwaombe sana warudi kwanza kwenye msingi, halafu tutaweka nguzo ili tufike kule tunakokusudia kuelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaomba kutumia fursa hii nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake mzuri, maelekezo yake na miongozo yake, vimejenga msingi imara wa kuwa na Taifa moja ambalo linazingatia ulinzi na usalama. Pia kuwa kichagizo au fursa inayotolewa kwa kuwepo kwa usalama. Hapo ndipo tunapopata maendeleo na shughuli za kiusalama zinakuwa zimetekeleza wajibu wake kutoa mchango wa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Emmanuel Nchimbi, yeye pamoja na Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Zanzibar.

Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi na miongozo na maelekezo mazuri ambayo amekuwa akiyazingatia. Aidha, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wote wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa wao pia wamekuwa ni sehemu ya kutusaidia sisi kuweza kutekeleza majukumu yetu vizuri katika kuhakikisha kwamba Taifa letu linakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, nizidi kuwashukuru pia wakuu wetu wa vyombo vya ulinzi na usalama, sitawataja kwa sababu ya muda ambao nimepangiwa, lakini niwashukuru sana kwa uzalendo wao, uhodari wao na ushupavu wao ambao umesaidia leo Taifa la Tanzania liko salama na watu wanaendelea na majukumu yao kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana pia Wizara ya Mambo ya Ndani, watendaji wote kuanzia Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani mpaka askari na watumishi wasio askari wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wameifanya. Kwa kweli wamekuwa wakinipa ushirikiano mkubwa sana katika kutekeleza majukumu yangu ambayo nimekasimiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua hoja zilizozungumzwa nikianza pia maalum kabisa kushukuru sana Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo imekuwa ikitupa miongozo, imetupa maelekezo na wakati wote wametushauri kwa umahiri na uhodari sana kuweza kuhakikisha kwamba majukumu yale yaliyopangwa na mikakati ya Serikali iliyopangwa inatekelezwa kama jinsi ambavyo imekusudiwa, hivyo kuleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mwenyekiti wake Mheshimiwa Najma Giga na Makamu wake Mheshimiwa Paschal Chinyele pamoja na Wajumbe hawa. Wamefanya kazi kubwa na nzuri sana, kwa kweli wanastahili pongezi na sisi tunawaombea dua nyingi sana ili waendelee kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nikushukuru wewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mmekuwa mkituongoza vyema na kutusimamia katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu yetu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda ninaomba nijielekeze sasa katika hoja ambazo zimetolewa na Kamati yetu ambayo imetoa ufafanuzi katika taarifa iliyosomwa hapa kabla. Pia nieleze juu ya hoja zile ambazo zote zimetolewa zinazohusiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, ninatambua mengi yalikuwa maelekezo ambayo yametolewa kimsingi kwa maana ya kuonesha namna gani ambavyo tunaweza tukatekeleza vizuri sheria. Ipo michango ambayo imetoa ufafanuzi, lakini pia kama ushauri, mapendekezo na zaidi kuonesha dira ya namna gani ya kuweza kusimamia vyombo hivi kwa umahiri na uhodari ili mwananchi Mtanzania aweze kupata haki yake kwa jinsi inavyostahili kwa kuhakikisha kuwa anakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa maelezo hayo na kwa hoja zilizotolewa na Kamati nitambue na kukiri kwamba tumezipokea na zote tutakwenda kuzitolea majawabu. Pia ziingie katika kitabu chako cha Kumbukumbu za *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda nitazingatia kutoa ufafanuzi kwa mambo machache, lakini wajue kwamba tumetambua na kuheshimu yale yote ambayo wamekuwa wakitushauri kwa hoja zao miongozo na maelekezo ambayo tumekuwa tukiyapata katika namna tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja ambazo tumezipata kwa maandishi, nazo tunazichukua lakini zipo hoja za Waheshimiwa Wabunge 11 ambao wameweza kupata fursa ya kuchangia nazo pia kwa heshima kubwa tunazichukua kwa ajili ya kufanya maboresho na kuweza kuhakikisha kwamba tunaleta ile nafuu ya kuhakikisha huduma zilizokusudiwa kutolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani na taasisi zake zote zinatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kama ningetoa majawabu kwa kusoma ninayo, ni mengi kidogo, lakini nijielekeze kwenye baadhi ya hoja zile ambazo zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kwanza ambao ni muhimu sana sisi kama Taifa na viongozi lazima tuutambue na kuujua, tunayo nchi yetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni nchi ambayo ni *sovereign state,* ni nchi ambayo inaongozwa kwa mujibu wa Katiba, ni nchi ambayo inafuata misingi yote ambayo imefungamanishwa katika Katiba, na ni nchi ambayo inafuata utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni nchi ambayo inasimamia utawala wa sheria, inaheshimu haki za binadamu, lakini vivyo hivyo ni nchi ambayo inatambua na kuheshimu mihimili ya iliyopo (Bunge na Mahakama). Kwa hiyo, ni nchi ambayo imefungamanishwa katika *constitutionalism. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikielekea katika Ibara ya Nane ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukiacha mambo mengine yote baada ya kuwa *constituted* kwenye *preamble* kwamba tunasema sisi ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeunganishwa na kufungamanishwa kwa pamoja. Katika Ibara ya 28 inasema; "Kila mtu ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi kuimarisha uhuru, mamlaka na kulinda ardhi na umoja wa Taifa." Kwa hiyo, jukumu la ulinzi wa nchi hii ni jukumu la kwetu sisi sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na msingi mkuu katika mazungumzo na hoja ambazo zimetolewa zote nawakumbusha na kutoa rai kwa Taifa, Waheshimiwa Wabunge, pamoja na viongozi kwamba

mlinzi mkuu wa nchi yetu kabla ya yeyote ni Mwenyezi Mungu. Katika msingi huo, Mwenyezi Mungu ndiye mlinzi wa nchi yetu, ndiye aliyetambua nchi yetu iweze kuwepo na hatimaye tukaji-*constitute*. Msingi wa pili katika ulinzi ni wa kwetu mtu mmoja mmoja na ndiyo maana unaona katika Katiba inasema kila mtu anao wajibu kwa Taifa letu. Taifa letu ni moja, Mama Tanzania, lazima tumlinde sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya jukumu hilo la Mwenyezi Mungu la kwanza, la pili ni la mtu binafsi au wote kwa pamoja, la tatu ni la jamii na taasisi zake, zikiwemo taasisi za dini na za elimu. Jukumu la nne linaenda kuwa la Serikali, ambalo msingi wake ndiyo mifumo ya kisheria, sera na taratibu ambazo zipo, zinazosimamiwa na kuongozwa ndani ya Serikali, ndipo tunakuta dola.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo ndiyo utaona msingi mkuu wa Serikali na vyombo vyake ni wa mwisho katika kusimamia haki, usalama na ulinzi wa masuala yote jinsi ilivyo tofauti. Kwa hoja nitakazozisema hapa, utaona lawama ya kwanza kabla ya kutimiza wajibu wetu kwa mujibu wa sheria tunapeleka katika vyombo mbalimbali vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, utaangalia katika hoja ambazo zilitolewa, moja ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa heshima na taadhima zote kwa pamoja, tunashukuru zile zilizozungumzwa na kujenga hoja ya kwamba tunahitaji sasa Wizara ya Fedha iweze kuzingatia na kutoa fedha ambazo zitasaidia katika kuimarisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Aidha, tuendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya maboresho makubwa sana katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mojawapo ni ujenzi wa makazi ya askari pamoja na ofisi za kisasa ambao unaendelea hapa nchini. Pia tumeendelea kuona vifaa vya kisasa katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimeendelea kutolewa ikiwa ni sambamba na kuangalia ujenzi wa Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamejenga hoja na wameomba ujenzi wa vituo vya polisi vya ngazi na madaraja mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge nawahakikishia, kwa Rais huyu tutaweza. Tutakwenda kujenga vituo vya polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiacha baadhi ya vituo ambavyo vilipata madhila, nafahamu hata sipaswi kurudia hapa, tulipata hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 12, lakini hii ilikuwa ni kuturudisha nyuma katika hatua ambayo maeneo muhimu na nyeti yaliyokuwa yakihitaji vituo vya polisi na vile vilivyokuwa vinafanya kazi, vipo ambavyo sasa hivi tunahitaji kwenda tena kujenga upya. Ni maumivu makubwa ambayo kama nchi tumeyapata na Taifa limepata, lakini lazima katika hayo Mheshimiwa Rais alisema, *never again* na ndiyo maana ameridhia kuendelea kutoa fedha, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vilivyoharibiwa.

Mheshimiwa Spika, pia tunaenda kujenga vituo vya *Class A*, *Class B* na *Class C*. Katika ujenzi wa kituo cha *Class A* ambacho ni cha ngazi ya mkoa ni shilingi bilioni 1.6. Ukitaka kujenga kituo cha *Class B* ni shilingi milioni 800 na ukitaka kujenga kituo cha *Class C* ni shilingi milioni 165. Utaweza kuona jinsi gani ambavyo tulipata changamoto kwenye hayo maeneo, lakini Mheshimiwa Rais kwa nia yake njema na upendo wa dhati ameridhia tuendelee na ujenzi wa ofisi na vituo vya polisi na kuweza kuboresha makazi ya askari wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja zilivyo nyingi, utaniwia radhi kidogo japo pia nitazingatia huo muda ambao umenipatia.

Mheshimiwa Spika, yapo mafunzo ambayo yanaendelea kutolewa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambavyo mpaka sasa hata *peacekeeping mission* vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimeendelea kuonesha umahiri wake katika nyanja za kitaifa, kimataifa na maeneo mengi duniani, huko tumepeleka askari wetu na wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nazidi kuwapongeza sana *IGP*, *CGP*, *CGF, CGI* na Mkurugenzi wa *NIDA*. Katika maboresho ambayo

tunayafanya ya kisasa tunazingatia sana na tunakwenda kwenye TEHAMA. Tunakwenda kwenye kutoa huduma kwa urahisi zaidi na kutengeneza ufikivu. Hata Magereza tumeanza kusikiliza kesi kupitia mtandao.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Jeshi la Polisi sasa hivi, tunaenda moja kwa moja katika maboresho ya mifumo ya kidijitali, ikiwa ni pamoja na kwenda kwenye *smart city*. Pia ni pamoja na uboreshaji na upimaji wa magari kwa mifumo ya kiteknolojia ya kisasa ambayo kwa sababu ya muda, kitabu changu cha hotuba kinaeleza na *Hansard* yako itaweza kuchukua.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengine ambayo ni muhimu nikayazungumzia hapa. Tumezungumza kuhusiana na masuala ya *visa*, *referral visa* pamoja na *visa on arrival;* haya tayari tumeyachukua, tutayafanyia kazi na tutatolea majawabu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ya masuala ya uraia; hili nalizungumza pia kwa herufi kubwa. Masuala ya uraia, pamoja na nchi yetu kuwa na sheria zinazoruhusu mtu kuomba uraia, ni vizuri tukatambua kwamba *this is not an absolute right*. Ni haki ambayo anaweza kuipata mtu yeyote mgeni, lakini siyo haki ya lazima ya moja kwa moja kulingana na utaratibu wa kisheria. Mtu anayeomba uraia lazima akidhi vigezo na vigezo hivyo vipo vimeainishwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati mwingine katika utaratibu wa utoaji wa uraia, tutaendelea kuzingatia vigezo vilivyopo kwa mujibu wa sheria na kuweza kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama hata pale ambapo tutafika kuweza kutoa huo uraia ili mwisho wa siku Taifa letu Tanzania libaki kuwa salama na tuweze kurithisha kwa vizazi hata vizazi. Hili niseme tu kwamba tutaendelea kutoa, lakini tutazingatia masharti na vigezo viliyoainishwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengine pia yamezungumziwa kuhusiana na maslahi ya askari. Limegusiwa

jambo hapo kuhusiana na mafao; kikokotoo tumekirekebisha chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa sasa marekebisho yanaendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na agizo la Mheshimiwa Rais la masuala ya bima na maboresho ya askari; amepandisha vyeo, ameongeza mishahara, anazidi kuongeza na ataendelea kufanya hivyo kwa sababu ya maboresho ya askari wetu vijana ambao wanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe unafahamu, umekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa muda mrefu, ukiwa askari, ndiyo maana tunasema tunaandikisha, maana yake ni huyu ameshajitoa rehani. Ukimuona askari anarudi nyumbani kwenye familia yake ni jambo la kushukuru sana familia zao kwa sababu akitoka maana yake anaenda kukabiliana na chochote kitakachokuja hata kama ni kifo, kwa ajili ya ulinzi wa Taifa letu. Mheshimiwa Rais amezidi kuzingatia hilo na kuboresha maslahi yao ikiwa ni pamoja na hilo lililozungumzwa la kikokotoo.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu amezungumza pale, Mheshimiwa Mbunge, akasema amemkuta anasukuma baiskeli na nini! Huwezi kujua ukiwa askari, hata ukistaafu unaendelea kuwa askari, huwezi kujua alikuwa anafanya kazi gani. Huwezi kustaafu katika utumishi wa askari. Hata hivyo, pale inapotokea changamoto za askari yeyote, sisi Wizara ya Mambo ya Ndani tumeendelea kufanya kazi kuhakikisha kwamba changamoto hizo kwa askari wetu tunaziondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa maeneo mawili/matatu, moja ya malengo ni masuala ya ujenzi wa ofisi. Mahitaji yetu ni makubwa sana kwa sababu lengo ni tunataka tujenge vituo vya polisi 3,900 kwa nchi nzima, lakini mpaka sasa kulingana na upatikanaji wa fedha, tumejiwekea mpango wa kujenga vituo 669 katika maeneo hayo ambayo bado yatahitaji shilingi bilioni 108, ukiacha hivi ambavyo vimeathirika. Kwa hiyo, utaratibu unaendelea na sisi tunafanyia kazi maeneo hayo yote ili kuweza kuhakikisha kwamba tunaleta na tunatengeneza mazingira mazuri, rafiki na wezeshi. Tumeanza ujenzi wa maeneo ya makazi na tunaendelea kuhakikisha kwamba mambo haya yote tutayaboresha.

Mheshimiwa Spika, nikimalizia, hoja nyingine ni suala la wizi wa mtandao. Tumelitolea maelekezo, wahusika hapa tutazidi kuchukua hatua kwa sababu suala hili ukiacha wizi, yapo matumizi mabaya pia ya mitandao ambapo tunayo Sheria yetu ya *Media Content Regulation* ya mwaka 2005. Tunayo Sheria ya *Electronic and Postal Communication* na tunayo Sheria ya Kanuni za Adhabu.

Mheshimiwa Spika, tunayo sheria yetu, Katiba ambayo inahitaji mtu asitweze wala kudhalilishwa. Tunazo sheria na sera mbalimbali ambazo zimetungwa kwa ajili ya watu kutotumia mitandao kutweza utu wa mtu au kudhalilisha watu.

Mheshimiwa Spika, ninalisema hili kwa uchungu mkubwa kwa sababu wapo watu ambao wamejaribu kutweza utu na heshima za watu. Wapo ambao wamewadhalilisha kwa kuwavumishia na kuwazushia mambo ya uongo. Pia wapo ambao wamesababisha kutoa taarifa za uongo, uzushi na uchochezi.

Mheshimiwa Spika, nikitolea mfano, juzi ipo picha moja maarufu iliyoonesha mfungwa mmoja, ambao sisi tunawaita wanafunzi wa maadili, akiwa amevaa hereni na amevaa nguo za Magereza. Ile picha ilitengenezwa, ni ya *AI*. Jeshi la Magereza haliandiki Magereza, picha ile, nembo iliyobandikwa imeandikwa Magereza, lakini pia hapa urekebishaji ndiyo nembo ambayo ni sahihi. Hivyo, imejaribu kutengenezwa, mfungwa anakuwa na *label* inayoonesha siku aliyoingia na wakati ambao anapaswa kutoka katika kipindi cha utumishi wa nafasi yake. Pale imewekwa *logo* ambayo haieleweki ni ya wapi, lakini watu waliamini, kwa hiyo sasa matumizi mabaya kama hayo ya mtandao na yale ya kutweza utu na heshima za watu, udhalilishaji na utukanaji wa viongozi, tutaendelea kuchukua hatua kwa sababu, sheria tayari tunazo na hakuna mtu ambaye atakwepa mkono huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utapeli, tumefanya mazungumzo na Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri anayehusika na masuala ya Mawasiliano. Tumezungumza na Mheshimiwa Makonda kwenye masuala yale yanayohusiana na habari zinazochapishwa

na kutangazwa ambazo ni za uongo na uzushi, ili tuanze kuchukua hatua. Tunayo Sheria ya Madhara, mtu akidhalilisha au akisema jambo la uongo dhidi ya Serikali au dhidi ya mtu, tunamchukua na kumpeleka mahakamani; akizungumza katika muktadha wa siasa, kwa ajili ya kujipatia umaarufu wa kisiasa unaogandamiza wengine, tutachukua hatua kali.

Mheshimiwa Spika, natoa rai, hatujakusudia kutaka kuumiza watu, tunakusudia kwenda kusimamia sheria, taratibu na kanuni ambazo tumekubaliana ziweze kusimamiwa. Bentham aliwahi kusema, sheria zimetungwa kwa ajili ya kuleta *maximum pleasure* na *minimum pain*. *Minimum pain* itatolewa kwa wale ambao watakiuka sheria.

Mheshimiwa Spika, sheria tulizozitunga zitatoa furaha na mafanikio ya kiuchumi, kiafya na mazingira kwa sababu sheria njema tunazo, kwa hiyo, wale ambao watakiuka itakuwa ni bahati mbaya sana kwao kwa sababu hatukusudii. Imefika hatua sasa Taifa letu kila mtu ni msemaji, tumefika hatua Taifa letu sasa kila mtu anaweza akaamua kutweza utu wa mtu bila kuzingatia kuna sheria. Tumefika hatua ya kutoa maneno ya uchochezi, uzushi na uongo kwa kutumia teknolojia ya sasa ya *AI*. Yule anayefanya na anayetengeneza *content* hiyo na yule ambaye chombo chake kinatumika kuisambaza, tutachukua hatua kwa sababu tumejifunza na *never again,* Taifa letu halitafika kwenye maangamizi kwa sababu ya watu wachache ambao hawatutakii mema.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo pia ambayo yamezungumzwa kuhusiana na wahamiaji haramu. Moja ya matishio makubwa ya kiusalama, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wananisikia, ni matishio makubwa ya kiusalama. Tunaweza tukawa na taasisi, tunaweza tukawa na mifumo na kila kitu, lakini matishio ya kiusalama ya nchi yoyote duniani yanaanza na mtu mmoja mmoja. Mtu akiwa na *criminal mind*, mtu akiwa na *overt act,* anatenda matendo ambayo sheria haziruhusu, kanisa haliruhusu wala msikiti, matendo yake mtu mmoja yanaweza kuangamiza Taifa au jamii.

Mheshimiwa Spika, matishio ya kiusalama, inaweza ikawa ni taasisi ambazo zimeunganishwa kwa mujibu wa mifumo, ikiwa ni pamoja na taasisi ambazo zimeunganishwa kwa mfumo wa kisheria. Ikiwa jamii yetu itaona maovu kwa sababu, wezi wako kwenye mitaa yetu, ni jirani zetu, ni ndugu zetu, majambazi wako kwenye mitaa yetu, mipango mibaya inapangwa kwenye mitaa yetu na machafuko yanaratibiwa kwenye mitaa yetu. Tukinyamaza na kukaa kimya dhidi ya wahalifu wachache, maangamizi yataenda kwa Taifa letu, kwa hiyo, matishio ya usalama ni kila mahali tulipo.

Mheshimiwa Spika, tishio lingine la usalama ni pamoja na vyombo vilivyoundwa au kusajiliwa kwa mujibu wa sheria na vikakiuka utaratibu wa kutekeleza yale yaliyosajiliwa, vikafanya vitu kinyume chake. Mojawapo ni taasisi au asasi zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria, ikiwa hazitatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria, yale wanayoyafanya kinyume chake, tumeona wapo waliochagiza masuala ya mapenzi ya jinsia moja, tumechukua hatua na tutaendelea kuchukua hatua. Zipo taasisi ambazo zilikuja kuhamasisha watu hapa, ni taasisi iliyosajiliwa na imeeleza kwenye Katiba yake kwamba haijihusishi na masuala ya siasa, lakini iko *busy* kufadhili vyama vya siasa, tutachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo pia taasisi za dini; wakati wa Mtume Muhammad *Sallallahu Alayhi Wasallam*, wakati wa Issa bin Mariam, Yesu Kristo, wakati ule, hao wote ni viongozi wa dini nyingine. Tutakumbuka kwa kizazi cha sasa na *generation* inavyoenda, kama hatutajisimamia na kujiratibu vizuri kwenye masuala ya mtandao, usimamizi wa *Instagram*, *Facebook* na kadhalika, viongozi hao wa dini ambao ni waja wa Mwenyezi Mungu, Mtume Muhammad *Sallallahu Alayhi Wasallam* na Yesu Kristo, kwa matumizi mabaya ya mitandao inavyotumika leo, hata kama wao wangekuwepo wangeweza kukwazika na wangeweza kuchorwa vikatuni vya ajabu ajabu.

Mheshimiwa Spika, Serikali zote duniani zinatumia Sheria, Mikataba ya Kimataifa au Katiba zake. Serikali zote duniani zinatumia sera, lakini taasisi za dini zinatumia sheria kwa sababu

ndizo zinazozisajili. Taasisi za dini mwongozo wake ni mkubwa, Biblia Takatifu au Msahafu na hakuna sehemu ambayo inaruhusiwa kuingiliana kwenye haya maeneo. Kwa hiyo, kila mmoja ataheshimu na kuhifadhi mipaka yake. Pale ambapo tutaenda kinyume na hapo, napo pia tutazidi kukumbushana wajibu wetu ili kazi hii iweze kuendelea kufanyika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana viongozi wa taasisi zote za dini nchini, wameendelea kutuunga mkono, wako na sisi na wengi wao wako hapa na wengine wengi nje ambao wanawaongoza, tunawashukuru sana kwa sababu wamekuwa sehemu ya kusaidia Taifa letu. Kama taasisi za dini zitaendelea kutekeleza wajibu wake vizuri, tutapunguza wahalifu, tutapunguza watu ambao wana tamaa za madaraka, tutapunguza watu ambao wakipata nafasi wanaweza wakatumia vibaya ili kuweza kuangamiza walio wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia katika viongozi wa dini waliopo, wengi wako pamoja na Serikali, tunafanyanao kazi vizuri, tunashirikiananao na wameendelea kuhamasisha amani ya Taifa letu. Tunawashukuru sana waheshimiwa viongozi wa dini, muendelee kutekeleza wajibu wenu na Serikali tunawahakikishia tuko pamoja nanyi.

Mheshimiwa Spika, tishio lingine la usalama ni yapo pia mazingira ambayo hata taasisi zilizosajiliwa ikiwemo vyama vya siasa vinafanya kazi yake nzuri. Nchi yetu imejikita Kikatiba kutambua kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Hata hivyo, vyama vya siasa visipotumika vizuri ni tishio kubwa la usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tishio kubwa ni kama viongozi wa vyama vya siasa watatumia ndimi na kauli zao, maandiko na machapisho kuhamasisha vurugu na siyo mapatano. Pale zitakapotumika ndimi na kauli zao kuhamasisha wananchi kwenda kufanya mambo ambayo yanasababisha kuvunja amani ya nchi, tutazidi kukumbushana na kusimamia taratibu kwa sababu Wizara ya Mambo ya Ndani ni *custodian* wa masuala yote ya amani, usalama na nidhamu ya Taifa kwenye utekelezaji

wa sheria na ndiyo maana utakuta dakika ya mwisho wanalaumu Jeshi la Polisi au wanalaumu huyu na yule, lakini je, tumetekeleza wajibu wetu?

Mheshimiwa Spika, upo upotoshaji mkubwa ambao unatumika wa matumizi ya *basic and fundamental rights (bills of rights)*. Haki za binadamu katika Katiba yetu zimeelezwa kwenye Ibara ya 12 mpaka 29. Katika msingi huo, Katiba imeruhusu sheria nyingine zitungwe katika usimamizi wa masuala mbalimbali. Sheria hizo ambazo zimetungwa zinaendana na matakwa na matarajio ya Taifa, sera na misingi ya maendeleo ambayo yote yanakusudia zaidi katika kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa hayo, imekuwa si Bahati, wakati mwingine unakuta ambayo yanafanywa au kutekelezwa, mtu akijua kabisa kwamba kila haki ina wajibu wake katika utekelezaji, lakini tumekuwa tukizungumza na kuhubiri kwamba kuna haki, kuna haki. Qurani Tukufu na Biblia Takatifu zinatueleza; Biblia Takatifu ina masharti 10 ambayo ukiyatekeleza hayo ndiyo utaona ufalme wa Mungu, utaenda mbinguni.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo duniani hapa, tunazo sheria zinatuelekeza utaratibu wa kufanya kitu kwa ufasaha na usahihi. Ikitokea umeenda tofauti, ndipo hapo mkono wa sheria unachukua mkondo wake na hatimaye inaonekana kama mtu amelengwa. Sisi upande wa vyombo vya ulinzi na usalama, wajibu wetu ni kutafsiri sheria, kuangalia sheria zilizopo. Ikiwa kuna tuhuma zozote ambazo zimejitokeza za mtu kuvunja sheria, tutaendelea kufanya utaratibu huo kuweza kuhakikisha kwamba watu hawa wanaenda katika kuhakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake kwa utaratibu, bila vikwazo.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuboresha Tume ya Haki Jinai ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliiunda. Imetoa ushauri mzuri na ulikuwa jumuishi. Umehusisha vyama va siasa, umehusisha wananchi, umemhusisha kila Mtanzania na hatimaye wakatoa mwelekeo wa namna gani ambavyo tutaenenda.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie kwamba sisi tunakwenda kufanya maboresho makubwa kwa kufuata utaratibu uliotolewa, ushauri uliotolewa na Bunge, Tume na Kamati mbalimbali na kujifunza *best practice* duniani kote kwenye maeneo ambayo yamekuwa yakifanya vizuri ili kuhakikisha lile tabasamu ambalo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliliahidi kwa wananchi, tunaendelea kulitekeleza. *(Makofi*

Mheshimiwa Spika, aidha, mwisho ninakushukuru sana wewe na niendelee kuliahidi Bunge lako Tukufu kuwa kwenye maeneo yote yale ambayo yametolewa hoja na Waheshimiwa Wabunge na hatujaweza kujibu hapa kwa sababu ya muda, tutakwenda kuyafanyia kazi kikamilifu ili kuhakikisha kwamba tunapunguza changamoto na kuziondoa pale inapobidi ambazo sizo za lazima ili kuhakikisha Watanzania wanaishi kwa amani, usalama na utulivu.

Mheshimiwa Spika, moja ya vielelezo leo utaona hata maduka, kwa sababu ya uwepo wa amani, siku hizi hatuweki milango ya mbao wala ya mabati, kuna vioo watu wanafanya kazi. Kwa sababu ya amani, shughuli za kiuchumi kila mahali zinaendelea. Kwa sababu ya amani, kuna nchi ambazo hawawezi kukaa kwenye Mabunge kama hivi, ni kwa sababu ya amani na kazi kubwa ambayo inafanywa na askari wetu. Tuwatie nguvu na tuwatie moyo askari wetu, tusiwatweze na kuwaumiza kwa kauli na kuwaumiza. Wanajitoa muhanga, wametoa maisha yao na wamekuwa tayari kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale yanapotokea machafuko tunakumbuka askari wako wapi, pale ambapo foleni zimejaa, magari hayasongi mbele, tunauliza *traffic* wako wapi, pale ambapo tunapata shida mipakani, tunauliza uhamiaji wako wapi, pale ambapo tumepata wavamizi, wahamiaji haramu, tunauliza *NIDA* na watu wengine wako wapi, pale ambapo wahalifu wanapoingia kwenye mitaa yetu na kufanya uhalifu na bila kukamatwa, tunauliza polisi wako wapi, lakini ikifika sehemu ambapo tumevaa tai, tumechomekea, tunafanya kazi za kisiasa, tuko vizuri tunawasahau askari.

Mheshimiwa Spika, sisi tumeoneshwa mfano na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amewavika nishani na kofia ya heshima askari wetu, tuendelee kuwaunga mkono. Kwa sababu usalama wa Taifa letu unawategemea askari wetu, unawategemea wanajeshi wetu. Sisi wenyewe tuwe chachu katika tuwakemee walio waovu, kwa sababu waovu ni wachache, lakini watu wengi walio wema hatuwasemi. Hiyo ilikuwa ni kauli ya Albert Einstein.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nizidi kukushukuru wewe, nilishukuru Bunge lako Tukufu, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge. Baada ya kumaliza hapa, tutakuja kwenye ziara kuweza kuhakikisha kwamba kila eneo linakuwa salama. *(Makofi*

Mheshimiwa Spika, yapo pia ambayo yamekuwa yakizungumzwa, kwa mfano ambayo sisi tutayazungumza kwenye hatua mbalimbali. Niliona nisiyazungumze hapa kwa sababu mengine yanatokana na utaalamu wa masuala ya kijeshi, ni mambo ambayo yana usiri wake kwenye masuala ya jinai ambayo sikupaswa kuweza kuyazungumza hapa, lakini ninatambua kwamba hoja hizo nimezichukua, nyingine nimeletewa kwa maandishi na pale inapolazimu, tutayachukulia hatua.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie, hata pale ambapo kwa mujibu huo huo, sheria ni msumeno, wale askari ambao imetokea wamefanya makosa, tumeendelea kuchukua hatua. Wapo tuliowafukuza kazi, wapo ambao tumewapa adhabu mbalimbali za kijeshi na wapo ambao tutaendelea kuwachukulia hatua ili mradi tu wamekiuka. Tunazo sheria zetu, tuna *PGO*, tuna sheria za vyombo vya ulinzi na usalama na pia tunao utaratibu wetu. Tuna vyombo vyetu na mahakama zetu za ndani na zina utaratibu wake. Kuna wakati unaweza ukadhani askari hajachukuliwa hatua, lakini tuna taratibu zetu za kijeshi ndani ambazo tunaendelea kuchuliana hatua. Kwa hiyo, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba askari mmoja anayefanya akatweza na kuharibu sifa ya vyombo vya ulinzi na usalama hauwezi kuwa ndio msimamo wa jeshi letu lote.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuchukua hatua na mimi nikiwa Mwenyekiti wa Tume hiyo ya askari wote wa Jeshi la Polisi, Tume ya Magereza, lakini pia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na vyombo vingine, tutasimama na tutafuata utaratibu wa kisheria ili kuhakikisha kuwa wale ambao watakiuka utaratibu, kama jinsi ambavyo raia pia itakapotokea wamekiuka utaratibu, sheria itachukua mkondo wake na sheria ni msumeno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wote Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa anasimamia na amesema wakati wote, hakuna aliye juu ya sheria. Huo ndio msingi wa Wizara ya Mambo ya Ndani katika kusimamia utaratibu. Tusioneane huruma, tusiweke muhali katika kusimamia masuala ya sheria na pia tusiwe na hatua yoyote ile ya kutengeneza huruma kwamba umevunja sheria, halafu unatengeneza huruma ili uweze kuonewa huruma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa kutoa hoja. Ahsante. *(Makofi*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Waziri hongera sana. Wakati unamalizia, nilikuwa ninamwona Mheshimiwa Ado naye anapiga makofi kuwa anashukuru maneno yako uliyosema ni mazito.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako ijielekeze katika Kitabu cha Pili, Matumizi

ya Kawaida, Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, katika ukurasa wa 491.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.........................Sh.44,870,862,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nina ombi la mshahara wa Mheshimiwa Waziri kutoka kwa Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuniona. Nitangulie kwa kusema kwamba ninasimama chini ya Kanuni ya 125(1), kanuni ambayo inatoa nafasi kwa Mheshimiwa Mbunge kutaka maelezo ya ziada, huo ndio msingi wa kusimama kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini mwetu kumekuwepo na matukio ya utekaji, watu kupotea na watu kujeruhiwa. Tukio la karibuni zaidi ni tukio lililomkuta Msaidizi wa Mwenyekiti wa CHADEMA, Ndugu David Juma. Kwa vile Wizara hii inahusu usalama wa raia, nimesimama kutaka maelezo ya ziada kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Je, ni upi mwelekeo wa Serikali juu ya matukio haya? Ni hatua gani zinachukuliwa ili kuhakikisha vitendo hivi vinakomeshwa kabisa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Ado Shaibu, Mbunge na wakili msomi kwa hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleeza na kwa sababu ya ufinyu wa muda, nina *reference* ya taarifa mbalimbali juu ya ukiacha matukio kama haya ya utekaji aliyoyaeleza, katika

ujumla wake ni matukio yote ya jinai. Kwa sababu matukio ya jinai yanamgusa mtu moja kwa moja na wajibu na msingi mkuu wa Kikatiba na sheria ni kusimamiwa na Serikali na ndiyo maana makosa yote ya jinai yanasimamiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili, ameuliza mambo mawiili, la kwanza ni mwelekeo na la pili hatua. Kuhusiana na masuala ya mwelekeo, tayari tunayo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inakataza na inakataa masuala haya. Vivyo hivyo tunayo sheria nyingine ya Kanuni za Adhabu *(Penal Code Cap 16)*, hii sheria inaeleza kwamba kama kutatokea tukio la namna yoyote ile dhidi ya shambulio kwa mtu au kwa utaratibu ambao upo nje ya utaratibu wa sheria, maana yake ni kwamba chombo ambacho kinahusika na masuala ya usimamizi wa ulinzi na usalama na upelelezi itachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wote tumekuwa tukipata matukio haya ya utekaji, Jeshi la Polisi limeendelea kusimama imara, limekuwa likifanya upelelezi na uchunguzi juu ya hoja na changamoto mbalimbali za masuala ya utekaji. Kitu ambacho kitaendana na kile nilichokizungumza, kuna masuala ya uzandiki na *subversion*, yapo pia ambayo yanatokea. Tunazo kesi za utekaji ambazo zipo, zinaendelea kuchukuliwa hatua mbalimbali za kiupelelezi. Siwezi kuzungumza hapa kwa sababu ya faida ya taratibu za kiupelelezi na Mheshimiwa Ado anafahamu *The Criminal Procedure,* hainiruhusu kueleza juu ya mambo mbalimbali ambayo yanahusiana na masuala ya upelelezi. Yapo mambo ambayo kwa sababu ni mbinu za kimkakati ambazo ni za kimedani zinazotumika katika kutafuta wahalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo kesi mbalimbali katika mahakama zetu ambazo zilipelekewa kwa utaratibu ule wa kama makosa ya jinai ambazo nazo pia zipo zinazoendelea, zipo ambazo zilionekana hazina mashiko, kwa sababu suala la kusema jambo au kutuhumu ni moja, lakini la pili ni ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ado anafahamu kwamba hata kama ungekuwa na ubora Mheshimiwa Waziri na

ushahidi unategemeana na jinsi ambavyo mtu atalisimamia. Kwa hiyo, kuna kesi ambazo zilifutwa kwa kukosa ushahidi na hazikwenda kwenye hatua ya mbele zaidi. Pia zipo kesi nyingine za masuala ya utekaji ambazo zilibainika kwamba yalitokana na visasi vya mambo mbalimbali. Mojawapo ni visasi vya masuala ya biashara, uhasama unaohusiana na masuala mbalimbali ya kimahusiano ya katika jamii. Inawezekana ni biashara, inawezekana ni siasa. Masuala haya, yamekuwa yakipelekea kupata matukio ya namna hiyo. Matokeo yake pia yapo masuala ya utekaji ambayo yalitokea, na watu kufanya, rekodi tunayo, waliamua kusema kuhusiana na kwamba nimetekwa na ikazushwa hivyo na hatimaye tulikuja kugundua kwamba ulikuwa ni mchoro au mchongo wa kisiasa, kwa lugha ya kisasa wanayoisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Taifa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara ya Mambo ya Ndani na sheria zake zote, juzuu 438, hakuna sehemu tunayoruhusu mambo haya na ikitokea popote pale, tutachukua hatua na hata yale yaliyotokea, tunaendelea kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na mwelekeo, mwelekeo ni…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni moja tu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** … msingi uleule wa kusimamia haki za binadamu na utawala wa sheria. Tutaendelea kusimama na hilo. Nimpe *trust* hiyo msomi mwenzangu kwamba sisi tutaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha kuwa jambo hili linafikia mwisho. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ado ameridhika na majibu sahihi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*......Sh.1,173,497,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*......Sh.1,792,654,000
Kifungu 1004 – *Probation Services Division*......Sh.8,177,634,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*......Sh.1,038,606,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*......Sh.951,206,000
Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*......Sh.916,803,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*......Sh.1,039,093,000
Kifungu 1009 – *Complaints Unit*......Sh.827,103,000
Kifungu 1010 – *Legal Services Unit*......Sh.1,019,006,000
Kifungu 1011 – *The Police, Prisons, Fire & Rescue and Immigration Services Commission*......Sh.1,537,990,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*......Sh.1,101,951,000
Kifungu 2001 – *Registrar of Societies Unit*......Sh.1,843,458,000
Kifungu 4001 – *Refugees Services Division*......Sh. 4,593,423,000
Kifungu 4002 – *Anti – Trafficking in Person Secretariat*......Sh.1,752,447,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2001 – *Immigration Zanzibar*......Sh.21,108,000,000
Kifungu 2002 – *Immigration Head Quarter*......Sh.149,135,059,000
Kifungu 2003 – *Immigration Ilala*......Sh.76,875,000
Kifungu 2004 – *Tanzania Regional Immigration Training Academy*......Sh.471,000,000
Kifungu 2005 – *Immigration Kinondoni*......Sh.70,680,000
Kifungu 2006 – *Immigration Temeke*......Sh.70,680,000
Kifungu 2007 – *Immigration Arusha*......Sh.199,605,000
Kifungu 2008 – *Immigration Dar es Salaam*......Sh.249,475,000

Kifungu 2009 – *Immigration Dodoma*............................Sh.235,072,000
Kifungu 2010 – *Immigration Geita*................................Sh.249,598,000
Kifungu 2011 – *Immigration Iringa*..................................Sh.218,173,000
Kifungu 2012 – *Immigration Kilimanjaro*........................Sh.278,212,000
Kifungu 2013 – *Immigration Kigoma*..............................Sh.320,119,000
Kifungu 2014 – *Immigration Katavi*................................Sh.236,041,000
Kifungu 2015 – *Immigration Kagera*..............................Sh.326,887,000
Kifungu 2016 – *Immigration Lindi*...................................Sh.235,270,000
Kifungu 2017 – *Immigration Mwanza*............................Sh.265,315,000
Kifungu 2018 – *Immigration Manyara*...........................Sh.248,632,000
Kifungu 2019 – *Immigration Mbeya*..............................Sh. 256,636,000
Kifungu 2020 – *Immigration Morogoro*..........................Sh.258,472,000
Kifungu 2021 – *Immigration Mtwara*..............................Sh.256,546,000
Kifungu 2022 – *Immigration Mara*...................................Sh.270,349,000
Kifungu 2023 – *Immigration Njombe*.............................Sh.237,445,000
Kifungu 2024 – *Immigration Pwani*.................................Sh.280,756,000
Kifungu 2025 – *Immigration Ruvuma*.............................Sh.244,213,000
Kifungu 2026 – *Immigration Rukwa*................................Sh.244,051,000
Kifungu 2027 – *Immigration Simiyu*.................................Sh.236,080,000
Kifungu 2028 – *Immigration Singida*..............................Sh.241,345,000
Kifungu 2029 – *Immigration Shinyanga*.........................Sh.216,015,000
Kifungu 2030 – *Immigration Tanga*................................Sh.270,079,000
Kifungu 2031 – *Immigration Tabora*..............................Sh.247,546,000
Kifungu 2032 – *Immigration Songwe*............................Sh.241,795,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services*.................Sh.23,217,188,000
Kifungu 3006 – *Arusha Regional Office*.......................Sh.2,030,767,000
Kifungu 3007 – *Dodoma Regional Office*..................Sh.3,266,592,000
Kifungu 3008 – *Mwanza Regional Office*...................Sh.2,702,851,000
Kifungu 3009 – *Mbeya Regional Office*.....................Sh.2,409,039,000
Kifungu 3010 – *Kinondoni Regional Office*................Sh.2,511,823,600
Kifungu 3011 – *Mara Regional Office*.........................Sh.1,170,772,000
Kifungu 3012 – *Kigoma Regional Office*.....................Sh.1,485,899,000
Kifungu 3013 – *Pwani Regional Office*.......................Sh.2,936,223,100

Kifungu 3014 – *Manyara Regional Office*..................Sh.1,500,164,000
Kifungu 3015 – *Geita Regional Office*........................Sh.1,313,530,000
Kifungu 3016 – *Temeke Regional Office*...................Sh. 5,511,679,900
Kifungu 3017 – *Singida Regional Office*.....................Sh.1,233,657,000
Kifungu 3018 – *Tabora Regional Office*.....................Sh.1,399,444,000
Kifungu 3019 – *Iringa Regional Office*........................Sh.1,579,487,000
Kifungu 3020 – *Rukwa Regional Office*......................Sh.1,471,961,000
Kifungu 3021 – *Ruvuma Regional Office*...................Sh.1,448,475,000
Kifungu 3022 – *Kagera Regional Office*.....................Sh.1,250,832,000
Kifungu 3023 – *Mtwara Regional Office*....................Sh.1,375,526,000
Kifungu 3024 – *Lindi Regional Office*..........................Sh.1,284,530,000
Kifungu 3025 – *Njombe Regional Office*....................Sh.1,387,728,000
Kifungu 3026 – *Shinyanga Regional Office*...............Sh.1,476,375,000
Kifungu 3027 – *Ilala Regional Office*..........................Sh.2,958,940,000
Kifungu 3028 – *Kilimanjaro Regional Office*..............Sh.1,371,528,000
Kifungu 3029 – *Morogoro Regional Office*................Sh.2,453,990,000
Kifungu 3030 – *Katavi Regional Office*.......................Sh.1,160,266,000
Kifungu 3031 – *Tanga Regional Office*.......................Sh.2,006,573,200
Kifungu 3032 – *Simiyu Regional Office*.......................Sh.1,217,245,000
Kifungu 3033 – *Songwe Regional Office*....................Sh.1,363,147,000
Kifungu 3034 – *Fire and Rescue Training College*................................................Sh.3,927,016,700

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Kifungu 1001 - *Administration And Human Resources Management*...............Sh.254,077,745,464
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*.................Sh.331,272,709,200
Kifungu 1003 – *Internal Monitoring and Evaluation Unit*.............................Sh. 353,380,670
Kifungu 1004 – *Legal and Research Services Unit*...........................................Sh.878,637,100
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 660,787,100
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*................................Sh. 236,417,000
Kifungu 2001 – *Police Main Force*.............................Sh. 6,123,401,136

Kifungu 2002 – *Police Marine*......................................Sh. 2,047,693,000
Kifungu 2003 – *Railway Police Division*.......................Sh.5,947,798,000
Kifungu 2004 – *Police Signals Branch*.........................Sh.4,795,055,000
Kifungu 2005 – *Police Zanzibar*.................................Sh.12,276,152,000
Kifungu 2006 – *Police Air Wing*...................................Sh.2,999,077,000
Kifungu 2007 – *Tazara Police*......................................Sh.2,760,344,000
Kifungu 2008 – *Field Force Unit*..................................Sh. 2,464,147,300
Kifungu 2009 – *Traffic Police*.......................................Sh.1,068,432,000
Kifungu 2010 – *Police Airport*......................................Sh.4,907,938,200
Kifungu 2011 – *Police Dogs and Horses*.....................Sh.1,430,416,000
Kifungu 2012 – *Dar es Salaam Special*
*Zone*..................................................Sh.1,430,416,000
Kifungu 2013 – *Police Ilala*........................................Sh.16,248,862,600
Kifungu 2014 – *Police Kinondoni*..............................Sh.20,693,926,800
Kifungu 2015 – *Police Temeke*..................................Sh.12,558,400,000
Kifungu 2016 – *Police Arusha*...................................Sh.21,907,032,000
Kifungu 2017 – *Police Iringa*......................................Sh.13,219,242,000
Kifungu 2018 – *Police Kilimanjaro*............................Sh.18,748,529,500
Kifungu 2019 – *Police Kigoma*..................................Sh.15,751,166,000
Kifungu 2020 – *Police Kagera*...................................Sh.17,149,992,000
Kifungu 2021 – *Police Lindi*.........................................Sh.11,531,031,000
Kifungu 2022 – *Police Mwanza*.................................Sh.27,853,076,500
Kifungu 2023 – *Police Mara*.......................................Sh.12,631,756,000
Kifungu 2024 – *Police Tarime – Rorya*.......................Sh.11,185,658,000
Kifungu 2025 – *Police Mbeya*...................................Sh.17,866,675,000
Kifungu 2026 – *Police Mtwara*...................................Sh.13,664,898,000
Kifungu 2027 – *Police Morogoro*.............................Sh. 21,824,001,000
Kifungu 2028 – *Police Manyara*................................Sh.11,684,461,000
Kifungu 2029 – *Police Singida*...................................Sh.13,244,189,000
Kifungu 2030 – *Police Pwani*......................................Sh.14,720,286,000
Kifungu 2031 – *Police Ruvuma*..................................Sh.13,302,957,000
Kifungu 2032 – *Police Rukwa*.....................................Sh.10,792,441,000
Kifungu 2033 – *Police Shinyanga*.............................Sh.13,871,424,000
Kifungu 2034 – *Police Tabora*...................................Sh.14,643,964,000
Kifungu 2035 – *Police Tanga*....................................Sh.18,257,486,000
Kifungu 2036 - *Police Mjini Magharibi*......................Sh.14,227,029,000
Kifungu 2037 – *Police Kusini Unguja*...........................Sh.8,145,195,000
Kifungu 2038 – *Police Kaskazini Unguja*.........................Sh.445,672,400
Kifungu 2039 – *Police Kusini Pemba*..........................Sh.5,975,878,000

Kifungu 2040 – *Police Kaskazini Pemba*......................Sh.5,848,443,000
Kifungu 2041 – *Police Dodoma*..................................Sh.29,133,156,000
Kifungu 2042 – *Police Geita*.......................................Sh.13,039,208,000
Kifungu 2043 – *Police Katavi*.......................................Sh.9,154,147,000
Kifungu 2044 – *Police Njombe*..................................Sh.10,524,389,000
Kifungu 2045 – *Police Simiyu*.....................................Sh.10,055,335,000
Kifungu 2046 – *Police Songwe*...................................Sh. 8,785,713,000
Kifungu 2047 – Police Rufiji..........................................Sh. 8,271,605,000
Kifungu 2048 – *TPF Corporation Sole Unit*..................................................Sh.185,328,000
Kifungu 2049 – *Police Bandari*....................................Sh.3,630,614,344
Kifungu 2050 – *Police Band*.........................................Sh.2,493,117,672
Kifungu 2051 – *Police Bohari*.......................................Sh. 4,896,816,320
Kifungu 3001 – *Police College Moshi*........................Sh. 36,438,281,894
Kifungu 3002 – *Police College*.....................................Sh.3,910,590,000
Kifungu 3003 – *Operations and Training*....................Sh.5,633,432,000
Kifungu 3004 – *Zanzibar Police College*......................Sh.1,861,098,000
Kifungu 3005 – *Mwanza Marine Police College*..................................................Sh.2,370,908,000
Kifungu 3006 – *Tanzania Police Staff College - Kidatu*...................................Sh.928,513,848
Kifungu 4001 - *Police Vehicles Maintenance Unit*................................Sh.5,084,350,000
Kifungu 5001 – *Police Medical Unit*.............................Sh.4,910,362,000
Kifungu 6001 – *Police Ujenzi*........................................Sh.1,083,604,000

Kifungu 7001 – *Criminal Investigation Division*................................................Sh.11,094,955,000
Kifungu 7002 – *Stock Theft Prevention Unit*..........................................................Sh.972,076,000
Kifungu 7003 – *Criminal Intelligence Bureau*...................................................Sh3,551,198,000
Kifungu 7004 - *Forensic Intelligence Bureau*...................................................Sh.6,117,959,900
Kifungu 7005 – *Community Engagement*..................Sh.1,329,908,200

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 29 – Jeshi la Magereza

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh.76,175,495,688
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*......................................Sh.3,149,087,100
Kifungu 1003 – *Public Relations and Communication Unit*.............................Sh. 357,860,600
Kifungu 1004 – *Intelligence and Operations Unit*...................................Sh.1,374,137,610
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*................................Sh.1,300,354,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*................................Sh.2,941,611,760
Kifungu 1007 - *Information And Communication Technology Unit*....................................Sh.1,363,991,760
Kifungu 2001 - *Legal and Prisons Unit*........................................................Sh.6,036,982,100
Kifungu 2002 - *Correctional and Rehabilitation*...................................Sh.131,113,167,587
Kifungu 2003 – *Resettlement of Offenders*.............................................Sh.5,808,592,660
Kifungu 2004 – *Prisons Arusha*.....................................Sh.9,667,538,420
Kifungu 2005 – *Prisons Dar es Salaam*......................Sh.15,133,587,510
Kifungu 2006 – *Prisons Dodoma*..................................Sh.9,267,133,900
Kifungu 2007 – *Prisons Kigoma*.....................................Sh.1,377,384,642
Kifungu 2008 – *Prisons Tanga*......................................Sh.7,441,485,240
Kifungu 2009 – *Prisons Kagera*....................................Sh.6,283,700,580
Kifungu 2010 – *Prisons Mwanza*...................................Sh.5,456,888,160
Kifungu 2011 – *Prisons Tabora*.....................................Sh.2,100,162,050
Kifungu 2012 – *Prisons Mbeya*.....................................Sh.7,135,258,210
Kifungu 2013 – *Prisons Singida*....................................Sh.1,365,288,390
Kifungu 2014 – *Prisons Coast*......................................Sh. 9,953,139,200
Kifungu 2015 – *Prisons Lindi*........................................Sh. 2,998,742,640
Kifungu 2016 – *Prisons Manyara*.................................Sh.4,619,608,730
Kifungu 2017 – *Prisons Mtwara*...................................Sh.4,313,845,810
Kifungu 2018 – *Prisons Ruvuma*..................................Sh.1,305,408,520
Kifungu 2019 – *Prisons Rukwa*....................................Sh.3,630,340,582
Kifungu 2020 – *Prisons Mara*......................................Sh.5,827,766,770

Kifungu 2021 – *Prisons Iringa*........................................Sh.3,210,475,020
Kifungu 2022 – *Prisons Kilimanjaro*...............................Sh.6,919,202,060
Kifungu 2023 – *Prisons Morogoro*.............................Sh.12,145,844,442
Kifungu 2024 – *Prisons Geita*.......................................Sh.3,479,236,870
Kifungu 2025 – *Prisons Katavi*......................................Sh.3,479,236,870
Kifungu 2026 – *Prisons Njombe*.....................................Sh. 730,987,500
Kifungu 2027 – *Prisons Simiyu*......................................Sh.1,308,303,230
Kifungu 2028 – *Prisons Shinyanga*.................................Sh. 921,941,910
Kifungu 2029 – *Prisons Songwe*..................................Sh. 3,637,498,020
Kifungu 3001 – *Ukonga Prisons Staff College*...............................................Sh.6,304,394,372
Kifungu 3002 – *Kingolwira Prisons Driving School*......................................Sh.1,503,138,080
Kifungu 3003 – *Ruanda Prisons Trade School*.......................................Sh.1,449,508,740
Kifungu 3004 - *Prisons College Kiwira*..................................................Sh.2,048,246,980
Kifungu 4001 - *Prison Building Brigade*................................................Sh.6,156,098,097
Kifungu 4002 – *Prison Industries*......................................................Sh.0
Kifungu 4003 – *Prison Farms*...........................................................Sh.0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services*.................Sh.14,534,113,000
Kifungu 3007 – *Dodoma Regional Office*...................Sh.600,000,000
Kifungu 3008 – *Mwanza Regional Office*.....................Sh. 400,000,000
Kifungu 3009 – *Mbeya Regional Office*.....................Sh.1,736,000,000
Kifungu 3011 – *Mara Regional Office*........................Sh.1,636,000,000
Kifungu 3012 – *Kigoma Regional Office*....................Sh.1,736,000,000
Kifungu 3013 – *Pwani Regional Office*..........................Sh.600,000,000
Kifungu 3014 – *Manyara Regional Office*.....................................Sh.0

Kifungu 3015 – *Geita Regional Office*............................................Sh.0
Kifungu 3017 – *Singida Regional Office*.....................Sh.1,636,000,000
Kifungu 3018 – *Tabora Regional Office*.........................................Sh.0
Kifungu 3019 – *Iringa Regional Office*...........................................Sh.0
Kifungu 3021 – *Ruvuma Regional Office*....................................Sh.0
Kifungu 3022 – *Kagera Regional Office*........................................Sh.0
Kifungu 3024 – *Lindi Regional Office*.............................................Sh.0
Kifungu 3025 – *Njombe Regional Office*.......................................Sh.0
Kifungu 3026 – *Shinyanga Regional Office*...............Sh.1,736,000,000
Kifungu 3028 – *Kilimanjaro Regional Office*..................Sh.600,000,000
Kifungu 3029 – *Morogoro Regional Office*...................................Sh.0
Kifungu 3030 – *Katavi Regional Office*..........................................Sh.0
Kifungu 3031 – *Tanga Regional Office*..........................................Sh.0
Kifungu 3032 – *Simiyu Regional Office*..........................................Sh.0
Kifungu 3033 – *Songwe Regional Office*.......................................Sh.0
Kifungu 3034 - *Fire and Rescue Training College*................................Sh.2,799,400,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*..................Sh.128,742,068,071
Kifungu 2004 - *Police Signals Branch*....................Sh. 28,210,172,170
Kifungu 2005 – *Police Zanzibar*........................................Sh.400,000,000
Kifungu 2013 – *Police Ilala*...........................................Sh.1,231,999,256
Kifungu 2014 – *Police Kinondoni*................................Sh.1,260,000,000
Kifungu 2015 – *Police Temeke*....................................Sh.2,412,330,749
Kifungu 2016 – *Police Arusha*........................................Sh.330,000,000
Kifungu 2017 – *Police Iringa*.......................................Sh.1,610,228,990
Kifungu 2018 – *Police Kilimanjaro*.................................Sh.445,000,000
Kifungu 2020 – *Police Kagera*.......................................Sh.809,000,000
Kifungu 2021 – *Police Lindi*...........................................Sh.971,000,000
Kifungu 2022 – *Police Mwanza*..................................Sh.1,678,550,582
Kifungu 2023 – *Police Mara*..........................................Sh.918,000,000
Kifungu 2024 – *Police Tarime – Rorya*............................Sh.628,449,490
Kifungu 2025 – *Police Mbeya*........................................Sh.165,000,000
Kifungu 2026 – *Police Mtwara*.......................................Sh.809,000,000

Kifungu 2027 – *Police Morogoro*....................................Sh.502,000,000
Kifungu 2028 – *Police Manyara*.....................................Sh.809,000,000
Kifungu 2031 – *Police Ruvuma*......................................Sh.400,000,000
Kifungu 2032 – *Police Rukwa*........................................Sh.565,228,990
Kifungu 2033 – *Police Shinyanga*................................Sh.1,443,449,490
Kifungu 2034 – *Police Tabora*.......................................Sh.165,228,990
Kifungu 2035 – *Police Tanga*......................................Sh.1,720,000,000
Kifungu 2036 – *Police Mjini Magharibi*...........................Sh.255,000,000
Kifungu 2038 – *Police Kaskazini Unguja*.........................Sh.560,672,400
Kifungu 2039 – *Police Kusini Pemba*...........................Sh.1,735,000,000
Kifungu 2040 – *Police Kaskazini Pemba*........................Sh.137,000,000
Kifungu 2041 – *Police Dodoma*..................................Sh.2,798,000,000
Kifungu 2042 – *Police Geita*..........................................Sh.509,857,688
Kifungu 2044 – *Police Njombe*.........................................................Sh.0
Kifungu 2045 – *Police Simiyu*......................................Sh.1,774,228,990
Kifungu 2046 – *Police Songwe*.......................................Sh.809,000,000
Kifungu 2051 – *Police Bohari*.....................................Sh.15,240,577,144
Kifungu 3001 – *Police College Moshi*.............................Sh.600,000,000
Kifungu 3004 – *Zanzibar Police College*........................Sh.480,000,000
Kifungu 3005 – *Mwanza Marine Police College*..........Sh.300,000,000
Kifungu 3006 – *Tanzania Police Staff College – Kidatu*....................................Sh.330,000,000
Kifungu 7005 – *Community Engagement*..................Sh.1,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...................................Sh.3,289,065,000
Kifungu 2002 – *Correctional and Rehabilitation*..................................Sh.10,000,000,000
Kifungu 4001 – *Prison Building Brigade*.......................Sh.7,900,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*....................Sh.132,262,495,000
Kifungu 4002 – *Anti - Trafficking in Person Secretariat*...............................Sh.6,143,877,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2002 – *Immigration Head Quarter*..............Sh.99,485,448,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Hivyo, ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa Na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda, Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa kazi nzuri wewe na Mheshimiwa Naibu na timu yako, ukianzia Wizarani na vyombo vyenyewe, mnafanya kazi nzuri, hongereni sana.

Ninasisitiza tu, labda muwe na *regulations* za kuweka kamera hata kwenye maduka ya watu binafsi, kamera ambazo zinatazama katika *3D position* zisaidie kukamata uhalifu na kuona vitendo ambavyo vinafanywa, ili kulinda watu na mali ya mwenye duka mwenyewe.

*Otherwise,* ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maswali mazuri, na mimi ndiyo maana ninawapenda Waheshimiwa Mawaziri ninyi, kwa sababu mnayo majibu sahihi ya kuwaambia watu. Serikali haiogopi maswali magumu, majibu yake yapo. Wengine wanafikiri wakiomba kuuliza maswali kwa Mheshimiwa Waziri, wanafikiri labda majibu tu yanakimbiwa, majibu yanajibiwa na yanajibiwa kwa ufasaha na watu wenye maswali wanaelewa ukweli ulivyo. *(Makofi)*

Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuboresha miundombinu mingi ya Wizara yako. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya machache, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.17 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 26 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA